**16 JUNI, 2025**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Arobaini na Sita – Tarehe 16 Juni, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. BAHATI KHAMIS KOMBO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Tathmini ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2024, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Mapendekezo ya Makadirio ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bahati Kombo, ahsante sana.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali, tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Daniel Tlemai Awack, Mbunge wa Karatu, sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Joseph Mkundi.

Na. 585

### Hitaji la Wodi ya Wazazi na Maabara Kituo cha Afya Oldeani – Karatu

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI K.n.y. MHE. DANIEL T. AWACK** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatoa fedha za ujenzi wa Wodi ya Wazazi na Jengo la Maabara Kituo cha Afya Oldeani Karatu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Oldeani kilichopo katika Kata ya Oldeani, Halmashauri ya Karatu, kilijengwa mwaka 1971. Kituo hicho kina upungufu na uchakavu wa baadhi ya majengo yakiwemo Wodi ya Wazazi, Jengo la Kuhudumia Wagonjwa wa Nje *(OPD)*, Jengo la Upasuaji, Jengo la Wazazi, Jengo la Maabara na Jengo la Huduma za Baba, Mama na Mtoto *(RCH)*.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha miundombinu ya kituo hicho, Serikali imekiingiza kwenye orodha ya vituo vya afya kongwe 203 ambavyo Serikali ilivifanyia tathmini kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu yake.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakamilisha ukarabati wa hospitali 50 kongwe nchini, na baada ya hapo itafanya ukarabati

wa vituo vya afya na zahanati kongwe kote nchini kikiwemo Kituo cha Afya cha Oldeani Karatu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru. Ninaipongeza Serikali kwa tathmini hiyo na hatua waliyoifanya. Hata hivyo, nilitaka kujua, swali langu la kwanza; kwa kuwa tayari tathmini imefanyika, sasa kuna mpango gani wa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Karatu ili kuona kwamba maeneo yote ambayo ni chakavu na yana changamoto kama hizo kwenye Jimbo la Karatu, basi vituo hivyo vinafanyiwa marekebisho?

Mheshimiwa Spika, kwenye Jimbo la Ukerewe kuna Kituo cha Afya cha Nakatunguru ambacho kilijengwa mwaka 2012 na kina upungufu mkubwa sana wa majengo kiasi kwamba baadhi ya huduma zinashindwa kufanyika kwa sababu ya miundombinu kutokuwa kamilifu. Je, ni lini sasa Ofisi ya Rais, TAMISEMI watasaidia kukamilisha majengo kwenye kituo hiki cha afya ili wananchi waweze kupata huduma stahiki kwenye kituo hicho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge Joseph Mkundi, kwa niaba ya Mheshimiwa Daniel Tlemai Awack, kwamba, Serikali ilishafanya tathmini ya majengo na uchakavu wa Kituo cha Afya cha Oldeani, na tayari tumeanza kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa majengo ikiwemo Jengo la huduma ya kujifungulia.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2024/2025 jumla ya shilingi milioni 20 zimepelekwa kwa ajili ya ukarabati. Vilevile, mwaka ujao wa fedha, mapato ya ndani, shilingi milioni 28 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa jengo la upasuaji. Kwa hiyo, haya yanafanyika wakati Serikali Kuu ikiandaa fedha kwa ajili ya kwenda kufanya upanuzi na ukarabati mkubwa wa kituo hiki cha afya.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na hoja ya pili kuhusu Kituo cha Afya cha Nakatunguru katika Jimbo la Ukerewe, ni kweli kwamba, Serikali ilipeleka fedha mwaka 2012 na kituo cha afya kimejengwa na kimeanza kutoa huduma.

Mheshimiwa Spika, vituo hivi vya afya tunavijenga kwa awamu. Huu ujenzi ulikuwa ni wa awamu ya kwanza. Sasa tunakwenda kuandaa mpango kwa ajili ya ujenzi wa awamu ya pili ili kukamilisha majengo ambayo yamesalia. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mkundi kwamba Serikali inalitambua hilo na tayari imeweka mpango kwa ajili ya kwenda kumalizia majengo yaliyobaki katika awamu ya pili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, swali la nyongeza.

**MHE. TUMAINI B. MAGESA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Kituo cha Afya Chikobe kilijengwa mwaka 1976. Hali yake ya utendaji kwa sasa siyo bora tena. Je, ni lini Serikali itafanya uboreshaji ili kiweze kuwahudumia wananchi vizuri zaidi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Chikobe, kimewekwa kwenye Mpango wa Benki ya Dunia Awamu ya Pili, ambapo tunatarajia mwaka ujao wa fedha 2025/2026 tutapeleka fedha kwa ajili ya kuanza ukarabati na kuongeza majengo katika Kituo cha Afya cha Chikobe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene, sasa aulize swali lake.

Na. 586

**Zahanati Mpya Kutoa Huduma – Bukene**

**MHE. SELEMANI J. ZEDI** aliuliza: -

Je, lini Zahanati za Buhulyu, Mogwa, Mwanzilwo na Gulyambi - Bukene zitaanza kutoa huduma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kujenga vituo vya kutolea huduma na kuvisajili ili vianze kutoa huduma za afya. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 hadi 2024/2025 jumla ya zahanati 1,158 zimejengwa na kusajiliwa na zinatoa huduma.

Mheshimiwa Spika, Zahanati ya Buhulyu, Mogwa na Gulyambi zimekamilika, zimesajiliwa na zinatoa huduma. Aidha, Zahanati ya Mwanzwilo ujenzi umefikia hatua ya ukamilishaji 80% ambapo Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Nzega imetenga shilingi milioni 30 katika mwaka wa fedha 2025/2026 kwa ajili ya ukamilishaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, swali la nyongeza.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Zahanati za Buhulyu, Mogwa na Gulyambi zimekamilika na zinaanza kutoa huduma. Hata hivyo nimezitembelea hizi zahanati zote.

Mheshimiwa Spika, kuna changamoto kubwa kwamba zote hizi hazina bajeti yake ya dawa; na wanalazimika kuazima tu dawa chache kutoka zahanati za jirani. Wao kwanza hawana dawa za kutosha na zile zahanati za jirani wanazipunguzia dawa. Je, Serikali wana mpango gani, kwamba hizi zzhanati zinapoanza kutoa huduma ziwe zimekamilika na ziwe na bajeti yake yenyewe ya dawa badala ya kuanza kwa kuazima azima dawa chache kutoka zahanati za jirani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Katika ujenzi wa zahanati na vituo vya afya, kwa kawaida pale ambapo tunaweka maoteo ya ukamilishaji wa majengo hayo na kuanza kutoa huduma, halmashauri ina wajibu kupitia Mganga Mkuu wa Halmashauri, pamoja na Mganga Mkuu wa Mkoa kupeleka taarifa mapema Bohari kuu ya Dawa *(MSD)* ili iweze kuwekwa kwenye orodha ya vituo ambavyo vinahitaji kupata dawa mara baada ya kusajiliwa.

Mheshimiwa Spika, ikiwa imekamilika katikati ya mwaka wa fedha, mara nyingine inakuwa na changamoto ya kuingizwa kwenye mfumo wa dawa kwa sababu bajeti yake inaingizwa mwaka unaofuata wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, kwamba, tumefanya hivyo ili angalau wananchi katika maeneo haya waanze kupata za afya za msingi. Mwaka ujao wa fedha, kwa maana ya mwezi ujao Julai tutahakikisha kuwa zahanati hizi zinaingia kwenye bajeti, lakini pia zinaingia kwenye mfumo wa *MSD* ili zianze kupokea dawa hizo kwa mujibu wa taratibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Toufiq Salim Turky, Mbunge wa Mpendae, kwa niaba yake Mheshimiwa Shally Josepha Raymond.

Na. 587

**Kupandisha Hadhi Vituo vya Afya na Zahanati Nchini**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND K.n.y. MHE. TOUFIQ SALIM TURKY** aliuliza: -

Je, Serikali imejipangaje kutatua changamoto ya ucheleweshwaji wa kupandisha hadhi vituo vya afya na zahanati zinazookoa maisha ya wananchi nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kupandisha hadhi kituo cha kutolea huduma kutoka ngazi ya chini kwenda ngazi ya juu unazingatia miongozo na vigezo mbalimbali vya ngazi husika ya kituo. Miongoni mwa vigezo hivyo ni pamoja na uwepo wa eneo toshelezi kwa ngazi ya kituo, miundombinu, vifaatiba na watumishi.

Mheshimiwa Spika, katika kuharakisha taratibu za usajili na kupandisha hadhi vituo vya kutolea huduma za afya, Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeboresha utaratibu kwa kuanzisha mfumo wa kuwasilisha maombi kwa njia ya mtandao kutoka ngazi ya msingi hadi ngazi ya Wizara *(Health Facility Registration System)*.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu umewezesha kupunguza mlolongo wa kuwasilisha na kujibiwa kwa maombi ya usajili na upandishaji hadhi wa vituo vya afya kutoka siku 60 hapo awali hadi siku saba ikiwa kituo kinachopandishwa hadhi vimekidhi vigezo husika.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kupandisha hadhi vituo vya kutolea huduma za afya ambavyo vimekidhi vigezo katika ngazi ya afya ya msingi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; ili kituo cha afya au zahanati ikidhi kigezo cha kupandishwa hadhi ni pamoja na zahanati hiyo kuwa na miundombinu yote ya kupandishwa.

Mheshimiwa Spika, ninaishukuru sana Serikali kwa jinsi ambayo imetoa mwongozo. Je, ni lini Zahanati ya Rononi iliyopo

Uru Kaskazini itamalizika kwa kupata vyoo na samani ili iweze kuwa katika hali ya kuwa zahanati kwa hakika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, pamoja na zahanati hiyo kuna zahanati nyingine ya Fumbuni ambayo kwa kweli tangu imejengwa miundombinu yote imechakaa na haiwezi tena kuwa katika hali nzuri. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kufuatana na mimi tukimaliza Bunge hili ili akatutatulie matatizo hayo katika eneo letu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza, ninaomba nimhakikishie mama yangu Mheshimiwa Shally Raymond kwamba, Serikali inatambua kwamba zahanati hiyo ambayo ipo Uru Kaskazini ya Runoni haijakamilika na inahitaji kukamilisha miundombinu na vifaatiba.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie kwamba, kupitia halmashauri pamoja na fedha ya Serikali Kuu, tutaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba zahanati hiyo inakamilika mapema na inaanza kutoa huduma zote muhimu kwa ngazi ya zahanati.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, hoja hiyo tumeichukua na mara baada ya kutoka hapa nitawasiliana na Mkoa wa Kilimanjaro ili tuweze kuweka utaratibu na kujua gharama inayohitajika kwa ajili ya ukamilishaji wa zahanati hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa swali la pili, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, zipo zahanati ambazo ni kweli ni chakavu, kongwe na za siku nyingi. Tumeainisha zahanati zote chakavu na vituo vya afya vyote chakavu. Tunakamilisha ukarabati wa Hospitali za Halmashauri 50 kongwe na chakavu; na mara baada ya ukamilishaji huo, tutaanza ukarabati wa vituo vya afya na zahanati zote kongwe, na zahanati hiyo tutaipatia kipaumbele.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Kilimanjaro, naona wote mmesimama leo. Mheshimiwa Priscus Tarimo, swali la nyongeza.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana. Ninaomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri, zahanati ya Kiboriloni ndiyo tuliyoichagua kama Kituo cha Afya cha Kimkakati. Je, ni lini fedha zitakwenda kwa ajili ajili ya Kituo hicho cha Afya cha Kiboriloni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ni kweli Mheshimiwa Mbunge alishawasilisha Kata ya Kiboriloni katika Zahanati ya Kiboriloni kuwa ni kata ya kimkakati kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya. Tayari Mheshimiwa Rais ameshatenga fedha ya dharura shilingi bilioni 53,500. Tayari shilingi bilioni 30 zimeshatolewa kwa ajili ya majimbo 120 ya awali na zipo katika halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutahakikisha pia tunapeleka fedha hizo kwa ajili ya kwenda kujenga Kituo cha Afya Kiboriloni ili tusogeze huduma za ngazi ya kituo cha afya kwa wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ardhi katika Jimbo la Vunjo ni ghali sana na ni adimu sana. Je, ni lini Serikali itatoa mwongozo wa kuruhusu kujenga vituo vya afya kwa mfumo wa ghorofa kwenye maeneo ambayo ardhi ni adimu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba yapo baadhi ya maeneo hususan ya miji na majiji ambayo ardhi ni finyu, pia ni ya ghali zaidi. Tayari

ilishatoa mwongozo na michoro kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya kwa utaratibu wa maghorofa; na tayari imeshajengwa katika maeneo mbalimbali. Ukienda Dar es Salaam, Mbeya na maeneo mengine ya Arusha na kadhalika, tunajenga vituo vya afya, hospitali na mara nyingine hata zahanati katika mfumo wa maghorofa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, kwamba tupate tu maombi kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Moshi, kwamba eneo hilo linahitaji kujengwa kituo cha afya kwa mfumo wa ghorofa ili tuweze kuipitia michoro, kukubaliana na tuanze kujenga fedha kwa awamu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba kituo hicho cha afya kinajengwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, Zahanati ya Shirimgungani, Kata ya Mnadani tuliomba kupandishwa hadhi kuwa kituo cha afya. Je, Serikali ina mpango gani wa kuipandisha hadhi ikizingatia Kata ya Mgungani haina kituo cha afya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka utaratibu kwa halmashauri husika kutuma maombi ya kupandisha hadhi zahanati kuwa kituo cha afya. Utaratibu huo sasa umeboreshwa zaidi tofauti na siku za nyuma ambazo walikuwa wanalazima kuandika barua kuja kwa Katibu Mkuu, TAMISEMI kwa ajili ya maombi hayo, ambapo ilikuwa inachukua muda mrefu hadi siku 60.

Mheshimiwa Spika, sasa tuna mfumo ambao ni wa kidigitali *(Health Facilities Registration System)* ambayo inawezesha Halmashauri kutuma maombi yao *online*. Timu ya ukaguzi kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kushirikiana na mkoa kufanya ukaguzi wa majengo katika zahanati ile, eneo na idadi ya wananchi ambao wanatarajiwa kuhudumiwa ili kama inakidhi vigezo tuweze kuipandisha hadhi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba kumwambia Mheshimiwa Saashisha, kwamba jambo hili tumelichukua Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tutafuatilia na tuone kama inakidhi vigezo ili tuweze kuanza utaratibu wa kuipandisha hadhi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, Mbunge wa Bunda Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 588

**Ujenzi wa Kituo cha Zimamoto – Bunda**

**MHE. ROBERT C. MABOTO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Zimamoto katika Halmashauri ya Mji wa Bunda?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa niaba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na jitihada za kusogeza huduma za zimamoto na uokoaji karibu na wananchi kwa kujenga vituo vya zimamoto na uokoaji. Aidha, katika mwaka 2025/2026 Serikali kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji imetenga fedha kiasi cha shilingi milioni 400 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Zimamoto na Uokoaji katika Halmashauri ya Mji wa Bunda.

**SPIKA:** Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, swali la nyongeza.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi. Nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Mji wa Bunda au Wilaya ya Bunda ina zaidi ya majimbo matatu ya uchaguzi na ina idadi kubwa sana ya watu. Je, Serikali katika mpango iliyonao katika orodha ya magari ambayo ilisema inayaleta kwa ajili ya zimamoto, Halmashauri ya Mji wa Bunda kwenye orodha hiyo imo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kama ulivyotolewa mwongozo wa orodha ya magari yatakayosambazwa kwenye halmashauri, ninao uhakika Bunda ni moja kati ya Halmashauri zitakazopata magari.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, Mbunge wa Kishapu, sasa aulize swali lake.

Na. 589

**Ujenzi wa Barabara ya Kolandoto – Kishapu hadi Mwangongo**

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatangaza *tender* ya ujenzi wa Km 20 kwa kiwango cha lami Barabara ya Kolandoto - Kishapu hadi Mwangongo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Mhandisi Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya Kolandoto – Kishapu hadi Mwangongo yenye urefu wa kilometa 52.79 unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Hadi sasa jumla ya kilometa 2.58 zimejengwa kwa kiwango cha lami katika Mji wa Mhunze (Kishapu). Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu iliyobaki, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza, napongeza kwa majibu haya ya Serikali, lakini ninataka niseme yamekuwa ni majibu ya matumaini tu kila wakati. Ahadi ya mwaka huu wa fedha (mwaka 2025/2026) ilikuwa ni kutekeleza kilometa 20 za kiwango cha lami kati ya kilometa 52. Serikali ilifikia hatua ya kutangaza *tender,* lakini haijatangaza tatizo ni nini ama changamoto ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa mwaka mzima barabara hii tumekuwa tukitumia shilingi milioni 850 kwa ajili ya matengenezo ya kawaida, gharama ambayo ni kubwa sana. Sasa Serikali haioni kwamba ni wakati wa kutekeleza mradi huu katika kiwango cha lami ili kupunguza gharama kwa Serikali? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyosema tulikuwa tumepanga tuanze kuijenga hiyo barabara na taratibu zote zilikuwa zimekamilika na mpaka tunamaliza mwaka hatujaanza kuijenga, na ndiyo maana hata katika mwaka wa fedha unaokuja tumepanga barabara hii tuanze kuijenga kwa kiwango cha lami ambayo ninaamini tutaitangaza yote, japo tutaanza kujenga pia kulingana na upatikanaji wa fedha kama nilivyosema.

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba nia ya Serikali ni kujenga barabara nyingi na hasa mojawapo hiyo ambayo ni barabara kuu kwa kiwango cha lami barabara zote zile kuu. Ndiyo maana mpaka sasa hivi tunaendelea, jitihada za Serikali ni kuzijenga barabara zote hizo lakini kabla hatujazijenga lazima tuendelee kuzikarabati hata kama ni kwa gharama ili ziweze kutoa huduma kwa wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

WAheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki, Mbunge wa Tarime Mjini, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa…

**SPIKA:** Mheshimiwa ngoja kwanza, Mheshimiwa Maboto, si umetoka kuuliza swali moja? Ninaona kuna Mbunge mwingine amesimama huku, labda kama wewe ndio una majibu! Basi atauliza huyu kwa niaba yake; Mbunge mwingine ambaye hajapata nafasi ya kuuliza kabisa. Mheshimiwa Janejelly Ntate, kwa niaba ya Mheshimiwa Michael.

Na. 590

**Masharti Kandamizi kwa Wawekezaji wa Ndani**

**MHE. JANEJELLY J. NTATE K.n.y. MHE. MICHAEL M. KEMBAKI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua masharti kandamizi kwa wawekezaji wa ndani kama kukadiria na kulipa kodi kabla ya kuanza biashara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Hamad Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupita Bunge lako Tukufu, ilifanya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi *(Tax Administration Act, 2015)* Kifungu cha 22, ili kuahirisha wajibu wa kulipa kodi ya awamu chini ya Sheria ya Kodi ya Mapato kwa kipindi cha miezi sita tangu tarehe ambayo Nambari ya Utambulisho ya Mlipaji *(TIN)* ilipotolewa kwa mtu yeyote anayesajiliwa na kupewa *TIN* kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, kwa mabadiliko haya, mfanyabiashara aliyesajiliwa kwa mara kwanza atalipa jumla ya kodi aliyoahirishiwa baada ya miezi sita kwa awamu tatu. Lengo la mabadiliko haya ya sheria ni kuweka mazingira wezeshi kwa wafanyabiashara na wawekezaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Janejelly Ntate, swali la nyongeza.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali na kuweka hiyo sheria, lakini swali la kwanza, hiyo sheria bado haijaanza kutekelezwa kwa wafanyabiashara, na bado haiendi kama inavyosema, miezi sita wanalipishwa kabla ya miezi sita.

Mheshimiwa Spika, pili, mwekezaji wa nje anapewa miaka mitano, na Mtanzania anapewa miezi sita, kutakuwa na ushindani wa uwiano? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, swali lake la kwanza nitoe maelekezo kwa Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania wahakikishie kwamba watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania wanafuata taratibu na sheria ambayo imewekwa. Mtu anatakiwa alipe baada ya miezi sita tangu amepewa *TIN*.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, tofauti hii ambayo amezungumza, naomba tuichukue twende tukaifanyie kazi. Ushauri wake tutaenda kuuweka vizuri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, swali la nyongeza.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Tumekuwa na maswali mbalimbali kwa kuhusiana na kigezo hiki cha wananchi kuchajiwa kodi kabla ya kuanza biashara na maafisa wetu wa kodi kukiuka kigezo hiki cha sheria cha kukusanya kodi kabla ya miezi sita; na Mheshimiwa Waziri amekuwa akitoa majibu haya, na kutoa maelekezo haya kwa watu wa *TRA* ili kuhakikisha sheria hii inafuatwa na kutekelezwa kama ilivyo. Sasa maelekezo haya yamekuwa hayafanyiwi kazi. Nini kauli ya Serikali juu ya maafisa ambao wanaendelea kukiuka maelekezo ya Serikali katika kifungu hiki hata baada ya maelekezo kuwa yanatolewa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kama nimejibu suala hili, lakini kwa nyongeza haigombi. Tunasema kwamba wale ambao hawatafuata sheria na taratibu, basi Sheria ya Kiutumishi itachukua mkondo wake. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Lugangira, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, katika muktadha huu huu wa kulinda na kuinua wawekezaji wa ndani, je, Serikali haioni iko haja ya kubadilisha sheria na kuona namna ambavyo itaweza kuwapatia wajasiriamali wadogo hususan vijana na wanawake ile likizo ya kutolipa kodi kama ambavyo wawekezaji wa nje wanapata ili waweze kurasimisha biashara zao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ushauri wake tumeupokea na tunaenda kuufanyia kazi. Tukiona ipo haja na tija ya kufanya hivyo, tutaleta Muswada huo katika Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kupitisha sheria hiyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, sharti hili ambalo linawabana wafanyabiashara kulipa kodi kabla hawajaanza kufanya biashara, kwa kweli ni mojawapo ya vigezo ambavyo vinafanya wafanyabiashara wengi washindwe kufanya biashara. Je, kwa nini Serikali isiondoe sharti hili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka sheria ambayo Bunge lako Tukufu limepitisha sheria hiyo. Kwa hiyo, cha msingi hapa ni kuhakikisha kwamba watumishi wetu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania na taasisi nyingine kufuata sheria na taratibu ambazo zimewekwa na Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Said Issa, Mbunge wa Konde, sasa aulize swali lake.

Na. 591

***Mfumo wa Kuchakata Kodi ya Forodha (Single Window)***

**MHE. MOHAMED SAID ISSA** aliuliza: -

Je, changamoto zipi zinazorotesha ukusanyaji wa mapato katika mfumo mpya wa kuchakata Kodi ya Forodha ambao ni "*single window*"?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, *single window* ni dirisha moja la kufanikisha uwasilishaji wa nyaraka mbalimbali kutoka kwa wadau wote muhimu katika mnyororo wa ugomboaji mizigo ya forodha.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa kabla ya Mfumo wa *Single Window,* mteja alilazimika kuwasilisha nyaraka na vielelezo

mbalimbali kwenda kila idara ya Serikali inayohusika katika mnyororo wa ugomboaji wa mizigo, na hivyo kusababisha usumbufu mkubwa na kuchelewesha ugomboaji wa mizigo forodhani.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutoa hofu kuwa *single window* haitaweza kupelekea uzoroteshaji wa ukusanyaji mapato ya Serikali bali utasaidia kuondoa usumbufu kwa wateja na kurahisisha ukokotoaji wa kodi mbalimbali kupitia Mfumo wa *TANCIS* uliohuishwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Said Issa, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, ninaipongeza Serikali kupitia *TRA* kwa kupunguza changamoto nyingi za mfumo huu. Wakati ninauliza swali hili kulikuwa na changamoto nyingi ambazo zilikuwa zinawafanya watu kuchukua hadi wiki tatu kutoa mizigo bandarini, sasa hivi imeboreshwa. Sasa nina maswali yangu mawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, mifumo hii imekuwa ikibadilika mara kwa mara. Tulianza na mfumo ambao siyo rasmi ambao ulikuwa ni kujaza *data* tu kwenye mfumo, lakini tukaja na mfumo wa pili uliokuwa unaitwa *ASYCUDA* ukabadilishwa tukaja na mfumo wa tatu ambao ulikuwa unaitwa *TANCIS* ambao ndiyo uko sasa, nao unabadilika maana yake baadaye uliitwa *TASUS* ambao ni huu Mheshimiwa Waziri amesema unakuwa ukiboreshwa na sasa hivi unaitwa *TANESW*. Maana yake, kila siku mifumo hii inabadilika.

Mheshimiwa Spika, sasa wakati wa kubadilika inakuwa inaleta changamoto katika utoaji wa mazigo bandarini. Je, ni kwa sababu gani inakuwa inabadilika mara kwa mara? Je, wataalamu wetu hawafanyi utafiti wa kutosha katika kuhakikisha tunakuwa na mifumo bora na imara?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwamba kwa upande wa Zanzibar imekuwa tunapofanya *document* kwa ajili ya kutoa mizigo ya forodha tunakuwa na changamoto kwamba bila

kujaza mkoa ambao unatoka Tanzania Bara huwezi kuendelea na *procedure*. Maana yake huwezi kusema nipo Malindi, huwezi kusema niko Darajani, huwezi kusema niko Zanzibar; unapaswa useme niko Kariakoo, niko Arusha, niko wapi; je, ni kwa nini, Zanzibar haitambuliki katika mfumo huo? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kwanza tunapokea pongezi zake kwa Serikali. Ni ukweli alichokisema kwamba changamoto zilikuwa nyingi, lakini baada ya mfumo huu, changamoto karibu 95% zimeondoka.

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kupitia *TRA* inafanya tafiti za kila siku za mara kwa mara na kufuatilia mwenendo wa mfumo huu. Kwa hiyo, hapa Serikali iko makini sana, na nikutoe hofu kabisa kwamba hayo yaliyotokea nyuma hayatatokea tena kwa tafiti ambazo tuko nazo. Pia, Serikali imeunda timu maalumu, tuna tume maalumu ambayo inafuatilia masuala ya mfumo na iko vizuri kabisa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili ambalo amelisema, tayari tumeanza kufuatilia changamoto hii, na nitoe maelekezo kwa Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania afuatilie kwa karibu sana. Kama bado inajitokeza changamoto hii, basi twende kuifanyia kazi na kuitatua kwa haraka ili kuondoa usumbufu kwa wafanyabiashara wa pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaenda kwenye Wizara ya Viwanda na Biashara, ninaahirisha shughuli za Bunge kwa dakika mbili, nina dharura kidogo.

*(Saa 4.01 Asubuhi Bunge Lilisitishwa kwa Dharura)*

*(Saa 4.02 Asubuhi Bunge lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 592

**Wanawake Kutumia Teknolojia ya Habari Katika Biashara**

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA** aliuliza: -

Je, Serikali ina Sera za kuwawezesha wanawake wajasiriamali kutumia teknolojia ya habari kuongeza ufanisi wa biashara zao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa niaba ya Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Patrobass Katambi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI) K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia mamlaka zake ina sera mbalimbali za kuwawezesha wananchi wakiwemo wajasiliamali wanawake kutumia teknolojia ya habari ili kuongeza ufanisi wa shughuli zao ikiwemo biashara. Sera hizo ni pamoja na Sera ya Taifa ya Biashara ya Mwaka 2003 Toleo la 2023, Sera ya Taifa ya Posta ya Mwaka 2003, Sera ya Taifa ya Mawasiliano ya Mwaka 1997 na Sera ya Taifa ya TEHAMA ya Mwaka 2016 ambazo zinatambua Biashara Mtandao inayowezeshwa na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa kutambua uwepo wa changamoto za Teknolojia ya Habari katika kufanya biashara,

Serikali imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa Biashara Mtandao *(National Electronic Commerce Strategy)* ili kuwawezesha wajasiriamali wakiwemo wanawake kufanya biashara mtandaoni. Ninakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, swali la nyongeza.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa majibu mazuri ya Serikali lakini nilikuwa na swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni kwa namna gani Serikali inashirikiana na sekta binafsi ili kuhakikisha wanawake wajasiriamali wanapata vifaa na mafunzo ya TEHAMA ili waweze kushiriki kikamilifu katika uchumi wa kidigiti? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI) K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mahawanga, ni kwamba Serikali tayari imeshaanza utaratibu wa kuhakikisha kwanza inashirikiana na sekta binafsi kupitia Mabaraza ya Biashara yaliyoko nchini kote katika mikoa, lakini pia Baraza la Biashara la Wilaya na ngazi hizo zinaratibiwa kupitia halmashauri pamoja na Baraza la Taifa la Biashara.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, upo mpango mwingine wa Serikali kupitia Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, vyote kwa pamoja vinafanya kazi kwanza ya kuwatambua wafanyabiashara, na pili kuwaratibu na kuwasajili, na hatua ya tatu, wanafanya mafunzo kwenye maeneo haya ya biashara, na ni biashara zote za wajasiriamali katika nafasi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, upo mkakati mzuri ambao umeanzishwa hivi karibuni kupitia agizo la Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Waziri wa Viwanda

na Biashara ambao unaitwa MKUMBI kama Mkakati wa Kuboresha Mazingira ya Biashara.

Mheshimiwa Spika, tayari wameshaanza kuangalia namna gani wanaweza kuboresha mazingira ya biashara ikiwemo hii ya mtandao na kupitia Sera ya Biashara Toleo la Mwaka 2023 ambayo inahusiana na masuala ya kuboresha biashara za mtandaoni.

Mheshimiwa Spika, pia, utoaji wa anwani za makazi kulingana na sera ya posta, zote hizi zimekuwa zikitumika kuweza kusaidia hawa wajasiriamali wadogo wadogo waweze kupata uratibu huo. Wanapata mawasiliano mazuri zaidi kupia Wizara ya Mawasiliano ambapo kwa Mfuko wa *UCSAF* wameanza kutoa kompyuta kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo shule na kuwaanda wafanyabiashara kupitia elimu ya TEHAMA. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema ulishauliza swali. Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo sasa aulize swali lake.

Na. 593

**Geti la Kuingia Hifadhi ya Mto Ugala – Urambo**

**MHE. MARGARET S. SITTA** aliuliza: -

Je, lini Geti la kuingilia Watalii Hifadhi ya Mto Ugala Wilaya ya Urambo litawekwa?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa niaba ya Wizara ya Maliasili na Utalii Mheshimiwa Pinda, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa Hifadhi ya Taifa ya Mto Ugala inakuwa miongoni mwa Hifadhi bora nchini, Serikali imepanga kuiendeleza Hifadhi hiyo kwa awamu ambapo katika awamu ya kwanza Serikali imetumia shilingi 2,000,000,000.00 kuboresha miundombinu muhimu ya Hifadhi ikiwemo ujenzi wa mtandao wa barabara hifadhini, ujenzi wa jengo la utawala, nyumba za watumishi, vituo vya askari, visima vya maji na maeneo ya kupumzika wageni.

Mheshimiwa Spika, mara baada ya kukamilika kwa awamu hii, Serikali itajielekeza kwenye kujenga malango manne ambayo ni Lunyeta, Lumbe, Iluma na Izengabatogilwe kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, swali la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nilikuwa na swali moja la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa eneo kubwa la hifadhi ambalo linatumika na watalii lipo upande wa Usoke, je, ni lini Serikali itajenga barabara nzuri ili kuwezesha watalii waingie kwenye hifadhi kwa kupitia Usoke? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, tunaiendeleza mbuga hii kwa awamu, na awamu ya kwanza zimetolewa shilingi bilioni mbili ambazo kama nilivyojieleza zinaendelea kuchakata kwenye maeneo haya ya maboresho ya hifadhi yetu.

Mheshimiwa Spika, kutegemeana na fedha zitakavyoendelea kupatikana kwa awamu ya pili inayokuja, jambo la Mheshimiwa Mbunge litachukuliwa umuhimu wa kipekee kuona kwamba lango la Usoke linafunguliwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maji, Mheshimiwa Katani Ahmed Katani, Mbunge wa Tandahimba swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota.

Na. 594

**Miradi ya Maji Kutokamilika kwa Muda Mrefu**

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA K.n.y. MHE. KATANI A. KATANI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itawalipa Wakandarasi wa Miradi ya Maji fedha zao kutokana na miradi mingi kutokamilika kwa kukosa malipo kwa wakati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi kwa niaba ya Wizara ya Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI K.n.y. NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kulipa madeni ya wakandarasi, wataalam washauri na watoa huduma mbalimbali wanaotekeleza au kutoa huduma kwenye ujenzi wa miradi ya maji nchini ikiwemo Wilaya ya Tandahimba. Hadi kufikia mwezi Mei, 2025, jumla ya shilingi 2,548,920,536.19 kati ya shilingi 3,999,970,936.19 za madai ya wakandarasi na watoa huduma wanaotekeleza miradi mbalimbali ya maji Wilayani Tandahimba zimelipwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itaendelea kulipa madai yote ya wakandarasi, wataalam washauri na watoa huduma wa miradi ya maji nchini kadri fedha zinavyopatikana ili miradi hiyo iweze kukamilika kwa wakati na kuanza kutoa huduma iliyokusudiwa kwa wananchi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na kwamba Serikali inatafuta fedha kumalizana na wakandarasi, lakini kuna wakandarasi wawili; mmoja anajenga mradi wa Makonde ambao unahudumia halmashauri nne; Newala Mjini, Newala Vijijini, Tandahimba na Nanyamba, yeye ana madai ya muda mrefu na bado hayajashughulikiwa na mkandarasi ambaye anaboresha mradi wa Mnyawi kwenda Nanyamba na yeye ana madai ya muda mrefu.

Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kuwalipa wakandarasi hawa ili waendelee na kazi yao ya kutekeleza miradi na hatimaye wananchi wapate maji ambayo ni shida yao ya siku nyingi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, tunakiri kwamba wakandarasi hao wawili ni wakandarasi ambao wamefanya kazi nzuri sana. Nimwahidi Mheshimiwa Mbunge na hao wakandarasi pamoja na wananchi ambao watapata hiyo huduma kwamba Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba tunapoanza tu muhula wa kwanza, kwa maana ya *quarter* ya kwanza ya mwaka wa bajeti, wakandarasi hao watalipwa fedha yao, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kavejuru Felix, swali la nyongeza.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Spika, kule Buhigwe tuna mradi wa vijiji nane ambao unatekelezwa na mzabuni Rukolo, muda wa ukamilishaji wa mradi huo umeshapita na mkandarasi huyo bado anadai fedha nyingi zaidi ya shilingi bilioni mbili na mradi umesimama. Lini atalipwa fedha zake ili akamilishe huo mradi kwa sababu muda wa ukamilishaji wa mradi huu umeshapita?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kama nilivyojibu katika jibu la

msingi, tunatambua kazi nzuri ambayo amefanya huyo mkandarasi na Serikali ilishapokea hati yake ya madai kuhakikisha kwamba analipwa. Pia nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaandaa malipo ili aweze kumlipa mkandarasi na aweze kukamilisha hiyo kazi ambayo bado haijakamilika hadi mwisho.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge wa Buyungu sasa aulize swali lake.

Na. 595

**Wakala wa Mamlaka ya Maji Mjini – Kakonko**

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA** aliuliza: -

Je, lini Wilaya ya Kakonko itakuwa na Wakala wa Mamlaka ya Maji Mjini katika Mji wa Kakonko?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma ya majisafi na salama kwa wananchi, Serikali imeanzisha Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kakonko *(KAUWASA)* ambayo inahudumia Kata tano za Kakonko, Kasuga, Kanyonza, Kiziguzigu na Kasanda. Usimamizi wa utoaji huduma chini ya Mamlaka hiyo ulianza rasmi mwezi Septemba, 2024.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, swali la nyongeza.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi, aidha nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali. *KAUWASA* kwa maana ya Mamlaka ya Maji katika Mji wa Kakonko unahudumia Kata za Kanyonza, Kasuga, Kiziguzigu, Kasanda na Kakonko. Vyanzo vya maji ambavyo vinahudumia Mji wa Kakonko ni chanzo cha kutoka Kijiji cha Kasuga na chanzo cha Maji cha Kijiji cha Nyakayenzi.

Mheshimiwa Spika, katika vyanzo hivyo viwili, kinachofanya kazi ni chanzo cha maji cha Kasuga, lakini chanzo cha maji cha Nyakayenzi hakifanyi kazi pamoja na kwamba Serikali ilishapeleka fedha zaidi ya shilingi bilioni 2,800, kwa ambacho kinazungumzwa kwamba ni changamoto katika usanifu lakini na ujenzi. Nini kauli ya Serikali kuhakikisha kwamba mradi huo sasa unaokolewa ili uweze kufanya kazi uliyokusudiwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, upo mradi wa maji wa Kijiji cha Kabale ambapo zaidi ya shilingi milioni 803 zimepelekwa pale, zilikusudiwa kupelekwa pale, lakini shilingi milioni 300 zimeshapelekwa, mradi haujakamilika tangu mwaka 2024 mwezi wa 12 ujenzi umesimama. Nini kauli ya Serikali kuonesha kwamba mradi sasa unaokolewa na unafanya kazi kama ambavyo ilikusudiwa tangu mwanzo? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ninakiri tu kwamba Mheshimiwa Mbunge pamoja na kuuliza hili swali hapa lakini pia amefika ofisi za maji kufuatilia changamoto za mradi huu, nami kwenye swali lake la kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya kupokea hayo malalamiko, Wizara ya Maji imeshaandaa wataalam ambao watakwenda Wilaya ya Kakonko kwenda kuangalia changamoto na kufanya tathmini na waweze kushauri Serikali hatua za kufanya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kabla ya mwezi Julai wataalam hawa watakuwa wamefika katika Wilaya ya Kakonko ili kufanya hiyo tathmini na kushauri Serikali hatua za kufanya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hiki chanzo cha maji katika Kijiji cha Kabale ambacho bado hatujakamilisha kupeleka fedha, Serikali imepanga katika muhula wa kwanza wa mwaka wa bajeti, fedha zitapelekwa ili mradi huo uweze kukamilishwa ambao ulikuwa umesimama.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Kilimo,

Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 596

**Changamoto za Ununuzi wa Mbegu za Ruzuku**

**MHE. CECILIA D. PARESSO** aliuliza: -

Je, Serikali imejipangaje kutatua changamoto zilizojitokeza wakati wa ununuzi wa mbegu za ruzuku kwa wakulima nchini?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, usambazaji wa mbegu za mahindi kwa mpango wa ruzuku ulianza msimu wa 2024/2025. Katika utekelezaji wa mpango huo, Serikali imebaini changamoto mbalimbali ikiwemo wakulima kukosa namba ya usajili ya ruzuku; bei elekezi ya ruzuku kushindwa kutekelezwa kwa wauzaji wadogo walioko katika ngazi za kata na vijiji; baadhi ya mawakala na makampuni ya mbegu wasio waaminifu kuuza mbegu nje ya mfumo wa ruzuku; na idadi ndogo ya wauzaji wa mbegu hususan katika ngazi za kata na vijiji.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kuchukua hatua mbalimbali ili kukabiliana na changamoto hizo kwa ajili ya msimu wa 2025/2026. Hatua hizo ni kuhakikisha wakulima wa zao la mahindi wanasajiliwa kwa wakati katika mfumo wa pembejeo za kilimo; kutoa elimu kwa umma kuhusu utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbegu za mahindi; kufanya mapitio ya bei elekezi ya mbegu inayotumika ili kuwezesha mawakala wadogo kuingizwa kwenye mfumo wa ruzuku; kuchukua hatua kali kwa mawakala wa mbegu watakaouza mbegu za mahindi bila kufuata bei elekezi ya ruzuku; na kuzielekeza Kampuni za mbegu kuongeza idadi ya mawakala wa mbegu wanaosambaza mbegu za ruzuku hususan vijijini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, niipongeze Serikali kwa utaratibu huu mpya wa kutoa ruzuku kwa mbegu za mahindi.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Changamoto nyingine ambayo wanakutana nayo wananchi ni pale wanapoenda kwa mawakala kunapewa mbegu iliyopo na siyo mbegu wanayoihitaji. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba aina zote za mbegu kulingana na uhitaji inapatikana pindi ambapo mkulima anaenda?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kampuni za mbegu zimekuwa na masharti magumu hivyo kuwafanya mawakala kushindwa kukidhi yale masharti kiasi kwamba inasababisha idadi ya mawakala kwenye wilaya zetu kuwa wachache kulingana na hayo masharti. Je, Serikali haioni ipo haja sasa kuangalia haya masharti yanayowekwa na makampuni makubwa ili kuyapunguza na kuwawezesha mawakala wengi waingie kusambaza mbegu hizi ili kuhakikisha upatikanaji wa mbegu mpaka maeneo ya vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nami nimpongeze Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso kwa kufuatilia jambo hili kuhusiana na masuala ya mbegu. Pia nimthibitishie tu kwamba moja ya maelekezo ambayo Wizara tumeyatoa kwa mawakala ni kuhakikisha katika vituo vyao kunakuwa na mbegu za aina zote ili mkulima anapohitaji mbegu hiyo aweze kupatiwa ile ambayo inatokana na aina za mbegu ambazo zinapatikana katika eneo lake. Kwa hiyo, hilo ni eneo ambalo maelekezo tuliyatoa na tumeshawaelekeza *TOSCI* kufuatilia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masharti, ndiyo maana katika jibu la msingi utaona nimejibu hapo kwamba moja ya maelekezo ambayo tumeyapa makampuni ni kuhakikisha yanaongeza idadi

ya mawakala. Kwa hiyo, makampuni yenyewe, cha kwanza wanapaswa kuwa na mawakala wao katika maeneo mbalimbali ili lile suala la kwamba sijui hujatimiza vigezo na nini, tuweze kuliondoa. Kwa hiyo, jambo hilo tumeshawaelekeza, lakini vilevile waweze kuwachunguza wale mawakala wapya ambao wanatosha na wana vigezo kwa ajili ya kusambaza mbegu hii. Kwa hiyo, hayo ni sehemu ya maelekezo na tumeshayatoa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Serikali kwa kutupatia ruzuku ya mbegu ya ngano kwa wananchi kwa Jimbo la Makete. Swali langu, wananchi hawa wamekuwa wakilima na mliwahakikishia kwamba somo litakuwepo, lakini wanunuzi wamekuwa wakinunua ngano na hawalipi kwa wakati. Ni ipi kauli ya Serikali ili wananchi wetu waweze kulipwa hasa wa Kata ya Kigala, Lupila na Ikuwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Festo Sanga kwa kazi nzuri anayofanya katika Jimbo lake la Makete, na ninajua moja ya watu ambao wamefanya kazi kubwa katika mpango huu wa ruzuku ya ngano ni pamoja na Mheshimiwa Festo. Nimthibitishie tu kwamba maelekezo ambayo Mheshimiwa Waziri ameyatoa wiki iliyopita, ni makampuni yote ambayo yanahitaji kuagiza ngano kutoka nje ya nchi, moja ya sharti la kwanza ni kuhakikisha wananunua ngano ya ndani ya nchi na kulipa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi tutaenda kuongeza usimamizi na ufuatiliaji ili wananchi wake walipwe kwa wakati. Kwa hiyo, jambo hilo tunaomba tulipokee na tukalifanyie kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Tunaishukuru sana Serikali kwa kuwapatia wakulima wa Jimbo la Moshi Vijijini miche bora ya kahawa kwa

kuwapa bure. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia wakulima hawa wapate viuatilifu bure au kwa bei ya ruzuku kwa sababu kuna uharibifu mkubwa sana unaotokana na wadudu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ninampongeza vilevile Prof. Ndakidemi ambaye amefanya kazi nzuri sana pale Moshi Vijijini na kufuatilia zao la kahawa. Nami ni moja ya watu ambao nilishiriki pamoja naye kugawa bure miche ya kahawa kwa mfumo wa ruzuku.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimthibitishie tu kwamba kwenye upande wa viuatilifu kama ambavyo tunafanya katika korosho, vilevile tutafanya katika kahawa kwa sababu mpango wa sasa ni kuhakikisha tunawawezesha wakulima kupunguza gharama za uzalishaji katika mazao yote ya kimsimu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumekuwa tukienda kwa awamu, tunatoka kwenye korosho tunakwenda kwenye kahawa na tutakwenda katika mazao mengine. Kwa hiyo, lipo katika sehemu ya mipango ya Serikali, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendela na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda Mbunge wa Viti Maalum, umeshauliza swali lako, kwa hiyo, naangalia ambaye hajauliza swali leo. Haya jamani, naambiwa yeye ndiye ana majibu yake Mheshimiwa Mbunge. Mheshimiwa Cecilia Paresso.

Na. 597

**Hitaji la Ardhi ya Mwekezaji wa Chai Rungwe**

**MHE. CECILIA D. PARESSO K.n.y. MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itamwomba Mwekezaji wa Chai Rungwe kuachia ardhi ambayo haitumii kwa wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Pinda, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Shamba la Chai Rungwe lipo Kata ya Ilima na Bujela na linamilikiwa na Kampuni ya *Mohamed Enterprises*. Kwa kuwa shamba hili linamilikiwa kisheria na mwekezaji ambaye tayari ameliendeleza kwa kulima zao la chai, na kwa kuzingatia umuhimu wa sekta ya kilimo hususan uhitaji wa uwekezaji katika zao la chai, Serikali itahakikisha shamba hili linatumika ipasavyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Ninaomba kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu haya ya Serikali, Mheshimiwa Mbunge pia alipenda kufahamu kwamba, ingawa eneo linatumika, bado kuna uhitaji wa wananchi wengine kupata eneo hilo. Hata hivyo, kuna sheria inayoruhusu, je, Serikali haioni sasa ni wakati mwafaka wa kufikiria kuligawanya kwa wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, shamba hili linamilikiwa kihalali kabisa na *Mohamed Enterprises* na hakuna taarifa rasmi kuwepo kwa maeneo ambayo yanaweza yakapunguzwa kutoka kwa mmliki. Labda tulichukuwe kwa ajili ya kwenda kulifanyia kazi na kuona maeneo hayo ambayo wananchi wanaweza wakapewa. Lakini vinginevyo lipo kwenye miliki halali kabisa ya *Mohamed Enterprises*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa Mkoa wa Njombe na Mkoa wa Iringa, Kijiji cha Nyigu ambacho kipo Wilaya ya Mufindi, *GN* ya Kijiji cha Nyigu inaonesha iko katika Mkoa wa Njombe. Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kuja ili kuwaunganisha viongozi wa mikoa wote wawili ili aoneshe *GN* ya kijiji hicho kimilikiwe na Njombe kama ilivyo kwenye *GN*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Tumelichukua jambo la Mheshimiwa Mbunge, na tuwaelekeze Kamishna wa Ardhi wa Taifa apange timu ya kwenda pale kwenye mipaka ya Iringa na Njombe ili kwenda kuiweka sawa hali hiyo ili kumaliza utata uliopo katika ya mikoa hii miwili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Kakunda, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Katika Wilaya ya Sikonge, kwa mujibu wa bajeti ambayo tunayo sasa hivi tunaendelea nayo, Serikali ilikuwa imeleta hapa Bungeni maombi tupitishe bajeti ya kupima vijiji vyote 65 vilivyokuwa vimebaki, lakini mpaka sasa hivi fedha iliyotolewa ni ya kupima vijiji 16 tu na bado wiki mbili ili Bunge livunjwe. Je, tuna uhakika wa kupata hiyo fedha kweli ya kupima vijiji vyote 65 mwaka huu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu wa fedha ambao unaisha wiki moja inayokuja, siyo rahisi kusema tutaleta fedha hizi katika kipindi hiki, lakini tushukuru kwamba katikati hapo tulipata karibu shilingi bilioni tano ambayo tumeitawanya nchi nzima angalau kugusa kidogo kidogo.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge kwamba kwenye bajeti ijayo tumetenga; vilevile kupitia tume tutaendelea na mpango wetu wa kukamilisha vijiji vyote katika jimbo la Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kumekuwa na migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji, na kuna wawekezaji wengi wakubwa wamewekeza na hawaendelezi yale maeneo, je, Serikali haioni kuna umuhimu wa kuwagawia wahitaji yale maeneo ambayo hayajaendelezwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, nadhani ni kama wiki sasa tumejibu mwelekeo, nini tunafanya katika Wizara ya Ardhi. Tumeunda timu ya ufuatiliaji wa uendelezaji wa haya mashamba na yale yatakayobainika kwamba yametelekezwa na hayana uendelezaji wowote, Serikali inapanga kuyarejesha mikononi mwake, na wazo sasa kwenda kwa wananchi litafuata baada ya kuwa tumekamilisha hii hatua ambayo tunaendelea nayo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka Serikalini. Sasa nilete tangazo la wageni ambao wako hapa Bungeni asubuhi hii. Kwanza ni wageni 30 wa Mheshimiwa Deus Clement Sangu, ambaye ni Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Hawa ni wanakwaya wa Mtakatifu Petro kutoka Mkoani Rukwa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, ambaye ni Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Huyu ni Dkt. Jane Mpapalika, Mtafiti Mwandamizi kutoka *REPOA*, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni 10 wa Mheshimiwa Festo Richard Sanga, ambao ni ndugu zake kutoka Makete, mkoani Njombe, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 11 wa Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, ambao ni Wenyeviti wa Kata Jimbo la Busanda, Mkoani Geita, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 31 wa Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, ambao ni kikundi cha Wanawake wa *Comfort Zone Group* kutoka Jijini Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 38 wa Mheshimiwa David Mathayo David ambao ni wanafunzi 35 na walimu watatu wa Shule ya Sekondari Kwakoko kutoka Same Mkoani Kilimanjaro, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 33 wa Mheshimiwa Mary Francis Masanja, ambao ni wanafunzi na walimu wa shule ya msingi na sekondari kutoka Kituo cha *Village of Hope* cha Jijini Mwanza, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Yupo Ndugu Enock Babu, Mkulima kutoka Wilaya ya Muleba, Mkoani Kagera, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Allen Leonard Ngongi kutoka Chuo Kikuu cha Kyrenia Nchini Cyprus, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao Walimu 10 na Wanafunzi 90 wa Shule ya Msingi Lucky Vincent kutoka Kata ya Olasiti, Halmashauri ya Jiji la Arusha. Karibuni sana. *(Makofi)*

Walimu 10 na Wanafunzi 90 kutoka Shule ya Msingi Exodus ya Halmashauri ya Misungwi kutoka Mkoani Mwanza. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2025
### *(The Finance Bill, 2025)*

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2025 *(The Finance Bill 2025),* umeshasomwa kwa mara ya kwanza hapa Bungeni. Kwa utaratibu wetu Muswada huu nitaupeleka kwenye Kamati inayohusika na Muswada huu unapelekwa kwenye Kamati yetu ya Bunge ya Bajeti ili na wao waweze kutazama kwa utaratibu ule wa kawaida kabisa, watapokea maoni kutoka kwa wadau mbalimbali pia. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, Muswada umeshasomwa kwa mara ya kwanza.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2024 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;
### na
### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa Oran Manase Njeza, aje awasilishe maoni ya Kamati. *(Makofi)*

**MHE. ORAN M. NJEZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 124(8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023

na kwa kuzingatia kifungu cha 9(1) na (2) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu tathmini ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2024, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2024/2025, Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/2025, pamoja na Mapendekezo ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii imegawanyika katika sehemu Kumi kama inavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati. Naomba taarifa yote ya Kamati iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake za kuhakikisha kuwa, uchumi wa nchi unaimarika kwa kuendelea kuwekeza katika sekta ya kilimo, kuboresha miundombinu ya usafiri na usafirishaji, kulinda amani na utulivu, kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara, kusimamia vizuri sekta ya fedha na kuboresha huduma za kijamii. Hakika Mheshimiwa Rais anastahili miaka mitano tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kielelezo namba mbili kwenye taarifa kinaonesha mchanganuo; mchango wa shughuli za kiuchumi katika pato la Taifa kwa mwaka 2024. Kamati inaishauri Serikali kufanya mageuzi katika sekta ya kilimo, madini na utalii ili kuongeza tija, thamani na kuboresha masoko. Vilevile, Serikali iweke mikakati thabiti ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi yanayoweza kuathiri sekta ya kilimo. Hatua hizi kwa pamoja zitaleta manufaa katika uchumi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mfumuko wa bei wa Taifa, katika mwaka 2024 ulikua kwa wastani wa 3.1% ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.8 kwa mwaka 2023 na 4.3% kwa mwaka 2022. Kushuka kwa mfumuko wa bei nchini kumechangiwa na utekelezaji madhubuti wa sera ya fedha na bajeti, kutengamaa kwa bei ya mafuta katika soko la dunia na kuimarika kwa upatikanaji wa chakula katika masoko ya ndani na nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, mwenendo huu himilivu wa mfumuko wa bei nchini umekuwa na manufaa kama vile kuvutia uwekezaji, kulinda thamani ya shilingi, kuwa na uchumi unaotabirika na kuwa na jamii yenye utulivu. Napenda kumpongeza tena Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuimarisha uchumi ili kuhakikisha unakuwa imara na unaotabirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu akiba ya fedha za kigeni. Kwa mujibu wa ripoti ya Sera ya Fedha *(Monetary Policy Report)* ya Benki Kuu ya mwezi Aprili, 2025 hadi kufikia Machi, 2025 kiwango cha akiba ya fedha za kigeni kilifikia Dola za Marekani bilioni 5.6 kutoka dola za Marekani bilioni 5.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, hii ni sawa na ongezeko la 5.7%, kiasi hicho kilitosheleza malipo ya uagizaji bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha miezi minne na nusu. Kuongezeka kwa akiba ya fedha za kigeni nchini katika kipindi hiki kumesababishwa na mpango wa ununuzi wa dhahabu, utekelezaji wa mikakati ya kuongeza mauzo ya nje na kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mwenendo wa viwango vya riba na huduma za kibenki. Wastani wa riba za mikopo ulipungua kutoka 15.75% mwaka 2023 hadi 15.47% mwaka 2024. Vilevile, katika kipindi hicho viwango vya riba za akiba za wateja vilipungua toka 10.08% mpaka 8.14%. Kamati inaishauri Serikali kufanya marejeo ya viwango vya riba vya hati fungani za Serikali ili kutoathiri ukopaji kwa sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tathmini ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025, iliyoidhinishwa na Bunge ilikuwa shilingi trilioni 50.29. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 33.86 ilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 16.43 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo, sawa na 67.34% na 32.66% ya bajeti yote mtawalia.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Mei, 2025, Serikali imefanikiwa kukusanya jumla ya trilioni 45.07 sawa na

89.62% ya bajeti nzima ya Serikali na ikiwa ni pungufu ya shilingi trilioni 6.22. Kwa kuwa ukusanyaji wa mapato wa shilingi trilioni 4.3 kwa mwezi, ni dhahiri kuwa ifikapo tarehe 30 Juni, 2025 Serikali itakuwa imefikia ukusanyaji kwa zaidi ya 98.17% ya lengo la mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, ufanisi huu umekuwepo kwa miaka minne mfululizo. Katika mwaka 2020/2021, 2021/2022, 2022/2023 na pia 2023/2024, Bajeti ya Serikali imekuwa ikitekelezwa kwa wastani wa 96%. Hivyo, naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais tena, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ufanisi huu katika utekelezaji wa Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapato ya kodi, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Mei, 2025, jumla ya shilingi trilioni 26.86 zilikusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* sawa na 91.23% ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 29.42. Aidha, ufanisi huu umechagizwa na kuongezeka kwa mapato ya kodi ya forodha ambapo katika kipindi cha Julai, 2024 mpaka Februari, 2025, jumla ya shilingi trilioni 8.26 zilikusanywa, sawa na ongezeko la shilingi trilioni 1.18 ikilinganishwa na shilingi trilioni 7.08 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa ufanisi huo wa ukusanyaji wa mapato. “Kodi Yetu, Maendeleo Yetu”. Kielelezo namba nne kwenye taarifa ya Kamati kinaonesha mwenendo wa ukusanyaji huo wa mapato toka mwaka 1999 mpaka 2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ufanisi wa makusanyo ya kodi umetokana na matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika kukusanya mapato, mwamko wa wananchi kulipa kodi kwa hiari, ongezeko la rasilimali watu kwa Mamlaka ya Mapato, kukua kwa uchumi na ongezeko la biashara na uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, bado kuna changamoto ambazo zinarudisha nyuma jitihada za Serikali katika kuongeza mapato ya kodi. Changamoto hizo ni: -

(i) Idadi ndogo ya walipa kodi hai;

(ii) Uwepo wa sekta isiyo rasmi; na

(iii) Wingi wa mamlaka za udhibiti.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo: -

(i) Kuongeza mchango wa kodi kutoka biashara ndogo ndogo na za kati;

(ii) Kuhamasisha matumizi ya mifumo ya Kitehama kwa ajili ya malipo *(cash right);*

(iii) Kuendelea kutoa elimu ya mlipakodi ili isaidie kujenga utamaduni wa ulipaji kodi kwa hiari na umuhimu wote katika maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, jedwali namba sita kwenye Taarifa ya Kamati linaonesha mwenendo wa makusanyo ya mapato kuanzia mwaka 2022/2023 hadi mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapato yasiyo ya kodi, kwa kipindi cha miaka minne kuanzia 2020/2021 hadi 2023/2024 mapato yasiyo ya kodi yamekuwa yanakusanywa kwa wastani wa 78.33%. Pamoja na kwamba ufanisi huu ni wa kiwango cha kuridhisha, mapato hayo yangeweza kukusanywa zaidi endapo mifumo ya kitehama ingetumika katika kukusanya ada na tozo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa maduhuli pamoja na kuchukua hatua za kinidhamu kwa Wizara, Idara, na Taasisi za Serikali ambazo hazitatumia mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Serikali za Mitaa zilikusudia kukusanya jumla ya shilingi trilioni 1.36. Hadi Mei, 2025 kiasi cha shilingi trilioni 1.26 kilikusanywa sawa na 92.65% ya lengo la mwaka. Ufanisi huu umetokana na matumizi ya Mfumo wa *TAUSI* katika ukusanyaji wa mapato.

Kamati inaipongeza Serikali kwa kutumia mfumo huu ambao umepunguza upotevu wa mapato ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kukamilisha usajili wa majengo ili kuongeza mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa na kuweza kujitegemea kimapato.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mwenendo wa matumizi, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali iliweka maeneo ya vipaumbele yenye lengo la kuweka chachu ya ukuaji wa uchumi na kuongeza ajira. Hadi mwezi Mei, 2025, ridhaa ya matumizi iliyokuwa imetolewa na Serikali ilikuwa shilingi trilioni 42.90 sawa na 85.31% ya bajeti ya Serikali ya shilingi trilioni 50.29. Kati ya fedha hizo, matumizi ya kawaida ni shilingi trilioni 30.63 sawa na 90.8% ya lengo la mwaka la shilingi trilioni 34.94.

Mheshimiwa Spika, aidha, kiasi cha shilingi trilioni 15.74 kilitolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo sawa na 95.8% ya lengo la mwaka la shilingi trilioni 16.43. Jedwali namba saba kwenye taarifa ya Kamati linaonyesha fedha za matumizi ya maendeleo kwa mwaka 2020/2021 – 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ugharamiaji wa deni la Taifa, hadi mwezi Mei, 2025 Serikali ilitumia jumla ya shilingi trilioni 11.16 kwa ajili ya kugharamia deni la Taifa ikiwa ni 85.08% ya lengo la mwaka la kulipa jumla ya shilingi trilioni 13.12. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua ilizozichukua katika kuimarisha thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani ambazo zimeenda kupunguza gharama kwenye malipo ya deni la nje ambalo 62% lipo kwa dola za Marekani.

Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Mei, 2025 ridhaa ya matumizi ya maendeleo iliyotolewa ilikuwa shilingi trilioni 15.7 sawa na 95.8% ya lengo la mwaka la shilingi trilioni 16.43. Katika kipindi hicho, Serikali iliendelea kugharamia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwa ni pamoja na ukamilishaji wa miradi ya Bwawa la Julius Nyerere, Daraja la Kigongo - Busisi na mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa ya *SGR*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na uchambuzi wa mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2025/2026. Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa mwaka 2024/2025 ni wa nne katika utekelezaji wa Mpango wa tatu wa maendeleo wa miaka mitano (2021/2022 – 2025/2026).

Mheshimiwa Spika, mpango huo ulikuwa na dhima ya kujenga uchumi shindani na wa viwanda kwa maendeleo ya watu. Mpango wa mwaka 2024/2025 ulitarajiwa kugharimu kiasi cha shilingi trilioni 16.43 sawa na 32.67% ya bajeti yote ya Serikali. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 12.78 ni fedha za ndani na shilingi trilioni 3.64 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Mei, 2025 jumla ya shilingi trilioni 15.74 zilitolewa sawa na 95.1%. Kamati inaendelea kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa nia yake thabiti ya kuwaletea Watanzania maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mpango wa mwaka 2025/2026 unatarajiwa kugharimu kiasi cha shilingi trilioni 17.49 sawa na 30.96% ya bajeti yote ya mwaka 2025/2026. Mpango huu umejikita katika kuendeleza na kukamilisha utekelezaji wa afua zinazotoa matokeo katika maeneo matano ya kipaumbele ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano kama yanavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Afya ilipangiwa kutumia jumla ya shilingi trilioni 1.31 katika mwaka wa fedha 2024/2025. Hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya shilingi trilioni 1.23 zilipokelewa sawa na 94%. Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Sekta hii imeidhinishiwa bajeti ya shilingi trilioni 1.62 sawa na ongezeko la 23.67%. Aidha, katika kipindi cha miaka mitano (2021/2022 – 2025/2026) tumeshuhudia bajeti ya Sekta hii ikiongezeka kutoka shilingi trilioni 1.03 hadi shilingi trilioni 1.62 sawa na ongezeko la 56.47%.

Mheshimiwa Spika, hakika haya ni maendeleo makubwa, na Kamati inaipongeza Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi mahiri ambao umeleta mageuzi makubwa katika Sekta ya Afya. Hatua hii ilipelekea kupata tuzo kwa Mheshimiwa Rais ya *The Global Goalkeeper Award* kutoka taasisi ya *The Gates*. Mafanikio ya Sekta hii ni kama yanavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2024/2025, Sekta ya Madini ilitengewa bajeti ya shilingi bilioni 531.27. Hadi kufika Machi, 2025 sekta hii ilikuwa imepokea shilingi bilioni 392 sawa na 73.85%. Aidha, katika mwaka 2024, sekta hii imekua kwa 8.3% na kuchagia 10.1% katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuipongeza Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kipindi cha uongozi wake, bajeti ya Wizara ya Madini imeongezeka kutoka shilingi bilioni 66.82 mwaka 2021/2022 hadi shilingi bilioni 531 mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la 695%. Ongezeko hilo linaonyesha nia ya dhati ya kuboresha sekta ya madini. Mafanikio ya sekta hii ni kama yanavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi huo, kwani umewezesha upatikanaji wa dhahabu kwa ajili ya Hazina ya Taifa ya Fedha za Kigeni *(Foreign Reserves)*, ambapo hadi Mei, 2025 Benki Kuu ilinunua takribani tani 4.8 ya dhahabu iliyozalishwa na kuchakatwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ili kuendelea kuongeza ufanisi na tija katika sekta hii, Kamati inaishauri Serikali kufanya mabadiliko ya sheria zote ambazo zinakwamisha uwekezaji kwenye sekta ya madini, kupunguza kodi, kudhibiti utoroshwaji wa madini na kuhakikisha kuwa madini yanaongezwa thamani nchini kabla ya kusafirishwa kwenda nje.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, sekta ya utalii ilichangia 17.2% ya pato la Taifa na kuchangia 26% ya mapato ya

fedha za kigeni na hivyo kuwa miongoni mwa sekta zilizochangia kwa kiasi kikubwa katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuimarisha Sekta ya Maliasili na Utalii kwa kuendeleza na kukuza vivutio mbalimbali vya utalii ikiwemo kuanzishwa kwa programu maalum za kuitangaza Tanzania Kimataifa kama vile filamu ya *The Royal Tour* pamoja na filamu ya *Amazing Tanzania*.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mchango wa sekta hii katika uchumi, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa Mamlaka za Uhifadhi zinatengewa fedha za kutosha kwa ajili ya kuendeleza miundombinu muhimu ya sekta hii na kujiendesha kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali pia itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kutangaza nchi yetu Kimataifa ili kuvutia watalii wengi zaidi. Hatua hizi ziende sambamba na kurejewa kwa mifumo ya kodi na tozo ili kutatua changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Spika, pia kuna hoja mahususi. Katika mwaka wa fedha 2023/2024, masuala 22 yaliibuka wakati wa majadiliano Bungeni kwa mujibu wa Kanuni ya 124(1). Kati ya masuala hayo, masuala 10 yalihitaji ufuatiliaji na masuala 12 Kamati ilikubaliana na hatua za utekelezaji zilizochukuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika mwaka wa fedha 2024/2025, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(3) na (4), masuala 17 yaliibuliwa na Kamati za Kisekta. Kati ya masuala hayo, masuala saba yalihitaji ufuatiliaji na masuala 10 Kamati ilikubaliana na hatua za utekelezaji zilizochukuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, taarifa ninayoiwasilisha ni muhtasari wa ufuatiliaji wa maagizo ya Kamati ya Uongozi kwa Serikali kuhusiana na baadhi ya masuala muhimu.

Mheshimiwa Spika, suala la kwanza, hoja zilizotekelezwa kikamilifu na Serikali kutokana na maagizo ya Kamati ya Uongozi kwa mujibu wa Kanuni ya 124(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, kurejesha ukusanyaji wa mapato kwa Mamlaka ya Bandari.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya kurejesha ukusanyaji wa mapato yanayotokana na tozo ya gati kwa Mamlaka ya Bandari kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania. Serikali ilikubali pendekezo hilo na kufanya mabadiliko kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2024 na kurejesha jukumu hilo kwa Mamlaka ya Bandari.

Mheshimiwa Spika, hatua hizo za utekelezaji zinaonyesha ahadi ya Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutekeleza maazimio ya Kamati ya Uongozi. Hakika *4R* za Mheshimiwa Rais anazitekeleza kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa na masuala ya utekelezaji kwa mujibu wa Kanuni ya 117(3) na (4) yaliyotokana na utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na makadirio ya bajeti kwa mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kwamba katika marejeo ya Bajeti ya Serikali mwezi Februari Mwaka 2025 *(Supplementary Budget)*, Serikali ilikubali kutenga jumla ya shilingi 123,500,000,000.00 kwa ajili ya kukamilisha maboma na ujenzi wa vituo vya afya vya kimkakati. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 70 ni kwa ajili ya maboma na shilingi bilioni 53.5 ni kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya vya kimkakati.

Mheshimiwa Spika, hadi tarehe 31 Mei, 2025 Serikali ilikuwa imetoa jumla ya shilingi bilioni 70. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 40 zimetolewa kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma; na shilingi bilioni 30 zimetolewa kwa ajili ya vituo vya afya vya kimkakati.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa fedha zilizosalia, kiasi cha shilingi 53,500,000,000.00 Serikali imeahidi kutoa kabla ya mwaka wa fedha 2024/2025 kukamilika ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa fedha hizi zinatumika wakati wa utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2025/2026 kupitia utaratibu wa fedha zinazovuka mwaka *(carryovers)* kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti, Sura ya 439.

Mheshimiwa Spika, pia tunatoa taarifa kuhusu sura ya bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Pamoja na mambo

mengine, bajeti hii itatumika kugharamia Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2025. Hatua hii inalifanya Taifa letu kutotegemea mtu, taasisi au Taifa lolote kufadhili uchaguzi wetu na hivyo viongozi watakaochaguliwa watatokana na kura za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali imepanga kukusanya na kutumia jumla ya shilingi trilioni 56.49, sawa na ongezeko la 12.3% ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2024/2025 ya shilingi trilioni 50.29. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 38.99 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 82.23 ya bajeti ni kwa ajili ya kugharamia deni na mishahara pamoja na stahiki ya watumishi wa Umma. Shilingi trilioni 17.49 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo sawa na 30.96% ya bajeti. Bajeti ya maendeleo inajumuisha shilingi trilioni 12.12 fedha za ndani na shilingi trilioni 5.38 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatarajia kukusanya jumla ya shilingi trilioni 40.47. Kati ya fedha hizo, mapato ya kodi ni shilingi trilioni 34.10 na mapato yasiyotokana na kodi ni shilingi trilioni 6.36. Makadirio ya makusanyo ya mapato ya ndani kwa mwaka 2025/2026 yatapelekea uwiano wa mapato ya ndani na pato la Taifa kufikia 16.8%.

Mheshimiwa Spika, mapato ya ndani yanaweza kugharamia bajeti ya Serikali kwa 71.64%. Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuimarisha sera na mifumo ya ukusanyaji wa mapato iliyosababisha sehemu kubwa ya bajeti kugharamiwa na mapato ya ndani.

Mheshimiwa Spika, sera ya matumizi. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imepanga kutumia kiasi cha shilingi trilioni 56.49 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Ili bajeti hiyo itekelezwe kwa ufanisi, Kamati inashauri masuala yafuatayo: -

(i) Kuhakikisha mikopo yote inaelekezwa kwenye maeneo ya uzalishaji kama inavyoelekeza Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya Serikali Sura ya 134;

(ii) Kusimamia Waraka Na. 1 wa Hazina wa mwaka 2018/2019 kuhusu Mikakati wa kudhibiti madeni ya Serikali;

(iii) Kukamilisha miradi iliyopo sasa kabla ya kuanzisha miradi mipya;

(iv) Kupanga bajeti kwa kuangalia mahitaji halisi ya sasa na siyo kwa kufuata mwenendo wa bajeti zilizopita; na

(v) Kufanya mapitio ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa lengo la kupunguza matumizi yasiyo ya lazima.

Mheshimiwa Spika, jedwali Na. 11 kwenye taarifa ya Kamati linaonyesha ulinganisho wa Sura ya Bajeti kati ya mwaka 2024/2025 na 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi wa hatua za Kikodi. Kamati ya Bajeti imefanya uchambuzi wa hatua zote za kikodi zilizopendekezwa na Serikali na kubaini zimegawanyika katika makundi makuu matatu. Makundi hayo ni Sheria za Kodi za Ndani, Sheria ya Usimamizi wa Ushuru wa Forodha wa Afrika Mashariki ya Mwaka 2004, na Mabadiliko ya Kanuni zilizotungwa chini ya sheria mbalimbali zilizopo. Madhumuni ya mapendekezo yamefafanuliwa kwa kila kundi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Sheria za Kodi za Ndani. Katika uchambuzi wa mapendekezo ya Serikali kwenye Sheria za Kodi za Ndani, Kamati imebaini kwamba mapendekezo hayo yanalenga masuala yafuatayo: -

(i) Kuchochea uzalishaji wa viwanda vya ndani pamoja na kuvilinda vilivyopo dhidi ya ushindani usio sawa;

(ii) Kuongeza mapato ya Serikali kwa kupanua wigo wa kodi, kuongeza walipa kodi wapya pamoja na kuboresha mifumo ya ukusanyaji na usimamizi wake;

(iii) Kukuza na kuendeleza Sekta ya Bima nchini pamoja na kuvutia wawekezaji katika sekta hiyo;

(iv) Kuongeza mchango wa Mashirika ya Umma kwenye Mapato ya Serikali kupitia Msajili wa Hazina;

(v) Kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (MKUMBI);

(vi) Kuwalinda wananchi dhidi ya madhara ya kiafya yanayoweza kujitokeza kutokana na matumizi ya vyakula au bidhaa za aina fulani hatari; na

(vii) Kuongeza mapato ya Serikali ili kuziba nakisi inayotokana na baadhi ya wafadhili na washirika wa maendeleo kusitisha kugharamia programu mbalimbali hususan kwenye sekta ya afya.

Mheshimiwa Spika, jumla ya sheria 23 za kodi za ndani zinatarajiwa kufanyiwa maboresho. Pamoja na kwamba Kamati itapata nafasi ya kutoa maoni yake kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2025, ninaomba uniruhusu nitoe maoni kwa muhtasari maeneo yatakayozingatiwa.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya marekebisho ya utoaji wa leseni za biashara Sura 101. Katika aya ya 168 ya Hotuba ya Bajeti ya Serikali, Serikali imekusudia kuweka mazingira mazuri ya ufanyaji biashara baina ya wazawa na wageni kwa kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Utoaji wa Leseni za Biashara, Sura 101.

Mheshimiwa Spika, marekebisho hayo pamoja na mambo mengine yanalenga kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya masuala ya biashara kuainisha shughuli za kibiashara ambazo hazipaswi kufanywa na wageni. Hatua hii inalenga kuondoa kero iliyopo nchini hivi sasa ya wafanyabiashara wageni kufanya biashara za jumla, rejareja na uchuuzi ambazo zilikuwa ni shughuli zinazofanywa na wazawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, wakati wa majadiliano ya Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2025, Kamati itaishauri Serikali kuweka adhabu kwa wageni watakaokiuka masharti ya kanuni hizo ikiwa ni pamoja na kuwafutia vibali vya kazi na *VISA*

pamoja na wanaothibitika. Hakika usikivu huu wa Mheshimiwa Rais ni jambo la kuigwa na uwe mfano kwa nchi nyingine za Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria ya Hifadhi ya Taifa, Sura 282, Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, Sura 284, na Sheria ya Msajili wa Hazina (Mamlaka na Majukumu), Sura 370. Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubali kufanya mabadiliko kwenye sheria hizi ili kurejesha utaratibu wa kukusanya na kutumia mapato yao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kiwango cha asilimia kinachopendekezwa kwenye mgao ni jambo ambalo litajadiliwa kwa kina na Serikali kwa sababu kuu mbili; moja ni hali ya ukwasi wa taasisi hizo, ili ziweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu kwenye sekta ya utalii na pili ni endapo kiwango kinachobakishwa kinaweza kukidhi mahitaji ya taasisi kujiendesha kwa misingi ya kibiashara na kwa ufanisi. Pia, kuna Sheria ya Mabadiliko ya Usimamizi wa Ushuru wa Forodha ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, Kamati imepitia hatua zote zilizoridhiwa na Mkutano wa Mashauriano ya Kibajeti wa Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika tarehe 20 Mei, 2025, Jijini Arusha na kubaini kwamba, hatua mpya ni 13 na hatua 48 ni mwendelezo wa hatua ambazo zilichukuliwa katika miaka ya fedha iliyotangulia. Hatua hizo kwa ujumla wake zinalenga maeneo yafuatayo: -

a) Kulinda ajira na uzalishaji wa viwanda ambavyo vipo ndani ya Jumuiya ya Afrika mashariki;

b) Kuchochea uzalishaji wa bidhaa mbalimbali viwandani katika Jumuiya; na

c) Kukuza biashara baina ya nchi wanachama wa Jumuiya.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Waziri

wake wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, imekuwa ikishirikisha Kamati ya Bajeti kuhusu Mapendekezo ya Serikali ya hatua ambazo zinapendekezwa na Serikali juu ya mabadiliko ya Sheria ya Usimamizi wa Ushuru wa Forodha.

Mheshimiwa Spika, hakika huu ndiyo ushirikiano na maridhiano ambayo ni lazima Bunge lako litambue na kuenzi. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba, utaratibu huu unaendelea kuwepo kwa kipindi kijacho kwa sababu, umethibitisha kuwa na manufaa.

Mheshimiwa Spika, pia, kuhusu Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali pamoja na Kanuni, Kamati ya Bajeti katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo imekuwa ikiishauri Serikali mambo makuu matatu;

a) Kuhakikisha mabadiliko ya kanuni zinazoanzisha tozo, faini na ada zinabadilishwa, sambamba na Mabadiliko ya Sheria ya Fedha;

b) Mabadiliko ya Kanuni yanayotangazwa na Wizara ya Fedha kupitia Hotuba ya Bajeti ya Serikali kuwa sehemu ya Hotuba, ili kuwandaa wafanyabiashara ambao ni walipa kodi; na

c) Kanuni zinazotungwa na kutangazwa na Waheshimiwa Mawaziri mbalimbali kuhusu ada, tozo na faini zithibitishwe na Mheshimiwa Waziri wa Fedha kabla ya kutangazwa.

Mheshimiwa Spika, la leo lisingoje kesho. Naomba nitoe pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kusikiliza, kukubali na kufanyia kazi mapendekezo ya Kamati. Hatua hii inaenda kuondoa udhaifu uliokuwepo ambapo Mamlaka na Wakala wa Serikali zilikuwa zikianzisha tozo, ada na faini katikati ya mwaka wa fedha na hivyo kuleta taharuki kwa wafanyabiashara. Maboresho hayo yanaenda kufanyika kupitia Sheria ya Bajeti, Sura ya 439 na Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hatua za kikodi zilizowasilishwa zimegusa maeneo mengi, na Kwa kuwa, kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (2), Kamati ina wajibu wa kualika umma kutoa maoni, rai yangu kwa Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote wenye nia ya kutoa maoni juu ya hatua za kikodi zinazopendekezwa, kufika mbele ya Kamati mara baada ya kupokea tangazo la kupokea maoni ya umma. Maoni ya wadau yamekuwa na mchango mkubwa katika kuboresha Sheria ya Fedha ya kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, maoni ya jumla. Matumizi ya mfumo wa ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi *PPP* katika kugharamia miradi ya maendeleo. Naomba kunukuu Aya ya 123 ya Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha; "Mheshimiwa Spika, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, mikataba minne ya ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi *PPP* yenye mtaji wa jumla ya shilingi bilioni 681.53 imesainiwa katika mwaka 2024/2025, kwa ajili ya kutoa huduma ya usafiri wa mabasi katika mradi wa mabasi yaendayo haraka *(BRT)* kwa awamu ya kwanza." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, kongole kwa Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa mara ya kwanza Sheria ya Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Sura ya 103, iliyotungwa na Bunge mwaka 2010 na kufanyiwa marekebisho yake mwaka 2023 inaenda kutekelezwa kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, ili Serikali iendane na kutekeleza miradi kwa mfumo huu ambao unapunguza mahitaji ya fedha kwa Serikali, na ili kutekeleza miradi ya maendeleo yenye sura ya kibiashara, Kamati inaitaka Serikali, moja ya masharti kwenye Mwongozo wa Maandalizi ya Bajeti ya mwaka 2026/2027 iwe ni kuwataka Maafisa Masuuli wote kuwasilisha miradi inayotekelezwa kwa njia ya *PPP* kabla ya kuwasilisha miradi itakayotekelezwa kwa fedha za umma. Miradi hiyo ichambuliwe na Tume ya Mipango kwa kushirikiana na Kituo cha Ubia, yaani *PPP,* na itekelezwe katika bajeti ya mwaka husika.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni *diaspora* na fedha za kutoka nje *(remittances)*. Kama nchi, haijaweza kufanya vizuri katika kupokea fedha kutoka kwa Watanzania waishio ughaibuni, ambao ni muhimu katika ukuaji wa uchumi na kama msaada wa kifedha *(financial lifeline)* katika kuchochea ukuaji wa uchumi, maendeleo ya nchi na mtu mmoja mmoja, chanzo hiki ni muhimu kutokana na mchango wake, sio tu katika uwezo wa ununuzi wa kaya, lakini hata kwenye kujenga akiba ya fedha za kigeni nchini, hivyo, kuzifanya kuwa eneo muhimu la kuzingatiwa kwa maendeleo ya uchumi jumuishi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2024 Tanzania ilipokea kiasi cha jumla ya dola za Marekani milioni 757, kama *remittances*, tofauti na nchi nyingine za Afrika Mashariki. Mfano, katika mwaka 2024, nchi ya Kenya ilipokea jumla ya dola za Marekani bilioni nne na milioni 400, kama *remittances,* ikiwa ni zaidi ya mapato yanayotokana na mauzo nje ya Kenya ya kahawa na utalii. Aidha, ongezeko hili limetokana na kuboreshwa kwa huduma za kifedha za kidijitali ambazo huwezesha kutuma pesa kwa haraka na nafuu zaidi kuliko hapo awali.

Mheshimiwa Spika, hivyo, Serikali ifanye utafiti wa kina katika eneo hili ili kuangalia ni namna gani inaweza kufaidika na chanzo hiki cha mapato. Jedwali Namba 12 kwenye Taarifa ya Kamati linaonesha takwimu za fedha zinazopokelewa kutoka ughaibuni, fedha kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kuwezesha kimtaji Benki ya Maendeleo ya Kilimo *(TADB)* na Benki ya Uwekezaji Tanzania *(TIB)*. Jukumu kuu la Benki ya Kilimo ni kuwa chachu ya utoaji wa mikopo ya muda mfupi, wa kati na mrefu, kwa ajili ya kufanikisha maendeleo jumuishi ya sekta ya kilimo nchini. Kuchangia katika Dira ya Taifa ya Maendeleo katika kuhakikisha utoshelevu na usalama wa chakula, maendeleo ya uchumi na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, tangu kuanzishwa kwake mwaka 2015, *(TADB)* Benki ya Kilimo imefanikiwa kutoa mikopo ya shilingi bilioni 972 ikinufaisha zaidi ya wakulima 1,948,801; biashara 686; na biashara endelevu ni 478. Kwa sasa benki hii ina mtaji wa jumla ya

shilingi bilioni 924,000,000,000.00. Hata hivyo, benki hii haipokei amana kama ilivyo kwa benki za biashara.

Mheshimiwa Spika, ili kutimiza kikamilifu dhamira ya *TADB* na kukidhi mahitaji yanayoongezeka ya fedha kwa ajili ya kilimo, na ukiangalia uwekezaji kwenye kilimo uliofanywa na Serikali, benki hii inahitaji jumla ya shilingi 2,950,000,000,000.00, hivyo kuifanya kuwa na nakisi ya shilingi 2,026,000,000,000.00. Benki ya *TIB* ina jukumu la kutoa huduma za fedha kwa miradi ya maendeleo kwa gharama nafuu, ili kujenga Taifa lenye uchumi shirikishi mseto, mahiri na wenye ushindani.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, mwenendo wa ufanisi wa benki hiyo siyo wa kuridhisha kwa sababu, katika kipindi cha miaka mitatu, mapato ya benki yamekuwa yakishuka kutoka shilingi bilioni 62,700 mwaka 2022 hadi shilingi bilioni 35,600 kwa mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kushuka kwa kasi ya utoaji wa mikopo kutokana na kiwango hafifu cha mtaji, hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2024, mtaji wa benki kwa mujibu wa kanuni za taasisi za fedha *(core capital)* ulikuwa ni shilingi 90,226,000,000.00 kiwango ambacho ni kidogo ikilinganishwa na kiwango cha shilingi 200,000,000,000.00 kinachotakiwa kwa mujibu wa Kanuni za Taasisi za Fedha za Maendeleo zilizotolewa na Benki Kuu ya Tanzania mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, benki za maendeleo kwa nchi zilizo na uchumi wa kati wa juu zina mtaji wa 2% wa pato la Taifa. Kwa kuwa, Tanzania kufikia 2050 itakuwa katika kundi hilo, Serikali haina budi kuziwezesha kifedha benki hizo ili ziwe na mtaji unaotakiwa na hivyo kuongeza ufanisi na kuziwezesha kuwa shindani. Vilevile Kufanya mabadiliko kwenye Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa, Sura ya 437, ili mfumo wa malipo kwa njia ya kielektroniki, *CashLite,* uanze kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kuhusu kupunguza matumizi ya fedha taslimu na kutumia mifumo ya kielektroniki katika kufanya malipo ili kuzuia upotevu wa mapato yatokanayo na kodi. Malipo ya kielektroniki

ni miamala inayofanyika kupitia kadi za malipo, simu za mkononi na malipo ya papo kwa papo. Lengo ni kurahisisha miamala na kupunguza utegemezi wa fedha taslimu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaisisitiza Serikali kufanya mabadiliko katika Kifungu cha Nane cha Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa, Sura ya 437, pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438, ili kuanzisha sharti la lazima la kufanya malipo kwa njia ya kieletroniki wakati wa kufanya manunuzi ya huduma na bidhaa. Mfano, Serikali inaweza kuweka ukomo wa malipo ya fedha taslimu wa kiwango cha chini pamoja na kupunguza gharama za kufanya miamala, ili kutohamasisha matumizi ya fedha za taslimu kwenye malipo ya manunuzi ya bidhaa na huduma.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kukushukuru wewe mwenyewe, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mbunge, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa kwanza mwanamke wa Umoja wa Mabunge Duniani *(IPU);* kwanza kwa kuniamini kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na pili, kwa miongozo thabiti iliyowezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Uyole linaweza kuwa Jimbo jipya la uchaguzi, lakini kwako ni nyumbani, hata wananchi wa Mbeya Vijijini nao wanakufahamu vizuri, ni jirani zako, hivyo Wanauyole hawatasita kukupa ushindi wote. Sisi Mbeya Vijijini tutakuwa sambamba nao kuhakikisha kuwa unashinda kwa kishindo.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge na Naibu Spika, kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge lako Tukufu. Nimtakie kila lililo jema kwenye uchaguzi unaokuja. Hakika Ilala bado inamhitaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuwashukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba Madelu, Mbunge na Waziri wa Fedha; Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, Mbunge na Waziri wa Mipango na Uwekezaji; Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri wa Fedha; na Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mbunge, na Naibu Waziri wa Mipango

na Uwekezaji, kwa ushirikiano wao kwa Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yao. Nawatakia kila la heri, na ni imani yangu watarejea tena mwezi Novemba, 2025 tutakuwa wote hapa.

Mheshimiwa Spika, vilevile, nawashukuru Dkt. Natu El-Maamry Mwamba, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mlipaji Mkuu wa Serikali; *CPA* Charles Edward Kichere, Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali; Dkt. Tausi Mbaga Kida, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji; pamoja na Dkt. Fred Msemwa, Mtendaji Mkuu wa Tume ya Mipango. Pia, nawashukuru Manaibu Katibu Wakuu wa Wizara ya Fedha, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Makamishna, Wakuu wa Taasisi na Wataalam wote kwa ushirikiano wao kwa Kamati katika kipindi chote katika uhai wake.

Mheshimiwa Spika, kwa upendo wa dhati napenda kumshukuru Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, Mbunge na Makamu Mwenyekiti wa Kamati, kwa kunisaidia wakati wote wa shughuli za Kamati. Nawaomba wananchi wa Jimbo la Kibiti kumwamini na kumpa fursa tena ili awatumikie kwa miaka mingine mitano.

Mheshimiwa Spika, aidha, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kuniamini kuwa kiongozi wao, na kunipa ushirikiano katika kipindi chote cha uhai wa Kamati. Nawaombea kila mmoja wenu, ikimpendeza Mwenyezi Mungu, tukutane tena mwezi Novemba, 2025. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama walivyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ila siyo kwa umuhimu, ninamshukuru Ndugu Baraka Leonard, Katibu wa Bunge, kwa niaba ya Watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu uliowezesha kufanikisha shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**16 JUNI, 2025**

## MAONI YA KAMATI KUHUSU TATHMINI YA HALI YA UCHUMI WA TAIFA KWA MWAKA 2024, UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2024/25, UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2024/25 PAMOJA NA MAPENDEKEZO YA MPANGO NA BAJETI YA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### 1.0. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 124(8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 na kwa kuzingatia kifungu cha 9 (1) na (2) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Tathmini ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2024, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2024/25, Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/25 pamoja na Mapendekezo ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/26.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu kumi (10) kama ifuatavyo: -

i. Sehemu ya kwanza ni Utangulizi;
ii. Sehemu ya Pili ni Tathmini ya Mwenendo wa Viashiria vya Uchumi jumla kwa mwaka 2024;
iii. Sehemu ya Tatu ni Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/25;
iv. Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25 pamoja na Uchambuzi wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2025/26;
v. Sehemu ya Tano ni Hoja Mahsusi;
vi. Sehemu ya Sita ni Sura ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/26;
vii. Sehemu ya Saba ni Uchambuzi wa Hatua za Kikodi Zilizopendekezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/26;
viii. Sehemu ya Nane ni Uchambuzi wa Mapendekezo ya Mabadiliko ya Sheria zinazosimamia Ukusanyaji wa Kodi za Ndani;

ix. Sehemu ya Tisa ni Maoni ya Ujumla; na
x. Sehemu ya Kumi ni Hitimisho.

## 2.0. TATHMINI YA MWENENDO WA VIASHIRIA VYA UCHUMI JUMLA KWA MWAKA 2024

### 2.1. Mwenendo wa Hali ya Uchumi wa Dunia

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Taarifa ya Mwenendo wa Hali ya Uchumi wa Dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa Mwezi Aprili, 2025 *(World Economic Outlook Report, April 2025)* inaonesha kuwa uchumi wa dunia ulikua kwa wastani wa **asilimia 3.3** kwa mwaka 2024 ikilinganishwa na **asilimia 3.5** ya mwaka 2023. Ukuaji huu ni chini ya makadirio ya kiwango cha ukuaji wa **asilimia 3.5.** Hali hii ilisababishwa na athari zilizotokana na utekelezaji wa sera ya fedha ya kupunguza ukwasi katika kukabiliana na mfumuko wa bei katika nchi zilizoendelea; migogoro ya kisiasa hususan Ulaya Mashariki na Mashariki ya Kati; gharama kubwa za mikopo katika masoko ya fedha zilizoathiri zaidi nchi zinazoendelea pamoja na athari za mabadiliko ya tabianchi. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kutekeleza Mkakati wa kupambana na vihatarishi hivyo ili pindi vitakapo jitokeza Uchumi usiathirike kwa kiasi kikubwa.

**Jedwali Na. 1: Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi wa Dunia 2020 – 2024**

| Kundi/Mwaka | Ukuaji Halisi (Asilimia) | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
| Dunia | -2.7 | 6.6 | 3.6 | 3.5 | 3.3 |
| Nchi Zilizoendelea | -4.0 | 6.0 | 2.9 | 1.7 | 1.8 |
| Nchi Zinazoibukia na Zinazoendelea | -1.7 | 7.0 | 4.1 | 4.7 | 4.3 |
| Nchi za Asia Zinazoendelea | -0.5 | 7.8 | 4.7 | 6.1 | 5.3 |
| Nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara | -1.5 | 4.7 | 4.1 | 3.6 | 4.0 |

***Chanzo: Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF-WEO), Aprili 2025***

## 2.2. Uchumi wa Taifa pamoja na Nchi za Afrika Mashariki na SADC

### 2.2.1. Uchumi wa Nchi za Afrika Mashariki na SADC

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2024 ukuaji wa uchumi wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki - EAC ulishuka na kufikia wastani wa **asilimia 1.5** ikilinganishwa na **asilimia 5.2** mwaka 2023. Ukuaji huo ulitokana na ukuaji hasi wa nchi ya Sudani Kusini wa **asilimia -27.5** kutokana na hali ya usalama iliyopo katika nchi hiyo**.** Aidha, ukuaji wa uchumi wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika – SADC ulifikia wastani wa **asilimia 3.1** mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa **asilimia 3.9** mwaka 2023. Mabadiliko ya tabianchi yaliyoathiri sekta ya kilimo na miundombinu pamoja na migogoro ya kisiasa inayoendelea katika baadhi ya nchi ikiwemo DRC na Sudani, inatajwa kuwa chanzo cha kushuka kwa uchumi kwa nchi hizi.

**Jedwali Namba 2. Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi wa Nchi zaAfrika Mashariki na SADC (2020-2024)**

| Nchi/Mwaka | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| **Ukuaji wa Nchi za SADC** | | | | | |
| Angola | -4.0 | 2.1 | 4.2 | 1.0 | 4.5 |
| Botswana | -8.7 | 11.9 | 5.5 | 3.2 | -3.0 |
| Comoros | -0.2 | 2.0 | 2.6 | 3.0 | 3.3 |
| Tanzania | 4.5 | 4.8 | 4.7 | 5.1 | 5.5 |
| DRC | 1.7 | 1.7 | 9.2 | 8.5 | 6.5 |
| Eswatin | -1.6 | 10.7 | 0.5 | 5.0 | 3.7 |
| Lesotho | -5.3 | 1.9 | 2.0 | 2.0 | 2.6 |
| Madagascar | -7.1 | 4.7 | 4.2 | 4.2 | 4.2 |
| Malawi | 1.0 | 4.6 | 0.9 | 1.9 | 1.8 |
| Mauritius | 14.5 | 3.4 | 8.7 | 5.0 | 4.7 |
| Msumbiji | -1.2 | 2.4 | 4.4 | 5.4 | 1.9 |
| Namibia | -8.1 | 3.6 | 5.4 | 4.4 | 3.7 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Seychelles | -11.7 | 0.6 | 12.7 | 2.3 | 3.0 |
| Afrika Kusini | -6.2 | 5.0 | 1.9 | 0.7 | 0.6 |
| Zambia | -2.8 | 6.2 | 5.2 | 5.4 | 4.0 |
| Zimbabwe | -7.8 | 8.5 | 6.1 | 5.3 | 2.0 |
| **Wastani** | **-4.5** | **4.6** | **4.9** | **3.9** | **3.1** |
| **Ukuaji wa Nchi za EAC** | | | | | |
| Burundi | 0.3 | 3.1 | 1.8 | 2.7 | 3.5 |
| Kenya | -0.3 | 7.6 | 4.9 | 5.6 | 4.5 |
| Rwanda | -3.4 | 10.9 | 8.2 | 8.3 | 8.9 |
| Somalia | -2.8 | 3.5 | 2.7 | 4.2 | 4.0 |
| Sudan Kusini | -6.5 | 5.3 | -5.2 | 2.5 | -27.6 |
| Tanzania | 4.5 | 4.8 | 4.7 | 5.1 | 5.5 |
| Uganda | -1.1 | 5.5 | 6.2 | 4.9 | 6.3 |
| DRC | 1.7 | 1.7 | 9.2 | 8.5 | 6.5 |
| **Wastani** | **-1.0** | **5.3** | **4.1** | **5.2** | **1.5** |

***Chanzo**: Taarifa ya Hali ya Uchumi, 2024*

**2.2.2.Uchumi wa Taifa**

**Mheshimiwa Spika,** uchumi wa Tanzania umeendelea kuimarika kufikia **asilimia 5.5** mwaka 2024 ikilinganishwa na **asilimia 5.1** mwaka 2023 na **asilimia 4.7** mwaka 2022. Aidha, uchumi unakadiriwa kukua kwa **asilimia 6** mwaka 2025 na **asilimia 6.4** mwaka 2026. Kamati ilifanya tathmini ya ukuaji wa uchumi kuanzia mwaka 2020 hadi 2024 na kubaini kwamba pamoja na kuyumba kwa uchumi wa dunia, uchumi wa Tanzania ulikua kwa wastani wa **asilimia 5** katika kipindi hicho. Mwenendo wa ukuaji wa uchumi ni kama unavyoonekana katika **kielelezo namba 1.**


**Kielelezo Na 1. Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi wa Taifa (2020-2024)**

| Mwaka | Ukuaji wa Uchumi (Asilimia) |
|---|---|
| 2020 | 4.8 |
| 2021 | 4.9 |
| 2022 | 4.7 |
| 2023 | 5.1 |
| 2024 | 5.5 |

**Chanzo**: **Wizara ya Fedha**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali chini ya Uongozi wa **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa jitihada zake za kuhakikisha kuwa Uchumi wa nchi unaimarika kwa kuendelea kuwekeza katika sekta ya kilimo, kuboresha mindombinu ya usafiri na usafirishaji, kulinda amani na utulivu, kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara, kusimamia vizuri sekta ya fedha, kuboresha huduma za jamii. **Hakika Mhe. Rais anastahili Miaka Mitano Tena.** Kielelezo hapo chini kinaonyesha mchango wa kila sekta kwenye pato la Taifa.

**Kielelezo Na. 2: Mchango wa Shughuli za Kiuchumi katika Pato La Taifa kwa Mwaka 2024 (Asilimia)**




**Chanzo:** *Wizara ya Fedha*

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kwamba sekta ya kilimo inachangia **asilimia 26.3** ya pato la Taifa bado ukuaji wake ni **asilimia 4.1** tu licha ya uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali ikiwa ni pamoja na kuongeza bajeti ya sekta hii kutoka **Shilingi bilioni 294** mwaka 2021/22 hadi kufikia **Shilingi trilioni**

**1.249** kwa mwaka wa fedha 2024/25 sawa na ongezeko la **asilimia 383.53**. Sekta hii pia imekuwa na mafanikio mbalimbali katika mwaka 2024. Baadhi ya mafanikio hayo ni:-

i. Kuongezeka kwa thamani ya mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi kutoka **dola za Marekani bilioni 1.2** Mwaka 2019/20 hadi **dola za Marekani bilioni 3.54** Mwaka 2023/2024 sawa na ongezeko la **asilimia 195**;
ii. Uzalishaji wa mazao ya chakula umeongezeka kutoka **tani 17,148,290** Mwaka 2021/2022 hadi **tani 22,803,316** Mwaka 2023/2024 sawa na ongezeko la **asilimia 33** na kufanya utoshelevu wa chakula nchini kufikia **asilimia 128**;
iii. Kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo *(Agriculture Development Fund – ADF);*
iv. Kuongeza upatikanaji wa mbolea kufikia **tani 1,213,729** Mwaka 2024/25 kutoka **tani 678,017** Mwaka 2020/21; na
v. Kuongezeka kwa eneo la kilimo cha umwagiliaji kufikia **hekta 727,280.6** ikiwa na lengo la kufikia **hekta 1,200,000** mwaka 2025/26.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na mafanikio hayo na kwa kuwa sekta hii imeajiri takribani **asilimia 65** ya watanzania, ina uwezo mkubwa wa kupunguza umaskini kwa kiasi kikubwa. Kamati inaishauri Serikali iongeze kasi ya kufanya mageuzi ya kilimo ili kiwe na tija, cha kisasa na chenye masoko ya uhakika. Vilevile, Serikali iweke mikakati thabiti ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi yanayoweza kuathiri sekta ya kilimo Hatua hizi kwa pamoja zitaleta manufaa katika Uchumi.

## 2.3. Mwenendo wa Mfumuko wa Bei

### 2.3.1. Mfumuko wa Bei wa Dunia


**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2024, mfumuko wa bei wa dunia umeendelea kupungua na kufikia wastani wa **asilimia 5.8** ikilinganishwa na wastani wa **asilimia 6.7** mwaka 2023. Kwa nchi zilizoendelea ulifikia wastani wa **asilimia 2.6** mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa **asilimia 4.6** mwaka 2023. Aidha, kwa nchi za Asia zinazoibukia na zinazoendelea ulikuwa wa

wastani wa **asilimia 2.0** mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa **asilimia 2.4** mwaka 2023.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya mwenendo wa mfumuko wa bei duniani kuendelea kuimarika, Kamati imebaini kwamba mfumuko wa bei kwa nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara ulikuwa wastani wa **asilimia 18.3** mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa **asilimia 17.6.** Vilevile, mfumuko wa bei kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ulikuwa wastani wa **asilimia 54.6** mwaka 2024 ikilinganishwa na **asilimia 50.3** mwaka 2023. Aidha, mfumuko wa bei kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ulikua kwa wastani wa **asilimia 23.4** mwaka 2024 ikilinganishwa na **asilimia 15.5** mwaka 2023.

**Mheshimiwa Spika,** kuongezeka kwa kasi ya mfumuko wa bei kwa nchi za Afrika kumetokana na sababu mbalimbali zikiwemo athari za kushuka kwa thamani ya fedha, kushuka kwa uzalishaji katika shughuli za kilimo kwa baadhi ya nchi pamoja na ongezeko la mfumuko wa bei kwa nchi za Zimbabwe, Malawi na Angola.

**Kielelezo Na. 3: Mfumuko wa bei duniani**




***Chanzo:*** *Taarifa ya IMF ya Hali ya Uchumi Aprili, 2025)*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba moja ya sababu iliyosababisha kupanda kwa mfumuko wa bei katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini Mwa Afrika - SADC ni ukosefu wa chakula. Hivyo, Tanzania inaweza kutumia fursa hiyo ili kuzalisha chakula

cha kutosha nchini na kukiuza nje hatua ambayo itasaidia kuongeza mapato ya kigeni.

**2.3.2.Mfumuko wa Bei wa Taifa**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2024 mfumuko wa bei ulifikia wastani wa **asilimia 3.1**, ikilinganishwa na wastani wa **asilimia 3.8** mwaka 2023 na **asilimia 4.3** mwaka 2022. Mwenendo huu uko ndani ya lengo la muda wa kati la **asilimia 5.0** na ndani ya wigo uliowekwa kwa mujibu wa vigezo vya mtangamano wa kiuchumi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), kiwango ambacho hakizidi **asilimia 8.0** na wigo uliowekwa na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) wa kati ya **asilimia 3.0** na **7.0**. kushuka kwa mfumuko wa bei nchini kumechangiwa na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti, kutengemaa kwa bei za mafuta katika soko la dunia na kuimarika kwa upatikanaji wa chakula katika masoko ya ndani na ya nchi jirani.

**Mheshimiwa Spika,** mwenendo huu himilivu wa Mfumuko wa bei nchini umekuwa na manufaa kama vile kuvutia uwekezaji, kulinda thamani ya Shilingi, kuwa na uchumi unaotabirika na kuwa na jamii yenye utulivu. Napenda kumpongeza **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuimarisha uchumi ili kuhakikisha unakuwa imara na unaotabirika.**

**Mheshimiwa Spika,** ili Tanzania iendelee kuwa na mfumuko wa bei himilivu ni lazima kuendelea kuwa na chakula cha kutosha, kudhibiti bei za nishati ikiwa ni pamoja na kutumia nishati inayopatikana nchini ikiwemo gesi asilia, kuchochea uzalishaji wa ndani wa bidhaa za viwandani ili kuepuka mfumuko wa bei unaotokea nje (imported inflation) na kusimamia vyema sera za kifedha kwa sababu mfumuko wa bei ukipanda una athari ya moja kwa moja kwenye riba.

**Jedwali Na 3. Mwenendo wa Mfumuko wa Bei (2020-2024)**

| Mfumuko wa Bei | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | Wastani |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Msingi | 2.3 | 4.1 | 3.0 | 2.3 | 3.4 | 3.02 |
| Chakula | 5.0 | 4.3 | 7.3 | 6.8 | 2.1 | 5.1 |
| Nishati | 5.0 | 3.1 | 9.1 | 2.3 | 9.3 | 5.76 |
| Mfumuko wa Bei | 3.3 | 3.7 | 4.3 | 3.8 | 3.1 | 3.64 |

**Chanzo**: *Taarifa ya Hali ya Uchumi, 2024*

### 2.4. Mwenendo wa Viwango vya Ubadilishaji Fedha

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka, 2024, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa **Shilingi 2,610.5** ikilinganishwa na **Shilingi 2,395.7** katika kipindi kama hicho mwaka 2023, sawa na kushuka thamani ya Shilingi dhidi ya dola ya marekani kwa **asilimia 9.0** ikilinganishwa na **asilimia 3.5** katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Kushuka kwa thamani ya Shilingi dhidi ya dola ya marekani kulichangiwa na masuala mbalimbali ikiwemo kuongezeka sera za fedha za nchi ya Marekani katika kudhibiti mfumuko wa bei pamoja na masalia ya athari za ugonjwa wa **UVIKO - 19**.

**Mheshimiwa Spika,** hali ya upatikanaji wa fedha za kigeni imeendelea kuimarika baada ya mauzo ya mazao ya kilimo kuongezeka pamoja na sekta ya utalii kufanya vizuri. Hata hivyo njia ya uhakika ya kuhakikisha kwamba Shilingi inakuwa na thamani dhidi ya dola na sarafu nyingine za washirika wa kibiashara ni kuongeza mauzo nje ya nchi hasa ya bidhaa zilizoongezwa thamani na huduma. Rai ya kamati kwa Serikali ni kujielekeza kwenye utakelezaji wa miradi ambayo itachochea mauzo nje.

**Jedwali Na. 4: Mwenendo wa Thamani ya Fedha za Nchi za Afrika Mashariki Dhidi ya Dola za Marekani (2021-2024)**

| Fedha | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | % Kushuka Thamini |
|---|---|---|---|---|---|
| **Tanzania (Tsh)** | 2,307.4 | 2,320.2 | 2,395.7 | 2610.5 | 8.9 |
| **Kenya (Ksh)** | 109.7 | 123.4 | 150.0 | 174.51 | 16 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Uganda (Ush)** | 3,586.6 | 3,714.0 | 3,723.01 | 5,152.42 | 38 |
| **Rwanda (RWF)** | 1008.34 | 1035.7 | 1,158.5 | 1,709.56 | 48 |
| **Burundi (BIF)** | 1,974.5 | 12,042.2 | 2,877.5 | 3,798.15 | 32 |

**Chanzo:** IMF, 2025

### 2.5. Akiba ya Fedha za Kigeni

**Jedwali Na.5. Mwenendo wa Akiba ya Fedha za Kigeni (2021-2025)**

| Mwaka | Akiba (USD Bilion) |
|---|---|
| 2021 | 6.56 |
| 2022 | 5.58 |
| 2023 | 5.01 |
| 2024 | 5.30 |
| 2025 | 5.60 |

**Chanzo:** *Taarifa za Hali Uchumi*

### 2.6. Sekta ya Nje

**Mheshimiwa Spika**, thamani ya bidhaa zilizouzwa nje mwaka 2024 ilikuwa **dola za Marekani milioni 9,121.9** sawa na ongezeko la **asilimia 26.28** kutoka **dola za Marekani milioni 7,223.8** mwaka 2023. Aidha, thamani ya huduma zilizouzwa nje mwaka 2024 zilifika **dola za Marekani milioni 4,290.5** sawa na ongezeko la **asilimia 11.85** kutoka **dola za Marekani milioni 3,835.9** mwaka 2023. Urari wa biashara na bidhaa na urari wa huduma kwa pamoja kumechangia kuwa na ziada kwenye urari wa malipo yote wa **dola za Marekani milioni 80.5** mwaka 2024 ikilinganishwa na ziada ya **dola za Marekani milioni 41.9** mwaka 2023.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2024 sekta ya madini iliongoza kwa mchango wa mauzo nje ya nchi kwa **asilimia 45.2** ikifuatiwa na bidhaa za viwandani zilizokuwa na mchango wa **asilimia 14.7**. Aidha, mauzo ya mazao ya sekta ya kilimo

yamechangia **asilimia 20.3** kwa mchanganuo ufuatao: korosho **asilimia 5.9,** tumbaku **asilimia 5.6,** mboga na maua **asilimia 5.6** na kahawa **asilimia 3.2**. Hivyo basi, ili sekta ya nje iendelee kuimarika ni muhimu Serikali ikachochea mauzo ya nje ya nchi ya madini, bidhaa za viwandani na mazao ya kilimo.

### 2.7. Mwenendo wa Viwango vya riba na Huduma za Kibenki

**Mheshimiwa Spika,** wastani wa riba ya dhamana za Serikali za muda mfupi katika soko la fedha baina ya benki uliongezeka kutoka **asilimia 5.37** mwaka 2023 hadi **asilimia 7.50** mwaka 2024, riba ya jumla ya dhamana za Serikali za muda mfupi iliongezeka kutoka **asilimia 7.32** mwaka 2023 hadi **asilimia 10.67** mwaka 2024. Vilevile, wastani wa riba za amana za muda maalumu uliongezeka kutoka **asilimia 7.07** mwaka 2023 hadi **asilimia 7.85** mwaka 2024. wastani wa riba za mabenki kwa amana za mwaka mmoja uliongezeka kutoka **asilimia 8.65** mwaka 2023 hadi **asilimia 9.17** mwaka 2024.

**Mheshimiwa Spika,** wastani wa riba za jumla za mikopo ulipungua kutoka **asilimia 15.75** mwaka 2023 hadi **asilimia 15.47** mwaka 2024. Viwango vya riba za mikopo ya mwaka mmoja vilipungua kutoka **asilimia 16.53** mwaka 2023 hadi **asilimia 15.82** mwaka 2024. Vilevile katika kipindi hicho viwango vya riba kwenye akiba za wateja vilipungua toka **asilimia 10.08** mpaka **asilimia 8.14.** Kamati imebaini kwamba benki za biashara nchini zinahodhi takribani **asilimia 33.1** ya deni la Serikali la ndani kutokana na riba inayotolewa kwenye hati fungani na hivyo kuvutiwa zaidi kuikopesha Serikali kuliko watu binafsi. Kamati inaishauri Serikali kufanya marejeo ya viwango vya riba vya hatifungani za Serikali ili kutoathiri ukopaji wa sekta binafsi.

## 3.0. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/25, Bajeti ya Serikali iliyoidhinishwa na Bunge ilikuwa **Shilingi trilioni 50.29.** Kati ya kiasi hicho **Shilingi trilioni 33.86** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi trilioni 16.43** ni kwa ajili ya matumizi ya

maendeleo sawa na **asilimia 67.34** na **asilimia 32.66** ya bajeti yote mtawalia.

### 3.1. Utekelezaji wa Bajeti katika kipindi cha Julai 2024 hadi Mei, 2025

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Mei, 2025, Serikali imefanikiwa kukusanya jumla ya **Shilingi trilioni 45.07** sawa na **asilimia 89.62** ya bajeti nzima ya Serikali na ikiwa ni pungufu ya **Shilingi trilioni 6.22.** Kwa kuwa wastani wa ukusanyaji wa mapato ni **Shilingi trilioni 4.3** kwa mwezi, ni dhahiri kuwa ifikapo tarehe 30 Juni, 2025 Serikali itakuwa imefikia ukusanyaji kwa zaidi ya **asilimia 98.17** ya lengo la mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** ufanisi huu umekuwepo kwa miaka minne mfululizo. Katika mwaka 2020/21, 2021/22, 2022/23 na 2023/24 Bajeti ya Serikali imekuwa ikitekelezwa kwa **asilimia 89.7, 97.2, 94 na 96.7** mtawalia. Hivyo, bila tashwishwi naomba nimpongeze **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ufanisi huu katika utekelezaji wa bajeti ya Serikali**.

**Mheshimiwa Spika,** Mafanikio hayo yamepatikana kwa sababu zifuatazo:-

i. Kuimarika kwa mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa;
ii. Kutekeleza Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo *(Development Corporation Framework – DCF)* na hivyo kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo;
iii. Kudhibiti matumizi ya fedha za umma yasiyo ya lazima pamoja na kuhimiza nidhamu ya fedha za umma; na
iv. Kutekeleza sera za Fedha na Kibajeti zinazochochea ukuaji wa Uchumi na kupanua wigo wa kodi.

### 3.2. Mwenendo wa Ukusanyaji wa Mapato

**Mheshimiwa Spika,** mapato ya Serikali yanatokana na vyanzo vikuu sita ambavyo ni mapato ya kodi, mapato yasiyo ya kodi,


mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, misaada na mikopo nafuu kutoka nje, mikopo ya ndani pamoja na mikopo yenye masharti ya kibiashara ya nje.

Ukusanyaji wa mapato katika kila chanzo ni kama inavyoonekana hapo chini.

### *3.2.1.Mapato ya Kodi*

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Mei, 2025, jumla ya **Shilingi trilioni 26.86** zilikusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania – TRA sawa na **asilimia 91.23** ya lengo la kukusanya **Shilingi trilioni 29.42**. Aidha ufanisi huu umechagizwa na kuongezeka kwa mapato ya kodi ya forodha ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Februari 2025 jumla ya **Shilingi trilioni 8.26** zilikusanywa, sawa na ongezeko la **Shilingi trilioni 1.18** ikilinganishwa na **Shilingi trilioni 7.08** zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Kamati inaipongeza Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa ufanisi huo wa ukusanyaji wa mapato. "***Kodi Yetu, Maendeleo Yetu".***

**Kielelezo Na. 4. Mwenendo wa Ukusanyaji wa Mapato ya Kodi (1999/00 – 2023/24)**




**Mheshimiwa Spika,** ufanisi wa makusanyo ya kodi umetokana na matumizi ya mifumo ya tehama katika kukusanya mapato, muamko wa wananchi kulipa kodi kwa hiari, ongezeko la rasilimali watu kwa Mamlaka ya Mapato, kukua kwa uchumi na ongezeko la biashara na uwekezaji nchini. Pamoja na mafanikio hayo bado kuna changamoto ambazo zinarudisha nyuma jitihada za Serikali katika kuongeza mapato ya kodi.

Changamoto hizo ni:-

i. **Idadi ndogo ya walipa kodi hai.**
**Mheshimiwa Spika**, hadi Desemba 2024, idadi ya walipa kodi ilikuwa **2,467,049**, kati ya hao mashirika ya umma yalikuwa **257,993** na watu binafsi ni **2,209,056**. Hata hivyo idadi ya walipakodi hai ilikuwa ni **687,565 tu** sawa na **asilimia 27.89.** Hivyo ni lazima kuongeza usajili wa walipa kodi ili kutimiza kauli mbiu ya "**Kodi Yetu, Maendeleo Yetu".**

ii. **Uwepo wa sekta isiyo rasmi.**
**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Taarifa za Benki ya Dunia, sekta isiyo rasmi nchini ni **asilimia 54** ya uchumi. Changamoto hiyo inasababishwa na mazingira yasiyo rafiki kwa wafanyabiashara kuto ona tija ya kurasimisha biashara zao.

iii. **Wingi wa Mamlaka za Udhibiti.**
**Mheshimiwa Spika,** Wafanyabiashara wengi huogopa kuwa rasmi kwa sababu ya ada,tozo na faini zinazokusanywa na Mamlaka za udhibiti na hivyo kuongeza gharama ya biashara.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo:-

i. Kuongeza mchango wa kodi kutoka Biashara ndogo na za Kati *(Small and Medium Medium Enterprises SME's)*. Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania ***(Tanzania Chamber of Commerce, Industry and Agriculture - TCCIA),*** *h*ivi sasa **asilimia 95** ya biashara zote nchini ziko kwenye kundi la SME's na mchango wake kwenye Pato la Taifa ni **asilimia 35**. Hata hivyo, mchango wa biashara zilizo katika kundi hilo kwenye mapato ya kodi yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato ni takribani **asilimia 20.** Hatua hizi ziende sambamba na kuboresha mazingira ya Biashara na uwekezaji na kupunguza mamlaka za udhibiti;

ii. Kurejea upya utaratibu wa ulipaji kodi na viwango vinavyotozwa kwa lengo la kuboresha **na** kuchochea ulipaji wa kodi kwa hiari; na

iii. Kuendelea kutoa elimu ya mlipa kodi ili isaidie kujenga utamaduni wa ulipaji kodi kwa hiari na umuhimu wake katika maendeleo ya nchi.

**Jedwali Na. 6: Mwenendo wa Makusanyo ya Mapato (2022/23 – 2024/25)**

| Idara za Kodi | Mapato ya Ndani | Forodha na Ushuru | Walipa Kodi Wakubwa | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| **2022/23 (Tzs'm)** | 5,277,012 | 9,353,978 | 9,052,690 | 23,683,680 |
| **Uwiano wa mapato ya ndani kwa jumla ya makusanyo (%)** | 22 | 39 | 38 | 100 |
| **2023/24 (Tzs'm)** | 5,276,239 | 10,530,478 | 11,307,720 | 27,114,432 |
| **Uwiano wa mapato ya ndani kwa jumla ya makusanyo (%)** | 19 | 39 | 42 | 100 |
| **2024/25 - hadi Desemba 2024 (Tzs'm)** | 1,754,043 | 3,501,370 | 3,296,742 | 8,552,154 |
| **Uwiano wa mapato ya ndani kwa jumla ya makusanyo (%)** | 21 | 41 | 39 | 100 |

***Chanzo**: Tanzania Chamber of Commerce, Industry and Agriculture - TCCIA*

### *3.2.2.Mapato yasiyo ya Kodi*

**Mheshimiwa Spika,** mapato yasiyo ya kodi yanatokana na makusanyo ya Wizara, Idara, Mamlaka, Wakala na Taasisi za Serikali kulingana na fursa za mapato zilizopo katika sekta husika. Hadi kufikia Mei, 2025 jumla ya **Shilingi trilioni 2.97** zilikusanywa sawa na **asilimia 77.34** ya lengo la mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha miaka minne **kuanzia** 2020/21 hadi 2023/24 mapato yasiyo ya kodi yamekuwa yanakusanywa kwa wastani wa **asilimia 78.33.** Pamoja na kwamba ufanisi huu ni wa kiwango cha kuridhisha, mapato hayo yangeweza kukusanywa zaidi endapo mifumo ingetumika katika kukusanya ada na tozo. Aidha, baadhi ya Mashirika ya umma yana ufanisi mdogo katika utendaji kazi ikilinganishwa na fursa zilizopo. Sababu nyingine inayochangia ukusanyaji hafifu ni kutokukamilika kwa miradi ya sekta husika iliyotarajiwa kuongeza mapato. Mfano miradi ya umwagiliaji chini ya Tume ya Umwagiliaji.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa maduhuli pamoja na kuchukua hatua za kinidhamu kwa Wizara, Idara, na Taasisi za Serikali ambazo hazitatumia mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato.

***3.2.3.Mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa***

**Mheshimiwa Spika,** Serikali za Mitaa zilikusudia kukusanya jumla ya **Shilingi trilioni 1.36.** Hadi Mei, 2025 kiasi cha **Shilingi trilioni 1.26** kilikusanywa sawa na **asilimia 92.65** ya lengo la mwaka. Ufanisi huu umetokana na matumizi ya Mfumo wa Tausi katika ukusanyaji wa mapato. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutumia mfumo huu ambao umepunguza upotevu wa mapato ya Serikali za Mitaa.

**Mheshimiwa Spika,** moja ya chanzo cha mapato ya Serikali za mitaa ni kodi ya majengo. Hata hivyo, chanzo hicho bado hakijaweza kuchangia kikamilifu mapato ya Serikali za Mitaa. Ili chanzo hiki kiweze kuchangia kikamilifu, Kamati inaishauri Serikali kukamilisha usajili wa majengo ili kuanza kutoza kodi ya jengo kwa thamani ya nyumba na sio kiwango mfuto kinachotumika hivi sasa. Hatua hii itaongeza mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa na kuweza kujitegemea kimapato.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba kuna kasi ndogo ya usajili kutokana na sababu mbalimbali hususan ukosefu wa fedha kwa ajili ya kutekeleza shughuli hiyo.

Hivi sasa Halmashauri zinarejeshewa **asilimia 20** ya kodi ya majengo ambazo zinapaswa kutumika kwa ajili ya kufanya usajili. Kiasi hicho hakitoshelezi mahitaji. Hivyo, Serikali ione umuhimu wa kuziwezesha Halmashauri kifedha ili ziweze kutekeleza kazi hii mapema iwezekanavyo.

***3.2.4.Misaada na Mikopo Nafuu Kutoka Nje***

**Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Mei, 2025 jumla ya kiasi cha **Shilingi trilioni 5.32** kilipokelewa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo sawa na **asilimia 87.5** ya lengo la mwaka la kukopa **Shilingi trilioni 6.08.** Ufanisi huu unatokana na Serikali kuendelea kutekeleza makubaliano ya kimkataba ikiwemo kusimamia ukuaji wa uchumi, kuongeza ukusanyaji wa mapato, kuboresha huduma za jamii na kusimamia matumizi ya fedha za umma. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuimarisha mahusiano yake na Washirika wa Maendeleo hivyo kuendelea kupata fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

***3.2.5.Mikopo ya Ndani***

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/25, Serikali ilikusudia kukopa **Shilingi trilioni 6.62** kutoka soko la ndani kwa ajili ya kulipia hatifungani zilizoiva na kutekeleza miradi ya maendeleo**.** Hadi mwezi Mei, 2025 kiasi cha **Shilingi trilioni 6.23** zilikopwa sawa na **asilimia 94.1** ya lengo. Ufanisi huu unaashiria uwezo wa Serikali kukopa na kulipa. Kwa kuwa miongozo ya Benki Kuu inaruhusu Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuwekeza hadi **asilimia 100** ya michango ya wanachama.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri kwamba asilimia kubwa ya michango ya wanachama kuwekezwa katika dhamana za Serikali ukizingatia kuwa ni salama zaidi ikilinganishwa na maeneo mengine ya uwekezaji. Vilevile, Serikali iendelee kuhamasisha watu binafsi kushiriki katika ununuzi wa dhamana za Serikali ili kugharamia miradi ya maendeleo.

***3.2.6.Mikopo ya Masharti ya Kibiashara***

**Mheshimiwa Spika,** hadi mwezi Mei, 2025 mikopo ya masharti ya kibiashara ya nje ilifikia **Shilingi trilioni 2.43** sawa na **asilimia 81.27** ya lengo la mwaka la kupokea **Shilingi trilioni 2.99** kwa

ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Ufanisi huu umetokana na matokeo ya tathmini ya uwezo wa nchi kukopesheka iliyofanywa na kampuni za *Moody's Investors Service* na *Fitch Ratings* ambayo yaliiweka Tanzania katika Daraja la B1 na B+ mtawalia. Aidha, pamoja na mafanikio hayo Kamati bado inaendelea kuishauri Serikali kutumia vyanzo bunifu kama vile, hatifungani za manispaa na hatifungani za miundombinu ili kupunguza utegemezi wa mikopo kutoka nje ambayo haitabiriki na ni gharama.

### 3.3. Mwenendo wa Matumizi

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/25 Serikali iliweka maeneo ya vipaumbele yenye lengo la kuweka chachu ya ukuaji wa uchumi na kuongeza ajira. Hadi mwezi Mei 2025, ridhaa ya matumizi iliyokuwa imetolewa na Serikali ilikuwa **Shilingi trilioni 42.90** sawa na **asilimia 85.31** ya bajeti ya Serikali ya **Shilingi trilioni 50.29**. Kati ya fedha hizo matumizi ya kawaida ni **Shilingi trilioni 30.63** sawa na **asilimia 90.8** ya lengo la mwaka la **Shilingi trilioni 34.94**. Aidha, kiasi cha **Shilingi trilioni 15.74** kilitolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo sawa na **asilimia 95.8** ya lengo la mwaka la **Shilingi trilioni 16.43.**

**Jedwali Na. 7. Fedha za Matumizi ya Maendeleo (2020/21 – 2024/25 (Bilioni)**

| MWAKA | BAJETI | BAJETI YA MAENDELEO | ASILMIA |
|---|---|---|---|
| **2020/21** | 34,879.8. | 12,779.3 | 36.64 |
| **2021/22** | 37,992.5 | 15,259.7 | 40.17 |
| **2022/23** | 41,480.6 | 15,006 | 36.18 |
| **2023/24** | 44,388.1 | 14,077.22 | 31.71 |
| **2024/25** | 50,291.4 | 16,427.7 | 32.67 |

#### *3.3.1. Ugharamiaji wa Deni la Serikali*

**Mheshimiwa Spika,** hadi mwezi Mei, 2025 Serikali ilitumia jumla ya **Shilingi trilioni 11.16** kwa ajili ya kugharamia deni la Serikali ikiwa ni **asilimia 85.06** ya lengo la mwaka la **Shilingi trilioni 13.12.** Pamoja na uwepo wa changamoto ya kushuka kwa thamani ya shilingi inayoathiri ulipaji wa deni, Serikali imeweza

kulipa madeni yake kama ilivyopanga. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua ilizozichukua katika kuimarisha thamani ya Shilingi dhidi ya dola ya Marekani ambazo zimeenda kupunguza gharama kwenye malipo ya deni la nje ambalo **asilimia 62** lipo kwenye dola za marekani. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kukopa kwa kutumia sarafu zaidi ya moja (currency diversification) ili kupunguza ongezeko la deni endapo thamani ya Shilingi itashuka dhidi ya dola ya Marekani.

***3.3.2.Matumizi ya Maendeleo***

**Mheshimiwa Spika,** hadi mwezi Mei, 2025 ridhaa ya matumizi ya maendeleo iliyotolewa ilikuwa **Shilingi trilioni 15.74** sawa na **asilimia 95.8** ya lengo la mwaka la **Shilingi trilioni 16.43.** Katika kipindi hicho, Serikali iliendelea kugharamia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwa ni pamoja na ukamilishaji wa miradi ya Bwawa la Julius Nyerere (JNHPP) MW 2,115, Daraja la Kigongo Busisi na treni ya kisasa ya SGR.

## 4.0. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2024/25 PAMOJA NA UCHAMBUZI WAMAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFAKWA MWAKA 2025/26

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa mwaka 2024/25 ni wa nne katika utekelezaji wa Mpango wa tatu wa maendeleo wa miaka mitano (2021/22 – 2025/26). Mpango huo ulikuwa na dhima ya Kujenga "***Uchumi Shindani na wa viwanda kwa Maendeleo ya Watu"***. Mpango wa mwaka 2024/25 ulitarajiwa kugharimu kiasi cha **Shilingi trilioni 16.43** sawa na **asilimia 32.67** ya bajeti yote ya Serikali. Kati ya fedha hizo, **Shilingi trilioni 12.78** ni fedha za ndani na **Shilingi trilioni 3.64** ni fedha za nje. Hadi kufikia mwezi Mei, 2025 jumla ya **Shilingi trilioni 15.74** zilitolewa sawa na **asilimia 95.1**. **Kamati inampongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa nia yake thabiti ya kuwaletea Watanzania maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa mwaka 2025/26 ni wa mwisho katika utekelezaji wa Mpango

wa tatu wa maendeleo wa miaka mitano (2021/22 – 2025/26). Mpango huo unatarajiwa kugharimu kiasi cha **Shilingi trilioni 17.49** sawa na **asilimia 30.96** ya bajeti yote ya mwaka 2025/26. Mpango huu umejikita katika kuendeleza na kukamilisha utekelezaji wa afua zinazotoa matokeo katika maeneo sita ya kipaumbele ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambayo ni:-

i. Ukuaji endelevu wa uchumi;
ii. Kupunguza umaskini;
iii. Kuzalisha ajira;
iv. Kuimarishwa kwa ushindani katika masoko ya Kikanda na Kimataifa;
v. Maendeleo endelevu; na
vi. Utawala bora.

***4.1.1.Sekta ya Afya***

**Mheshimiwa Spika,** sekta hii ilipangiwa kutumia jumla ya **Shilingi trilioni 1.31** katika mwaka wa fedha 2024/25. Hadi kufikia mwezi Machi, 2025 jumla ya **Shilingi trilioni 1.23** zilipokelewa sawa na **asilimia 94**. Katika mwaka wa fedha 2025/26 sekta hii imeidhinishiwa bajeti ya **Shilingi trilioni 1.62** sawa na ongezeko la **asilimia 23.67.** Aidha, katika kipindi cha miaka mitano (2021/22 – 2025/26) tumeshuhudia bajeti ya sekta hii ikiongezeka kutoka **Shilingi trilioni 1.03** hadi **Shilingi trilioni 1.62** sawa na ongezeko la **asilimia 56.47**. Hakika haya ni maendeleo makubwa na Kamati inaipongeza Serikali inayoongozwa na **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa uongozi mahiri ambao umeleta mageuzi makubwa katika sekta ya afya. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni kama ifuatavyo:-

i. Ukuaji wa sekta hii kwa **asilimia 10.3** mwaka 2024 na kuchangia **asilimia 1.3** katika Pato la Taifa;
ii. Kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya ambapo vituo vya kutolea huduma za afya nchini vimeongezeka kutoka vituo **8,458** mwaka 2020 hadi **9,826** mwaka 2024 sawa na ongezeko la **asilimia 16.17;**

iii. Kukamilika kwa awamu ya kwanza ya ujenzi na kuanza kutoa huduma kwa hospitali mpya za Rufaa katika mikoa ya Songwe, Geita, Simiyu na Katavi;
iv. Ujenzi wa vituo vya afya katika kila Tarafa na baadhi ya Kata za kimkakati;
v. Kuimarika kwa hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kufikia **asilimia 86.0** mwaka 2024 ikilinganishwa na **asilimia 75.6** mwaka 2023;
vi. Kupunguza idadi ya vifo vitokanavyo na uzazi kufikia **104** kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2022 na kuvuka lengo la vifo 180 mwaka 2025/26;
vii. Kuongezeka kwa wastani wa idadi ya uzazi uliohudumiwa na mhudumu wa afya mwenye ujuzi kufikia **asilimia 94.7** mwaka 2023 ikilinganishwa na lengo la **asilimia 85** kwa kila vizazi 1000 mwaka 2025/26;
viii. Wajawazito wanaojifungulia katika vituo vya afya kufikia **asilimia 86** mwaka 2022 ikilinganishwa na **asilimia 80** mwaka 2020,
ix. Kuongezeka kwa wastani wa umri wa kuishi kutoka **miaka 67.8** mwaka 2023 hadi ya **miaka 68.0** mwaka 2024; na
x. Kuwezesha **asilimia 80** ya wananchi kupata huduma za afya ndani ya **kilomita 5**.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo bado sekta hii inakabiliwa na ukosefu wa watoa huduma, wauguzi wanoendana na ongezeko la vituo vya afya, ukosefu wa vifaa tiba na dawa, na ongezeko la magonjwa yasiyoambukizwa. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutatua changamoto hizo ili kuboresha ustawi wa wananchi kupitia utolewaji wa huduma za afya zenye ubora.

### *4.1.2.Sekta ya Elimu*

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/25 sekta ya elimu ilitengewa bajeti ya **Shilingi trilioni 1.97** ambapo hadi kufika Aprili, 2025 jumla ya **Shilingi trilioni 1.54** zilitolewa sawa na **asilimia 78.17.** Katika mwaka wa fedha 2025/26 sekta hii imeidhinishiwa jumla ya **Shilingi trilioni 2.44** sawa na ongezeko la **asilimia 23.86.** Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada

ilizochukua ili kuhakikisha kila mtanzania anapata elimu bora na hili linathibitishwa na baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika sekta hii ambayo baadhi ni:-

i. Kuongezeka kwa bajeti ya Wizara ya Elimu kutoka **Shilingi trilioni 1.39** mwaka 2021/22 hadi **Shilingi trilioni 2.44** mwaka 2025/26 sawa na ongezeko la **asilimia** 56.97;
ii. Kuongezeka kwa bajeti ya mikopo ya elimu ya juu na vyuo vya kati kutoka **Shilingi bilioni 570** mwaka 2021/22 hadi **Shilingi bilioni 784.4** mwaka 2024/25 na kuwezesha wanafunzi wengi hasa watoto wanaotoka katika familia za kipato cha chini kupata elimu;
iii. Kuendelea na sera ya elimu bila ada kuanzia shule za awali hadi kidato cha 6 na hivyo kuongeza ari ya uandikishaji wa wanafunzi katika shule za msingi na sekondari;
iv. Mtaala mpya wa elimu kuanza kutekelezwa;
v. Kutoa ajira **229,840** kwa walimu wa shule za msingi, **128,686** walimu wa shule za sekondari, **1,633** walimu wa vyuo vya ualimu na wahadhiri **8,625**;
vi. Ujenzi wa shule za amali nchini ambazo zitawezesha wanafunzi kupata elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi; na
vii. Kuandaa Mwongozo wa Matumizi ya akili mnemba (Artificial Intelligence) katika Elimu; na viii. Ukuaji wa **asilimia 6.2** na kuchangia **asilimia 2.2** kwenye Pato la Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo bado sekta hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile uhaba wa walimu usioendana na ongezeko la idadi ya wanafunzi; upungufu wa miundombinu ya kufundisha na kufundishia; mdondoko wa wanafunzi (drop out); matumizi hafifu ya sayansi na teknolojia pamoja na kutokutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya utafiti. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutatua changamoto hizo katika mwaka wa fedha 2025/26 ili kuboresha sekta hiyo na kufikia lengo la kuwa na jamii

iliyoelimika. Vilevile, Serikali iendelee kuhamasisha matumizi ya TEHAMA katika ngazi zote za elimu.

### *4.1.3.Sekta ya Mifugo na Uvuvi*

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2024 sekta ya mifugo na uvuvi zimekua kwa wastani wa **asilimia 5.5** na kuchangia **asilimia 4.05** katika Pato la Taifa. Sekta ya uvuvi pekee imechangia **asilimia 3** ya mapato yanayotokana na mauzo nje. katika kipindi cha miaka minne kuanzia 2021/22 hadi 2024/25 bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeongezeka kutoka **Shilingi bilioni 169.19** hadi **Shilingi bilioni 460.33** sawa na ongezeko la **asilimia 172.08**. Mafanikio mengine yaliyopatikana katika sekta hii ni:-

i. Kuongezeka kwa viwanda vya kuchakata nyama inayouzwa nje ya nchi kutoka viwanda vitatu hadi saba;
ii. Kupungua kwa kiwango cha magonjwa ya mifugo kutoka **asilimia 5** mwaka 2021/22 hadi **asilimia 2.5** mwaka 2024/25;
iii. Kuongezeka kwa uzalishaji wa nyama kutoka **tani 769,966.65** mwaka 2021/22 hadi **tani 1,054,114.03** mwaka 2024/25;
iv. Kuongezeka kwa Mauzo ya nyama nje ya nchi kutoka **tani 10,415** mwaka 2021/22 hadi **tani 14,900** mwaka 2024/25;
v. Ujenzi wa bandari ya uvuvi Kilwa Masoko ambao umefikia **asilimia 81.9**;
vi. Kuongezeka kwa mauzo ya mazao ya uvuvi nje ya nchi kutoka **tani 167,256.16** mwaka 2021/22 hadi **tani 199,387.26** mwaka 2024/25 ; na
vii. Kutoa ajira kwa watanzania zaidi ya **milioni 6.**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo mchango wa sekta hii katika Pato la Taifa bado ni mdogo ikilinganishwa na nchi nyingine kama Namibia na Mauritania ambazo huchangia **asilimia 10** na nchi ya Ushelisheli ambayo huchangia **asilimia 16** ya Pato la Taifa. hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuhamasisha sekta binafsi kushiriki katika uvuvi wa bahari kuu, kuongeza thamani ya mazao kabla ya

kuyasafirisha nje, kuendelea kuboresha afya ya mifugo sambamba na kuajiri maafisa ugani wa kutosha na kuwapatia vitendea kazi. Hatua hizi kwa pamoja zitaongeza mchango wa Sekta hii katika pato la Taifa.

***4.1.4.Sekta ya Miundombinu***

**Mheshimiwa Spika,** Katika sekta ya miundombinu Serikali imepata mafanikio yafuatayo:-

i. Kuongezeka kwa mizigo inayotoka nje kuelekea nchi za jirani kupitia nchini kutoka tani **milioni 30.1** mwaka 2021/22 hadi tani **milioni 34.7**;
ii. Kupungua kwa gharama za uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam kutoka **Shilingi bilioni 975.0** hadi **Shilingi bilioni 685.2**;
iii. Ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege 11 nchini;
iv. Ununuzi wa ndege saba ambapo ndege sita ni za abiria na ndege moja ni ya mizigo, na hivyo Shirika kuwa na jumla ya ndege 16 kutoka ndege tisa zilizokuwepo mwaka 2020/21;
v. Kuongezeka kwa mtandao wa barabara zinazounganisha wilaya, mikoa na nchi jirani zinazosimamiwa na TANROADS kutoka **kilometa 36,361.95** mwaka 2021 hadi **kilometa 37,435.04** Aprili 2025. Aidha, mtandao wa barabara umeongezeka kutoka **kilometa 108,946.18** mwaka 2020 hadi **kilometa 144,429.77** mwaka 2025; na
vi. Ukamilishaji wa ujenzi wa daraja la Kigongo – Busisi lenye urefu wa **kilometa 3** na barabara unganishi zenye urefu wa **kilometa 1.66**.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio haya sekta hii inakabiliwa na changamoto zifuatazo; wakandarasi kutolipwa kwa wakati, ukarabati wa barabara kutofanyika kwa wakati, barabara za vijijini kujengwa chini ya kiwango na hivyo kuharibika kipindi cha mvua, uwepo wa wakandarasi wasio na uwezo, baadhi ya wasafirishaji kuzidisha uzito na ushirikishwaji duni wa Sekta Binafsi katika ujenzi na uendelezaji wa miundombinu. Kamati inaamini changamoto hizi zikifanyiwa kazi manufaa mengi zaidi yatapatikana kupitia miundombinu

***4.1.5.Sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji***

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2024/25 sekta ya viwanda ilitengewa Bajeti yenye jumla ya **Shilingi bilioni 110.89,** hadi mwezi Machi, 2025 **Shilingi bilioni 89.52** zilikuwa zimetolewa sawa na **asilimia 80.72.** Sekta ya viwanda imekuwa na mafanikio yafuatayo:-

i. Imekuwa kwa **asilimia 4.8** na kuchangia **asilimia 7.3** kwenye Pato la Taifa;
ii. Mchango wake kwenye mauzo nje ya nchi umeongezeka hadi kufika **asilimia 39** ya mauzo yote ya nje na hivyo kuchangia **asilimia 19** ya mapato yote ya mauzo ya bidhaa nje;
iii. Kuchangia **asilimia 12.8** ya ajira pamoja na kuchangia **asilimia 19** katika mapato ya mauzo nje ya nchi; na
iv. Kuongezeka kwa thamani ya miradi ya uwekezaji kutoka **dola za Marekani bilioni 2.37** mwaka 2021/22 hadi **dola za Marekani bilioni 8.81**ya mwaka 2024/25;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuchukua hatua mbalimbali za kukuza na kuendeleza viwanda pamoja na kuboresha mazingira ya ufanyaji wa biashara na uwekezaji. Baadhi ya hatua zilizochukuliwa ni kufanya maboresho ya Sheria 12 ili kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji na kuleta unafuu kwa wawekezaji wa sekta binafsi. Aidha, Serikali imefuta au kupunguza tozo, ada na faini zipatazo **383** zilizobainishwa kuwa kero katika ufanyaji wa biashara.

Hatua zote hizi zina lengo la kutekeleza Mpango wa Pili wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji nchini. Ili kuongeza ufanisi katika sekta ya viwanda, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta hii, ikiwemo kurahisisha mfumo wa ulipaji wa kodi kwa kuanzisha sera ya kodi, kupunguza Mamlaka za udhibiti, kudhibiti biashara za magendo na kutekeleza miradi iliyokwama kwa muda mrefu.

***4.1.6.Sekta ya Madini***

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2024/25 sekta ya madini ilitengewa bajeti ya **Shilingi bilioni 531.27** na hadi kufika Machi, 2025 sekta hii ilikuwa imepokea **Shilingi bilioni 392.36** sawa na **asilimia 73.85**. Aidha, katika mwaka 2024 sekta hii imekua kwa **asilimia 8.3** na kuchagia **asilimia 10.1** katika Pato la Taifa. **Kamati inaipongeza Serikali inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** katika kipindi cha uongozi wake bajeti ya Wizara ya Madini imeongezeka kutoka **Shilingi bilioni 66.82** mwaka 2021/22 hadi **Shilingi bilioni 531** mwaka 2024/25 sawa na ongezeko la **asilimia 695.08.** Ongezeko hilo linaonyesha nia ya dhati ya kuboresha sekta ya madini. Yafuatayo ni baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka minne:-

i. Kupungua kwa asilimia ya mauzo ya madini ghafi nje kutoka **asilimia 10.45** mwaka 2022/23 hadi **asilimia 9** mwaka 2023/24;
ii. Kuongezeka kwa idadi ya leseni katika shughuli za madini kutoka leseni **9,642** mwaka 2022/2023 hadi leseni **11,510** mwaka 2023/2024 zikiwemo leseni **8,795** za uchimbaji mdogo wa madini;
iii. Kuongezeka kwa viwanda 13 vya kuchenjua dhahabu;
iv. Kuongezeka kwa mchango katika mapato yatokanayo na mauzo ya bidhaa nje kutoka asilimia 45.9 mwaka 2021/22 hadi asilimia 60 mwaka 2023/24;
v. Kuongezeka kwa mapato ya fedha za nje kutoka dola za Marekani bilioni 3.05 mwaka 2021/22 hadi dola za Marekani bilioni 4.12 mwaka 2024/25;
vi. Kudhibiti utoroshwaji wa madini;
vii. Kuhamasisha uwekezaji kwenye shughuli za madini;
viii. kurejesha minada ya madini ya vito; na ix. Ununuzi wa mitambo 10 ya uchorongaji miamba kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilianzisha utaratibu wa kununua dhababu fedha kama sehemu ya akiba ya fedha za kigeni. Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi huo kwani

umewezesha upatikanaji wa dhahabu kwa ajili ya Hazina ya Taifa ya fedha za kigeni (Foreign Reserves), ambapo hadi Mei 2025 Benki Kuu ilinunua takribani **tani 4.8** za dhahabu iliyozalishwa na kuchakatwa hapa nchini. Hata hivyo, ili kuendelea kuongeza ufanisi na tija katika sekta hii, Kamati inaishauri Serikali kufanya mabadiliko ya Sheria zote ambazo zinakwamisha uwekezaji kwenye sekta ya madini, kupunguza kodi, kudhibiti utoroshwaji wa madini na kuhakikisha kuwa madini yanaongezwa thamani nchini kabla ya kusafirishwa kwenda nje.

***4.1.7.Sekta ya Utalii***

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2023/24 sekta ya utalii ilichangia **asilimia 17.2** ya Pato la Taifa na kuchangia **asilimia 26** ya mapato ya fedha za kigeni na hivyo kuwa miongoni mwa sekta zinazochangia kwa kiasi kikubwa katika Pato la Taifa. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuimarisha sekta ya maliasili na utalii kwa kuendeleza na kukuza vivutio mbalimbali vya utalii ikiwemo kuanzishwa kwa Programu maalum za kuitangaza Tanzania kimataifa kama vile filamu ya Tanzania – *The Royal Tour* pamoja na filamu ya *Amazing Tanzania*.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na jitihada hizo, idadi ya watalii imeongezeka kutoka watalii **1,183,416** mwaka 2020 hadi watalii **5,360,247** mwaka 2024 sawa na ongezeko la **asilimia 352.95**. Vilevile, mapato yatokanayo na watalii wa nje ya nchi yameongezeka kutoka **dola za Marekani milioni 715.0** mwaka 2020 hadi **dola za Marekani bilioni 3.9** mwaka 2024. Mafanikio hayo yameiwezesha Tanzania kutambulika Kimataifa ambapo imeshika nafasi ya tisa duniani na nafasi ya tatu barani Afrika mwaka 2024 kwa ongezeko la mapato yatokanayo na shughuli za utalii, ikilinganishwa na kipindi cha kabla ya janga la **UVIKO-19**.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia mchango wa sekta hii katika uchumi, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa Mamlaka za Uhifadhi zinatengewa fedha za kutosha kwa ajili ya kuendeleza miundombinu muhimu ya sekta hii na kujiendesha kwa ufanisi. Aidha, Serikali pia itenge fedha za kutosha kwa ajili

kutangaza nchi yetu Kimataifa ili kuvutia watalii wengi zaidi. Hatua hizi ziende sambamba na kurejewa kwa mifumo ya kodi na tozo ili kutatua changamoto zilizopo.

#### *4.1.8. Sekta ya Ardhi na Mazingira*
#### *4.1.8.1. Sekta ya Ardhi*
**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/25 sekta hii ilitengewa bajeti ya **Shilingi bilioni 243.46** na hadi kufika mwezi Mei, 2025 jumla ya **Shilingi bilioni 189.55** zilitolewa sawa na **asilimia 77.86** ya utekelezaji. Katika kipindi hicho, Wizara iliandaa na kusajili vyeti vya Ardhi ya Kijiji **766** hivyo kuwa na jumla ya vijiji **10,987** vyenye Vyeti vya Ardhi ya Kijiji kati ya vijiji **12,333** vilivyopo nchini. Katika kipindi hicho pia kumekuwa na ongezeko la utoaji na usajili wa Hatimiliki kutoka Hati **67,331** katika mwaka 2020/21 hadi Hati **99,366** mwaka 2023/24.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo bado sekta hii inakabiliwa na changamoto zifuatazo:- kukithiri kwa migogoro ya ardhi, uanzishwaji na uendelezaji wa makazi holela, kukosekana kwa mipango miji, kuchelewa kwa utolewaji wa hatimiliki, biashara holela ya ardhi na matumizi hafifu ya teknolojia. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutatua changamoto hizi ili kuchochea matumizi bora ya ardhi.

#### *4.1.8.2. Sekta ya Mazingira*
**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya mazingira nchini ni muhimu kwa maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi. Sekta hii ina jukumu la kulinda rasilimali za asili kama misitu, maji, hewa safi, ardhi, viumbe hai, pamoja na udhibiti wa taka, uchafuzi wa mazingira na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo. Katika mwaka 2024/25 sekta hii ilitengewa jumla ya **Shilingi bilioni 45.72** na hadi kufikia mwezi Machi, 2025 jumla ya **Shilingi bilioni 29.49** zilipokelewa sawa na **asilimia 64**.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha miaka mitano bajeti ya sekta hii imeongezeka kutoka **Shilingi bilioni 19.99** mwaka 2021/22 hadi Shilingi **bilioni 61.92** sawa na ongezeko la **asilimia 209.75.** Kamati inaipongeza Serikali kwa kutambua umuhimu wa sekta hii na kuiwezesha wizara kwa rasilimali fedha ili

kuendelea kutekeleza majukumu mbalimbali. Aidha, katika mwaka 2024 sekta hii ilikua kwa **asilimia 6** kutoka **asilimia 2.5** mwaka 2021 na kuchangia **asilimia 6** kwenye Pato la Taifa kutoka **asilimia 3.5** mwaka 2021.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo bado nchi haijaweza kunufaika kikamilifu na Mifuko inayofadhili afua za mazingira ikiwa ni pamoja na Mfuko wa Mazingira Duniani (GEF), Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (GCF) pamoja na Mfuko wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi (Adaptation Fund). Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuongeza ushawishi wake katika Mifuko hiyo ili iweze kupata rasilimali fedha za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

## 5.0. HOJA MAHSUSI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 117 fasili ya 3 na 4 na Kanuni ya 124 fasili ya 1 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ina jukumu la kufanya mashauriano kuhusu masuala muhimu yaliyojitokeza Bungeni wakati wa kujadili utekelezaji wa Bajeti za Wizara kwa mwaka wa fedha unaoisha na makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/24 masuala 22 yaliibuka wakati wa mjadala Bungeni kwa mujibu wa Kanuni ya 124(1). Kati ya masuala hayo, masuala 10 yalihitaji ufuatiliaji na masuala 12 Kamati ilikubaliana na hatua za utekelezaji zilizochukuliwa na Serikali. Vilevile katika mwaka wa fedha 2024/25, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(3) na (4), masuala 17 yaliibuliwa na Kamati za Kisekta. Kati ya masuala hayo, masuala 7 yalihitaji ufuatiliaji na masuala 10 Kamati ilikubaliana na hatua za utekelezaji zilizochukuliwa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ninayoiwasilisha ni muhtasari wa ufuatiliaji wa maagizo ya Kamati ya Uongozi kwa Serikali kuhusiana na baadhi ya masuala muhimu.

## 5.1. Utekelezaji wa Masuala Muhimu kwa Mujibu wa Kanuni ya 124 (1) Yaliyotokana na Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 na Makadirio ya Bajeti ya Mwaka 2024/25

### *5.1.1. Hoja zilizotekelezwa kikamilifu na Serikali kutokana na Maagizo ya Kamati ya Uongozi.*

#### 5.1.1.1. Mgawanyo wa Fedha za Mfuko wa Maji

**Mheshimiwa Spika,** Fedha za Mfuko wa maji zilikuwa zimegawanyika katika makundi mawili ambapo miradi ya maendeleo ilikuwa inachukua **asilimia 88** na gharama za uendeshaji zilikuwa zinachukua **asilimia 12** ya mapato yote. Changamoto iliyokuwepo ni kanuni kutobainisha kati ya **asilimia 88** ni asilimia ngapi inaelekezwa kwenya miradi ya maji inayotekelezwa vijijini chini ya RUWASA na asilimia ngapi inapelekwa kwenye Mamlaka za Maji zinazotekeleza miradi ya maji mijini.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imefanya marekebisho ya Kanuni za Mfuko wa Taifa wa Maji za Mwaka 2019 kupitia Tangazo lililotolewa kwenye Gazeti la **Serikali** Na. 266 la Tarehe 2/5/2025 *(The National Water Fund (Amendment) Regulations, 2025)*. Kanuni hizo zimebainisha mgao kama ifuatavyo: **asilimia 60** ya fedha za Mfuko zitaelekezwa RUWASA kwa ajili ya miradi ya maji vijijini**, asilimia 29** zitaelekezwa katika Mamlaka za Maji kwa ajili ya miradi ya maji mijini, **asilimia 10** zitaelekezwa katika shughuli za uhifadhi na ulinzi wa vyanzo vya maji kupitia Bodi za Maji za Mabonde na **asilimia moja** itaelekezwa katika kuimarisha ubora wa maji.

#### 5.1.1.2. Kurejesha ukusanyaji wa Mapato kwa Mamlaka ya Bandari (TPA).

**Mheshimiwa Spika,** kulikuwa na hoja ya kurejesha ukusanyaji wa mapato yanayotokana na tozo ya Gati *(Wharfage)* kwa Mamlaka ya Bandari (TPA) kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Serikali ilikubali pendekezo hilo na kufanya mabadiliko kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2024 na kurejesha jukumu hilo kwa Mamlaka ya Bandari**.**

**Mheshimiwa Spika**, hatua hizo za utekelezaji zinaonyesha nia ya dhati ya Serikali inayoongozwa na **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kutekeleza maagizo ya Kamati ya Uongozi. Hakika 4R za **Mhe. Rais** anazitekeleza kwa vitendo.

### 5.2. Hoja ambazo zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji

#### *5.2.1. Urejeshaji wa ukusanyaji wa Mapato kwa Mamlaka za TAWA, TANAPA na NCAA.*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa kwamba Serikali itashughulikia suala hili wakati wa kujadili muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2025.

#### *5.2.2. Urejeshwaji wa ukusanyaji wa tozo ya abiria kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania* (Tanzania Aviation Authority-TAA).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa kwamba mpaka hivi sasa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege haijawasilisha mpango wa namna watakavyotumia makusanyo hayo kufanya uwekezaji endapo jukumu la ukusanyaji litakaporejeshwa ili kuongeza mapato zaidi. Hivyo, Kamati inaitaka TAA kuwasilisha mpango huo kwa Wizara ya Fedha ili uchambuliwe na pale ambapo itaona unafaa warejeshewe ukusanyaji na matumizi ya mapato hayo kama Serikali ilivyofanya kwa Mamlaka ya Bandari.

### 5.3. Utekelezaji wa Masuala Muhimu kwa Mujibu wa Kanuni ya 117(3) na (4) yaliyotokana na Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 na Makadirio ya Bajeti ya Mwaka 2025/26

#### 5.3.1. Utoaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya vya kimkakati na umaliziaji wa maboma yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** utakumbuka kwamba katika marejeo ya Bajeti ya Serikali mwezi Februari Mwaka 2025 (Supplementary Budget), Serikali ilikubali kutenga jumla ya **Shilingi 123,500,000,000** kwa ajili ya kukamilisha maboma na ujenzi wa vituo vya afya vya kimkakati. Kati ya fedha hizo **Shilingi 70,000,000,000** ni kwa ajili ya maboma na **Shilingi**

**53,500,000,0000** ni kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya vya kimkakati. Hadi tarehe 31 Mei, 2025 Serikali ilikuwa imetoa jumla ya **Shilingi 70,000,000,000.** Kati ya kiasi hicho **Shilingi 40,000,000,000** zimetolewa kwa ajili ya ukamilishaji wa Maboma na **Shilingi 30,000,000,000** zimetolewa kwa ajili ya vituo vya afya vya kimkakati.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia utolewaji huu wa fedha, Kamati inaitaka Serikali kutekeleza masuala yafuatayo: -

i. Serikali kutoa kiasi kilichobaki cha **Shilingi 53,500,000,000** ili kiende kumaliza awamu ya pili ya ujenzi wa vituo vya afya vya kimkakati pamoja na maboma yaliyoanzishwa kwa nguvu ya wananchi; na
ii. Kwa kuwa mwaka wa fedha 2024/25 unaenda ukingoni, Serikali kupitia Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na mlipaji Mkuu wa Serikali kutoa idhini ya kuwaruhusu Maafisa masuuli kuhama na fedha hizo kwenda mwaka wa fedha 2025/26 kwa kufuata utaratibu uliobainishwa kwenye Sheria ya Bajeti pamoja na Kanuni zake.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa kwamba kwa fedha zilizotolewa zenye jumla ya **Shilingi 70,000,000,000**, Wizara ya Fedha watakaa na OR-TAMISEMI kufanya usuluhishi wa fedha ili kuwezesha Wakurugenzi kutumia fedha hizo zinazoonekana kwenye mfumo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa fedha zilizosalia kiasi cha **Shilingi 53,500,000,000** Serikali imeahidi kutoa kiasi hicho kabla ya mwaka wa fedha 2024/25 kukamilika ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa fedha hizi zinatumika wakati wa utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2025/26 kupitia utaratibu wa fedha zinazovuka mwaka ***(Carry-overs)*** kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti, Sura ya 439. Aidha, kwa kuwa Serikali inatekeleza bajeti yake kwa kutumia mfumo wa fedha zinazokusanywa ndio zinapangiwa matumizi, Serikali itatoa fedha hizo kwenye mgao wa mwezi Juni baada ya kuwa mapato yote ya mwezi huo yamewasilishwa Mfuko Mkuu.

## 6.0. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI ZA MIFUKO MAALUM YENYE VYANZO VILIVYOLINDWA (RINGFENCED FUNDS)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya mapitio ya utekelezaji wa bajeti za Mifuko maalum yenye vyanzo vilivyolindwa kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa bajeti zake. Utekelezaji wa bajeti ya mifuko kwa kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka 2021/22 hadi mwaka 2024/25 ni kama ifuatavyo:-

### 6.1. Mfuko wa Taifa wa Maji *(The National Water Fund – NWF)*

**Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Taifa wa Maji ulianzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 44 cha Sheria Na. 12 ya mwaka 2009 ya Huduma za Maji safi na Usafi wa Mazingira ambapo utekelezaji rasmi ulianza katika mwaka wa fedha wa 2015/16. Lengo la kuanzisha Mfuko huu ni kuwa na rasilimali fedha ya uhakika kwa ajili ya kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya maji itakayoboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji nchini.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka 2021/22 hadi Desemba, 2024/25, Mfuko wa Taifa wa Maji uliidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 700.89** na fedha zilizopokelewa katika kipindi hicho ni **Shilingi bilioni 493.43** sawa na **asilimia 70.51** ya bajeti iliyoidhinishwa. Aidha, ili kuongeza mapato ya mfuko huu mwezi Februari, 2023 Mfuko ulizindua dirisha la mikopo ya masharti nafuu kwa watekelezaji wa miradi ya maji nchini hususani Mamlaka za Maji.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufika mwezi Desemba 2024, Mfuko umefanikiwa kutoa mikopo yenye thamani ya **Shilingi 5,300,000,000.00** kwa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira za DAWASA, Bunda na Tanga kwa ajili ya kutekeleza miradi ya usambazaji maji. Aidha, maombi ya mkopo yenye thamani ya **Shilingi 2,010,000,000.00** kutoka Mamlaka za Maji yapo katika hatua mbalimbali za malipo. Mwenendo wa malipo unaonyesha Mfuko umekusanya marejesho ya mikopo yenye jumla ya **Shilingi 274,100,000.00**.

### 6.2. Mfuko wa Maendeleo ya Reli *(Railway Development Fund* – RDF)

**Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Maendeleo ya Reli ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Reli Sura ya 170 kwa lengo la

kuendeleza na kukarabati miundombinu ya reli nchini pamoja na kugharamia mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR. Chanzo kikuu cha fedha za Mfuko huu ni tozo ya **asilimia 1** ya thamani ya bidhaa zinazoingizwa nchini (imports) kwa matumizi ya ndani ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha miaka mitatu (2022/23 hadi Desemba, 2024), Mfuko ulipokea kiasi cha **Shilingi bilioni 437.97** sawa na **asilimia 49.52** ya bajeti ya **Shilingi billion 884.40.**

### 6.3. Mfuko wa Barabara *(Road Fund)*

**Mheshimiwa Spika**, Mfuko huu ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Tozo ya Barabara na Mafuta Sura ya 220, na chanzo kikuu cha Mfuko ni tozo ya **Shilingi 263** kwa kila lita ya mafuta ya dizeli na petroli. Katika kipindi cha miaka minne, kuanzia mwaka 2021/22 hadi Aprili, 2024/25, Mfuko wa Taifa wa Barabara uliidhinishiwa jumla ya **Shilingi trilioni 3.48** na fedha zilizopokelewa katika kipindi hicho ni **Shilingi trilioni 3.06** sawa na **asilimia 87.95** ya bajeti iliyoidhinishwa.

***Jedwali Na. 8. Mwenendo wa Utolewaji wa Fedha za Mfuko wa Barabara kwa kipindi cha miaka minne***

| Mwaka | Bajeti | Kiasi kilichokusanywa | Kiasi kilichopokelewa | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 2021/22 | 908,355,896,000 | 1,027,035,559,222 | 1,027,035,559,922 | 113.1 |
| 2022/23 | 856,794,953,999 | 1,014,442,602,780 | 816,450,294,898 | 95.3 |
| 2023/24 | 856,794,953,999 | 1,113,274,420,552 | 836,723,932,251 | 75.16 |
| 2024/25 | 856,794,953,999 | 900,863,555,674 | 379,521,229,696 | 42.13 |
| **Jumla** | **3,478,740,757,997** | **4,055,616,138,228** | **3,059,731,016,767** | **87.95** |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Bodi ya Mfuko wa Barabara*

### 6.4. Mfuko wa Nishati Vijijini *(Rural Energy Fund – REF)*

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Nishati vijijini ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Nishati Vijijini, Sura ya 321. Katika kipindi cha miaka minne, kuanzia mwaka 2021/22 hadi Machi, 2024/25, Mfuko wa Nishati Vijijini uliidhinishiwa jumla ya **Shilingi trilioni 1.92** na fedha zilizopokelewa katika kipindi hicho ni **Shilingi trilioni 2.31** sawa na **asilimia 120.24** ya bajeti

iliyoidhinishwa. Kuvuka kwa lengo la utekelezaji wa bajeti umetokana na washirika wa maendeleo kutoa fedha zaidi ya walizokuwa wameahidi.

**Jedwali Na. 9. Mwenendo wa Utolewaji wa Fedha za Mfuko wa Nishati Vijijini**

| Mwaka | Bajeti | Kiasi kilichopokelewa | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 2021/22 | 414,272,100,000.00 | 481,613,933,688.60 | 116.26 |
| 2022/23 | 508,812,125,000.00 | 554,367,163,284.19 | 108.95 |
| 2023/24 | 514,819,760,652.00 | 895,283,289,996.01 | 173.9 |
| 2024/25 | 483,674,448,000 | 379,348,729,101.21 | 78.43 |
| **Jumla** | **1,921,578,433,652.00** | **2,310,613,116,070.01** | **120.24** |

***Chanzo:*** *Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti za Mifuko*

### 6.5. Masuala yaliyobainika wakati wa uchambuzi wa utekelezaji wabajeti za Mifuko Maalum iliyolindwa

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilichambua utekelezaji wa bajeti ya mifuko Maalum iliyolindwa na kubaini changamoto zifuatazo:-

i. Bajeti ya mifuko kutengwa chini ya uhalisia wa makusanyo;
ii. Matumizi ya fedha zilizoko kwenye akaunti za mifuko kuhitaji idhini ya mlipaji mkuu wa Serikali ili zitumike; na
iii. Changamoto za ukwasi kwenye mfuko mkuu wa Serikali kuathiri uwasilishaji wa makusanyo kwenye mifuko iliyolindwa;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaitaka Serikali kushughulikia changamoto hizo ili makusanyo ya fedha za mifuko yenye vyanzo maalumu vilivyolindwa yakatekeleza shughuli za mifuko zilizopangwa.

## 7.0. SURA YA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26

**Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya Serikali ya mwaka 2025/26 ni bajeti ya mwisho katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26). Dhima kuu inayoongoza bajeti ya mwaka 2025/26 ni "**Mageuzi Jumuishi ya Uchumi kupitia Uimarishaji wa Ukusanyaji Mapato ya Ndani, Uwekezaji wa Kimkakati wenye Kuzalisha Fursa za Ajira na Uboreshaji wa Hali ya Maisha ya Wananchi".** Bajeti hii inatekeleza vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2025/26.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mambo mengine bajeti hii itatumika kugharamia Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2025. Hatua hii inalifanya Taifa letu kutotegemea mtu, taasisi au Taifa lolote kufadhili uchaguzi wetu na hivyo viongozi watakaochaguliwa watatokana na kura za wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/26 Serikali imepanga kukusanya na kutumia jumla ya **Shilingi trilioni 56.49**, sawa na ongezeko la **asilimia 12.3** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2024/25 ya **Shilingi trilioni 50.29**. Kati ya kiasi hicho, **Shilingi trilioni 38.99** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia **82.23** ya bajeti kwa ajili ya kugharamia deni na mishahara pamoja na stahiki ya watumishi wa Umma. **Shilingi trilioni 17.49** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo sawa na **asilimia 30.96** ya bajeti. Bajeti ya maendeleo inajumuisha **Shilingi trilioni 12.12** fedha za ndani na **Shilingi trilioni 5.38** ni fedha za nje.

### 7.1. Mapato ya Ndani

**Mheshimiwa Spika**, Serikali inatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi trilioni 40.47,** kati ya fedha hizo Mapato ya kodi ni **Shilingi trilioni 34.10** na mapato yasiyotokana na kodi ni **Shilingi trilioni 6.36** yanayotokana na Michango na gawio la Mashirika, kampuni na taasisi za umma na Mapato ya Idara na Wizara zinazojitegemea na Mapato ya Halmashauri. Makadirio ya ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa mwaka 2025/26 yatapelekea uwiano mapato ya ndani kwa Pato la Taifa

kufikia **asilimia 16.8**. Mapato yote ya ndani yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania na Serikali za Mitaa yanaweza kugharamia Bajeti ya Serikali kwa **asilimia 71.64**. **se**

### 7.2. Misaada na Mikopo

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2025/26 Serikali itagharamia nakisi ya bajeti kupitia misaada na mikopo ya **Shilingi trilioni 16.02.** Mchanganuo wa misaada na mikopo ni kama inavyoonekana kwenye jedwali namba 10.

**Jedwali Na. 10: Mchanganuo wa Mikopo na Misaada kwa mwaka wa fedha 2025/26**

| Mikopo/Misaada | Kiasi (Shilingi trilioni) |
|---|---|
| **Mikopo ya ndani** | **6.28** |
| Dhamana za serikali zilizoiva | 3.32 |
| kuziba nakisi ya bajeti | 2.95 |
| **Mikopo ya Nje** | **8.68** |
| Mikopo yenye masharti nafuu kwenye miradi ya maendeleo | 4.42 |
| mikopo yenye masharti nafuu (GBS) | 1.63 |
| mikopo yenye masharti ya kibiashara | 2.63 |
| **Misaada** | **1.06** |
| **Jumla ya Mikopo na Misaada** | **16.02** |

**Chanzo:** *Hotuba ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2025/26*

### 7.3. Sera ya Matumizi

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/25 Serikali imepanga kutumia kiasi cha **Shilingi trilioni 56.49** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Ili bajeti hiyo itekelezwe kwa ufanisi, Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo:-

i. Kuhakikisha mikopo yote inaelekezwa kwenye maeneo ya uzalishaji kama inavyoelekeza Sheria ya Mikopo, dhamana na Misaada ya Serikali Sura ya 134;

ii. Kusimamia Waraka Na. 1 wa Hazina wa mwaka 2018/19 kuhusu Mkakati wa kudhibiti madeni ya Serikali;
iii. Kukamilisha miradi iliyopo sasa kabla ya kuanzisha miradi mipya;
iv. Kupanga bajeti kwa kuangalia mahitaji halisi ya sasa na si kwa kufuata mwenendo wa bajeti zilizopita; na
v. Kufanya mapitio ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa lengo la kupunguza matumizi yasiyo la lazima.

**Jedwali Na. 11: Ulinganisho wa Sura ya Bajeti kati ya mwaka 2024/25 na 2025/26**

| NA | | 2024/25 | 2025/26 | TOFAUTI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| | **MAPATO** | **B1** | **B2** | **B2-B1** | **(B2-B1)/B1*100** |
| **1** | **Mapato ya Ndani** | **34,610,646** | **40,466,132** | **5,855,486** | **16.92** |
| | Mapato ya Kodi (TRA) | 29,415,289 | 34,103,890 | 4,688,601 | 15.94 |
| | Mapato yasiyo ya kodi (Michango na gawio ya Mashirika na mapato ya wizara, idara na taasisi zinazojitegemea) | 3,839,017 | 4,681,735 | 842,718 | 21.95 |
| | Mapato ya Halmashauri | 1,356,341 | 1,680,507 | 324,166 | 23.9 |
| **2** | **Misaada kutoka Nje** | **794,390** | **1,069,884** | **275,494** | **34.68** |
| **3** | **Mikopo ya Ndani na Nje** | **14,886,372** | **14,954,236** | **67,864** | **0.45** |
| | Mikopo ya Nje | 8,268,582 | 8,676,050 | 407,468 | 4.93 |
| | Mikopo ya Ndani | 6,617,790 | 6,278,186 | -339,604 | -5.13 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **JUMLA YA MAPATO YOTE** | **50,291,408** | **56,490,252** | **6,198,844** | **12.32** |
| | | | | | |
| | **MATUMIZI** | | | | |
| **4** | **Matumizi ya Kawaida** | **34,937,809** | **38,996,519** | **4,058,710** | **11.62** |
| | Mishahara | 11,767,987 | 13,174,240 | 1,406,253 | 11.95 |
| | Matumizi Mengineyo (OC) | 7,433,542 | 9,184,809 | 1,751,267 | 23.56 |
| | Malipo ya deni | 13,121,466 | 14,208,979 | 1,087,513 | 8.29 |
| | Huduma za mfuko mkuu | 2,614,813 | 2,428,490 | -186,323 | -7.12 |
| **5** | **Matumizi ya Maendeleo** | **15,353,600** | **17,493,733** | **2,140,133** | **13.94** |
| | Fedha za Ndani | 11,712,762 | 12,117,828 | 405,066 | 3.46 |
| | Fedha za Nje | 3,640,838 | 5,375,905 | 1,735,067 | 47.65 |
| | **JUMLA YA MATUMIZI YOTE** | **50,291,408** | **56,490,252** | **6,198,844** | **12.32** |
| | **NAKISI YA BAJETI KWA ASILIMIA YA GDP** | **2.90%** | **3.00%** | | |

***Chanzo:*** *Hotuba ya Bajeti 2024/25 na 2025/26 na Taarifa ya Nyongeza ya bajeti 2024/25*

### 7.4. Vihataraishi vya Utekelezaji wa Bajeti

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wa vihatarishi vilivyobainishwa na Serikali ambavyo vikijitokeza vinaweza kuathiri utekelezaji wa Bajeti na kubaini kwamba baadhi ya vihatarishi hivyo havikidhi maana halisi ya Vihatarishi. Kihatarishi ni jambo ambalo bado halijajitokeza na litakapojitokeza linaweza kuathiri utekelezaji wa Bajeti. Katika aya ya 179 ya Hotuba ya Bajeti ya Serikali iliyosomwa na Waziri wa Fedha, imebainisha vihatarishi 8. Kamati pia imepitia na kuchambua Taarifa ya Vihatarishi vya Kibajeti vya mwaka 2025/26 *(Fiscal Risk Statement 2025/26)* ambayo ni kiambatisho cha Hotuba iliyowasilishwa na Mhe. Waziri.

**Mheshimiwa Spika,** moja ya kihatarishi ambacho kimebainishwa na Kamati inadhani hakistahili kuwa sehemu ya vihatarishi bali tatizo ambalo linatakiwa kushughulikiwa ni madeni sanjari ya Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kutochukulia suala hili kama kihatarishi bali tatizo ambalo lipo na linahitaji kushughulikiwa kwa haraka. Aidha, Serikali ihakikishe kuwa ina dhamini Mashirika ya Umma, Taasisi za Serikali na Serikali za Mitaa ambazo zinauwezo wa kurejesha mkopo kupitia mapato yake na hivyo kujihakikishia kuwa madeni hayo hayatokuja kuwa sehemu ya deni la Serikali endapo Mashirika ya Umma, Taasisi za Serikali na Serikali za Mitaa yatashindwa kulipa mikopo hiyo.

## 8.0. UCHAMBUZI WA HATUA ZA KIKODI

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti imefanya uchambuzi wa hatua zote za kikodi zilizopendekezwa na Serikali na kubaini zimegawanyika katika makundi makuu matatu. Makundi hayo ni Sheria za kodi za ndani, Sheria ya usimamizi wa ushuru wa Forodha wa Afrika Mashariki ya mwaka 2004 na mabadiliko ya kanuni zilizotungwa chini ya Sheria mbalimbali zilizopo. Madhumuni ya mapendekezo yamefafanuliwa kwa kila kundi kama ifuatavyo:-

### 8.1. Sheria za Kodi za Ndani

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wa mapendekezo ya Serikali kwenye Sheria za Kodi za Ndani, Kamati imebaini kwamba mapendekezo hayo yanalenga masuala yafuatayo:-

i. Kuongeza mapato ya Serikali kwa kupanua wigo wa kodi, kuongeza walipa kodi wapya pamoja na kuboresha mifumo ya ukusanyaji na usimamizi wake;
ii. Kuchochea uzalishaji wa viwanda vya ndani pamoja na kuvilinda vilivyopo dhidi ya ushindani usio sawa;
iii. Kukuza na kuendeleza Sekta ya Bima nchini pamoja na kuvutia wawekezaji katika Sekta hiyo;
iv. Kuongeza mchango wa Mashirika ya Umma kwenye Mapato ya Serikali kupitia Msajili wa Hazina;
v. Kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (MKUMBI);

vi. Kuwalinda wananchi dhidi ya madhara ya kiafya yanayoweza kujitokeza kutokana na matumizi ya vyakula au bidhaa za aina fulani; na
vii. Kuongeza mapato ya Serikali ili kuziba nakisi inayotokana na baadhi ya wafadhili na washirika wa maendeleo kusitisha kugharamia programu mbalimbali hususan kwenye sekta ya afya.

**Mheshimiwa Spika,** jumla ya Sheria 23 za kodi za ndani zinatarajiwa kufanyiwa maboresho. Pamoja na kwamba Kamati itapata nafasi ya kutoa maoni yake kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2025, naomba uniruhusu nitoe maoni kwa muhtasari maeneo yatakayozingatiwa.

***8.1.1.Mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria ya Utoaji wa Leseni za Biashara, SURA 101***

**Mheshimiwa Spika,** katika aya ya 168 ya Hotuba ya Bajeti ya Serikali, Serikali imekusudia kuweka mazingira mazuri ya ufanyaji biashara baina ya wazawa na wageni kwa kufanya marekebisho kwenye Sheria ya utoaji wa Leseni za Biashara, SURA 101. Marekebisho hayo pamoja na mambo mengine yanalenga kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya masuala ya biashara kuainisha shughuli za kibiashara ambazo hazipaswi kufanywa na wageni. Hatua hii ina lenga kuondoa kero iliyopo nchini hivi sasa ya wafanyabiashara wageni kufanya biashara za jumla, rejareja na uchuuzi ambazo zilikuwa ni shughuli zinazofanywa na wazawa.

**Mheshimiwa Spika, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** amesikia kilio cha wafanyabiashara na amewaondolea adha hiyo. Aidha, wakati wa majadiliano ya Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2025, Kamati itaishauri Serikali kuweka adhabu kwa wageni watakaokiuka masharti ya kanuni hizo ikiwa ni pamoja na kuwafutia vibali vya kazi na visa pale wanapothibitika.

**Mheshimiwa Spika, "wema hulipwa kwa wema"** Rai yangu kwa wafanyabiashara nchini ni kwamba ifikapo siku ya uchaguzi mwezi Oktoba, iwe ni siku ya kulipa fadhila kwa kumpa **Mhe.**

**Dkt. Samia Suluhu Hassan** kura ya **NDIO.** Hakika usikivu huu wa Mhe. Rais ni jambo la kuigwa mfano na nchi nyingine za Afrika.

**8.2. Baadhi ya Vyanzo vya Mapato vya Serikali za Mitaa kufanyiwa Mabadiliko wakati vimeshaingizwa kwenye Makadirio ya Makusanyo ya Mapato kwa Mwaka 2025/26**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inapendekeza kupunguza ushuru wa huduma ***(Service Levy)*** kutoka **asilimia 0.3** ya sasa hadi **asilimia 0.25.** Hatua hii ni njema kwa lengo la kupunguza gharama kwa wafanyabiashara, hata hivyo endapo makisio ya mapato yaliyofanywa na Serikali za mitaa yalizingatia mapato yatakayopatikana kwa utozaji wa **asilimia 0.3** ni wazi kwamba makusanyo yatashuka. Athari za kushuka kwa mapato ya ndani ***(Own Source)*** zitaonekana katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kutumia mapato ya Ndani. Hivyo, Kamati itafanya uchambuzi wa athari ya kimapato zitakazojitokeza na itaangalia endapo inafaa punguzo hili lianze kutumika katika mwaka wa fedha 2025/26 au mwaka 2026/27 ili kutoa nafasi kwa Halmashauri kujipanga.

**8.3. Misamaha ya Kodi, Punguzo la viwango pamoja na Tozo Mpya zinazopendekezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/26**

**Mheshimiwa Spika,** katika hatua za kikodi zinazopendekezwa na Serikali kuna misamaha imeondolewa na kuna misamaha mipya imeanzishwa. Baadhi ya misamaha iliyopo kwenye mapendekezo ni muendelezo wa misamaha iliyokuwepo. Hivyo, Kamati itafanya uchambuzi wa kuangalia misamaha inayopendekezwa ili kuangalia manufaa yatakayotokana na misamaha hiyo kwa mlaji wa mwisho wa bidhaa au huduma. Pale ambapo Serikali itashindwa kuthibitisha umuhimu wa misamaha hiyo kuondolewa au kutolewa Kamati haitasita kufanya mabadiliko katika mapendekezo ya Serikali.

**8.4. Mabadiliko ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Sura ya 147**

**Mheshimiwa Spika,** Mwaka 2023 Serikali ilifanya mabadiliko ya Kifungu cha 12(2) cha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Sura ya 147, kwa lengo la kuweka kalenda ya Kodi *(Tax Calender)* ambapo viwango vya ushuru wa bidhaa vinatakiwa kubadilika kila

baada ya miaka mitatu. Awali viwango hivyo vilikuwa vikibadilishwa kila mwaka kwa kuangalia mfumuko wa bei. Kamati inaikumbusha Serikali muda wa miaka mitatu umepita hivyo ni lazima itekeleze takwa hilo la kisheria kwa kufanya marejeo ya viwango vya ushuru wa bidhaa ambavyo vimekaa miaka zaidi ya mitatu bila kubadilishwa kabla ya utaratibu huu kuanza.

**8.5. Mapendekezo ya Mabadiliko ya Sheria ya Hifadhi za Taifa, SURA 282, Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, SURA 284, na Sheria ya Msajili wa Hazina (Mamlaka na Majukumu), SURA 370;**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubali kufanya mabadiliko kwenye Sheria hizi ili kurejesha utaratibu wa kukusanya na kutumia mapato mapato yao wenyewe. Hata hivyo, kiwango cha asilimia kinachopendekezwa kwenye mgao ni jambo ambalo litajadiliwa kwa kina na Serikali kwa sababu kuu mbili. Moja ni hali ya ukwasi wa Taasisi hizo ili ziweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu kwenye Sekta ya utalii na pili ni endapo kiwango kinachobakishwa kinaweza kukidhi mahitaji ya Taasisi kujiendesha kwa misingi ya kibiashara na kwa ufanisi.

**8.6. Uwasilishaji wa Muswada wa Sheria ya Fedha kwenye Kamati ya Bajeti**

**Mheshimiwa Spika,** katika Hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha aya 3 nanukuu ***"Mheshimiwa Spika, upo pia Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2025, Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2025 pamoja na Taarifa ya Vihatarishi vya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2025/26 ambayo ni sehemu ya bajeti hii***". Pamoja na kwamba Muswada ulitakiwa uwasilishwe sambamba na Bajeti bado Muswada huo haujawasilishwa.

**Mheshimiwa Spika,** kuchelewa kuwasilishwa kwa muswada wa Sheria ya Fedha kumekuwa kunasababisha Kamati kukosa muda wa kutosha kupokea maoni ya umma kwa mujibu wa Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la

Februari 2023, na muda wa kushauriana na Serikali yenyewe. Hivyo, naomba kiti chako kiiagize Serikali kuwasilisha muswada huo kesho tarehe 17 Juni, 2025 ili Kamati ipate muda wa kutosha wa kuufanyia kazi**.**

**Mheshimiwa Spika,** Pongezi humtia mtu bidii, kwa namna ya kipekee nimpongeze **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kusikia kilio cha wafanyabiashara na wawekezaji nchini na hivyo kufanya mabadiliko kupitia muswada huu ambao yataenda kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara. **Mwezi Oktoba Watanzania watafanya maamuzi sahihi kwa mtu sahihi nayo ni kumchagua aongoze tena kwa kipindi kingine cha miaka mitano.**

**8.7. Mabadiliko ya Sheria ya Usimamizi wa Ushuru wa Forodha ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2004**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imepitia hatua zote zilizoridhiwa na mkutano wa Mashauriano ya Kibajeti wa Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC Pre-Budget Consultative Meeting of Ministers of Finance)* uliofanyika tarehe 20 Mei 2025 jijini Arusha na kubaini kwamba hatua mpya ni 13 na hatua 48 ni muendelezo wa hatua ambazo zilichukuliwa katika miaka ya fedha iliyotangulia. Hatua hizo kwa ujumla wake zinalenga maeneo yafuatayo:-

i. Kulinda ajira na uzalishaji wa viwanda ambavyo vipo ndani ya Jumuiya ya Afrika mashariki;
ii. Kuchochea uzalishaji wa bidhaa mbalimbali viwandani katika Jumuiya; na
iii. Kukuza biashara baina ya nchi wanachama wa Jumuiya**.**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ya **Mhe**. **Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kupitia Waziri wake wa Fedha Mhe. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, imekuwa ikishirikisha Kamati ya Bajeti kuhusu Mapendekezo ya Serikali ya hatua ambazo zinapendekezwa na Serikali juu ya mabadiliko ya Sheria ya Usimamizi wa Ushuru wa Forodha. Hakika huu ndio ushirikiano na maridhiano ambayo ni lazima Bunge lako

litambue na kuenzi. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba utaratibu huu unaendelea kuwepo kwa kipindi kijacho kwa sababu umethibitisha kuwa na manufaa.

### 8.8. Mabadiliko ya Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo imekuwa ikiishauri Serikali mambo makuu matatu, kama ifuatavyo:-

i. Kuhakikisha mabadiliko ya kanuni zinazoanzisha tozo, faini na ada zinabadilishwa sambamba na mabadiliko ya Sheria ya Fedha;
ii. Mabadiliko ya kanuni yanayotangazwa na Wizara ya Fedha kupitia Hotuba ya Bajeti ya Serikali kuwa sehemu ya Hotuba ili kuwandaa wafanyabiashara ambao ni walipa kodi; na
iii. Kanuni zinazotungwa na kutangazwa na Mawaziri mbalimbali kuhusu ada, tozo na faini zithibitishwe na Waziri wa Fedha kabla ya kutangazwa.

**Mheshimiwa Spika,** la leo lisingoje Kesho, naomba nitoe pongezi za dhati kwa **Mhe. Dkt, Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kusikiliza, kukubali na kufanyia kazi mapendekezo ya Kamati. Hatua hii inaenda kuondoa udhaifu uliokuwepo ambapo Mamlaka na wakala wa Serikali zilikuwa zikianzisha tozo, ada na faini katikati ya mwaka wa fedha na hivyo kuleta taharuki kwa wafanyabiashara. Maboresho hayo yanaenda kufanyika kupitia Sheria ya Bajeti Sura ya 439 na Sheria ya Fedha za Umma Sura ya 348.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa hatua za kikodi zilizowasilishwa zimegusa maeneo mengi na kwa kuwa kwa mujibu wa Kanuni ya 97(2), Kamati inawajibu wa kualika umma kutoa maoni. Rai yangu kwa Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote wenye nia ya kutoa maoni juu ya hatua za kikodi zinazopendekezwa kufika mbele ya Kamati mara baada ya kupokea Tangazo la Kupokea Maoni ya Umma. Maoni ya

wadau yamekuwa na mchango mkubwa katika kuboresha Sheria ya Fedha ya kila mwaka.

**9.0. MAONI YA UJUMLA**

**9.1. Matumizi ya Mfumo wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) katika kugharamia Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika,** naomba kunukuu aya ya 123 ya Hotuba ya Waziri "***Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba mikataba minne (4) ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) yenye mtaji wa jumla ya Shilingi bilioni 681.53 imesainiwa katika mwaka 2024/25 kwa ajili ya kutoa huduma ya usafiri wa mabasi katika Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) kwa Awamu ya Kwanza"*** mwisho wa kunukuu. **Kongore kwa Serikali inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa sababu ni kwa mara ya kwanza Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi Sura ya 103 Iliyotungwa na Bunge mwaka 2010 na kufanyiwa marekebisho mwaka 2023 inaenda kutekelezwa kwa vitendo.

**Mheshimiwa Spika,** ili Serikali iendelee kutekeleza miradi kwa mfumo huu ambao unapunguza mahitaji ya fedha kwa Serikali ili kutekeleza miradi ya maendeleo yenye sura ya kibiashara, Kamati inaitaka Serikali moja ya sharti kwenye Mwongozo wa Maandalizi ya Bajeti ya mwaka 2026/27 iwe ni kuwataka maafisa masuuli wote kuwasilisha miradi itakayotekelezwa kwa njia ya PPP kabla ya kuwasilisha miradi itakayotekelezwa kwa fedha za umma. Miradi hiyo ichambuliwe na Tume ya Mpingo kwa kushirikiana na kituo cha Ubia na itekelezwe katika Bajeti ya mwaka husika.

**9.2. Mkakati wa Kuongeza Mapato na Kusimamia Matumizi**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi wa mikakati ya Serikali ya kuongeza Mapato na usimamizi wa Matumizi uliopo katika aya ya 135 na 136 na kubaini masuala yafuatayo:-

i. Serikali inahimiza utumiaji wa mifumo katika kukusanya mapato hata hivyo uwekezaji wake ni mdogo. Mfano TRA wanahitaji midaki ya kukagulia mizigo pamoja na kiasi cha **Shilingi bilioni 460** ili kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato lakini hadi hivi sasa kiasi hicho hakijatolewa;
ii. Bado hakuna Sheria wala Sera ya Tathmini na Ufuatiliaji hivyo ni vigumu kuwawajibisha wahusika pindi wanapofanya makosa yanayohusiana na Ufuatiliaji na Tathmini; na
iii. Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani haijaweza kuimarishwa kifedha, kimuundo na rasilimali watu ili iwe mlinzi wa kwanza kwenye matumizi ya fedha za umma kwa kufanya ukaguzi wa wakati *(Real Time Audit)* kabla ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ambae ni mkaguzi wa nje hukagua matumizi ambayo yamefanyika tayari.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaamini masuala hayo yakifanyiwa kazi yataongeza mapato ya Serikali na yatadhibiti matumizi mabaya ya rasilimali za umma.

### 9.3. Kupanua Wigo wa Mapato ya Ndani na Kupunguza Utegemezi wa Mikopo ya Nje.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa misaada Rasmi ya Maendeleo (Official Development Assistance-ODA) inapungua kwa kasi kutoka **dola za Marekani milioni 389** mwaka 2024 hadi makadirio ya **dola za Marekani milioni 118** mwaka 2025. Vilevile, Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID) lilifungwa mnamo Machi 2025, hatua iliyopelekea kusitishwa kwa takriban **asilimia 83** ya programu za USAID. Serikali inapaswa kuongeza uwezo wake wa kufadhili miradi ya maendeleo kwa kutumia vyanzo vya mapato vya ndani. Hii ni pamoja na kuweka vivutio vya kodi na sera zinazotabirika pamoja na upanuzi wa masoko ya mitaji.

### 9.4. Kutumia Migogoro ya Kimataifa kama Fursa

**Mheshimiwa Spika,** itakumbukwa kwamba migogoro ya Kimataifa imesababisha athari mbalimbali kama vile kuvuruga mnyororo wa biashara ya kimataifa kwa kuathiri masoko ya

bidhaa, minyororo ya usambazaji duniani, pamoja na bei za nishati. Kwa mfano Urusi na Ukraine ni miongoni mwa wakulima na wauzaji wakubwa wa ngano, mahindi, mbolea na mafuta ya alizeti duniani. Vita baina ya mataifa haya imeathiri uzalishaji na usambazaji wa bidhaa hizo. Vita vya Urusi na Ukraine pia vimeathiri usambazaji wa gesi asilia kwa nchi nyingi za Ulaya na kusababisha mgogoro wa nishati pamoja na kuathiri usalama wa nishati katika eneo hilo. Hivyo, ni vyema Serikali ikaangalia namna ya kutumia changamoto hizi kama fursa kwa kupanua masoko ya nje na kuboresha uwezo wa uzalishaji.

### 9.5. Diaspora na Fedha kutoka nje *(Remittances)*

**Mheshimiwa Spika**, kama nchi haijaweza kufanya vizuri katika kupokea fedha kutoka kwa Watanzania walishio ughaibuni (*remittances)* ambalo ni muhimu katika ukuaji wa uchumi na kama msaada wa kifedha (financial lifeline) katika kuchochea ukuaji wa uchumi, maendeleo ya nchi na mtu mmoja mmoja. Chanzo hiki ni muhimu kutokana na mchango wake sio tu katika uwezo wa ununuzi wa kaya lakini hata kwenye kujenga akiba ya fedha za kigeni nchini, na hivyo kuzifanya kuwa eneo muhimu la kuzingatiwa kwa maendeleo ya uchumi jumuishi.

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2024 Tanzania ilipokea kiasi cha jumla ya **dola za Marekani milioni 757** kama *remittance*s tofauti na nchi nyingine za Afrika Mashariki. Mfano, katika mwaka 2024, nchi ya Kenya ilipokea jumla ya **dola za Marekani bilioni 4.4** kama *remittances* ikiwa ni zaidi ya mapato yanayotokana na mapato ya mauzo nje ya Kenya ya Kahawa na utalii. Aidha, ongezeko hili limetokana na kuboreshwa kwa huduma za kifedha za kidijitali ambazo hufanya kutuma pesa kwa haraka na nafuu zaidi kuliko hapo awali. Hivyo, Serikali ifanye utafiti wa kina katika eneo hili ili kuangalia ni namna gani inaweza kufaidika na chanzo hicho. Jedwali Namba 12 linaonyesha takwimu fedha zinazopokelewa kutoka ughaubuni kwa nchi za

**Jedwali Na. 12: Fedha za Remittance kwa nchi za Afrika Mashariki kwa mwaka 2024**

| Na. | Nchi | Kiasi (Dola za Marekani Milioni) |
|---|---|---|
| 1. | Kenya | 4,800 |
| 2. | Somalia | 1,730 |
| 3. | Uganda | 1,490 |
| 4. | DRC | 1,350 |
| 5. | South Sudan | 1,140 |
| 6. | Tanzania | 757 |
| 7. | Rwanda | 557 |
| 8. | Burundi | 50 |

**Chanzo:** *Taarifa ya Remmitance kwa Nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara Februari, 2024*

**9.6. Mazingira Wezeshi ya Ufanyaji Biashara na Uwekezaji**

**Mheshimiwa Spika,** utitiri wa mamlaka za udhibiti, kodi, tozo na ada na urasimu uliokithiri zimekuwa ni changamoto za muda mrefu, zinazolalamikiwa kwa wingi na hivyo kuwa chanzo cha mazingira magumu ya ufanyaji biashara na hatimaye kutovutia uwekezaji. Hivyo, kuna haja ya suala hili kupewa kipaumbele na Serikali na kuweza kushughulikiwa haraka iwezekanavyo. Kama nia ya Serikali ni kushirikisha na kukuza ushiriki wa Sekta Binafsi basi Serikali ifanyie kazi eneo hili. Hatua hii itahimiza urasimishaji wa sekta binafsi nchini ambazo nyingi ni kampuni ndogo ndogo ambazo hazipo rasmi na Serikali haipati mapato stahiki.

**9.7. Kuwezesha kimitaji Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) na Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB)**

**Mheshimiwa Spika**, jukumu kuu la Benki ya TADB ni kuwa chachu ya utoaji wa mikopo ya muda mfupi, wa kati na mrefu kwa ajili ya kufanikisha maendeleo jumuishi ya sekta ya kilimo nchini, na kuchangia katika Dira ya Taifa ya Maendeleo katika kuhakikisha utoshelevu na usalama wa chakula, maendeleo ya uchumi na kupunguza umaskini. Tangu kuanzishwa kwake mwaka 2015, TADB imefanikiwa kutoa mikopo ya **Shilingi**

**971,890,000,000** ikinufaisha zaidi ya wakulima **1,948,801** na biashara **686** (biashara endelevu ni **478**). Kwa sasa Benki hii ina mtaji wa jumla ya **Shilingi 924,000,000,000**. Hata hivyo, benki hii haipokei amana kama ilivyo kwa benki za biashara. Ili kutimiza kikamilifu dhamira ya TADB na kukidhi mahitaji yanayoongezeka ya fedha kwa ajili ya kilimo, benki hii inahitaji jumla ya **Shilingi 2,950,000,000,000**, hivyo kufanya nakisi ya **Shilingi 2,026,000,000,000**.

**Mheshimiwa Spika**, Benki ya TIB ina jukumu la kutoa huduma za fedha kwa miradi ya maendeleo kwa gharama nafuu ili kujenga Taifa lenye uchumi shirikishi, mseto, mahiri na wenye ushindani. Hata hivyo, mwenendo wa ufanisi wa benki hiyo sio wa kuridhisha kwa sababu katika kipindi cha miaka mitatu mapato ya benki yamekuwa yakishuka kutoka **Shilingi 62,700,000,000** mwaka 2022 hadi **Shilingi 35,600,000,000** mwaka 2024 kufuatia kushuka kwa kasi ya utoaji wa mikopo kutokana na kiwango hafifu cha mtaji. Hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2024, mtaji wa benki kwa mujibu wa Kanuni za Taasisi za fedha (core capital) ulikuwa **Shilingi 90,226,000,000** kiwango ambacho ni kidogo ikilinganishwa na kiwango cha **Shilingi 200,000,000,000** kinachotakiwa kwa mujibu wa Kanuni za Taasisi za Fedha za Maendeleo zilizotolewa na Benki Kuu ya Tanzania mwaka 2021.

**Mheshimiwa Spika,** Benki za maendeleo kwa nchi zilizo na uchumi wa kati wa juu zina mtaji wa **asilimia 2** wa pato la Taifa. Hivyo, kwa kuwa kufika 20250 nchi imepanga kuwa imefika uchumi wa kati wa juu, Serikali haina budi kuziwezesha kifedha Benki hizo ili ziwe na mtaji unaotakiwa na hivyo kuongeza ufanisi na kuwezesha benki hizo kuwa shindani.

### 9.8. Kufanya mabadiliko kwenye Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa Sura ya 437 ili Mfumo wa malipo kwa njia ya kielektroniki (Cashlite) uanze kutekelezwa

**Mheshimiwa Spika**, kwa muda mrefu Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kuhusu kupunguza matumizi ya fedha taslimu na kutumia mifumo ya kielektroniki katika kufanya malipo ili kuzuia upotevu wa mapato yatokanayo na kodi. Malipo ya kielektroniki ni

miamala inayofanyika kupitia kadi za malipo, simu za mkononi na malipo ya papo kwa papo. Lengo ni kurahisisha miamala na kupunguza utegemezi wa fedha taslimu. Kamati inaisisitiza Serikali kufanya mabadiliko katika Kifungu cha 8 cha Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa Sura ya 437 pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura 438 ili kuanzisha sharti la lazima la kufanya malipo kwa njia ya kieletroniki wakati wa kufanya manunuzi ya huduma na bidhaa.

**Mheshimiwa Spika**, mfano Serikali inaweza kuweka ukomo wa malipo ya fedha taslimu wa kiwango cha chini pamoja na kupunguza gharama za kufanya miamala ili kutohamasisha matumizi ya fedha za taslimu kwenye malipo ya manunuzi ya bidhaa na huduma.

**10.0. HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika,** napenda kukushukuru wewe Mhe. Dkt. Tulia Ackson, Mb, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa kwanza Mwanamke wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU). Kwanza kwa kuniamini kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na pili kwa miongozi thabiti iliyowezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Uyole linaweza kuwa Jimbo jipya la Uchaguzi lakini kwako ni nyumbani. Hivyo, wanauyole hawatasita kukupa ushindi wa kishindo.

**Mheshimiwa Spika**, aidha napenda kumshukuru Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb, Naibu Spika kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge lako tukufu. Nimtakie kila lililo jema kwenye uchaguzi unaokuja, hakika Ilala bado inakuhitaji. Aidha, napenda kuwashukuru Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba Madelu, Mb na Waziri wa Fedha, Mhe. Prof. Kitila Alexander Mkumbo, Mb na Waziri wa Mipango na Uwekezaji, Mhe. Hamad Hassan Chande, Mb Naibu Waziri wa Fedha na Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo, Mb Naibu Waziri wa Mipango na Uwekezaji kwa ushirikiano wao kwa Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake. Nawatakia kila la kheri na ni imani yangu watarejea tena mwezi Novemba, 2025.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile, niwashukuru Dkt. Natu El-Maamry Mwamba, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mlipaji Mkuu wa Serikali, CPA(T) Charles Edward Kichere, Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, Dkt. Tausi Mbaga Kida, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji pamoja na Dkt. Fred Msemwa, Mtendaji Mkuu wa Tume ya Mipango. Pia, niwashukuru Manaibu Katibu Wakuu wa Wizara ya Fedha, Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji, Makamishna, Wakuu wa Taasisi na Wataalam wote kwa ushirikiano wao kwa Kamati katika kipindi chote katika uhai wake.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upendo wa dhati napenda kumshukuru **Mhe. Twaha Ally Mpembenwe,** Mb na Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa kunisaidia wakati wote wa shughuli za Kamati. Niwaombe wananchi wa Jimbo la Kibiti kumwamini na kumpa fursa tena ili awatumikie kwa miaka mingine mitano. Aidha, kipekee niwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kuniamini kuwa kiongozi wao na kunipa ushirikiano katika kipindi chote cha uhai wa Kamati. Nawaombea kila mmoja wenu ikimpendeza Mwenyezi Mungu tukutane tena mwezi Novemba, 2025. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Oran Manase Njeza, Mb | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Twaha Mpembenwe, Mb | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei, Mb | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Jonas William Mbunda, Mb | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Juma Hamad Omar, Mb | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Stella Alex Ikupa, Mb | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Joseph Zacharius Kamonga,Mb | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Rashid Abdallah Rashid, Mb | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mb | Mjumbe |

| | | |
|---|---|---|
| 18. | Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi, Mb | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Omar Ali Omar, Mb | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Yahaya Ally Mhata, Mb | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Bahati Keneth Ndingo, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** mwisho ila si kwa umuhimu, nimshukuru Bw. Baraka I. Leonard, Katibu wa Bunge kwa niaba ya Watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu uliowezesha kufanikisha shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Oran Manase Njeza
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**
16 Juni, 2025

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Bunge ya Bajeti, ahsante sana kwa wasilisho hilo.

Waheshimiwa Wabunge yapo majina hapa ya wachangiaji, lakini kabla hawajaanza kuchangia, basi nimwite Mheshimiwa Mwenyekiti aje kuendelea na ratiba.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na uchangiaji sasa. Tunaanza na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, na Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo ajiandae.

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa fursa hii adhimu ya kutoa mchango wangu katika Bajeti Kuu ya Serikali. Kampuni ya utengenezaji wa simu maarufu ya Samsung ya Korea Kusini ina kauli mbiu yake muhimu sana inayosema; "*We have a shortage of natural resources, but creativity in abundance.*" Hatuna rasilimali za kutosha, lakini tuna ubunifu wa hali ya juu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli hii inasadifu maneno aliyowahi kuyasema Mheshimiwa Waziri Mkuu wa zamani wa Tanzania, Hayati Edward Lowassa. Alisema akipewa nafasi ya kutaja vipaumbele vikuu vitatu vya mipango ya maendeleo ya Taifa, basi angetaja kipaumbele cha kwanza ni elimu, cha pili ni elimu na cha tatu ni elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapoitafsiri kauli hii utabaini kwamba elimu inapaswa kuwa kipaumbele cha kwanza na sekta kiongozi katika mipango ya maendeleo ya Taifa letu. Hata hivyo, ninatambua kuwa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanaweza kuwa na Mawazo tofauti. Wengine watasema kipaumbele cha kwanza ni kilimo, wengine maji, wengine miundombinu, wengine afya, wengine umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la msingi ambalo tunapaswa kujiuliza kama viongozi, je, miradi hiyo mikubwa itatekelezwa na nani? Kama itatekelezwa na wakandarasi kutoka nje, basi jambo hili halina afya kwa maendeleo ya Taifa letu, kwa sababu tutakuwa tunahamisha fedha za Taifa letu kuzipeleka nje. Hapa ndipo ile hoja ya kuwekeza katika sekta ya elimu hasa sayansi na teknolojia pamoja na utafiti inapokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapotafakari kwa makini, mipango yetu ya maendeleo na bajeti, ninaona kiwango cha fedha kinachowekezwa katika sekta ya elimu, hasa sayansi na teknolojia, utafiti na uvumbuzi hakilingani na dhamira ya Taifa letu ya kujenga uchumi ulio shindani. Huwezi kujenga uchumi ulio shindani kama hujawaandaa vizuri rasilimali watu ukawapa maarifa na ujuzi wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina Chuo cha Nelson Mandela cha Sayansi na Teknolojia, chuo ambacho kimeanzishwa kwa madhumuni ya kutoa shahada za juu za teknolojia ya habari, sayansi ya tiba na kilimo. Chuo hiki kwa bahati mbaya sana hakina maabara za kisasa ambazo zinaweza kufanya ugunduzi, uvumbuzi na utafiti wa kiwango cha Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu, iwapo tutawekeza kwenye chuo hiki, chuo hiki kinashika hatma ya Taifa letu. Kwa nini ninasema hivyo? Ni kwa sababu chuo hiki kinatoa mafunzo ya akili bandia pamoja na *data science,* taaluma ambazo ni muhimu sana katika mapinduzi manne ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana shaka sote tunakubaliana kwamba katika karne ya 21 sayansi ya *data* itakuwa ndiyo mgodi wa karne hii. Soko la matumizi ya *data* duniani yanaongezeka na soko lake ni kubwa sana. Nitatoa mfano hapa; China kuna watu bilioni 1.4, India kuna watu bilioni 1.4 na Afrika kuna watu wapatao bilioni 1.2; jumla yake ni bilioni nne. Hili ni soko kubwa sana ambalo linahitaji matumizi makubwa ya *data* hasa katika sekta za biashara, kilimo, afya na elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtakubaliana nami kwamba nchi zilizopiga hatua ya maendeleo ya kiuchumi zimewekeza kiasi kikubwa sana cha fedha katika utafiti wa kisayansi na masuala ya sayansi na teknolojia kwa ujumla wake. Nitatoa mifano ya nchi tatu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ya kwanza ni India. Mwaka 1966 Waziri Mkuu wa wakati ule Jawaharlal Nehru aliamua kuwekeza katika vyuo vya teknolojia pamoja na vyuo vya sayansi ya tiba. Leo ninapozungumza, nchi ya India ni moto wa kuotea mbali katika teknolojia ya habari na matibabu. Watu wanatoka sehemu mbalimbali za dunia kwenda India kutafuta matibabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa pili; China wakati wa uongozi wa Deng Xiaoping waliwapeleka vijana wao Marekani wapatao 100,000, mwaka 1978 ili kujifunza masuala ya sayansi pamoja na teknolojia ya kisasa. Leo tunajua sote Taifa la China lilipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa tatu ni Vietnam. Nchi hii mwaka 1980 ilikuwa maskini wa kutupwa, na pato la Taifa la Vietnam wakati ule lilikuwa ni dola bilioni 18. Leo baada ya kufanya mapinduzi ya sayansi na teknolojia, pato la Taifa la Vietnam ni bilioni za Kimarekani 476 wakati Tanzania sisi pato la

Taifa ni takribani kama bilioni 90 hivi. Tunaweza kujua kwa kiasi gani wenzetu wa Vietnam wameweza kupiga hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niseme mambo mawili kwa msisitizo mkubwa. Kwanza, ninatambua sana kwamba nchi yetu ni maskini, hauwezi kukidhi mahitaji yote ya sekta ya elimu. Hata hivyo, ukombozi wa uchumi ni kama vita, na vita hivi vinahitaji silaha, na silaha ya ukombozi wa uchumi ni sayansi na teknolojia pamoja na utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili. Mzee wetu Nelson Mandela aliwahi kusema kwamba elimu ndiyo silaha madhubuti tunayoweza kuitumia kuubadili ulimwengu. Kama Taifa langu la Tanzania linataka kubadili maisha ya Watanzania, kubadili maisha ya Waafrika na kuubadili ulimwengu, basi jambo pekee la kuwekeza kwa msisitizo mkubwa ni sekta ya elimu hasa katika masuala ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme jambo moja. Wako wataalamu wa masuala ya elimu wanaosema kwamba katika karne hii ya 21 vita havitapiganwa tena kwa kutumia mizinga, bali vita vitatumiwa kwa *cyber* na masuala ya teknolojia ya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, ninafikiri Tanzania, kama nilivyosema, tunayo nafasi hiyo ya kupambana kwa kutumia akili badala ya kutumia mizinga kwa sababu hatuna nguvu hizo; lakini akili Mwenyezi Mungu katupa. Tufanye hima basi kuziendeleza kwa maslahi ya nchi yetu na kwa maslahi ya Afrika. Ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, nilimtaja Mheshimiwa Sospeter Muhongo, Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya na Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, ajiandae.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia muda. Ninadhani mawazo yaliyotolewa na mwenzangu aliyetangulia ni mawazo muhimu kweli kweli. Hakuna Taifa ambalo litakwenda mbele bila kuwekeza kwenye sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nianze mchango wangu kwa kusema hivi, tunapiga kura Jumanne ya wiki ijayo, siyo ya kesho. Kwa niaba ya wakazi wa Jimbo la Musoma Vijijini nataka niwaeleze kuwa hii bajeti nitaipigia kura ya "Ndiyo" Jumanne. Hii ni kwa sababu miradi jimboni mwangu na Mkoa wa Mara inatekelezwa vizuri kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, hii bajeti ikipitishwa na tukaanza kuitekeleza tarehe moja mwezi wa saba Musoma Vijijini tutakuwa tumebakiza vitongoji 50 kati ya vitongoji 374 kufungiwa umeme. Vilevile nilimwomba Mheshimiwa Rais alivyokuja Musoma Vijijini miradi miwili. Mradi wa barabara na mradi mkubwa wa umwagiliaji. Ninatoa shukrani kwa Mheshimiwa Rais, miradi hiyo imepatikana na inatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ombi langu ni kwamba wale wataalamu wa *TANROADS* na Tume ya Umwagiliaji tumekubaliana kwamba mwezi wa Sita wanawakabidhi wakandarasi, na kweli naona wanafanya majadiliano. Kwa hiyo, mwezi wa Sita wakabidhi wakandarasi, na sisi Musoma Vijijini tunaunga mkono hii bajeti kwa nguvu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwenye mchango ambao ni mpana zaidi; mipango, uwekezaji na bajeti. Ndugu yangu aliyeanza kuongea tulikuwa hatujasemezana, kwa kuwa muda huwa ni mfupi, mimi ninaanza na mapendekezo mawili, na naomba yachukuliwe kwa uzito. Nimeanzia mwisho baadaye nitarudi huku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu la kwanza ni kwamba tuwekeze zaidi kwenye elimu na taasisi za elimu na hasa sayansi teknolojia na *innovation.* Nimekuja na hesabu. Hizi hesabu siyo za kufikirika tu. Tutumie *percent* mbili hadi *percent* tatu ya *GDP* yetu tuwekeze kwenye elimu na taasisi zake zote, na uzito mwingi kwenye elimu ya sayansi. Hii ni kwa sababu sisi Tanzania tumefanya kazi kwa karibu sana na Norway, tumekwenda kujifunza mambo mengi Norway.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wao wanawekeza *percent* 6.6 ya *GDP* yao kwenye elimu na taasisi zake. Wapo Watanzania wengi

tunapeleka watoto kusoma Uingereza na Marekani. Uingereza na Marekani wanawekeza 6.1% ya pato lao la Taifa *(GDP)* kwenye elimu na taasisi zake. Pendekezo la kwanza hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo la pili ninaweka tarakimu kwa ndugu yangu aliyeongea, kwamba, ni lazima tuwekeze kwenye ubunifu na utafiti. Dunia ya sasa hivi siyo *Research and Development,* vinakuwa vitatu; *Research, Development* na *Innovation*. Sasa nchi za kiafrika tulisema angalau asilimia moja, lakini ni *South Africa* tu walikuwa wamefikia *0.9*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napendekeza Tanzania tuwekeze angalau *percent* moja mpaka mbili ya *GDP* yetu kwenye mambo ya utafiti na ubunifu. Mfano mzuri ni hapa *Samsung,* anafanya vitu vyote hivi nchi ya *South Korea* wanawekeza *percent* 4.8 ya *GDP* yao kwenye utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu China sasa hivi hizi *solar panel* za dunia nzima, 90% ya *solar panel,* wacha vitu tunavyonunua Kariakoo, vinatoka China kwa sababu wanawekeza kwenye utafiti. Wao 2.7% ya *GDP* yao inawekwa kwenye utafiti. Kwa hiyo, hayo ndiyo mapendekezo ya kwanza mawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwenye bajeti. Bajeti yetu imesomwa kwa wakati mmoja ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Maana yake ni kwamba, ni lazima ya kwetu kidogo tulinganishe na wenzetu wakati tunajadili ya kwetu. Hatuwezi kujijadili sisi wenyewe tu. Sasa ninaomba Waheshimiwa wanifuate taratibu hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kwa sababu bajeti ilikuwa na nchi *za East Africa* na mimi nitaweka kwa dola ili iwe rahisi kulinganishwa na nchi nyingine. Bajeti yetu hii tuliyosomewa ni ya dola bilioni 21.6, sasa hivi Watanzania tuko milioni 70.5 *(70.5 million population)*. Kwa hiyo, *expenditure,* yaani matumizi ya bajeti tuliyosomewa kila Mtanzania ni dola 306, na pato letu *(GDP per capital)* sasa hivi ni dola 1,220.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kipimo kingine cha maendeleo ambacho hatukitumii sana, ninaomba Mawaziri Wawili muwe mnakiweka, msiwe mnakisahau. Ninajua mnacho, huwa mnakisahau, nacho ni hii *HDI (Human Development Index)*. Hii *GDP per capital* ni ya *World Bank* na *IMF,* tunaipenda sana. Kuna ya *UNDP* ambayo ni nzuri zaidi, nayo inaitwa *Human Development Index*. Hii ni nzito kwa sababu inachukua mambo ya afya, mambo ya elimu na maisha yetu, yaani *standard of living*. Kwa hiyo, ukichukua hii *HDI* Tanzania sasa hivi ni 0.555, tuko katikati *maximum* ni *one*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kenya bajeti yao shilingi bilioni 30.3, wako Wakenya milioni 57.5. Kwa hiyo, *expenditure* ya mtu mmoja kwenye bajeti ya Kenya ni dola 574, *GDP per capital* ya Kenya ni dola za Marekani 2,301. Sisi 1,220 wao 2,305 na *HDI (Human Development Index)* yao ni 0.628. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uganda wamesoma bajeti yao, ni shilingi bilioni 20.1. *Population* ya Uganda ni watu milioni 51.4. Kwa hiyo, *expenditure* ya bajeti yao kwa kila Mganda ni Dola za Marekani 391, *GDP per capital* yao ni dola 997 na *HDI* yao ni 0.582.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamalizia na Rwanda. Bajeti yao ni shilingi bilioni 4.9. Warwanda wako milioni 14.6. Kwa hiyo, *expenditure* ya bajeti yao, kila Mrwanda atatumia dola 336 na *GDP per capital* yao ni dola 1,071 na *HDI* yao 0.548. Kwa hiyo, ukiangalia bajeti iliyosomwa kwa nchi za Afrika Mashariki, usichukue tu tarakimu, zigawanye na *population,* utaona kwamba Wakenya ndio wanaoongoza; kila mtu atatumia dola 574 na sisi kila mtu atatumia dola 306. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kujilinganisha, nimechukua Seychelles na Mauritius, wao *GDP per capital* yao Seychelles ni dola 26,000; ni nchi inayohesabika kuwa imeendelea; na *HDI* yao ndiyo kubwa Afrika ni *0.848;* Seychelles *GDP per capital* ya Mauritius ni zaidi ya dola 11 na *HDI* yao bado 0.8. Kwa hiyo, ukiangalia kwa maendeleo yetu sisi tuko katikati kwenye hivyo viwango vya *HDI* nchi za Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja sasa kwenye mambo ya uchumi. Uchumi wetu tangu mwaka 2000 mpaka sasa hivi 2025 kwa miaka 25 umekua kati ya asilimia tano mpaka saba. Mwaka mmoja tu 2011 uchumi ulifika 7.5%. Ndugu zangu, wataalamu wote wa uchumi duniani kote wanasema ukitaka kuondoa umaskini uchumi uende kwa asilimia nane, kumi na zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu *reserve* ya dhahabu ni muhimu sana. Ninashukuru na Mwenyekiti wa Kamati ameisoma ambayo hesabu yetu inayojulikana huko duniani, tuna *reserve* ya tani 3.7 ukilinganisha China kama wenzetu wana zaidi ya tani zaidi ya 2,200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, India wana zaidi ya tani 800. Kwa hiyo, hii dira ya maendeleo tunayoimaliza sasa, malengo yetu yalitaka *GDP per capital* iwe ni *3,000 US Dollars;* ukichukua na *population* yetu ya watu 70 leo, hii *GDP* yetu inapaswa kuwa dola za Marekani bilioni karibu 210, lakini sasa hivi tuko kwenye bilioni 22. Tume-*perform by 10% (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima hapo tuongeze kasi ya ukuaji wa uchumi. Umeme tumefanya vizuri. Makisio ilikuwa tufikie *megawatts* 5,000 ukichukua umeme wa kwenye *grid* na kwenye *off grid,* tuna *megawatts* 4,300. *Performance* yetu imekuwa ni 86% ya malengo. Kwa hiyo, tumefanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji na matumizi ya umeme ndiyo yanaonesha kwamba kweli Taifa lako ni kubwa. Mwaka 2024 umeme ambao ulizalishwa na China unazidi umeme wa Marekani, *European Union* na wa India ukiweka pamoja. Kwa hiyo, uone wengine wanakwendaje. Takwimu, ninaona muda hauniruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tufanyeje? Nije kwenye mapendekezo ambayo ni ya muhimu. Tufanyeje uchumi wetu ukue kwenda asilimia nane mpaka kumi? *Sectors* ambazo tunapaswa kuwekeza zaidi ambazo ni msingi *(foundation)* au tuseme *primary sectors* ni kilimo na uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sekta hizi na nimetoa mapendekezo mchango wa *GDP,* hapa lazima twende kwenye *agriculture,* ufugaji *(animal husbandry),* uvuvi huu wa vizimba, *forestry* tuvune misitu halafu twende kwenye uchimbaji. Kwa hiyo, hizi *agriculture, animal husbandry, fisheries, forestry, and mining* hizi ndizo ziwe uti wa mgongo wa ukuaji wa uchumi wetu, na ikifaa tuwekeze hapo, uchumi ukue zaidi, tupate mchango wa 55% *(55% of our GDP)* itoke huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye uchimbaji hapa nitaongea na rafiki zangu; tumewekeza sana kwenye dhahabu, na ni kweli kwa sababu dhahabu imepanda bei, lakini kuna madini mengine ya muhimu sana. Kwa mfano, sasa hivi *ounce* moja ya dhahabu ni karibu dola 3,500, lakini kuna madini ambayo hatuyajui yanaitwa *rhodium* ambayo yako kwenye dola elfu tatu karibu na mia nane. Hii *rhodium* inaweza ikapatikana kwenye leseni tulizozitoa hizo. Sijui kama waliotoa leseni wanajua hayo madini yamo humo, sijui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongeza kingine kwenye pato letu la Taifa lazima twende kwenye huduma *(services)*. Hiyo inakuwa ni *secondary sector. Services* hapa ninamaanisha utalii, biashara *(finance)* mambo ya benki, mambo ya afya, mambo ya elimu na *water and electricity suppy*. Hizi za huduma, hawa wachangie 30%, hizi *services, 30% of our GDP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, karibu ninamalizia, nimejipanga kuendana na muda wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wa mwisho utatoka kwenye viwanda *(industrial sector)* yaani *manufacturing* na *construction* ituchangie 15% ya *GDP* yetu. Hivi nimevichukua baada ya kuangalia uchumi wa nchi mbili ambazo zimefanya vizuri ambazo ni China na India.

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka mwaka 2010 China imempita Marekani kwenye mambo ya *manufacturing* kwa mbali sana. Kwa hiyo, na sisi hizi sekta nimezi-*check* kwenye nchi zote zilizofanya vizuri, *sectors* ni hizi na huo ndiyo utakuwa mchango wa *GDP;* na soko lipo kwa sababu dira yetu ya maendeleo

inatupeleka mpaka 2050. Tukifika mwaka 2050 kuna soko duniani, tutakuwa watu bilioni 10 na soko la Afrika lipo, tutakuwa watu zaidi ya bilioni 2.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pendekezo langu ni hilo, uchumi ukue kwa zaidi ya asilimia nane na hizi sekta tatu: *primary sectors, secondary sectors* na hizi *tertiary sectors* ndiko tuwekeze na tutaweza kupunguza umaskini kwa kasi kubwa, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo. Tunaendelea na Mheshimiwa Prof. Shukrani Elisha Manya, Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei na Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, jiandaeni.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Bajeti Kuu ya Serikali. Nitangulie kusema kwamba ninaunga mkono hoja na pia nitapiga kura ya "Ndiyo" siku ya Jumanne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa neema ya kuwa Wabunge katika Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambalo sasa linafikia mwisho wake. Sisi sote tumekuwa sehemu ya mageuzi, na mafanikio makubwa ambayo yametekelezwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hivyo tuna sababu ya kumshukuru Mungu kwamba tumepata nafasi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Taifa wa Maendeleo ambao umesomwa wiki iliyopita ni wa mwisho katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Miaka Mitano, lakini pia ni wa mwisho katika Dira yetu ya Taifa ya Maendeleo ya Miaka 25. Ni kweli kwamba nchini kote utaona kwamba kuna mafanikio makubwa yaliyotokana na utekelezaji wa Dira yetu ya Miaka 25 na hasa katika nyanja za miundombinu, usafirishaji, kilimo, huduma za maji, afya pamoja na elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tunapokwenda kutekeleza bajeti hii, lakini pia na kuandaa dira ya miaka mingine

25 nilitamani kutoka ofisi ya mipango ya Taifa izingatie jambo hili moja. Katika nchi yetu, kuna maeneo ya pembezoni na maeneo haya mara nyingi yako katika changamoto ya kijiografia. Kwa hiyo, ninapenda kusema kwamba ni *disadvantaged areas.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ninasema hivi? Siyo bahati mbaya kwamba Mkoa wa Kigoma ndiyo uliokuwa wa mwisho katika kuwasha *grid* ya Taifa. Ni kwa sababu uko pembezoni mwa nchi yetu. Mfano mwingine ni maeneo yaliyo katika visiwa, katika mpango huu ambao unakamilika, kwa mfano eneo la miundombinu, tulipanga kwamba tunapomaliza dira yetu ya miaka 25 tuwe tumefanikiwa kuunganisha barabara za lami zenye viwango mkoa hadi mkoa, na ni kweli kwamba tumefanya vizuri katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuchukulie maeneo ya visiwa, wilaya zilizo katikati ya mkoa hadi mkoa zitaweza kuunganishwa na barabara hiyo, na kwa hiyo, kupitiwa na barabara, lakini haitakuwa hivyo katika maeneo ya visiwa. Hivi ninavyoongea, katika Kisiwa cha Ukerewe kuna barabara ya lami yenye urefu wa kilometa saba tu, kwa sababu gani? Ni kisiwa hakiunganishwi na mkoa mwingine. Kwa hiyo, nilidhani kwamba tunapokuwa tunapanga maeneo ambayo yanajikuta yana changamoto ya kijiografia yanahitaji kuonekana tofauti kuliko inavyokuwa inapangwa ili na wao waweze kufanikiwa na kupata matunda ya mipango hii ya Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ndivyo ilivyo katika eneo la nishati na elimu pia. Kwa hiyo, nilidhani kwamba tunapokuwa tunapanga, basi tuangalie maeneo yaliyo pembezoni; na Wabunge wengi wanapokuwa wanaongea hapa, mara nyingi wanatoa mifano ya kwamba hata watumishi wanaopelekwa katika maeneo ya pembezoni ambayo ni *disadvantage areas,* mara nyingi watumishi wale watatoroka kwa sababu ya mazingira ambayo siyo rafiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapopanga kama Taifa, nisingetegemea kwamba Ukererwe ambayo ni kisiwa useme kwamba leo baada ya miaka yote hii ina kilometa saba za lami tu, hii siyo sawa. Kwa hiyo, tunapopanga, tuangalie ili watu

wote waweze kufanikiwa, hata wale ambao wana changamoto ya kijiografia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, hilo linaelekezwa katika Ofisi ya Mipango ya Taifa. Tuiangalie Tanzania kwa ujumla wake, tuipange na kila mtu asipate hasara kwa sababu ama yuko kwenye kona fulani ya nchi au yuko katika kisiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tunakwenda kutekeleza bajeti ya shilingi trilioni 56.49. Ninapenda kuiita kwamba ni bajeti ya mwendelezo ambayo inaakisi kaulimbiu ya Kazi Iendelee. Ni bajeti ya mwendelezo kwa sababu inakwenda kuendeleza miradi mikubwa ya *SGR* ili kuifikisha Kanda ya Ziwa pamoja na Mkoani Kigoma. Miundombinu ya usafirishaji inapokuwa ni bora, pia ni kigezo kikuu cha nchi ambayo inapiga hatua za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuombe kwamba miradi hii itekelezwe kwa wakati kama ilivyopangwa ili tuendelee kuepuka na kukomesha kabisa riba inayotokana na miradi kutotekelezwa kwa wakati. Inaendelea kula fedha zetu jambo ambalo siyo la msingi kwa sababu ya ucheleweshaji wowote ule ambao unaweza kutokea. Ni bajeti ya mwendelezo kwa sababu inakwenda kuendeleza kilimo na sekta nyingine za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninataka niangazie kidogo kilimo na ni kwa sababu bajeti hii imeondoa *VAT* katika viuatilifu, na mbolea inayozalishwa ndani ili kuendelea kutoa tija katika eneo hilo la kilimo. Jambo ambalo ninatamani tulizingatie na ambalo limezungumzwa na wazungumzaji wawili waliotangulia ni kwamba tunatamani kuendelea kutumia utafiti katika kuleta tija katika kilimo. Kwa nini ninasema hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili la utafiti sitaki kulizungumzia katika sekta ya kilimo peke yake, lazima tufanye utafiti katika utekelezaji wote wa shughuli za Serikali pamoja na elimu. Mfano sasa hivi tunasema kwamba tunanunua ndege ya mizigo ili tuweze kusafirisha mazao yetu ya kilimo, matunda na mboga katika nchi za nje, lakini bado katika nchi ya Tanzania ukichukua mti wa mwembe au mchungwa, mti huo huo unatoa

matunda yaliyoiva, mengine machachu na mengine matamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua zabibu ukasema kwamba ni zabibu zilizoiva nyingine ni chachu, na nyingine ni tamu, sasa unavuna matunda ya jinsi hiyo umuuzie nani? Yaani mtu afike achukue matunda ambayo mengine ni makali na mengine yameiva, ni matamu katika mti huo huo? Hatuwezi kutoboa. Hatuwezi kuuza nje kwa mtindo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuwaombe watu wa kilimo waendelee kuwatumia watafiti wetu ili tuweze kupata ile ladha *uniform* inayotoka katika mazao yetu hasa ya matunda pamoja na mboga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, watafiti wasaidie katika hali hii lakini kama Serikali na kama alivyopendekeza Mheshimiwa Prof. Muhongo pamoja na mzungumzaji aliyetangulia kwamba hatuwezi tukaacha utafiti katika kupata tija katika utekelezaji wa shughuli zetu za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokwenda kuteleza bajeti yetu na kuendelea kujenga uchumi wa nchi yetu, ninatamani sana jambo ambalo limependekezwa liweze kufanyiwa kazi kwa uaminifu mkubwa, na jambo hili ni la kuwafanya wazawa wa Tanzania waweze kuwa ndio wamiliki wakubwa wa uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haipendezi kwamba hivi tunavyoongea katika eneo la uchimbaji mdogo leseni ya *PML* imedhamiriwa kwa ajili ya wazawa lakini ukienda katika migodi ya wachimbaji wadogo kuna raia wa kigeni ambao ndio wanaoendesha shughuli hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mwisho wa wakati huku tukitoa leseni ya *PML* kule madini kwamba ni ya wachimbaji wadogo, lakini uchimbaji wote unafanywa na wageni. Uchumi huo maana yake hautawaendea tena wazawa, badala yake utaenda kwa wageni. Hali ni hiyo katika biashara za uchuuzi Kariakoo pamoja na maeneo mengine ya sekta za uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kile ambacho tumekipendekeza hapa, tunaomba Wizara ya Kazi pamoja na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, wakae chini ili waone kwamba hawatoi vibali wala hawatoi ruhusa kwa shughuli ambazo zinapaswa kufanywa na wazawa, halafu zikafanywa na watu wa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuiombe sana Serikali yetu ikubali kwamba kilimo, uvuvi, ufugaji, na misitu, shughuli hizi kwa sehemu kubwa zifanywe na wazawa kwa sababu ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wetu. Kama kutahitajika wageni, wawe ni kwa ajili ya teknolojia, lakini sehemu kubwa ya shughuli hizi ziweze kufanywa na wazawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu uzoefu mkubwa ambao tumeupata katika utekelezaji wa miradi mikubwa na ya kimkakati. Ningetamani kwamba iwe ni chachu ya kuandaa wataalamu ambao watakuja ku-*take over* baadaye, tusi-*attach* watu kwa ajili ya kupata mshahara. Tu-*attach* watu ambao tuna mkakati ndani ya nchi *strategically* kwamba hawa watu tumewa-*attach* katika miradi mikubwa, lengo letu likiwa ni kwamba wachukue uzoefu ambao baada ya hapo watakuja ku-*take over* katika utekelezaji wa miradi hii mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi tukaruhusu kwamba tunazalisha uchumi ambao tunasema kwamba sasa unakua lakini uchumi huo ukiangalia kampuni kubwa zinazotekeleza miradi nchi hii, ni kampuni za kigeni. Kwa hiyo, ni sawa na kwamba umezalisha fedha nyingi ndiyo, na uchumi wako umekua ndiyo, lakini ni nani? *Who is the recipient of that economy?* Utakuta ni kampuni kubwa za kigeni ambapo sasa unafanya kazi hapa, lakini wao ndio wanaofaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, kwa hoja hiyo hiyo ndiyo maana ninapendekeza kwamba katika utekelezaji wa bajeti hii na katika dira yetu tunayokwenda kuiandaa huko mbele, tukubali kwamba tuna sababu ya kuimarisha mashirika yetu ya umma ili yaweze ku-*takeover.* Kwa mfano, hapa tunataka kufanya *LNG facility* pale Lindi tukitumia *Equinor* ambayo ni Kampuni ya Mafuta ya Norway. Ni ya Taifa la Norway ile kampuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tungetamani hata hapa Tanzania tujenge mashirika makubwa ambayo nayo yatakwenda kufanya shughuli nyingi ambazo uchumi unaendelea kubaki hapa ndani. Kinyume na hapo, tutakuwa tunaweka bajeti, lakini mwisho wa siku wanaofaidika na uchumi mkubwa wa shughuli kubwa ni kampuni za nje na hivyo unakuta sisi tunaendelea kupata zile ambazo ni masalia na mabaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilidhani kwamba niyaseme hayo kwamba tuendelee kuyaimarisha mashirika yetu ya umma na hasa mashirika kama ya *TPDC*. Kwenye upande wa mafuta, yapewe nyenzo muhimu ya kuweza kufanya kazi hiyo. Shirika letu la Madini *(STAMICO)* tuendelee kulifanya liwe shirika ambalo litafanya kazi hiyo kwa ushindani mkubwa, badala ya kuacha kampuni za nje kuja kuchimba madini. Faida kubwa inayopatikana itarudi kule ambako ndiyo *origin* ya hiyo nchi, lakini kama ni *TPDC,* au *STAMICO* maana yake ni kwamba hela hiyo inabaki hapa ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi. Ninaunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga na Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi, ajiandae.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais na wasaidizi wake, Waziri wa Fedha, Naibu wake, pamoja na Waziri wa Mipango na Uwekezaji, kwa kutuletea Mpango mzuri na bajeti nzuri kwa mwaka unaokuja wa 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nikikumbuka kwamba kweli huu ndiyo mchango wangu wa mwisho kwenye bajeti hizi za hili Bunge la Kumi na Mbili, mchango kwenye bajeti kuu ambayo naanza kwa kusema ninaunga mkono, nasema pia nawiwa kuwashukuru wananchi wa kule Vunjo kwa kunichagua kuwawakilisha kwenye Bunge hili, na ninaamini wanaridhika na wataridhika kwamba

nimewatendea haki kwa kupigania sehemu ya kutosha kwenye ugawaji wa keki hii ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini pia kwamba tunaunga mkono kwa sababu kuna miradi inaendelea. Miradi hiyo inajumuisha kuweka kwa kiwango cha lami barabara ile ya Pofo – Mandaka – Kilema, Barabara ya Uchira, Kisomachi – Kolarie, Chekereni – Kahe – Mabogini ambayo Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI aliipa shilingi bilioni saba siku za karibuni alipotembelea kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme hivi nami nianze hapa kwenye *RND* kwa sababu naona imezungumzwa na kila mtu kwa namna moja, lakini watu wanafikiri kwamba *RND* ni muhimu tu kwenye sayansi *(Fundamental Sciences),* lakini ukweli ni kwamba *RND* utafiti unahitajika sana kwenye kusaidia kutunga sera za maendeleo ya jamii na uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa bahati mbaya Bunge hili au wizara zinazohusika hazijatilia maanani kwamba tuna taasisi kama *REPOA*, *SRF, Uongozi Institute*, na kuna taasisi nyingine ambazo zinafanya *fundamental research* ambayo itasaidia pia hususan kutengeneza mipango ambayo iko *evidence based* na *decision* zifanyike kwa kutegemea na kwa kuchukulia mahitaji na matakwa muhimu ya jamii yetu kwenye maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba katika utekelezaji wa bajeti inayokuja, Mheshimiwa Waziri wa Mipango, alinihakikishia kwamba ameweka *vote* kidogo, lakini naomba hizo igawe vizuri kila taasisi iliyopo iweze kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye maeneo yote mawili; Bajeti na Mipango wamezungumzia *issue* ya hali ya Uchumi, na akasema hapa tuna *global by* 5.5% kwenye mwaka huu wa 2024. Ninashukuru kwamba hiyo ni *achievement* nzuri na ni ya kupongeza wahusika na kupongezwa Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba siyo tofauti sana na nchi nyingine za *East Africa Community* kwa sababu ni zina-

*grow* kwa wastani wa 5% wenyewe ukiondoa Sudan. Sudan ilianguka kwa 27.6% na tunajua sababu. Kwa hiyo, tunapojilinganisha, tuangalie kwamba hatujawa mbali, lakini tunaweza kuwa mbali kwa sababu tulikuwa tumewahi kufikia ongezeko la 7.5%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naseme hivi, pamoja na hivyo, kinachofurahisha au pia kinachokuwa changamoto ni kwamba ongezeko la pato la Taifa hapa kwetu limechangiwa zaidi na uwekezaji wa Serikali. Kwenye maeneo yale ambayo tunashangilia miundombinu, usafirishaji, mambo yote yanayohusika na *infrastructure, so to speak. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *private sector* inaonekana imedumaa, yaani uchangiaji wa *private sector* bado ni mdogo sana. Sasa ninachouliza ni hivi, tungejiuliza zaidi ni kwa nini na sababu zipo zinajulikana? Juzi Mheshimiwa Profesa Jeffery Sachs ambaye ni mmoja wa maprofesa mashuhuri duniani katika masuala ya uchumi. Alisema kwamba, ili kuwezesha nchi za Afrika ziweze kukua kwa zaidi ya asilimia saba inahitaji vitu vitatu au kitu kama hicho ni *entrepreneurship* na ubunifu, tunahitaji mikopo ya muda mrefu na yenye riba ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *issue* inageuka, kwa nini mikopo haipatikani? Hiyo mikopo inaweza ikapatikana, watu wanasema hakuna *sources,* lakini naamini kwamba mikopo hiyo inaweza ikapatikana kama tukilenga zaidi kwenye ku-*improve efficiency* ya *financial system* yetu na tukaifanya i-*deepen* zaidi.

*Mheshimiwa Mwenyekiti, of course* hatuwezi kutegemea tu benki za maendeleo zianzishwe na Serikali, lazima iweze kuvutia kwamba benki za nje au benki zilizopo zinaanzisha madirisha au *subsidiary* au kampuni tanzu za kuweza kutoa mikopo hii ya muda mrefu *(investments banking in a group)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba hivi, cha kwanza ni haya mabenki. Hata kama tunataka kusaidia mabenki, lazima yaongeze mitaji, na mitaji wa mabenki haitoki *from nowhere*. Yaani mitaji mingi ya mabenki inatoka *from growing organically,* maana yake ku-*retain profits.* Utakuta hapa mabenki yanapata

*profit* kubwa, lakini wanagawa kigodo, wanabakiza *the rest* ili ikuze mitaji yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hela iliyoko kwenye benki kama *shareholder funds* ndiyo zinaweza zikatumika kukopesha kwa muda mrefu. Kwa sababu hizo ni *home permanent;* ni *permanent source of funding,* ni mitaji ile watu wamefanya *paid up capital in equity.* Kwa hiyo, inabaki *forever* na *retain end* zinakuwa ni sehemu ya *shareholder funds* ambazo zinaweza zikatumika kusaidia kukuza mitaji na ukopeshaji wa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nashangaa kwamba tumeingiza kodi ya *withholding tax* kwenye *retain ends.* Namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, anajua vizuri sana kama benki iki-*retain* au kampuni yoyote iki-*retain* fedha ikaongeza kwenye mtaji wake kwa kupitia *plough back,* halafu wakasema haa, lipa *withholding tax* kwa sababu hujagawa, basi ina maana kwamba *corporate tax* inakuwa 40%, 10% *plus* 30% ambayo wameshalipa kwenye *profit* yao. Ni kwamba wewe umewatoza kodi ya 40%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kodi ya 40% hapa kwenye kanda hakuna wenzetu hapa wa kwenye *East Africa Community* wamepunguza *corporate tax,* zinakwenda mpaka 25%, 15%. Kwa hiyo, sisi tutajiondoa kabisa katika ushindani wa uwekezaji kwa sababu watu hawatawekeza wakijua watalipa 40% badala ya 30% au chini yake kwa sababu wenzetu wanashindana na sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba hilo liangaliwe, lakini liangaliwe pia *in the context* kwamba hiyo inasaidia kuongeza uwezo wa mabenki yetu kukopesha kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ambalo tunaliona kwa sasa, *okay* unayo fedha ya kukopesha muda mrefu, lakini riba ni ndefu, ni 16 *plus* au mpaka 20. Sasa *how do we go ahead addressing the challenge.* Nafikiri *challenge* ya riba tumekaanayo muda mrefu. Kwa nini? Kwa sababu mabenki yamepewa *facilities* zote na *incentives* zote za kupunguza riba, lakini hayapunguzi

riba. Riba zimebakia pale pale 16%, na tukiwauliza wanapata faida; mabenki yamepata faida ya *trillions* ukijumlisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri kwamba zile *incentive* tunazotoa hazisaidii kwa sababu kuna mtu anayetoa dhamana za Serikali akaipa kuponi ambayo ni 16% na anatangaza kabisa kwamba mimi nauza dhamana za Serikali kwa riba ya 16%, kila mtu anakimbilia kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mabenki yanasema kuwa sisi twende huko, tuanze kukimbizana na *private sector! Private sector* ambayo *risks* yake ni kubwa, *anything can happen. Covid* inaweza ikaja, tena nini wanasema hapo, ni hapo hapo, wanashikilia pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mimi, nawekeza kwa sababu kwa nini nikampe mtu. Hata ndugu yangu nimpe hela akatupe tupe huko; naweka kwenye dhamana ya Serikali kwa sababu riba ni kubwa. Sasa *issue* ni kwamba *how do you go ahead?* Lazima tubadilishe mfumo, *options* za dhamana za Serikali za *bonds,* maana yake usitangaze bei, usitangaze riba ya kuponi, ile riba, riba ya ile kuponi kwa sababu utaleta mtu, anajua lakini sasa wasipojua unasema hee! Sasa mimi niki-*bid above* 10% sitauziwa, watauziwa wale ambao wame-*bid below*. Kwa hiyo, kila mtu amekuwa kwenye *uncertainty*. Kwa hiyo, kila mtu anayetaka kuwekeza, anabuni riba ambayo ni *acceptable*. Sasa ninyi mnaitangaza, sijui mimi nafikiri hapo hapafai kabisa, twende kitofauti kabisa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme hivi, turudi kwenye mfumuko, *exchange rate. Exchange rate,* tunapongeza sana kusema kweli, kazi iliyofanyika na Wizara na Benki Kuu ni ya kupongeza, kwa sababu unajua imeserereka hivi; sisi yetu imeshuka mwaka uliopita 2024 kwa asilimia tisa. Sasa sikiliza, ya Kenya imeshuka kwa 16.3%; ya Uganda kwa 47%; sisi haijafika huko, si watu wange-*riots* hapa tungepata GeZ hapa watusumbue sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, bado tupo, imeshuka kwa asilimia tisa tu. Halafu Rwanda imeshuka kwa 48%, Burundi

kwa 32%. Kwa hiyo, nafikiri ni vizuri wamefanya, lakini pia hata kushuka kwa asilimia tisa ni *very easy to compare to others.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba pengine tungeweza pia kuangalia tukawa *more flexible* katika ku-*manage exchange rate* kwa kuruhusu *periodic movement* iwe kidogo inaenda juu kidogo lakini *it is a very good way* ku-*balance*-sha mauzo ya nje na *imports,* kwa sababu *imports* ikiwa rahisi sana, basi inakuwa kila mtu anataka tu *import* malighafi. Una-*import* kwa sababu *exchange rate* iko *very low*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme hivi, kuna *issue* ya mazingira rafiki ya uwekezaji ya *especially* kwa *private sector;* na nataka kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ameona umuhimu wa kusema kwamba hakuna kupandisha tozo kwa mamlaka na mamlaka zile zinazohusika na *regulations* na ya udhibiti wa sekta hizo bila idhini yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, zile zilizopo zipo, lakini amesema sasa kama unataka kubadilisha chochote lazima aione, nami nafikiri hicho ndicho kitu ambacho wadau walikuwa wanalia sana walipokuwa wanakuja kutuona. Wanasema tufanyaje? Hawa wanaweza wakaja tu vilevile, nchi inaweza ikaja ikaingiza, ikapandisha, ikaleta *left right* na bila kujali viwango, kwa hiyo kuzuia sana watu kupata motisha ya kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye jambo lingine ambalo ningetaka kutoa ushauri ni kwamba ukiangalia deni la Taifa malipo ya *debt services* yetu inatisha kidogo, lakini tuko wahimilivu bado kwenye deni, na tunapongeza hilo, lakini kuna jambo ambalo wale wachambuzi walidanganya kwa sababu utakuta tunakopa shilingi trilioni 15 kwenye mpango wa mwaka huu, lakini tunalipa shilingi trilioni 14.2 kama *debt services*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *net* ni *only point eighty of trillion,* ni kidogo sana. Sasa unasema ni kitu; naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha aangalie kile kitengo cha *Debt Management* waone tunafanyaje? Kwa sababu *is a lot,* huwezi kukopa ili ulipe. *Virtually* siku utakayokosa mkopeshaji uta-*default* na/au utapunguza sana matumizi mengine ya maendeleo. Kwa hiyo,

hilo ni jambo ambalo nimeliona, nikasema niliseme tu hapa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo tunapongeza sana ni kwenye sekta ya kijamii, na ninaamini kwamba, ukiangalia kwa mfano sekta ya afya; ndani ya miaka mitano bajeti ya sekta ya Afya imekua kwa 57%, bajeti ya elimu imekua kwa 57% hiyo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unaona kwamba kweli kuna jitihada ambazo zinaenda moja kwa moja kumgusa mwananchi, na inachangia sana kwenye masuala ambayo walizungumza akina Mheshimiwa Nahodha, Mheshimiwa Muhongo na hata Mheshimiwa Manya. Kwa hiyo, nafikiri hili ni jambo la kupongeza sana, nami nafikiri kwamba tukiendelea kuzilea vizuri itakuwa ni vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia uone jinsi ambavyo Mheshimiwa Rais anayejali mazingira, bajeti ya mazingira ilikuwa *twenty billion,* sasa hivi ni *sixty-two billion.* Kwa hiyo, imekua kwa 210%, ni *almost* zaidi ya mara mbili. Kwa hiyo, tuwashukuru sana hawa kwa sababu ni jambo ambalo kwa dunia nzima lazima wapongezwe na Serikali yetu ipongezwe kwa sababu tunajali kitu ambacho kinachangia maendeleo na uhimilivu wa dunia yetu kwenda mbele kwa kutunza mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba pamoja na mengine ambayo yamezungumzwa na wenzangu, naomba niwasilishe na niseme tena kwamba naunga mkono hoja ya Mipango na Bajeti, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei. Nilimtaja Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi na Mheshimiwa *Engineer* Dkt. Leonard Chamuriho wajiandae.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika hoja hii muhimu ambapo tunajadili Makadirio, Mapato na Matumizi kwa mwaka 2025/2026. Kwanza nianze kwa kumshukuru

Rais kwa kuwateua hawa vijana wawili maarufu kama Singida *boys,* wamefanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia hali ya uimara wa uchumi wetu kwa kipindi cha miaka hii miwili, kwa kweli uchumi umeendelea kukua, mfumuko wa bei umeendelea kuwa wa chini wastani wa asilimia tatu nukta moja ikiwa imepungua kutoka ile tatu nukta nane. Ni kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia, uchumi umekua kwa asilimia tano nukta tano na tuna makisio ya kukua uchumi kwa asilimia sita kwenye pato la Taifa, namaanisha hapo. Kwa hiyo, ni kazi nzuri ambayo kwa kweli imefanywa na hawa vijana pamoja na wasaidizi wao kwa maana ya Makatibu Wakuu na watendaji wengine, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumeangalia mapendekezo mengi, hata katika mipango yao ambayo ameweka pale ni mizuri ambayo inaashiria kwamba huko tuendako ni kuzuri. Sasa nami nitapenda nitoe mchango wangu kidogo niongezee katika msisitizo kidogo katika yale ambayo wenzetu wamezungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia katika eneo la bajeti kujitegemea, wameonyesha mipango kwamba, kama nchi kuna sababu ya baadaye kuendelea kujitegemea. Kuweza kugharamia bajeti yetu wenyewe ni jambo zuri. Sasa maeneo muhimu ambayo nchi hii bado tumeendelea kulegalega na Watanzania wengi kweli sio waaminifu katika eneo hili la kodi, Watanzania wengi bado hawaoni umuhimu wa kulipa kodi kwa hiari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili eneo ni muhimu sana kwamba kama Watanzania wenzetu pamoja nami hatutaki kulipa kodi kwa hiari, ni lazima tusimamiwe kwa nguvu na kuhakikisha kwamba kila Mtanzania anajua umuhimu wa kulipa kodi kwa sababu ya kujiletea maendeleo yake mwenyewe. Katika jambo hili tutafanyaje? Tuendelee kwanza kutoa elimu, yaani elimu iwe ni jambo la kila siku. Kwa nini Mtanzania ulipe kodi? Kwa nini kuna sababu ya kujenga uchumi wako mwenyewe? Hilo muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmezungumzia suala la kuwajengea uwezo pia wakandarasi wetu wa ndani katika baadhi ya miradi fulani na shughuli fulani kufanywa na Watanzania. Jambo hilo ninawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, kama tunatamani nchi hii Watanzania waweze kumiliki uchumi wao wenyewe ni lazima tuwe na mikakati madhubuti ya kuhakikisha kwamba baadhi ya miradi yenye kiasi fulani cha fedha, hiyo iwe inatengwa tu kwa ajili ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuwe na mtaji kama nchi, mtaji fulani ambao tumeuweka tu kwa ajili ya kuwaendeleza Watanzania. Nilisoma mahali fulani inaonekana kwamba, nchi ya Oman ilipeleka vijana kwenda kusoma mambo ya mafuta na mambo ya gesi, baadaye walivyorudi wakafunguliwa makampuni, na Serikali ikaweka fedha zake kwenye hayo makampuni ili hao wa Oman waendelee kufanya shughuli za uchimbaji wa mafuta kwa kutumia makapuni yao. Nasi kama Watanzania, tunaweza tukawa na mpango kama huo kwa ajili ya kuwasaidia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nilipenda kulizungumzia, Kiswahili chetu ni bidhaa muhimu sana ambayo sisi kama nchi tunaweza tukauza. Ukienda katika nchi mbalimbali, hata ukienda Marekani, Ulaya unakuta kwamba katika vyuo mbalimbali wanaofundisha Kiswahili hasa, ni wenzetu kutoka nchi ya jirani hasa Kenya, wakati tunasema Kiswahili kilizaliwa Tanzania. Kwa hiyo, nilikuwa napenda tuwe na mikakati ya kuzalisha rasilimali watu ambao tutakuwa tunaiuza nje kwa maana ya walimu kwenda kufundisha Kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango mwingine ambao naona unafanywa na hata nchi kama Marekani, sisi kama tunataka kukiuza Kiswahili katika nchi ambazo tunafanyanazo biashara kwa mara nyingi zaidi, tuwe na mkakati wa kuweka udhamini wa kusomesha vijana kutoka katika nchi hizo ambazo tunazilenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakuta kwamba Marekani inachukua vijana kutoka Tanzania au Angola, inachukua, wana

malengo, hee! Ya kukuza uchumi wao kwa kupitia hao ambao wanawasomesha na sisi tunaweza tukafanya namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia nchi kama Sudan Kusini tunafanya nao biashara kubwa, tunaweza kila mwaka tukawa na mpango wa kusomesha vijana kadhaa na nchi nyingine, hiyo itatusaidia kukuza Kiswahili na kutengeneza mazingira ya kuwafikia kibiashara katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia ni kwenye upande wa ardhi, nimekuwa nikizungumza mara nyingi kwamba kwenye upande wa ardhi bado hatujafanya vya kutosha. Tanzania tunategemea kilimo kama ndiyo uti wa mgongo, lakini wawekezaji wengi wanapokuja nchini hawapati maeneo ya kuwekeza. Ndiyo maana ninashauri ni muhimu sana kuwa na benki ya ardhi, kuwa na akiba ya ardhi itasaidia sana wawekezaji wakubwa wanapokuja nchini kujua ukitaka kwenda Iringa tuna hekta 100,000 au kiasi fulani ni rahisi kwenda kufanya hivyo na tukileta wawekezaji wakubwa katika eneo la kilimo, kwanza ile kushirikisha teknolojia na hawa wenzetu wanaotoka nje, itasaidia Watanzania wengi kupata teknolojia na pia kupata masoko ya bidhaa zetu kule wanapotoka. Hilo ni jambo ambalo tunaweza kulifikiria namna ya kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nimeona katika mapendekezo ya bajeti, wamependekeza kufuta kanuni za usimamizi wa mazingira, Kanuni ya Mwaka 2024 kwenye *GN* 588. Jambo hili mimi kama Mwenyekiti wa Kamati ya Maji na Mazingira sijaliunga sana mkono, kwa sababu sasa hivi kama dunia tunahangaika kutafuta fedha za kuweza kusimamia mazingira. Tulitarajia kwamba hizi kanuni ziwawezeshe wenzetu wa Baraza la Kusimamia Mazingira wapate fedha ili kukagua shughuli za mazingira zinazofanywa kwenye migodi na maeneo mbalimbali ambayo yana uzalishaji, viwanda na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, ninatamani eneo hili badala ya kuzifuta tuone namna gani tunaweza kufanya marekebisho, kwa sababu tukisema tunafuta moja kwa moja maana yake tatasababisha tukose fedha za kwenda kusimamia mazingira, jambo hili ninaliona halijakaa vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine pia kwenye matumizi makubwa ya fedha. Kwa muda mrefu tumekuwa tukitekeleza miradi mikubwa mingi na ya kielelezo. Sasa, miradi mikubwa hii ya kielelezo ambayo tumekuwa tukiitekeleza *SGR,* kwenye umeme na mambo mengine, kwenye barabara na madaraja tumezalisha madeni makubwa ambayo sasa yanasababisha riba kuongezeka. Ninafikiri tunavyoendelea tuone ile miradi mikubwa ya kielelezo tuanze kuipunguza kwanza, tumalize ile ambayo tunaendelea nayo ili Taifa lisiendelee kuzalisha madeni ya ndani na ya nje, lakini haya madogo kwa sababu lazima mzunguko wa fedha uendelee kuwepo ile miradi midogomidogo tuendelee kuitekeleza. Kwa hiyo, wenzangu katika mipango yao wataangalia kwamba ile miradi mikubwa ambayo inatumia trilioni za fedha kwa sasa tuipunguze ili tutekeleze ile ambayo tayari inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatamani sana tuweze kuimarisha Benki yetu ya Maendeleo, tukiimarisha Benki ya Maeneleo na tukawa tunatoa mikopo ya muda mrefu kwa wakulima na kwa wafugaji, eneo hili kwa sababu tunasema kilimo ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wetu ni muhimu sana kuwa na mtaji mkubwa kwenye Benki ya Maendeleo, tuwe tunakopesha mikopo ya muda mrefu kwa wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mtanzania anaweza kuanzisha ranchi yake mwenyewe akafuga mifugo na akaweza kuuza tunakuza uchumi. Pia hata kwenye kilimo, kwamba sasa Serikali inatengeneza miradi ya umwagiliaji lakini tunaweza tukaruhusu Watanzania mmoja mmoja akaweza kukopa kwenye Benki yetu ya Maendeleo na bado akaweza kutengeneza *irrigation scheme* yeye mwenyewe na baadaye akaanza kuilipa Serikali ili mradi tu tuone awe ana uwezo wa kuweza kusimamia na tayari tumeona anatekeleza, kwa hiyo katika eneo hili nalo ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo litapelekea kuwa na ustahimilivu wa uchumi wetu ni hili suala la kununua dhahabu. Tunaipongeza Serikali kwa hatua ambayo tayari wameanza kuifanya ya kuwa na akiba ya dhahabu kwenye Benki Kuu. Jambo hili tunaomba liwekewe mkakati mkubwa kwamba

kila mwaka tuwe na kiasi kikubwa cha dhahabu ambacho tunakinunua. Hiki kitatusaidia sana kuwa na uchumi himilivu na stahimilivu, jambo hili ninawapongeza lakini tuweze kuliongezea nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho sababu ninaona kengele pia imegonga, ninaishukuru sana Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa bajeti iliyotangulia kwa kweli Jimbo la Kalenga nalo limefaidika sana. Miradi mikubwa imetekelezeka katika miundombinu, kwa hiyo, tunawashukuru sana Serikali ikiongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuwashukuru sana wananchi wa Kalenga kwa kuniamini na kunileta katika jengo hili, ninawaambia kwamba, kazi waliyonituma nimewafanyia vizuri na ninaomba waendelee kuniamini kwa sababu yapo mengi mazuri yapo mbele ambayo tunakusudia kuwafanyia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Gideon Kiswaga. Kabla sijamtaja mchangiaji anayefuata ninaomba niwatangaze wageni ambao wapo Bungeni muda huu.

Tunao wageni Wanne wa Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Winfred Mahundi ambaye ni Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ambao ni Ndugu zake kutoka Jijini Mbeya. Karibuni sana wageni wetu kutoka Mbeya. *(Makofi)*

Tunao wageni 13 wa Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya ambao ni Kundi la Wamisionari wa Consolata kutoka Sanza - Manyoni, Mkoani Singida. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 12 wa Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole ambao ni Watumishi wa Serikali, Kata ya Isansa kutoka Mbozi, Mkoani Songwe. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 47 wa Mheshimiwa Ng’wasi Damas Kamani ambao ni wanafunzi 45 na Walimu Wawili wa Sheria kutoka Chuo

Kikuu cha *St. Augustine* Mkoani Mwanza. Karibuni sana wanafunzi wetu. *(Makofi)*

Tunao wageni 96 wa Mheshimiwa Jackson Gideon Kiswaga, ambao ni Maafisa Tarafa, Watendaji Kata na Watendaji wa Vijiji kutoka Kalenga Mkoani Iringa. Karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Jackson Gideon Kiswaga. *(Makofi)*

Pia, tunao wageni wa Mheshimiwa Balozi Liberata Mulamula, ambao ni Ndugu Olasimbo Sojinrin ni *CEO* wa *Solar Sister* Tanzania, wapo juu kule. Pia, tuna Ndugu Caesar Theresa Mloka huyu ni *Country Director Solar Sister* Tanzania, wapo kule juu kabisa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni ambao pia wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wapo Wanafunzi 46 na Walimu Saba wa Shule ya *Genius King's* kutoka Tabata Segerea, Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana wanafunzi wetu kutoka Tabata. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 127 na Walimu 13 wa Shule ya Awali na Msingi Monikamu kutoka Babati, Mkoani Manyara. Karibuni sana wanafunzi wetu wote pamoja na wageni wetu wote ambao mpo muda huu katika Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi, Mheshimiwa *Engineer* Leonard Chamuriho na Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, ajiandae.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukushukuru mno kwa kunipa nafasi kuchangia katika hoja hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kabisa kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya na kufika leo hii kwa sababu ni karibu kipindi cha miaka mitano, huu ndiyo mchango wangu wa mwisho katika Bajeti Kuu na katika Bunge hili la Kumi na Mbili tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana viongozi wa CCM katika Wilaya yangu ya Moshi Vijijini, Mkoa na Taifa kwa

kuniteua kuwa Mbunge, ninawashukuru wananchi wa Moshi Vijijini, nimefanya makubwa sana kwa kushirikiana na Serikali, kwa hiyo, ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kupongeza sana Mawaziri wote wawili kwa kazi kubwa wanayoifanya pamoja na wasaidizi wenu. Kusema kweli mnyonge mnyongeni lakini mpeni haki yake. Sisi kule Kilimanjaro katika hiki kipindi cha miaka mitano iliyopita, tumepata karibu trilioni 1.4, hii ni hela nyingi haijawahi kutokea. Kwenye Jimbo langu la Moshi Vijijini nimepata miradi mingi ya kuridhisha, bado haijatosha lakini inaridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo miradi ya shilingi bilioni 61, haba na haba hujaza kibaba. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Wasaidizi wake. Niendelee kumpongeza, kusema ukweli muundo wa bajeti unakwenda vizuri. Bajeti hii tunayoimalizia ilikuwa trilioni 50.29 na hii anayoomba tumpatie fedha sasa hivi ni trilioni 56.49, kuna ongezeko la shilingi trilioni 6.2 ambayo ni karibu *12.3 percent increment*. Kwa hiyo, ninampongeza sana tunakwenda vizuri, hii ni bajeti ya kihistoria na tunaendelea kumwombea kwa Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kuna kitu ninataka niseme hapa ambapo watu wengi hatujakisema. Tunaona kwenye miaka hii mitano tumepata mafanikio makubwa sana, kama tusingekuwa na Waziri makini wa kukusanya na kusimamia fedha hivi vicheko ambavyo tunasema tumeupiga mwingi isingekaa ionekane. Ni kwa sababu Waziri na wasaidizi wake wanakusanya vizuri, wanasimamia vizuri, tumepata miradi mingi ya maendeleo katika majimbo yetu sisi Wabunge wote. Ni kutokana na usimamizi mzuri wa Waziri na wasaidizi wake. Kwa hiyo, tunampongeza sana kwa hilo. Kusema kweli mnyonge mnyongeni, lakini haki yake lazima tumpe maua yake mkwe wangu, tunampa hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Moshi Vijijini ninajua nina miradi mingi niendelee kumwomba Waziri vile vituo vya afya viwili ambavyo bado sijapokea fedha, ninaomba nipate fedha, ukamilishaji wa zile barabara ambazo wameshaanza kupeleka fedha kule, tunaomba tuendelee kuzikarabati, ili mambo

yaendelee na watu wa Moshi Vijijini tuendelee kuipenda na kuiheshimu Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwa kuwaomba Watanzania kama alivyosema Mheshimiwa Kiswaga. Kama tunataka tupate maendeleo, tulipe kodi tuchangie kwenye maendeleo ya nchi yetu. Tusipolipa kodi kuna watu wanabeza, akiona kimeongezwa kitu kidogo anabeza wameongeza. Sasa wewe unataka huduma za afya, unataka huduma za elimu bure, maji, barabara zijengwe, nani unataka aje akusaidie kujenga barabara, vituo vya afya, kusomesha watoto wako kama siyo michango yetu sisi wenyewe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe Watanzania tusiwe wazito kuchangia kwenye kulipa kodi ambazo zitatusaidia kuendesha Serikali yetu. Tusipofanya hivyo itakuwa ni kitu cha ajabu sana. Niseme sasa hivi tumeona wadau wetu wa maendeleo wengi sijui niseme wametuchoka ama kuna kitu hakiendi sawa, sasa wale wakijitoa na sisi tusipochangia tunataka nani aendeleze maendeleo ya nchi yetu? Kwa hiyo, niendelee kuwaomba Watanzania tujitoe tuchangie ili tuweze kuiendesha nchi yetu sisi wenyewe. Tutafarijika sana na tutajisikia vizuri kama maendeleo yetu tutayaleta sisi wenyewe kwa kutumia fedha zetu za nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu kwenye kulipa kodi wanakuwa wagumu maana yake hata kwenye Biblia ukiangalia Mathayo 22:17-22, watu walienda kumuuliza Yesu je, tumlipe Kaisari kodi? Sasa, ubishi wa kulipa kodi ulikuwepo tangu enzi hizo. Yesu akawaambia ya Kaisari mpeni Kaisari na ya Mungu mpeni Mungu. Kwa hiyo, Kaisari pale alikuwa ni mtawala na hapa niendelee kuwaomba Watanzania wenzangu kama tulivyoelekezwa kwenye vitabu vitakatifu, tulipe kodi tumpe Serikali vya kwake, Serikali ndiyo Kaisari wetu ili iendelee kujiendesha vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Waziri kwa sababu kuanzia wakati wa lile janga la UVIKO tuliona uchumi haukufanya vizuri kidogo, ulishuka mpaka ukafika asilimia 2.2 na ukuaji wa uchumi kwa hii bajeti tunayomalizia umefikia asimilia 5.5 na bajeti

anayopendekeza huenda ikapanda mpaka ikafikia asilimia sita. Hii ni hatua nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mfumuko wa bei umeteremka, sasa hivi upo kwenye *digit* moja ambapo ni 3.*1 percent*, tunampongeza sana kwa hilo tunaendelea kukuombea kwamba hiki ulichoomba ukisimamie vizuri ili uchumi ufikie pale asilimia sita na mfumuko wa bei uendelee kushuka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizungumzia pato la Taifa limekua ni kitu kikubwa sana na chenye heri. Pato la Taifa linatakiwa likue liende sambamba na uchumi wa kila mtu mmoja mmoja. Sasa hapa ndiyo nina matatizo na ninapenda niishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru Mungu kwamba nchi yetu imeshaingia kwenye uchumi wa kati wa ngazi ya kwanza ambapo Pato la Mtanzania mmoja linakadiriwa kua dola 1,090. Ni jambo zuri lakini hebu tujiulize kiuhalisia wale wakulima wetu kule vijijini, wafugaji na wavuvi, Je, kuna mtu mwenye pato la uhalisia la dola 1,090? Mimi nitasema haya ni mahesabu ya kwenye makaratasi lakini kiuhalisia uchumi wa hawa watu kule vijijini haupo hivyo, upo duni na chini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu uchumi huu wa kitakwimu huwa wana-*calculate* ka kutumia *GDP* unagawa kwa idadi ya watu wote. Unachukulia kwa mfano uchumi wetu Wabunge mchango tunauotoa, akina Bakhresa, Mo Dewji, bodaboda wote wanaolipa, ukigawa kwa ile ndiyo unapata ile dola 1,090, lakini kiuhalisia kuna watu hawana hata dola 100 kwa mwaka, kuna watu huko vijijini hawana hata dola 500 kwa mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapendekea kwamba inabidi kwenye hii bajeti na mpango ambao mmeupitisha tuweke juhudi zaidi kwenye kuwasaidia wale watu wa vijijni ili uchumi tukisema kweli kama ni dola 1,090 wawe na hizo fedha. Kule vijijini tuna baraka kubwa mno. Tuna mitaji mikubwa ya ardhi inayofaa kulima na kufuga, tuna mitaji mikubwa ya maeneo ya bahari, maziwa na mito mikubwa, hivyo tunavyo vyote na tunayo baraka ya kuzalisha mazao ambayo unaweza ukayauza nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kahawa, katani, tumbaku, pamba, mchele na mahindi yote haya ni mazao ambayo tukilima yana soko kule nje. Sasa ni kwa nini 65% ya watu wetu wapo kule na tuna hizi baraka za ardhi, mazao tunayoyalima, mifugo tunayoifuga na uvuvi, kwa nini hawa watu bado uchumi wao ni duni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali kwamba tutumie hii mitaji vizuri, mpango wetu huu kama walivyoahidi tuwekeze kweli kweli kwa hawa watu ili tuwakwamue kutokana na changamoto za umaskini. Ninaishauri Serikali yangu pendwa, wote huku ni watoto wa wakulima, wafugaji na wavuvi, wafanyabishara ni wachache sana humu ndani. Ninaishauri Serikali tuendelee kuwekeza kikamilifu kwenye sekta za uzalishaji, kilimo, mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kuna ile *Malabo Declaration* na ile ya Maputo ambayo walipendekeza angalau 10% ya pato la Taifa ipelekwe kwenye hizi sekta za kilimo. Hili bado halijatekelezwa na hawa watu ndiyo wengi, tukitaka tuchomoke tupende tusipende tukiwekeza pale tutachomoka vizuri. Niendelee kumwomba Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla tuwekeze kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii bajeti ukweli wamefanya vizuri wameshaiongeza kiasi fulani, ninaomba hebu twende kama Malabo walivyopendekeza, waone maajabu kwa sababu hakuna ambacho kimeshaharibika sasa hivi, fedha kidogo ambazo wamewezeka, ninasema kidogo bado tunaona matokeo, Mheshimiwa Bashe na Waziri wa Mifugo wanafanya vizuri mambo yanaonekana. Hebu tuongeze bajeti ya Wizara ya Kilimo na ya Mifugo tuone maajabu ambayo yatatokea kwenye nchi hii kwenye kutuletea maendeleo. Kwa hiyo, wazo langu tuendelee kuziunga hizi sekta tuwapatie fedha za kutosha ile Miradi ya *BBT* ambayo imeanzishwa kama vile *BBT* Mifugo, *BBT* Kilimo na Uvuvi ili isaidie wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua muda ni kidogo pia niipongeze Serikali imeanzisha Mfuko maalum wa Bima ya Afya ili watu wetu waanze kupata huduma kule, hili ni jambo jema.

Nishauri pale walisema 70 kwenye *HIV* na 30 kwenye Mfuko wa Bima ya Afya, wengi wapo kwenye Mfuko wa Bima ya Afya watu wenye *HIV* ni kidogo zaidi. Kwa hiyo, ninapendekeza 70 ndiyo iende kwenye Mfuko na 30 irudi kwa watu wenye *HIV*. Katika hili ninaomba yale makundi maalum sasa, twende tukawasaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kabisa kwa ruhusa yako, pia niipongeze Serikali kwa kuongeza pensheni kwa wazee wastaafu. Hongera sana, wameongeza kwa zaidi ya 150%. Lilikuwa ni jambo ambalo Wabunge wamepiga kelele huku na wamewasikiliza. Hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali, wale wazee ambao hawapo kwenye ajira rasmi za Kiserikali kama ilivyo kule Zanzibar, Rais wa Zanzibar anawapa wale wazee kitu kidogo cha kununua sukari; nao tujiongeze tuangalie namna ya kuwasaidia wazee ambao hawako kwenye sekta rasmi nao wapate pensheni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi. Nilimtaja Mheshimiwa *Engineer* Dkt. Leonard Chamuriho, atafuatiwa na Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo na Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga wajiandae.

**MHE. ENG. DKT. LEONARD M. CHAMURIHO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hoja hii muhimu sana ya Bajeti Kuu. Kwanza ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuturuhusu kuwa hapa leo. Nimekuwa katika Bunge hili la Bajeti ambalo linakamilisha Bunge letu hili la Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kwanza kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutuongoza vizuri na Falsafa zake za *4R* ambazo zimedhihirisha kwamba tunakwenda

vizuri katika masuala yote na kwa kutuletea bajeti hii ambayo nitaiita ni bajeti ya kimkakati, bajeti bora kabisa ambayo nitaelezea huko mbele kwa nini nimeiita hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa vilevile kuwapongeza wasaidizi wa Mheshimiwa Rais ambao ni Makamu wa Rais Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango; Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa; Naibu Waziri Mkuu Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko na wengineo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa waandaaji wa bajeti hii nao ninawapongeza rasmi Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo pamoja na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba kwa kututengenezea kitu kizuri. Kwa sababu ya muda, ningependa vilevile kuwapongeza wasaidizi wao wote, nisiwataje majina; Naibu Mawaziri wote, Makatibu Wakuu na kadhalika kwa kutuletea kitu kizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii bajeti ni ya kimkakati kwa sababu ni kiunganisho kati ya mpango huu unaokwisha na ule mwingine unaoanza. Pia unafurahisha kwa sababu ukiuangalia muunganiko upo (kuna mwendelezo wa mambo yaliyopita na mambo ambayo tunayatarajia yatakuja). Kwa hiyo, ni kitu ambacho tunaanza kuona faida ya kuwa na Wizara kabisa ya Mipango na Tume ya Mipango, yaani ule muunganiko unaonekana vizuri na inaoana kama ambavyo inavyotarajiwa ili kuleta mwendelezo mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha uliopita 2024/2025 tulipanga kutumia shilingi trilioni 50.29 na hadi kufikia Mei tumetumia 89.6%. Kwa hiyo, tunatumia vizuri kadri tunavyopanga. Pia ukiangalia tuliopanga kutumia, tumetumia 85.3% ya hayo makusanyo. Kwa hiyo, hiyo inaonyesha tunatumia kadri tunavyopata. Basi tuboreshe makusanyo ya huko ambako tunakokusanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, nikiangalia vipaumbele vya bajeti vya mwaka huu kama ambavyo vimewekwa kwenye mpango, viko vitano.

(i) Kuna kuchochea uchumi shindani na shirikishi;

(ii) Kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma;

(iii) Kukuza uwekezaji wa biashara;

(iv) Kuchochea maendeleo ya watu; na

(v) Kuendeleza ujuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kwa nini ninasema ni bajeti ya kimkakati? Ukiangalia Dira tarajiwa hii ya mwaka 2050 ina nguzo tatu. Nguzo ya kwanza ni uchumi shindani na shirikishi na ukiangalia kwamba hiyo nguzo ndiyo hiyo hiyo ambayo ni kipaumbele cha bajeti yetu. Kwa hiyo, unaona muunganiko unakuwa ni mzuri ambao unatuletea matumaini makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nguzo ya pili ni uwezo wa rasilimaliwatu. Kwa hiyo, ukiangalia bajeti hii ilivyokuja rasilimaliwatu imepewa kipaumbele sana kwenye elimu. Bajeti ya Elimu inaashiria mkazo mkubwa katika kuendeleza rasilimaliwatu. Vilevile, kwenye afya bora, Bajeti ya Elimu nayo iko vizuri kwa kuonyesha kwamba tumeweka kipaumbele kikubwa katika kuboresha afya za Watanzania. Vilevile, tumeweka vigezo vya kuwa na rasilimaliwatu ambayo wamehamasika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nguzo ya tatu ni mazingira bora yenye kuhimili mabadiliko ya tabianchi na hii yote inajengwa na ile misingi miwili ya kwanza. Vichocheo ambavyo vimepangwa katika dira yetu hiyo, cha kwanza ni usafirishaji jumuishi. Hii wanaita *Integrated Logistics* na ukiangalia hotuba ya Bajeti Kuu, hii usafirishaji umepewa umuhimu mkubwa. Kwa hiyo, tutakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili; kuna sayansi na teknolojia; nimepitia ile bajeti, hotuba ya Wizara ya Elimu inaonyesha kwamba kuna mkazo mkubwa kwenye sayansi na teknolojia, mpaka kuna bajeti za wanafunzi waliofanya vizuri katika sayansi wanapewa *scholarship*. Kwa hiyo, ni vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu; kuna hili la utafiti na maendeleo na ubunifu wa *RND* ambayo nayo imeongelewa na wenzangu waliotangulia. Kwa hiyo, sitairudia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiangalia hapa kuna muunganiko mzuri sana kati ya Dira tarajiwa hiyo ya 2050, Mpango wa 2025/2026 pamoja na Bajeti Kuu. Sasa, nikiingia kwenye Bajeti Kuu moja kwa moja, nikiangalia katika aya ya 138 mpaka aya ya 170 kuna mabadiliko ya sheria pendekeze ili kuongeza uzalishaji katika viwanda vyetu. Hizo ni hatua za kikodi ambazo zimefanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia kwa mfano aya ya 139 kuna kusamehe *VAT* kwenye vipuri vya matrekta, magurudumu na kadhalika. Aya ya 146 kuna kudhibiti uingizaji wa bidhaa mbalimbali: nondo, misumari na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, hili la nondo nilitaka niliulizie hapa. Juzi nilipita kwenye *site* moja huko ambako tunakopitapita sisi wahandisi, nikavutiwa na kuangalia nondo. Nondo hizi zinatoka wapi? Nikabaini kwamba nondo hizi zinatengenezwa hapa hapa nchini, kampuni sitaitaja kwa sababu itakuwa namtangazia biashara, lakini viwango vyake ni vile vile ambavyo tunavitaka, ambavyo zamani tulikuwa tunaulizia kwamba tunataka nondo tunasema ya *BS (British Standard)*. Pia, ukiangalia hata hizi, viwanda vyetu vimeweza kutoa nondo za hali ya juu kiasi kwamba unaona wazi kwamba tunakwenda vizuri kulingana na mpango na tunakwenda vizuri kulingana na Dira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, hivi viwango vya kikodi vimelenga hasa katika kulinda bidhaa za ndani. Hii inakwenda vizuri lakini sasa ambacho sikukiona ni mpango au marekebisho ya sheria ambayo yanakwenda kulinda huduma hasa na nitaongelea hapa huduma za wakandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakandarasi wa ndani ambao wanatoa huduma nzuri kwetu sisi ambao tunataka hawa wakandarasi waweze kukua. Vilevile, waweze kutoka hata nje ya nchi yetu kwenda kufanya kazi zao hizo za ukandarasi. Sasa, ili

wafanye hivyo na huduma hii nayo inabidi tuilinde ili iweze kufikia mafanikio hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sheria ambazo zinalalamikiwa na hawa wakandarasi, basi hizo nazo tuzijumuishe katika mipango ya baadaye ya kuziboresha ili tuweze kuwa na wakandarasi ambao wanakuwa na ambao wanahamasika ili waweze kutoa huduma nzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependekeza kwa Waziri wa Fedha, lakini hata awamu ya sasa au ya baadaye waangalie. Kwa mfano wakandarasi, sheria ambazo wanazilalamikia sana ni sheria za kikodi ambazo wanalazimika kulipa kodi kabla hawajapokea fedha zao za kazi waliyoifanya. Sasa, hili linawaumiza kidogo. Kwa hiyo, katika haya mapendekezo ambayo ni ya kikodi ya kulinda bidhaa za ndani, basi tuwajumuishe na wao katika sheria za kikodi ambazo zitawalinda nao waweze kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, anapofanya kazi mkandarasi anapopewa ile *certificate* tayari *TRA* mwezi huo huo wanadai *VAT* ya gharama ile aliyotakiwa kulipwa. Sasa, ile anakuwa anatozwa fedha kabla hajapokea ile fedha. Kwa hiyo, kama mapendekezo ya sheria hizi yakiwajumuisha na wao itawasaidia sana ili waweze kupata *cashflow* nzuri, waweze kukua na waweze kuhamasika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mpango wa mwaka huu vilevile nimeangalia pale ukurasa wa 104 mpaka 122, Kiambatanisho Na. 1, kuna orodha ya miradi 423 ambayo imepangwa kutekelezwa katika mwaka ujao wa fedha na miradi hiyo jumla yake ni shilingi trilioni 15.86. Ni vizuri kabisa kwamba miradi hii imo kwenye mpango, lakini miradi hii ukiiangalia, ukiifanyia uchambuzi utaona iko ya aina mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi mikubwa, kuna miradi midogo, kuna miradi ambayo imekwishaanza kutekelezwa na kuna miradi ambayo ni mipya. Sasa, ninapendekeza kwa Waziri kwamba, kipaumbele kiende kwa miradi ambayo imekwishaanza ili iweze kukamilika na tuweze kupata manufaa yake ili isaidie katika kuendeleza pato la Taifa kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingi ambayo inayokaa kwa muda mrefu bila kukamilika, isipofanya hivyo kwa mapema inazua riba ambayo tena inatuletea gharama ambazo hatuzitarajii. Hivyo, ningeshauri miradi ambayo imekwishaanza ndiyo hiyo ambayo tuendelee nayo na tuikamilishe ili tuweze kupata manufaa yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia kengele imelia. Ninakushukuru kwa hayo, ninapenda kuunga mkono hoja na kuahidi kwamba katika siku ya kupiga kura bajeti hii nzuri nitaipigia kura ya ndiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Engineer* Dkt. Leonard Chamuriho. Tunaendelea na Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo ajiandae.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi hii, lakini ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu kunipatia nafasi hii tena ya kuchangia kwenye Bajeti Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti yetu hii ni bajeti ya kimkakati. Ukisoma utakutana na mambo ambayo yanaonyesha wazi kwamba kuna mambo ya kimkakati yameingia huku ndani. Kwa mfano wanapendekeza kwamba tunakwenda kusamehe ongezeko la *VAT* kwenye viuatilifu, (viua wadudu) kule mashambani na *codes* zake zimeonyeshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake kwenye Sekta ya Kilimo tunakwenda kufanya vizuri kwa sababu sasa wadudu wanaosumbua mashambani kwa kuondoa tu hiyo *VAT* tutakuwa na uwezo wa kuwafikia wengi zaidi na wataweza kufanya vizuri kwenye mashamba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiendelea unaona wanapendekeza kusamehe *VAT* kwenye miamala ya bima. Tunaona kabisa kwamba tunakwenda kuimarisha bima za kwetu hapa nchini ambazo vilevile zitakwenda kuvutia watu wengi

kushindana na hizo kampuni nyingine na wakati huo huo kuongeza ajira kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaona vilevile tunakwenda kuondoa *VAT* kwenye bidhaa za nguo ambazo zinaenda kutumia pamba inayotoka Tanzania. Kwa hiyo, utagundua kwamba pamba tunayolima sisi sasa itakwenda kuwa kama tumeongeza unafuu wa wale wakulima wetu kule shambani, kwa sababu ina maana viwanda tulivyonavyo ndani ya nchi hii vinavyotumia pamba hii ya kwetu vitakuwa vimepunguziwa *VAT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiendelea utagundua yako mengi yaliyotajwa. Mafuta yetu ya kula yameondolewa *VAT*. Yalikuwepo majaribio ya mwaka mmoja, sasa tunakwenda kuendelea na zoezi hilo. Tunaweka unafuu kwa Mtanzania wa kawaida aweze kununua mafuta yaliyo safi ndani ya nchi hii na hivyo hivyo kuweza kuviongezea uwezo viwanda vyetu vinavyotengeneza mafuta haya ya kula ambayo yatakuwa yanatumika nchini na wakati fulani yataweza kuuzwa hata nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaona kabisa kwamba kwenye bajeti hii wanakwenda kuweka unafuu au kuondoa kabisa *VAT* kwenye ununuaji wa matairi ya matrekta. Tunajua kabisa kilimo kwenye maeneo mengi ndani ya nchi hii kuna sehemu wanatumia matrekta. Sasa tunaenda kuyapunguzia haya matreka *VAT* hii. Maana yake mwenye trekta sasa anakwenda kupata matairi kwa bei nafuu kidogo. Maana yake ni kwamba tunakwenda vilevile kuwezesha kilimo chetu kiwe cha kisasa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaona pia wamesema wanakwenda kupunguza au kuondoa *VAT* kwenye gesi silia. Ukiondoa kwenye gesi asilia maana yake unaongelea habari ya kufanya sasa gesi asilia iwe na bei nafuu ambayo inaweza kutumika na watu wengi zaidi. Wanajua kabisa kwamba tumekuwa tunazungumzia ndani ya nchi hii kwamba tunahitaji ikiwezekana magari ya Serikali sasa yatumie gesi hii kwa ajili ya kupunguza gharama ya mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukiona bajeti ambayo inaongelea sasa kuondoa *VAT* kwenye eneo hili unaijua hii ni bajeti ya kimkakati. Kwa hiyo, yako mengi ambayo yameandikwa na ninaamini kabisa yakitekelezwa haya tutakwenda kuona unafuu mkubwa kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia tena kwenye Sura ya 342 ya kodi zetu, wamesema wanaenda kuweka unafuu katika kuondoa kwenye kodi ya mapato ya pikipiki au vifaa vyenye matairi mawili (pikipiki au bodaboda hizi) na guta ambavyo vinafanya kazi kubwa sana kule vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoondoa hiyo kodi ya mapato ikirekebishwa kule kwenye pikipiki (bodaboda), tuna watu wengi sana Tanzania sasa hivi ni bodaboda wameajiriwa kwenye Sekta hii. Kwa hiyo, maana yake tunaweka unafuu mkubwa kwenye wananchi wetu kule kwenye maeneo yale. Kwa hiyo, yako mengi ambayo yamesemwa hapa, ndiyo sababu nikasema hii inaonekana kabisa ni bajeti yetu ya kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Waziri wa Mipango na Uwekezaji, wataalam na Naibu Mawaziri, kwa kazi kubwa ambayo wamekuja nayo hapa ambayo inatupeleka mahali fulani ambapo tunapaona kwamba patakuwa ni pazuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ya utekelezaji wa Ilani au utekelezaji wa bajeti iliyopita. Tutakumbuka wazi kwamba tumeona hakuna sekta yoyote ambayo inaonekana imesimama kama ilivyo. Bajeti yenyewe ya mwaka jana ilikuwa shilingi trilioni 50.29 na bajeti ya mwaka huu imekwishakwenda kwenye shilingi trilioni 56.49. Maana yake kuna mambo yanakwenda kuongezeka hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba iko michango mingi imetoka huko nyuma ikionyesha kwamba inawezekana tuki-*equate* na kwenye dola tukaona kama bado siyo kubwa sana, lakini kiukweli ni kwamba bajeti imeongezeka na mambo makubwa yanakwenda kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye pato la Taifa tunaona kabisa kwamba pato la Taifa limekua kwenda kwenye asilimia 5.5. Ni kweli, uhalisia kwenye *researchers* unaonyesha wazi kwamba kama itakuwa linakuwa chini ya asilimia nane maana yake bado tutakuwa hatuendi vizuri sana. Kwa hiyo, niwapongeze watangulizi waliolisema hili kwa sababu hii ni wazi kwamba tunatakiwa tuendelee kusimamia hizo sekta za uzalishaji, zitutoe hapa tulipo twende kwenye pato la asilimia 8.8 kwenye ukuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika hizo kwenye utekelezaji, ukiangalia utekelezaji uliopita kwenye mwaka wa fedha uliopita yako mambo mengi yametokea ambayo yanatuashiria kwamba kama tukisimama imara tunaweza kwenda vizuri zaidi kuliko hata ilivyokuwa mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme, tunajua wote umeme ilikuwa ni changamoto lakini Bwawa la Mwalimu Nyerere lenye megawati 2,125 limekwishaongezea kwenye umeme. Hoja yetu kubwa sasa kama Wizara ya Fedha ni kuwezesha umeme huu sasa utumike kwenye viwanda tulivyonavyo na upatikane bila kuwa na *interruption* (usikatikekatike).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa tuliyonayo tena pamoja na kuwa na umeme ni ndugu zangu wa Viwanda kuhakikisha kwamba tunapata viwanda. Wale ambao tumehudhuria mawasilisho mengi imeonekana hata ile *American First* inatupatia sisi *tariff* ya chini. Tuna uwezo wa ku-*attract* wawekezaji wengi wakaja huku kwetu na tukaendelea kufanya vizuri zaidi tukiwa na umeme huu tulionao.

Japokuwa kwenye umeme bado tunatakiwa tuendelee kuweka mkazo kwamba, tunatakiwa tuongeze umeme kwa sababu, baadaye umeme tulionao utakuwa kidogo, ndani ya miaka mitano tu ijayo kwa sababu, uzalishaji utakuwa ni mkubwa. Tumeona kuna ujenzi wa daraja ambalo linafunguliwa tarehe 19, la Busisi – Kigongo. Ninatokea eneo lile, pale tulikuwa tunavuka kwa nusu saa, sasa hivi ninakadiria tutavuka kwa dakika sita au saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni sawasawa na *SGR*, tulikuwa tunasafiri kwenda Dar es Salaam kwa saa tisa, sasa tunakwenda kwa saa tatu na robo. Ukicheza na muda maana yake ni tayari ile sehemu inayobaki, wale wanaosoma *grant activities* zile utagundua, kama muda unaobaki tutaufanyia uzalishaji wa kitu kingine. Kwa hiyo, tutakuwa tunainua uchumi wetu kwa kadri ambavyo tunacheza na muda ule. Ukiangalia, pamoja na hiyo *SGR,* kuna vipande vingine ambavyo navyo kwenye bajeti iliyopita vimeanza kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipo cha Tabora, cha Isaka kwenda Mwanza kimeshakwenda 14% cha hapa kutoka Makutupora kwenda Tabora kipo asilimia takribani sita na vingine; kwenda Makutupora hapa kimeshakwenda kwa *percent* kubwa. Tuendelee kuweka mkazo kuhakikisha kwamba, haya mambo yanakamilika, kama tutaweza kuwa na reli inayotoka hapa kwenda Mwanza, inayotoka hapa kuunganisha Kigoma, uchumi huu utakimbia kuliko unavyokwenda leo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haya niliyoyazungumza hapa tuna mambo kadhaa yametokea kwenye sekta mbalimbali. Tumeona kwenye Sekta ya Elimu, wamelinganisha kutoka uhuru mpaka leo, kuna mahali fulani unaona uvivu kuisema kwa sababu, kuna mahali labda vyuo vilikuwa 41 leo vipo 2,000 na kitu, maana yake ni kwamba, kazi iliyofanyika ni kubwa sana. Sasa kama sekta hizi zimeshafanya kazi kiasi hiki, kazi yetu kubwa kwenye bajeti hii ni kuongeza kuchochea kuhakikisha kwamba, kwenye elimu tunakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshaonekana tunakwenda vizuri, lakini kwenye kilimo twende vizuri, kwenye ufugaji twende vizuri kwa sababu, hizi sekta za uzalishaji ndiko mahali tunapoweza kupata mapato haya, yakapanda haraka. Hata haya yanayoongelewa, yanaonekana ni madeni, tunaweza kuyalipa kwa urahisi kwa sababu, sekta za uzalishaji zimefanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tunategemea kuwa na skimu za umwagiliaji. Leo hii yapo maeneo mengi ambayo tungetegemea skimu ziwepo, hatujaenda vizuri sana kule, ni kwa

nini? Inawezekana tulibajeti kwamba, tutapeleka shilingi trilioni moja, lakini fedha iliyokwenda ni shilingi milioni 600 au ni bilioni 600 au bilioni 500, maana yake ni ile shilingi bilioni 500 ambayo haijaenda zile skimu hazijakamilishwa kama tulivyotarajia na matokeo yake sasa ni kile ambacho tunakifikiria, kama tunakwenda kwa kiwango hicho, tunakuwa hatujaenda kwa kiwango tarajiwa. Kwa hiyo, nawaomba sana, yale ambayo tumeyasema kwenye uzalishaji, leo tunasema tulikuwa na viwanda viwili au vitano vya nyama, lakini je, hiki ambacho tunakifanya sasa hivi tunaweza kukifanya tena miaka mingine miwili tukawa na viwanda labda 20 au 30, ili tuweze kuuza nyama yetu nyingi na maziwa mengi nje ya nchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna kazi kubwa kwenye bajeti hii tunayoishughulikia sasa hivi tuhakikishe kwamba, inakwenda kututoa mahali fulani kwenda mahali pengine kwa sababu, kilichoongezeka, kiongezeke vilevile katika uzalishaji kwenye sekta za uzalishaji. Tofauti na hivyo tunaweza kuwa tunafanya maoteo makubwa na kama inakwenda kidogo basi hatutaona matokeo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda ninaomba niunge mkono hoja na ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa. Nilimtaja Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, ajiandae.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Bajeti Kuu ya Serikali. Awali ya yote kwanza ninachukua nafasi hii kwa dhati kabisa kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Bahi kwa kuniamini kuwa mwakilishi wao ndani ya miaka hii mitano. Kwa ushirikiano wao na kwa pamoja na Serikali, wilaya na jimbo letu tumeweza kupata maendeleo makubwa katika nyanja mbalimbali. Ninapenda kuwashukuru kwa dhati kabisa kwa heshima kubwa hii ambayo wamenipa na nataka niwaahidi kwamba, bado nina nia ya kuendelea na sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu katika Ukanda wa *East and Central Africa* inaongoza kwa uzalishaji wa mahindi na kwa kiasi kikubwa Tanzania inategemewa. Biashara ya mahindi kwa *East and Central Africa* ni takribani dola bilioni 6.7, lakini *the epicenter* mzalishaji mkubwa akiwa ni Tanzania na mwaka jana, 2024, tulipata mavuno jumla ya tani milioni 8.01, lakini 70% ya uzalishaji huu ni jembe la mkono, 20% ni jembe la kukokotwa na ng'ombe na 10% ni *mechanization*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kiasi kikubwa pamoja na kwamba, tu sisi tunategemewa kwa Afrika Mashariki na Kati katika kuzalisha mahindi, lakini bado tunatumia jembe la mkono kwa sababu, 70% ya wakulima wetu ndio wanaochangia na wanatumia jembe la mkono. Ninadhani inatakiwa tuwe na kampeni mahususi ya kutoka kwenye jembe la mkono twende kwenye jembe la kukokotwa na ng'ombe; kama ambavyo tulifanya kampeni mahususi ya kumtua mama ndoo kichwani na kampeni mahususi ifanyike ya kuachana na jembe la mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa jembe la ng'ombe linauzwa 160,000 kwa bei ya rejareja, bei ya jumla ni 130,000, lakini majembe haya yanazalishwa nje ya Tanzania. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali, kwanza ichukue hatua madhubuti ya kutafuta muwekezaji aje kuweka kiwanda hapa cha kuzalisha majembe yanayokokotwa na ng'ombe, lakini vilevile, kama ambavyo tunatoa *incentives* kwa uwekezaji, huyu apate *incentives* kubwa sana, ili wananchi wetu waweze kupata jembe hili walau kwa 80,000 au 100,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivi tunaenda kuachana na kilimo cha kutumia jembe la mkono ambacho si kilimo, ni kilimo cha adhabu, ile ni *corporal punishment*. Kwanza kinakuzeesha, lakini vilevile unalima huku upo kwenye adhabu kwa hiyo, ninaomba Bajeti ya Serikali iangalie kumtafuta muwekezaji wa majembe ya kukokotwa na ng'ombe, tutoke kwenye 20% sasa tupande, tupunguze kule kwenye 70%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa mahindi kwa nchi yetu, umwagiliaji ni asilimia 2.5 tu. Mahindi yote haya asilimia kubwa yanategemea mvua kwa hiyo, kilimo chetu bado ni cha

kubahatisha na utaalam unaonesha kilimo cha umwagiliaji, kilimo cha kawaida cha mvua kinatoa tani 1.6 kwa hekta, lakini ukimwagilia kinatoa takribani tani tatu mpaka 5.7 kwa hekta. Kwa hiyo, kwa vile nchi yetu inategemewa kwa uzalishaji wa mahindi ipo haja ya kubadili Kilimo chetu, badala ya kuwa tunategemea mvua sasa kiwe kwa umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Kanda ya Kati tumekuwa waathirika zaidi, mwaka huu tuna mvua, mwaka mwingine hatuna mvua, njaa kubwa, hakuna njaa. Kwa hiyo, Serikali iangalie jambo hili kwamba, sasa tutoke kwenye kutumia mvua katika kilimo cha mahindi kiwe cha umwagiliaji. Kwa kufanya hivyo, tutaweza kuongeza mavuno ya kutosha na vilevile wakulima wetu waweze kupata ahueni kubwa sana ya kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye majembe; jembe la kukokotwa na ng'ombe Serikali ifanye uwekezaji, lakini vilevile kwa sasa kivutio kubwa cha kilimo ni kwenye bustani na matunda, ambayo tuseme ni *horticulture*. Kilimo hiki kinavutia zaidi vijana kwa sababu, vijana shuruba ile ya kutumia jembe la mkono wengi hawaiwezi kwa hiyo, wanaenda kwenye bustani, lakini kwenye bustani umwagiliaji unatakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo *pump* za umwagiliaji ambazo hutumii *solar energy* wala umeme, unatumia nguvu yako, kama ile *pump* ya *moneymaker* inauzwa shilingi laki tano, lakini nayo inazalishwa kutoka nje. Kwa hiyo, eneo hili nalo Serikali iangalie kwa makusudi kabisa iweke mwekezaji, kwa ajili ya kuzalisha mashine hizi. Tukifanya hivyo, tutaenda sawasawa na Sera ya Wizara ya Kilimo, ambapo wameongeza, wameleta magari, kwa ajili ya kutoboa visima vya umwagiliaji vijijini, tukiwa na eneo hilo tutaweza kuwapa vijana wengi fursa ya kununua mashine hizi, hizi *pump,* ili waweze kufanya kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu uwekezaji wa kilimo, sambamaba na reli ya *SGR*. Ukitoka kuanzia Soga *station* unashuka sasa huku huoni shamba lolote la kilimo la kibiashara. Mgeni akitoka nje ya nchi akipita kwenye reli anaona nchi hii hawalimi, *completely* hakuna *commercial farms*, hakuna

hata kilimo cha nyasi; kutoka Soga unapita pale Ruvu, maji yanatiririka hakuna hata kilimo cha matunda, hakuna hata kilimo cha nyasi, hakuna umwagiliaji, unakuja unashuka ukija Dodoma kwetu, huku sasa ndiyo kukavu. Kwa hiyo, mgeni akija jambo la kwanza atashangaa, nchi hii mbona hailimi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli ukitembea *along* reli huoni kama tunalima. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali kwanza ukiwekeza sambamba na reli unatengeneza *logistic harbour* nzuri za matunda na mbogamboga kwenda kuzipeleka katika masoko, lakini vilevile kama nilivyosema kuondoa aibu kwamba, nchi hii hawalimi ni kuweka *commercial farms*. Bahati mbaya Mkonge upo kule kwenye barabara, lakini kwenye reli hakuna kabisa ni nyasi. Kwa hiyo, Serikali iangalie namna ya kutoa aibu hii ambayo mtu akija anajua hawa watu hawalimi hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua nafasi hii kwa dhati kuipongeza Serikali, kwenye suala zima la kilimo imefanya uwekezaji mkubwa hususani katika sekta ya mabwawa. Kwenye mpunga tumeona fedha nyingi zimeenda, karibu mabwawa 780 yameweza kujengwa katika kipindi hiki cha miaka mitano, lakini kubwa zaidi tumeona ubunifu mkubwa uliofanyika wa kuwa na magari ya kuja kutoboa visima kwa wananchi wa vijijini badala ya kutumia maji, kwa ajili ya kunywa na matumizi mengine sasa twende katika sekta kubwa ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninashukuru sana. Ninampongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo katika kipindi hiki cha miaka mitano ya uongozi wake tumeona mapinduzi makubwa ya utekelezaji wa bajeti hii, ambayo imeenda zaidi ya nusu, ambavyo wakati mwingine ilikuwa haiwezi kufikia katika kiwango hiki. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo. Nilimtaja Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kupata nafasi hii kuchangia katika bajeti yetu hii ya mwisho, Bajeti Kuu ya Serikali. Kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge wenzangu hapa, ninaunga mkono hoja zote mbili kwa kishindo kabisa na nitaeleza msingi wa kuunga mkono hoja hizo kwa nguvu kabisa kwa sababu ya mambo makubwa ambayo tumeyapata katika jimbo letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uhakika kabisa tunacheza na tutashinda na kwa ridhaa ya wananchi na ridhaa ya Chama Cha Mapinduzi nina imani tutarudi tena hapa kuendeleza miradi mizuri, ambayo tulikuwa tumeianza. Kwa hiyo, wale ambao wanafikiri hatuchezi na hatutakuwa na nguvu ya kushinda, tutacheza na tutashinda kwa kishindo kikubwa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu, miradi mingi ambayo tumeipata katika Jimbo la Kilombero, Mkoa wa Morogoro na nchi yetu inatokana na mipango ya Serikali na ukusanyaji wa fedha unaoufanya wewe na watumishi wako wa chini pamoja na Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa sababu, hii ni hotuba yetu ya mwisho katika Bunge hili kabla hatujarudi hapa Novemba, *insha Allah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu ni muhimu tukawakumbusha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunaingia hapa mwaka 2020 Novemba, 2021, 2022, 2023, 2024, 2025 yapo mambo makubwa tulikuwa tunalalamikia katika jimbo letu. Leo nimesimama hapa kwa heshima kubwa kusema mambo yale yamekamilika na ni kutokana na mipango ya Serikali na utafutaji fedha wa Wizara ya Fedha kwa ujumla, chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, ndiyo maana tumeyapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kilombero ulikuwa unaweza kufanya yote, lakini kuna lami yao, ile barabara ya lami, kama haijakamilika ile haupati, huwezi kurudi kuchaguliwa tena. Leo ninazungumza hapa, nilikaa chini kwenye kapeti, nilikaa kwenye matope kupiga kelele kupata barabra ile, tumepata fedha, tumeletewa fedha, leo barabara ya lami watu wanateleza kutoka Ifakara kwenda Kidatu lami imekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, tumepata Barabara nyingine ambayo imesainiwa, ya Ifakara – Kikwawila – Mbasa – Lipangalala kwenda Malinyi. Tumepata barabara nyingine ya Ifakara kwenda Mlimba, ambayo Mkandarasi kaanza. Ninamwomba tu Mheshimiwa Waziri anihakikishie kwamba, imesainiwa barabara ya Ifakara kwenda Malinyi, basi ianze kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata Daraja jipya la Ruaha, tumepata kiwanda kipya cha sukari, shilingi bilioni 700, Mwenyezi Mungu anipe nini tena. Jimboni kwangu zimekuja karibu shilingi bilioni 750 za uwekezaji za kiwanda kipya cha sukari, *K4*, ambacho Mheshimiwa Rais ameweka jiwe la msingi na wakati wowote kinaweza kwenda kuzinduliwa, kilichobaki hapa sasa ni tunafuatilia tu kuhakikisha wakulima wetu wanapata haki yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu wilaya imeumbwa sasa hivi tumepata hospitali ya wilaya, vituo vya afya viwili, zahanati 12, sekondari za *O'level* 12, sekondari za *advance* tano, shule za msingi nane, madarasa zaidi ya 100, *substation* ya kuondoa kukatikakatika kwa umeme shilingi bilioni 25. Tumepata miradi ya maji mingi sana na mradi mmoja mkubwa wa shilingi bilioni 41, haijawahi kutokea katika Jimbo la Kilombero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu wilaya imeumbwa, jimbo limeumbwa, hatujawa na Mahakama ya Wilaya. Tumepata Mahakama nzuri ya Wilaya, tumepata Kituo cha Polisi kizuri cha Wilaya, tumepata magari ya polisi, magari ya zima moto, ofisi mpya ya Mkuu wa Wilaya ya ghorofa na minara ya simu zaidi ya sita. Sasa tumepata chuo cha *KATRIN,* kinaboreshwa, kitakuwa ni sehemu ya kuhaulisha vifaa vya Kilimo. Tumepata miradi ya bonde itakuja kujenga mabwawa ya umeme, Miradi ya *TACTIC* ya soko jipya, stendi mpya, lami, visima vya maji na tumepata ziara ya Mheshimiwa Rais; amekuja katika jimbo letu kutuzindulia kiwanda na barabara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya yote makubwa yamefanywa chini ya Wizara ya Fedha na mipango mikubwa ya nchi hii. Ninaunga mkono hoja kwa 100% kwamba, wananchi

wakitupa ridhaa tena tutaendeleza yale machache yaliyobaki, ambayo nitasema baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto kwenye barabara za mitaa, kuna changamoto kwenye mambo ya bei ya miwa na sukari ambapo tuna imani wakitupa ridhaa tena tutaendeleza kwa kiasi kikubwa. Haya niliyosema ni machache tu, lakini kwa undani wake kuna mambo makubwa sana, wananchi wangu wa Kilombero ninawaomba tushikane mkono na Chama Cha Mapinduzi, tumuunge mkono Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan na tusiwasikilize wale wapotoshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna rafiki yangu mmoja na rafiki yake kaka kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, anaitwa John, alikuja na chama chake siku za karibuni akaongea mengi sana ya kuiponda nchi. Anasema nchi gani hii? Inaongozwaje? Imeuza bandari, imeuza sijui nini! Waziri Mwigulu anazunguka tu duniani! Kaponda weee, kamaliza hata tofali moja hajaacha! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuibie siri, nimegundua kumbe wale watu wanaenda kuchangishachangisha pale elfu moja tuchangie mafuta, kumbe zile elfu mojamoja, elfu mbili, wengine wanawapa. Yaani inakuwa kama ile pata potea ya kamari ya Kariakoo, ukisimama ukijifanya unatoa hela unashiriki kwenye kamari kumbe unaliwa wewe, wenzako wanaenda kugawana pembeni baadaye. Kwa hiyo, wanawagawia wachache wanaenda kutoa elfu mojamoja, elfu mbilimbili na wengine wanapeleka mikono mitupu kwenye sanduku lile. Mtu anaongea mishipa mpaka inamtoka, anatukana watu nchi hii haina chochote, nchi hii haifai, nchi imeuza bandari! Mimi nipo Kamati ya Miundombinu na bandari haijauzwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumia fursa hii kuwaambia wananchi wa Jimbo la Kilombero haya mambo nimeyasema hapa yapo kule, hakuna maendeleo yanayokuja kwa kujengwa siku moja. Tumesema humu mikakati imewekwa, fedha zimetafutwa, tumepata miradi kwa hiyo, wasidanganyike na mtu yeyote, ambaye anataka kuleta propaganda na siasa nyepesi nyepesi, kama kaka yangu huyu John ambaye namheshimu

sana, lakini hajabisha kwamba, alilala na kusinzia kwenye treni, kama nilivyosema hapa. Katika Bunge lililopita alikuwa Mbunge alibisha kwamba, Serikali ya CCM haiwezi kujenga *SGR,* lakini nimemkuta kapanda na kasinzia kwenye *SGR*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kasema kule jimboni kwangu kwamba, japokuwa nimepanda nikasinzia, lakini treni sio la baba yako. Sijasema kama treni ni ya baba yangu, nimesema yeye alipinga humu CCM haiwezi kujenga, sasa hivi imejenga na yeye amepanda akasinzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, sisi changamoto kubwa ni barabara za mitaa. Tuna mpango wa kilometa 10 za barabara za mitaa kwa kila kata katika kata 19, imani yetu ni katika mpango ujao wa Serikali tukipata hiyo itatusaidia kupunguza changamoto kubwa za wananchi wetu. Tutasimamia hizi barabara za kuunganisha na wilaya nyingine, kilimo cha miwa, kituo hicho cha *KATRIN* na haya mabonde ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa ninamalizia yapo mazuri katika bajeti hii na kuna changamoto ambazo tutazishauri. La kwanza ni bima ya afya; wamesema Wabunge wengine hapa na mimi nina maoni, sasa hivi kuna vinywaji ambavyo tunakunywa baada ya miaka 20, 25, watu watapata *BP*. Kuna kinywaji kimeandikwa kabisa hii usinywe zaidi ya moja, energy, lakini kuna vijana wetu wanakunywa sana huko. Hakuna sababu ya vinywaji kama hivi kupunguza kodi, wekeni kodi iende bima ya afya isaidie masikini wa nchi hii kutibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza sana katika kupambana na *HIV/AIDS* na mpango mkakati wa kuzuia Bajeti ya Serikali na mitikisiko ya kiuchumi. Kwenye *economics* wanasema *certainty* zinazotokea duniani, juzi nimeona Israel na Iran imeanza, bei ya hisa na mafuta ime-*shake*, athari zitakuja kwetu. Kwa hiyo, wakati huu tupo kwenye bajeti tutazame kama zile shilingi bilioni 500 zinaweza zikajitosheleza zenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono zile kodi zote katika *elasticity of demand* ambazo mmezipandisha, kwa mfano bia na nini na nini, hivyo ambavyo hata vikipanda bei watu

wataendelea kunywa, ili viendelee kusaidia masikini. Viuatilifu wamepunguza kodi, nyongeza ya mishahara naunga mkono, kuwajali bodaboda na bajaji naunga mkono, namuunga mkono *TRA,* Mwenda anakusanya kodi bila kusumbua wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona Mheshimiwa Waziri amesema, katika sera hapa kwamba, hakuna kanuni inayokuja sasa, biashara hazitafungwa tena; ni jambo kubwa sana ninaliunga mkono na kwa kweli, tunatakiwa tumpongeze sana Kamishna wa *TRA,* hata juzi nilikuwa *TRA* pale. Nimeona asubuhi kwenye maswali hapa, kwamba, watu wanasema ile *TIN* miezi sita bado watu wanatozwa, mimi sijatozwa. Kwa hiyo, wameshafanya kazi kubwa na nimeona mfano mzuri kutoka *TRA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishati safi 80% kufikia 2034 ni jambo kubwa, ujenzi wa Makao Makuu Dodoma ninaunga mkono, kupandisha mishahara kima cha chini mpaka laki tano, ninaunga mkono na mkakati wa kupunguza *importation* na kuongeza *exportation* katika *economics* ni jambo la msingi sana. Mheshimiwa Waziri tunakutana na watu kibao, China kule Guangzhou, lakini ni muhimu tukawa na mipango na Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango, mtu anaenda China tum-*discourage* kama anaenda kununua ma-*toy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakutana na watu kule, China, dada zetu wengine mpaka unamshauri cha kununua. Yaani mtu anasafiri anaenda China anafungasha ma-*toy* wakati kuna bidhaa za msingi. Katika nchi yetu tunaweza ku-*discourage* vile vitu ambavyo havina maana kwa kuongeza kodi na kupunguza kwa vile vya muhimu, kama majembe ya umeme; sasa hivi kuna jembe unalivaa mgongoni tu hapa, linalima kama mota, tu-*discourage* wale wanaenda China kununua ma-*toy* na vitu ambavyo sio muhimu sana, ili kupunguza *importation* na kuongeza *exportation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kwa kumalizia changamoto na maoni yangu ni suala la kodi kwa hisa ambazo hazijagawanywa kwenye kampuni. Ninashauri Mheshimiwa Waziri, mjaribu kulifikiria, hili haliwezi kuwa *double tax*, sisi tuna kampuni yetu tumepata faida, tumelipa kodi zile hisa ambazo

hazijagawanywa, nafikiri Mheshimiwa Waziri atanisaidia kulifafanua vizuri jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, wakandarasi walipwe. Kuna miradi ya maji kule kwangu, kuna mzee wangu mmoja mpaka leo bado hajalipwa. Ninaomba alipwe na hapahapa Mheshimiwa Waziri nasema kwamba ni muhimu sana kabla ya kusaini miradi mingine mipya, hii mikubwa ya Serikali, ambayo imesainiwa basi ikamilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamalizia, Mheshimiwa Waziri watoe elimu kuhusu Deni la Taifa. Ninataka niwahakikishie kuna watu wanapotosha kuhusu Deni la Taifa na wengine wanafikiri Mheshimiwa Waziri Mwigulu akikaa pale anajiamulia tu kukopa. Kuna mwananchi wangu mmoja nilikuwa namwelimisha juzi, anafikiri Waziri Mwigulu nyuma ya mlango wake kule kuna fedha za wananchi. Anasema, bwana mafedha si anakaa nayo Wizarani pale na Waziri Mwigulu anavyong'aa hivi, basi anajua basi yeye ndiyo anakula tu fedha zetu, pole sana kaka yangu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inabidi mtoe elimu kuhusu Deni la Taifa kwa sababu, watu wengi sana wanapotosha. Kwa kumalizia naomba kusema kwamba, kwenye ujenzi, mabati ya *gauge* 30 sisi watoto wa fundi cherehani ndiyo tunatumia kujengea, kodi iwe *zero*. Nondo kwa mfano, chini ya milimita 16 ambazo tunajengea kwenye nyumba zetu kule kodi ipungue, *cement* ile 32.5% ipungue. Sisi tunajenga kwa matofali ya kuchoma na tope, tukifika pale tunakazia na nondo milimita 10, 11, mabati yangu mimi ni ya *gauge* 28 hayo, waweke kodi kwenye miradi huko, kwa wakandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bati *gauge* 30, ukikunja hivi linakunjika, kodi ya nini? Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mwigulu, amefanya kazi nzuri sana ili tuendelee kujenga nyumba huko tunakokwenda, wananchi wetu ni vizuri sana wakawasaidia katika kupunguza kodi katika vitu ambavyo wanavifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni dunia ya *artificial intelligence*. Juzi nilikuwa ninaona hata kama hujasoma *accounting* kuna *course* ukisoma miezi mitatu unaweza kufanya uhasibu, kama mhasibu, dunia ambayo tunaenda. Tunaomba sana, wwekeze huko wanakoenda katika mipango ya Serikali hii. Kama mwanafunzi anachukua mtihani anaupiga picha chaa! Unaenda *artificial intelligence,* unaleta majibu, ni dunia nyingine kabisa ambayo tunakuja nayo. Kwa hiyo, ni muhimu sana kupambana nayo hiyo, kuhakikisha tunaiendeleza nchi yetu katika sekta kama hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja na ninakushukuru sana. Tutacheza na tutashinda *insha Allah*, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, ambaye ndiye mchangiaji wetu wa mwisho kwa mchana huu. Ninawashukuru wote kwa michango yenu mizuri kwa Serikali.

Kabla sijasitisha Shughuli za Bunge, niwataje wachangiaji wa tatu wa mwanzo, ili waweze kujiandaa. Tutaanza na Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mheshimiwa Juma Usonge Hamad na Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, wengine wataendelea.

Baada ya kusema hayo, ninasitisha Shughuli za Bunge hadi Saa 11.00 Jioni.

*(Saa 7.04 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2024 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**
**na**
**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu. Tutaanza na Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga; Mheshimiwa Juma Usonge Hamad na Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate wajiandae. *(Makofi)*

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye ni mwingi wa rehema, ametulinda, lakini pia amenilinda mimi kama mwakilishi wa Wanakilolo kwa kipindi cha miaka mitano hii ya Bunge la Kumi na Mbili. Shukurani hizi ni kwa Mwenyezi Mungu kwa sababu ninajua mchango huu ninautoa kwa sababu ndio uchangiaji wa mwisho kwa Bunge la Kumi na Mbili. Kwa hiyo, sitapata tena fursa ya kuchangia mpaka Bunge lijalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia kushukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mambo makubwa sana ambayo ameyafanya katika nchi yetu. Si katika nchi yetu kwamba Kilolo haijaguswa pia kwa sababu amewagusa Wanairinga, lakini pia Wanakilolo kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo miradi mikubwa ambayo imetugusa sisi Watanzania wote, kama miradi ya umeme vijijini ambapo vijiji vyote vya nchi hii vikiwemo vijiji vyote vya Wilaya ya Kilolo na Jimbo la Kilolo vimepata umeme. Ipo miradi mikubwa kama ya *SGR* ambayo kwa sasa inawagusa Watanzania wengi sana ambao wanatumia usafiri huo, lakini pia wananufaika

kutokana na uchumi uliokua kutokana na miradi mikubwa ambayo nchi hii imefanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si miradi hiyo tu iko miradi mingi pia ambayo imegusa kila maeneo. Kwa mfano barabara za lami zinazojengwa kwenye maeneo mbalimbali; hata Wilaya ya Kilolo ambayo ilikuwa haijaunganishwa na barabara za lami sasa imeunganishwa na barabara za lami tunavyozungumza. Hii ni kazi kubwa sana iliyofanyika katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu mbalimbali pia ambazo hazikuwa na sekondari, sekondari zimejengwa na kuna miradi mingi ya maji inayoendelea. Wakati wote tunapozunguka tunaona jinsi ambavyo Watanzania kwa ujumla wana moyo wa shukurani kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua mchango mkubwa sana wa Waziri wa Fedha pamoja na Wizara yake katika kuhakikisha kuwa haya yote yanafanikiwa. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kuhakikisha kwamba mpangilio wa fedha unawagusa Watanzania, hasa kwa miradi ile ambayo nimeitaja na mingine mingi ambayo inaendelea kufanyika katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo mengi ambayo yamefanyika kwa Wilaya ya Kilolo nikisema nitaje orodha kwa kweli ni nyingi sana na kwa hiyo, itoshoshe kusema kuwa kipindi hiki cha miaka mitano kimekuwa kipindi cha mabadiliko na Watanzania wameona, wananchi wameona na wanajua nini cha kufanya katika kuendelea kuipa nafasi Serikali ya Chama Cha Mapinduzi kuendelea kuwatumikia Watanzania. Ninafahamu kuwa kauli mbiu zitapita, lakini Kauli Mbiu ya Oktoba Tunatiki itakuwa na nguvu zaidi kuliko kauli mbiu nyingine zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia na kusoma bajeti hii vizuri na ninavyo vitu kadhaa vya kupongeza, lakini pia vya kuwekea msisitizo kwenye bajeti hii. Katika kipindi hiki pia nimepata fursa ya kuwa Mjumbe wa Kamati ya UKIMWI wakati Kamati hii ilipokuwa iko pekee yake na hili suala la *Aids Trust Fund* lilianza kujadiliwa wakati huo. Nichukue fursa hii kumpongeza yeye, pia kuishukuru

Serikali kwa kutambua umuhimu wa sisi kama Watanzania kujitegemea katika kuwa na mifuko ya fedha zetu wenyewe zinazoweza kutufanya tuwe na mfuko wa fedha ambazo Watanzania wanaopata shida ya maradhi wanakuwa na chanzo ya kwetu sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo la kuanzisha vyanzo vya mapato kwa ajili ya *Aids Trust Fund* pia kwa ajili ya bima ya afya kwa wote ni wazo la msingi sana na kwa kweli linapaswa liungwe mkono na Watanzania, lakini na Wabunge wote, ili sisi Bunge hili la Kumi na Mbili tuweke historia ya kuwa chanzo cha kuendeleza utaratibu wetu wa kutafuta namna bora ya kujitegemea badala ya kuendelea kuegemea kwa wafadhili ambayo inaweza kutufanya watumwa hasa nyakati ambazo tunahitaji kufanya maamuzi yetu sisi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni la kupongeza sana na kwa kweli mimi moja kati ya vipengele vya bajeti ambavyo nimeviona ambayo vinaonesha umakini wa Serikali hii ya Awamu ya Sita ni pale ambapo kuna maeneo mengi yanayoonesha kwamba nchi yetu ina dhamira ya dhati ya kujitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hilo tu, hata kujitegemea kwa bajeti katika uchaguzi ni kielelezo cha uhuru wa Watanzania, ni kielelezo cha kwamba Watanzania wameamua kufanya demokrasia ya kwao wenyewe ambayo itaonesha uhuru wa kugombea, uhuru wa kuchaguana bila kuwa na msukumo kutoka mahali pengine popote. Jambo hili ni jambo la msingi sana na nina hakika ni jambo ambalo ni la kupigiwa mfano kwa maamuzi bora kama haya. Tumshukuru sana Mheshimiwa Rais na pia tumpongeze sana Waziri wa Fedha pamoja na timu yake kwa ajili ya maamuzi makubwa kama haya ambayo yana mustakabali mzuri kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mambo machache ambayo pengine ni vizuri kuangalia ni kuona jinsi gani tunaweza kuifanya nchi yetu ikue kiuchumi. Hili linagusa zaidi sekta ya mipango. Sekta ya mipango imefanikiwa sana kwenye baadhi ya vipaumbele, ninataka nitoe mfano jinsi ambavyo sekta ya mipango

imefanikiwa kwenye suala zima la kupeleka umeme vijijini na tukafanikiwa kwa 100% kwenye vijiji vyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili uchumi wa nchi hii uweze kukuwa ipo sekta moja ya muhimu. Nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Mipango aweze kuliangalia suala hili kwa kuangalia jinsi gani tunaweza ku-*copy* mpango wa *REA* kwenda *TARURA* kwa ajili ya barabara vijijini. Kama tutakuwa na mpango unaofanana na *REA* ambao umefanikiwa kupeleka vijiji vyote, wakati huu tunapoweka mpango wa miaka mitano ijayo kuhakikisha kwamba kwa mpango huo huo tunao mpango ambao unahakikisha hakuna barabara katika nchi hii kwenye kijiji chochote ambayo haipitiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini, inawezekana? Inawezekana kwa sababu gharama za kupeleka barabara vijijini maeneo mengi inaweza kuwa ndogo kuliko gharama tulizotumia kupeleka umeme. Kama tumefanikiwa kupeleka umeme kwenye vijiji vyote mimi sioni kikwazo cha kuweka mpango madhubuti wa kuhakikisha kwamba barabara kwenye vijiji vyote zinakuwa ni za angalau changarawe na nyingine za lami. Tunaweza tukaamua kwamba kusiwe na sehemu ambayo hata kama ni kipindi cha mvua kiasi gani barabara haitapitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalam wafanye kazi, tathmini ifanyike na baada ya hapo mpango wa miaka mitano ijayo uakisi suala hili na ambalo litakuwa ukombozi hasa kwenye maeneo ambayo hayapitiki kwa muda mrefu. Nikitolea mfano, hata Wilaya ya Kilolo ambayo changamoto kubwa sasa iliyobaki katika uzalishaji mali ni suala zima la barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoa mfano huo tu, lakini kwenye nchi yetu yako maeneo mengi sana ambayo unaona jinsi ukuaji wa uchumi unafanyika. Kwenye kilimo uwekezaji umeshafanyika fedha nyingi zimewekezwa kwenye umeme, umeme upo, kwenye sekta ya maji tumefanya vizuri tumepeleka maji kwa kiasi cha kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, uchumi unakua lakini sekta ya usafirishaji inakwamishwa hasa kwenye eneo la barabara ambalo mimi nina hakika watakapokaa na kuchakata na kuliwekea hesabu vizuri jinsi gani ya kukwamua eneo hilo watakuwa wamefanya jambo ambalo nina hakika kwamba litaleta tija kwenye nchi yetu. Niwaombe sana, kama litazingatiwa maana yake ni kwamba haliwezi kwenda kama kawaida. Umeme ulienda *REA* haikuwa kama kawaida, ilikuwa ni *project* maalum na ndio maana ilifanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utengenezaji wa barabara vijijini isiwe kama kawaida, iwe na mpango maalum na *project* maalum ambayo inahakikisha kwamba kuna ukombozi wa barabara kufikika maeneo yote ya nchi yetu ili Watanzania sasa waweze kuunganishwa na kufurahia usafirishaji wa mazao wanayoyazalisha kutokana na ruzuku za mbolea zilizowekwa, lakini pia na uzalishaji wanaofanya kutokana na umeme uliofika kwenye maeneo yao na maji ambayo tunaenda kwenye kuweka hizi za kwenye umwagiliaji. Ni lazima tufikiri namna bora ya kuimarisha miundombinu ya barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia ni namna gani tunavyoweza kukabiliana na changamoto ya mazingira pamoja na kuanza kufikiria kuweka kipaumbele kwenye motisha za watu wanaolima mazao ya misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka ya karibuni uvunaji wa miti ni mkubwa kuliko upandaji wa misitu. Maana yake ni kwamba, katika kipindi cha miaka michache ijayo nchi yetu itaingia kwenye changamoto ya kukosa mazao ya misitu, hasa mbao. Kwa sababu kwenye maeneo ambayo mazao hayo yanalimwa sasa watu wanahama kutoka kwenye kulima miti na kulima mazao mengine. Kwa mfano, Wilaya nyingine wanaanza kulima maparachichi na kadhalika. Nchi yetu hii ina uhitaji mkubwa sana wa mbao. Kwa hiyo, itafika wakati aidha bei ya mbao itapanda sana au utofauti na hiyo ambayo inaathiri uchumi kwenye sekta ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili hilo lisitokee maana yake kwenye mipango inayokuja ya miaka mitano ijayo ni lazima kuona Serikali inaweka motisha gani kwa wakulima wa mazao ya miti. Isipowekwa motisha yoyote maana yake ni kwamba wakulima wa mazao haya ambayo ni ya kusubiri muda mrefu bila kuvuna watapungua. Wakishapungua maana yake ni kwamba kutakuwa na kwanza athari za kimazingira ambazo zitaathiri kilimo cha kawaida kwenye maeneo lakini pili, tutakuwa na athari za kiuchumi hasa kwenye sekta ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni jinsi ambavyo Serikali yetu imefanya vyema katika bei za mazao mbalimbali. Mazao mengi ya kilimo huko siku za nyuma yalikuwa na shida sana kwenye bei, lakini tunakoenda unaona jinsi bei za mazao zinazidi kuongezeka, hasa mazao ya kilimo. Hata hivyo, katika uongezekaji huu wa bei za mazao iko changamoto ya vipimo. Ningependa kulizungumzia hili kwa sababu sasa hivi vipimo viko vya aina nyingi. Nikizungumzia kilimo kama cha vitunguu ambacho najua Mheshimiwa Waziri wa Fedha anafahamu, hata kule kwao wanalima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzoni walikuwa wanasema lumbesa, wakaikataza, sasa siku hizi wameleta neti. Neti maana yake ni kwamba haijai lakini inapanuka, yaani ule unene wa mfuko unakuwa mkubwa lakini juu ule ujazo unabaki vilevile. Hii imekuwa ni changamoto kiasi kwamba unajiuliza, je, Wakala wa Vipimo wenyewe hawajaliona hili na kama wameona ni nini wanachoweza kufanya? Kwa sababu hili linawakandamiza sana wananchi, wale wananchi ambao ni wa kawaida ilihali Serikali, wakati Mheshimiwa Rais anaendelea kutoa ruzuku ili Watanzania wapate bei nzuri *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati jambo linawafanya Watanzania wanafurahia sana kunakuja na changamoto ya wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu ambao wanataka kuwadidimiza wakulima. Jambo hili ni vizuri kwenye hatua zinazofuata kwenye siku zijazo kuliangalia ili liweze kuondoka. Likiondoka maana yake ni kwamba lazima tuweke utaratibu wa vipimo unaompa tija mkulima. Maana yake mkulima ambapo hajapata kipimo ambacho ni sahihi inamletea changamoto

kwenye bei kwa sababu anauza kingi kwa bei ndogo na kwa hiyo ile tija inakuwa kidogo. Hilo ningependa kusema kwamba ni jambo ambalo tunatakiwa kuliangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Serikali kwa ujumla kwa jinsi wanavyofanya juhudi ya kuendelea kuwalipa wakandarasi wa ndani. Juhudi zinaonekana; na kwa kweli ni jambo zuri sana kwamba wakandarasi wa ndani waendelee kulipwa ili kuchechemua uchumi; hasa wanaofanya sekta za maji, sekta za barabara na sekta nyingine. Ombi langu ni kwamba katika kipindi hiki wakandarasi wale ambao bado hawajalipwa waendelee kulipwa ili kuendelea kuhakikisha kwamba uchumi wetu unaendelea kuwa imara na kwamba Watanzania waliowekeza katika miradi mbalimbali ya Serikali wanaendelea kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba upo wakati ambapo tumeona jinsi ambavyo Serikali inatoa fedha nyingi kuwalipa wakandarasi hawa na kwa kweli pia hata namna ambavyo motisha kwa wakandarasi wa Tanzania inaonekana hata kiwango cha miradi wanayoweza kufanya tumeona kimeongezeka; kwamba ni fedha nyingi zaidi wanaweza kufanya miradi mikubwa zaidi. Watakapomaliza kufanya kazi pia vilevile ambavyo tunawapa kipaumbele basi pia tuwape kipaumbele katika ulipaji ili mzunguko wa fedha katika uchumi wa nchi yetu uendelee kuwa bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kumalizia niendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Rais. Nirudie tena kwa sababu Wanakilolo wanajua kazi kubwa aliyoifanya. Sisi Wanakilolo kwa ujumla wetu tumejipanga na tuko tayari kwa ajili ya Oktoba kuonesha shukurani zetu kwa Mheshimiwa Rais na kwa Serikali ya Chama Cha Mapinduzi ambayo imefanya mambo makubwa sana katika kipindi hiki cha mwaka huu, lakini pia katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Kwa kuwa kazi hiyo imeonekana na wananchi wote wa Kilolo mimi kwa niaba yao ambaye walichagua ili niweze kuwawakilisha ninafikisha shukurani hizi lakini huku nikisema tunajua kuwa bado ana miaka mingine mitano ya kututumikia na tuna uhakika atawatendea haki Watanzania

kama ambavyo amewatendea kwenye kipindi hiki cha miaka mitano iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuwaombea, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Waziri wa Mipango pamoja na Manaibu wao na wao pia warejee Bungeni ili waendelee kulitumikia Bunge letu. Mwenyezi Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana,Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga. Nilimtaja Mheshimiwa Juma Usonge Hamad, Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate na Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, wajiandae.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii jioni ya leo kuweza kuchangia kwenye Wizara hii ya Fedha na Wizara ya Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kutujalia leo hii tukakutana wazima. Pili, nikupongeze wewe tokea asubuhi upo kwenye Kiti kwa ajili ya kusimamia utaratibu. Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri wa Fedha pamoja na Waziri wa Mipango kwa uwasilishaji mzuri wiki iliyopita wa taarifa hii ya fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana pia Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ambayo anaifanya. Leo hii kabla sijazungumza yote ninaomba niunge mkono wa asilimia mia moja taarifa hii ili kuweza kumpa nguvu Mheshimiwa Waziri. Kutoka na mawazo ya Mheshimiwa Rais haya leo hapa tunayajadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa mno kwa kipindi chake hiki ambacho tayari amepokea kijiti. Ipo baadhi ya miradi mbalimbali ambayo kwa akili ya kawaida Watanzania walikuwa wanafikiri kama

Mheshimiwa Rais anaweza kuyatekeleza. Leo hii tunaona na tunashuhudia miradi mikubwa ya kielelezo ambayo ameiacha mtangulizi wake, Mheshimiwa Rais ameikamilisha. Kesho pia tutashuhudia huko Mwanza Mheshimiwa Rais nako anakwenda kukamilisha lile daraja kubwa ambalo Watanzania wa Mwanza, Geita na maeneo mengine jirani wanaenda kushuhudia na kuweka historia kubwa ya mama alivyokamilisha miradi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile ninatokea upande wa pili wa Zanzibar Mheshimiwa Rais pia nimpongeze sana kwa kazi nzuri ambayo tayari amefanya. Hatujawahi kushuhudia kwa namna ambavyo Mheshimiwa Rais, Mama Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuuenzi Muungano huu, lakini pia kushuhudia ile fedha ambayo inakwenda Zanzibar kama ya Muungano kwenye magawio anaisimamia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi na yeye pia kwa kusimamia vizuri zile fedha ambazo tayari zinaenda vizuri kwa ajili ya kuchochea maendeleo kwa upande wa Zanzibar. Tumeshuhudia miradi mbalimbali; hivi karibuni tu tuliingia kwenye janga kubwa la *COVID* tulipokea fedha nyingi sana, lakini kutokana na mapenzi makubwa aliyokuwa nayo Mheshimiwa Rais kuna fedha baadhi ya nusu zaidi ya bilioni 230 nayo ilikwenda kule Zanzibar ikatekelezwa miradi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama Mbunge wa Zanzibar ninavyo vijiji zaidi ya vitatu, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Zanzibar pamoja na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna walivyoshirikiana kwa pamoja kwenye fedha zile za *COVID* kwenda kujenga madarasa ya shule na pia kujenga miradi mbalimbali ya kimaendeleo ikiwemo miradi ya hospitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo pia miradi mbalimbali ya kimaendeleo kwa mfano kama ujenzi wa *Airport* ya kisasa ambayo inategemewa kujengwa kule Kisiwani Pemba, yote hayo ni mikakati pamoja na ushirikiano mazuri ya Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Dkt. Hussein Mwinyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashuhudia vile vile kuna ujenzi mkubwa wa Barabara ya Tunguu mpaka Makunduchi, nayo pia inatengenezwa kwa kushirikiana kwa Marais wetu hawa wawili. Pia, tunashuhudia ujenzi wa Barabara ya Chakechake - Wete nayo pia ni ushirikiano ya Marais wetu wawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia pia Nchi yetu ya Tanzania kwa namna ambavyo Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan aliyobeba ajenda ya nishati safi ambayo tunasema mitungi ya gesi, kwa namna ambavyo siyo huku tu Tanzania Bara mpaka kule Zanzibar nishati hiyo inatumiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimesema niunge mkono taarifa hii kwa sababu tunafahamu kwamba tunampa *mandate* mama ya kwenda kufanya kazi. Kwa hiyo, nikasema nimuunge mkono Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo miradi ya kimaendeleo kwa upande wa pili pia Zanzibar inaenda kufanya kazi Zanzibar yanaenda kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na hilo sasa niende kwenye mchango wangu kuja kwenye sekta ya kilimo. Juzi hapa tumemsikia Mheshimiwa Waziri kwa namna ambavyo kilimo chetu cha Tanzania kilivyopiga hatua, kutoka 2022 tulikuwa tunaambiwa tupo kwenye 2.5%, lakini kwa sasa hivi mpaka tunazungumza 2025 tupo kwenye hatua ya *4-point* na kadhalika kwenye kilimo. Hii yote inaonesha kwamba namna gani tulivyopiga hatua. Tunaambiwa tuna wastani wa chakula wa takribani 128%, yote inaonesha kwamba tumevuka mpaka kwa namna ambavyo tulivyokuwa na *reserve* ya kutosha ya chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Waziri Mheshimiwa Bashe, tumekuwa tukimpongeza hapa siku zote kwa namna ambavyo alivyokuwa na mipango ambayo inatekelezeka. Wizara hii huko nyuma hata bajeti yake ikipangwa ilikuwa inapangiwa bajeti ya fedha za kawaida, lakini tumeshuhudia mwaka huu Wizara yetu ya Kilimo imepangiwa fedha nyingi. Hii yote inaonesha imani kubwa ya Mheshimiwa Bashe, lakini imani kubwa na dira ya Mheshimiwa Rais ya kutaka kuleta mapinduzi makubwa ya kilimo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na hilo pia, kwenye kilimo tunaambiwa tunafanya vizuri zaidi, lakini bado hatujaangalia kutanua zaidi kwa ajili ya kusambaza vyakula vyetu nje ya nchi, yapo baadhi ya mazao machache ambayo tayari tunafanya *exportation*, lakini nishauri kupitia Wizara yetu ya Fedha pamoja na Mipango, sasa hivi lazima twende kwenye *modality* nyingine ya kilimo. Wapo wawekezaji mbalimbali duniani sasa hivi wanatumia mfumo wa *EPC+Finance,* hii ni miradi mizuri sana ambayo inatekelezwa na wenzetu, wanakuja ndani ya nchi, Serikali inawapa fedha wanatekeleza miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wao kama wao wanasimamia *in term of engineering*, *procurement* pamoja na masuala ya *construction*. Tukiwapa fedha wao watakuwa wanatengeneza miradi lakini vijana wetu ndio watakaopata ajira, lakini pia ardhi yetu ndio watakayoitumia. Pia, tukiwapa fedha maana yake tutakuwa tuna *guarantee* ya fedha zetu kwa namna gani ambayo tunaweza tukarejesha kwa kipindi kifupi, hii itatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ipo Miradi kama *BBT*, hili tumewaachia ndugu zetu vijana wetu wa Kitanzania ndio wanatekeleza, lakini miradi kama hii ambayo tayari inatekelezwa na wenzetu kutoka nje, lakini miradi ikishatekelezwa fedha inayopatikana itabakia ndani ya nchi lakini tutakuwa tuna uhakika wa masoko ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaiomba sana Wizara ya Fedha, hebu tuliangalie hii. Tumekuwa wagumu sana, tumekuwa wavivu kwenye eneo hili la kuweza kufikiria. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri Mwigulu Nchemba kakae na Mheshimiwa Bashe, ninadhani miradi kama hii inatekelezeka. Zipo baadhi ya Nchi kwa mfano wenzetu Zambia, wanatekeleza miradi kama hii, lakini hata ukienda hapo Uganda pia wanatekeleza miradi kama hii. Wageni wanasimamia miradi kama hii lakini fedha inayopatikana inabakia ndani ya nchi na tunakuwa tuna *guarantee* ya fedha zetu ambazo tayari tumeziwekeza kwenye eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuje kwenye eneo la pili, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais amekuwa msikivu sana kwa wafanyabiashara hususan wadogowadogo (machinga) juzi tumesikia hapa Mheshimiwa Rais ameridhia na ametoa *mandate* kwamba kutenganisha biashara za wazawa pamoja na wageni, hili ni jambo la kupongezwa sana kwa Mheshimiwa Rais. Tumeshuhudia kila siku kariakoo kwenye majiji wananchi wanalalamika kuonekana kazi ambazo zinaweza zikafanyika na wazawa lakini wageni wanafanya hizi kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kusikia kilio hiki, lakini pia kuielekeza Wizara kuweza kutathmini sasa hivi biashara gani wanaweza wakafanya wazawa na biashara gani wanaweza wakafanya wageni. Hili ni jambo zuri sana na lazima Mheshimiwa Rais apigiwe makofi mengi kwa namna ambavyo alivyowafikiria vijana wetu wa Kitanzania. Hii imechochea uchumi wetu katika nchi, lakini pia imewasaidia vijana wetu ambao tayari wanafanya kazi, wanafanya biashara ndogondogo, hawa vijana wetu ambao tunawaita machinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, tumekuwa tukilalamika sana hususan sisi Wabunge ambao tayari tunatokea Zanzibar kuhusiana na hizi tozo za forodha hususan za bandarini. Kumekuwepo na kama njama fulani za watu wa *tax* hawa *customer's duties* wa bandarini *either airport*. Kwa mfano, *airport* pale, utawakuta hawa watu wa *tax* wanasubiria ndege. Zinapokuja ndege za Uturuki, zinapokuja ndege za China au Dubai utawakuta wenzetu hawa watu wa *taxi* ndio wanaowaagizia wafanyabiashara, kwa hiyo hakuna *transparency* kabisa katika ku-*charge* kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda pale *airport* kuna kachumba maalum, ukifika unakadiriwa; hii nipe kiasi kadhaa, hii nipe kiasi kadhaa. Kwa hiyo, ninaiomba sana Wizara yako Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, hakuna *transparency* katika utozaji wa kodi hususan kwa bidhaa ambazo zinatoka nje ya nchi; na mfano huohuo ukienda pale bandarini hakuna *modality* ya bidhaa ambazo unatoka nazo Zanzibar unakuja nazo labda Tanzania Bara, hakuna *price* kabisa. Ukienda pale

mfanyabiashara unakadiriwa kwa namna ambavyo wanavyojisikia wao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe sana, haya malalamiko na changamoto kama hizi zinaweza zikatatulika, tusimsubiri tu mpaka Mheshimiwa Rais ndipo akemee na asemee haya mambo. Haya mambo yapo, tunaomba Wizara husika isimamie *transparency* tunaitaka hususan kwenye maeneo hayo katika nchi yetu. Kwa upande wa Zanzibar kuja Tanzania Bara na kwa upande wa *Airport*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, nikushukuru sana kwa kunipatia fursa hii na ninaunga mkono hoja iliyokuwepo mezani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Juma Usonge Hamad. Nilimtaja Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mheshimiwa Yahaya Omary Massare na Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji ajiandae.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kupata nafasi jioni hii ya kuweza kuchangia hoja iliyopo mezani. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai wa kusimama kwenye Bunge lako Tukufu kwa siku ya leo. Pili, nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa utashi wake na hiari ya makusudi ya kuhakikisha kwamba bajeti hii inatengenezwa vizuri kwa niaba ya maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza kabisa ninaunga mkono hoja iliyopo mezani kwa asilimia mia moja, lakini la pili, ninawapongeza Mawaziri wote wawili na watumishi waliopo chini yao wote kwa kutengeneza bajeti nzuri yenye mtazamo wa kuchechemua uchumi wa nchi yetu na kuhakikisha kwamba maendeleo yanatokana na bajeti iliyopangwa kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaelekea sana kwenye ushauri upande wa kilimo. Kwanza tunashukuru sana bajeti hii kwa kumwangalia mkulima kwa kumweka kipaumbele. Moja ni

kuondoa kodi kwenye viuatilifu ambavyo vinatumika kwa wakulima wetu. Hili jambo tutaliona ni dogo, lakini ni kubwa sana kwa wakulima wetu kwa sababu hivi viuatilifu ndivyo vinavyowafanya wakulima waweze kupambana na wadudu mbalimbali ambao wanaathiri mazao yetu ili kupata mazao zaidi. Kupunguzwa kwa kodi hii kutasababisha mkulima kuwa na *purchasing power* kubwa ya kupata hivi viuatilifu hatimaye kufanya matumizi yawe makubwa zaidi na kumfanya avune zaidi na Serikali kuvuna zaidi kutokana na kodi na tozo mbalimbali zinazotokana na mazao ambayo wakulima wanazalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo kwa kweli ni faraja kubwa na ni hiari ya Mheshimiwa Rais wetu, sambamba na hii ni pamoja na kuendelea kutoa ruzuku kwenye mbolea kwa wakulima. Hili jambo bado ni kubwa linaendelea kuhakikisha kwamba uzalishaji unaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee tumshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hasa sisi wananchi tunaotoka kwenye ukanda ule unaozalisha korosho. Tunamshukuru sana kwa hiari yake na kuamua kutoa *export levy* kwenye zao la korosho kwa 100%, tunashukuru sana. Kwa sababu hiyo ndiyo maana mpaka sasa tumeona uzalishaji wa korosho umetoka tani 323,000 mpaka kufika tani 528,000 ambayo ni zaidi ya 60% ya ongezeko lililotokana na uwezo wa Serikali kuwahudumia wakulima wetu kwa kuwapa pembejeo za *sulphur* na maji bure. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais, Mungu aendelee kumpa maisha marefu ili aendelee kuwahudumia wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa ushauri kwenye mazao mengine ya biashara, kwa mfano ilivyo kahawa, tumbaku na mazao mengine kama kokoa, waige mfano wa korosho. Tulivyoanzisha *export levy* 2009, ninadhani kama 2008 kama 2009 ilikuwa ni mahususi kwa ajili ya kuchechemua uzalishaji wa korosho pamoja na kuwezesha kuanzisha viwanda vya ubanguaji kwenye nchi yetu ili korosho iweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili jambo limeonesha kuleta mafanikio kwa sasa kwa sababu uzalishaji umeongezeka na dhamira ya Serikali kuanzisha kongamano la korosho katika

Halmashauri ya Nanyamba ni dalili ya kutosha kabisa kuonesha kwamba *export levy* imeleta matunda makubwa kwa wakulima wa korosho. Kwa hiyo, si dhambi kwenye mazao mengine wakaingiza mtindo huu au wa namna yoyote ile ya kuhakikisha kwamba na wenzetu hawa wanakwenda kwenye *export levy* itakayosaidia kuzalisha zaidi kwa sababu sehemu ya *export levy* kwa 100% inaenda kusaidia wakulima wenyewe kwa ajili ya kusaidia mashamba yao pamoja na wataalam kwenye eneo linalohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuiga hilo suala la *export levy* si dhambi nao wenzetu wakaendelea kuiga huu mtindo wa stakabadhi ghalani. Ninaomba nikufahamishe, kwenye maeneo yote yanayolima korosho, yanayotumia mfumo wa stakabadhi ghalani kwenye ufuta na mbaazi sasa hivi hatutamani kurudi nyuma kwenye mfumo ule wa zamani. Imeonesha mafanikio makubwa hasa kwenye upande wa kupanda bei na pili kwa halmashauri zetu za wilaya kwa kupata mapato ya uhakika zaidi kuliko ilivyo kwenye mfumo wa kiholela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali, kama halmashauri hizi za maeneo haya zinafaidika sana kwenye Mfumo huu wa Stakabadhi ya Ghalani kurahisisha upatikanaji wa ushuru wao kutoka kwenye mazao haya na kodi mbalimbali za Serikali. Kuna mazao ambayo wenzetu yamekuwa kama mazao ya biashara kama ilivyo Rukwa, Sumbawanga, Songea na Mbinga, zao la mahindi. Zao hili limekuwa ni zao la kibiashara kwao kwa sababu linasababisha wao kuwa na kipato kikubwa kutokana na mahindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mfumo wa kununua *NFRA* umeonesha udhaifu wa hali ya juu. Moja ya udhaifu wa mfumo ule sasa hivi wakulima ndiyo wanauza mahindi kwa watu wa katikati. Kwa hiyo, bei anayoitoa *NFRA* kwa wanaouza mahindi kwao wanapata watu wa kati, wakati wanapeleka fedha maana yake mkulima hana mazao kwenye maghala yake, mazao yote yapo kwa wafanyabiashara wa kati. Kwa hiyo, faida ile ya kilo shilingi 700 mpaka 800 kwenye upande wa mahindi inakwenda kwa wafanyabiashara wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Serikali, lengo la Serikali ni kuwasaidia wakulima, basi hii Mifumo ya Stakabadhi Ghalani kwenye maeneo yale yenye mazao mahususi yanayowasaidia wakulima kama mazao ya kibiashara ni vyema basi stakabadhi ghalani ikaelekea kusaidia wakulima wetu ambao watapata bei ile nzuri ya moja kwa moja kutoka kwa wanunuzi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si jambo rahisi kama mlivyoona wakati wa miaka ya nyuma, tunalumbana hapa kwenye ufuta, kwenye maeneo mengine lakini leo wanachekelea; kwenye kokoa leo wanachekelea; kwenye kahawa leo wakulima wanachekelea; basi ile itatusaidia na hao wa mahindi, maharage na mazao mengine ambayo yanalimwa kwa wingi kwenye maeneo haya wakapata bei nzuri; na wakulima wale wakaendelea katika kuhakikisha maisha yao yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine kwenye kilimo ni suala la umwagiliaji. Tunashukuru bajeti ya umwagiliaji imeongezeka, lakini tumwombe Waziri wa Fedha, tuna mipango mizuri, Mheshimiwa Bashe ana mabwawa chungu mzima hapa, ameyataja kuna miradi zaidi ya 900 ya umwagiliaji, shida pesa haiendi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umwagiliaji ni muhimu sana, tukiuanza mradi leo ukaishia katikati, mvua ikinyesha maana yake zitakapokuja hela unaanza upya, kitu ambacho kinarudisha nyuma miradi hii ya umwagiliaji. Inakuwa kila siku tunapeleka hela lakini miradi haiendelei. Kwa hiyo, tunaomba Waziri wa Fedha, wewe ni msikivu, unamsaidia sana mama kuhakikisha kwamba tunataka kuendelea kuzalisha zaidi, sasa tunaomba fedha za umwagiliaji ziende kama zilivyokusudiwa kwa sababu lengo la umwagiliaji ni kuhakikisha kwamba mkulima analima mwaka mzima na kuzalisha zaidi bila kutegemea mvua na ili Serikali iweze kupata fedha na mapato zaidi kutokana na tozo na kodi mbalimbali zinazotokana na biashara ya mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa siitendei haki Wilaya ya Tunduru na Jimbo la Tunduru Kusini kwa ujumla pamoja na Wilaya zote na Mikoa ya Kusini. Kuna suala la ujenzi wa *SGR*. Kwenye

mipango hii, bado tunakuwa na kizungumkuti cha kutengeneza *SGR* kutoka Mtwara – Tunduru - *Mbamba Bay* pamoja na matawi yake Nchuchuma na Liganga. Wakati tayari Serikali imeonesha dhamira yake ya kuanzisha Mradi ule wa Liganga na Mchuchuma kwa kuanza kulipa fidia kwa waathirika, tunaomba sana, miradi hii ni pacha ili iende sawasawa lazima iendene sambamba na ujenzi wa reli ya *SGR* kutoka Mtwara - Tunduru mpaka Mbamba Bay ili iweze kusaidia, itakapokamilika itasaidia Mradi wa Liganga na Mchuchuma kusafirisha zile bidhaa kwa urahisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana, hii mipango yetu tuamue kama tulivyoamua kwenye *SGR* reli ya kati, kama tulivyoamua kwenye *standard gauge* na kama tulivyoamua kwenye Daraja hili la Magufuli tuamue na kusini tujenge ile ili iweze kuchechemua uchumi wa kanda ya kusini. Tuamue kabisa kimsingi, tufumbe macho, Mchuchuma na Liganga isiwe historia ianze kufanya kazi ili wananchi wapande hii ya kusini wafaidike na biashara hii ya makaa ya mawe na mchuchuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninalisisitiza kwenye habari ya Benki ya Ushirika yetu ambayo imeanzishwa. Ninaomba sana, tumeanzisha kwa hela ndogo sana, lakini tutakavyoanza kujenga matawi tuangalie maeneo ambayo uzalishaji na vikundi vya ushirika vipo vingi sana ili iweze kusaidia kukua kwa haraka benki hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa mfano kwenye kanda hii ya korosho. Ni zaidi ya trilioni moja, benki zetu zinapitishwa kwa ajili ya wakulima na vyama vya ushirika kwa ajili ya malipo mbalimbali ya mazao. Sasa jambo hili kama litakuwa sambamba na kufungua matawi kwenye Mkoa wa Ruvuma ambapo sisi kuna vyama vitatu vipo *strong*, vinajitahidi, vinakwenda vizuri, *TAMCU*, *SUNAMCU* na *MBIFACU* ambavyo vinashughulika sana na wakulima kwenye kahawa, mahindi, ufuta, mbaazi pamoja na korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Mtwara napo uzalishaji wa korosho umekuwa ni mkubwa sana, wana haki ya kupeleka Tawi hili la Benki ya Ushirika ili likawasaidie wanaushirika wenzetu wa Tandahimba, Newala, Masasi, Mtwara pamoja na Nanyumbu

sambamba na vyama vya Mkoa wa Iringa, Lindi na Mkoa wa Pwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli hilo jambo la ushirika mimi kama mwanaushirika ambaye nimefanya kazi zaidi ya miaka 10 kwenye ushirika ni ndoto ya muda mrefu, ni zaidi ya miaka 10 benki hii imeasisiwa, lakini ninashukuru kwa kuanza rasmi kwa benki hii. Tunaomba dhamira ya kuwasaidia wakulima iende sambamba na kufungua matawi kwenye maeneo ambayo wanaushirika wapo wengi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ni suala la wafugaji holela. Katika maeneo yanayoathirika sana na ufugaji holela ni pamoja na Jimbo la Tunduru Kusini na Tunduru kwa ujumla pamoja na Kusini, Namtumbo na maeneo mengi ambayo zamani hatukuzoea kuona ng'ombe, kwa hiyo ng'ombe wamekuwa wengi sana. Kwetu Tunduru tulitenga vitalu, hebu tusaidieni kuwahudumia wafugaji hawa kwa kuwapelekea miundombinu kwa ajili ya maji pamoja na majosho kwa ajili ya kuhudumia mifugo yao. Tukiwa tayari kabisa kuwasaidia kwa mtindo huu wataacha ule ufugaji holela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumetenga vitalu zaidi ya 252. Tunapozungumza saizi, vile vitalu wameviacha, wanaenda kwenye mabonde ambako wakulima sasa wanalima, wanategemea kwa ajili ya mazao yao na sasa hivi wanavuna mipunga na mazao mengine, lakini hawa wenzetu sasa kwa kukosa miundombinu kwenye maeneo yale tuliyowatengea, basi wanakimbia wanaenda kwenye maeneo ambayo yana mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sasa suala la kuwasaidia hawa wafugaji kuhakikisha wanapata miundombinu na kuwafundisha ufugaji wa kisasa badala ya ufugaji wa kuhamahama. Serikali itoe kipaumbele ili kuhakikisha kwamba wafugaji hawa wanakaa sehemu kwa amani kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa ni ujenzi wa maghala kwenye vijiji vyetu. Tunazungumza vizuri uzalishaji umeongezeka, lakini nimesoma taarifa hiyo mwaka mzima, miaka

mitano hii tumejenga maghala 46 na vihenge 20 na nchi hii ni kubwa sana. Katika biashara ya mfumo wa stakabadhi ghalani kwa kutumia *TMX* suala la ubora wa mazao unaendana sambamba na suala la sehemu ya kuhifadhia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfumo wa Stakabadhi Ghalani unasema, mkulima atachukua mazao yake, atapeleka ghalani, atahifadhi kusubiri mteja wa kununua zao lake kwa namna ilivyo, Serikali iliamua kutumia vyama vya ushirika ili kurahisisha mfumo huu kwa sababu wakulima walio wengi uwezo wao ni mdogo. Wanavuna kilo 20, kilo 30, kilo moja, ni wachache ambao wanafika tani na zaidi ya tani, kilo 500. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuhifadhi yeye kama yeye kupeleka ghalani peke yake ni shida. Njia pekee ya kuhakikisha kwamba huu mfumo unaenda vizuri na ubora unakwenda sawasawa, tuwekeni mpango maalum kabisa wa kujenga maghala kwenye vijiji vyetu ili kuhifadhi mazao hayo kule kule wakulima ambako wanazalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inataka mfumo wa stakabadhi, ghala likiwa na uwezo wa kuhifadhi tani 200 tu, sheria inaruhusu kuendesha mfumo wa stakabadhi ghalani. Hebu tuamue na hili tuhakikishe kwamba tunakuwa na maghala ya kisasa kwenye vijiji vyetu ili mfumo huu waone wananchi wa kawaida jinsi unavyowajali uchumi wa mazao yao kwenye maeneo ambayo wanaishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate. Nilimtaja Mheshimiwa Yahaya Omary Massare. Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji na Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo, wajiandae.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii nami nimshukuru Mungu kwa kuniwezesha jioni ya leo kuweza kuchangia hotuba za Waheshimiwa Mawaziri hawa vijana wawili; Waziri wa Mipango na

Waziri wa Fedha, katika mustakabali mzima wa bajeti yetu ambayo tunaendelea nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita katika maeneo matatu. Kwanza ni kuishukuru Serikali kwa kile ambacho imefanya katika maeneo yangu ambayo ninawakilisha. Pili, nitapenda kutoa changamoto kadhaa ambazo tunaziona, lakini mwisho nitawashauri Waheshimiwa Mawaziri hawa vijana katika kuhakikisha basi tunakwenda mbele vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia Serikali hii ya Awamu ya Sita ilivyofanya kazi nzuri kwa kipindi chake chote. Katika elimu, shule nyingi katika maeneo yetu ya vijijini zimejengwa na zingine ni mpya kabisa. Hakukuwa na uwezekano wa wanafunzi wa wakulima na wafugaji kupata elimu, lakini leo hakuna changamoto hii tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jimbo langu tumejenga shule mpya 30 katika kipindi cha Mheshimiwa Rais Dkt. Samia. Maana yake ni sifa za kipekee mno kuwahi kutokea. Mwaka 2020 tulikuwa na shule 40 tu katika Jimbo zima la Manyoni Magharibi ambapo sasa ni Jimbo la Itigi, Halmashauri ya Itigi lakini kwa miaka minne tumejenga shule zaidi ya 30. Wananchi wa Itigi wamenituma humu nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, lakini na waliomshauri katika hili wakiwemo Mawaziri hao vijana katika kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika afya, tumejenga zahanati katika maeneo yetu, tumejenga vituo vya afya na leo tunajenga hospitali ya wilaya katika Halmashauri ya Wilaya ya Itigi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji hivyo hivyo; vijiji vyetu vingi vinaenda kupata huduma za maji japo ziko changamoto za hapa na pale. Kama nilivyosema, nalo nitakuja kulichangia lakini miundombinu, tunaunganishwa Mkoa wa Singida na Mkoa wa Mbeya kwa barabara za lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkandarasi alisimama kidogo na changamoto hizi zilishaelezwa, tunaamini tunapoenda mwishoni hapa basi makandarasi huyo atapewa pesa ili arudi kumalizia

kipande hiki cha kilomita 56.6 ambazo tunaamini zikishafunguka tayari *central corridor* kwa upande wa Singida kuunganisha na *southern corridor* na *northern corridor* upande wa Mkoa wa Simiyu na Mara na sisi tutakuwa tumefaidika kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nishati vijijini, tumeshuhudia vijiji vyote nami kwenye jimbo langu vikipatiwa umeme na sasa wanakwenda vitongojini, lakini kama nilivyosema, kuna changamoto chache ambazo tunaomba tuwaambie ili wakazifanyie kazi. Katika vijiji vyetu, Mheshimiwa Rais wetu alitangaza *Royal Tour* na sisi watu wa Itigi tunapakana na mapori ya akiba ya Muhesi na Rungwa. Kwa kiasi kikubwa kumekuwa na manufaa makubwa, lakini zipo changamoto za wanyama wakali na waharibifu ambao wanapita kwenye maeneo ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaambiwa kwamba ni *corridor* za Wanyama, lakini uhalisia ni kwamba inawezekana hawa wanyama inawezekana wameongezeka kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo, tunaomba juhudi za makusudi zifanyike ili kuwanusuru wananchi hawa ambao wengine wanauawa na wengine wanaliwa mazao yao kutokana na wanyama hawa kuwa wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wetu wa Fedha katika ukurasa wake wa 47, amezungumzia kilimo ambacho kimeongezeka kwa kiasi kikubwa. Tulikuwa na tani 17,148,290 mwaka wa fedha 2021/2022, lakini mwaka wa fedha 2023/2024 ziliongezeka kufikia tani 22,803,316. Maana yake ni nini? Kwamba uwekezaji wa Serikali katika sekta ya kilimo unaonyesha kuwa na manufaa makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ya kilimo kadri inavyoongezeka basi tunategemea kwa muda mfupi ujao iweze kuakisi lakini ongezeko hili la kujitosheleza kwa chakula hiki kwa 128% kwa nchi kama Tanzania ambayo ni *hub* ya chakula, bado tunatamani kuona inaongezeka kwa kasi zaidi kuliko hapa tulipo. Kwa sababu ongezeko la bajeti yetu kwa upande wa kilimo ni kwa zaidi ya 300%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa madini nako kuna ongezeko kidogo. Tulikuwa na asilimia sita nukta nane tu sasa tumefika kwa 10%. Bado natamani kuona tunakwenda mbele zaidi kwa sababu bajeti ya upande wa madini nayo imeongezeka kwa zaidi ya 600%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kiasi fulani tunawaomba Waheshimiwa Mawaziri hawa vijana ambao wameaminiwa na Mheshimiwa Rais waweze kuikwamua nchi hii kupitia maeneo haya ambayo ni rasilimali za nchi yetu. Tunajua uwezo wako mkubwa wa kusimamia, lakini tunafahamu namna ambavyo wanapaswa kuongeza jitihada na ubunifu mkubwa zaidi kuisaidia nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo jambo mahsusi sana, katika nchi yetu tuna Gesi ya *CNG,* lakini kuna mchakato unaoendelea wa *LNG* ambao ninaamini mchakato huu utatutoa katika manunuzi makubwa ya mafuta ya petroli. Ununuzi wa mafuta ya petroli unagharimu kiasi kikubwa sana cha mapato yetu kama nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutaweza kulimaliza hili kwa sababu gesi iko ndani, hata kama kuna changamoto zozote na wale wanaowekeza, lakini ninahakika kwa sababu jambo litakuwa ndani itakuwa ni rahisi sana, hatutakuwa na uagizaji mkubwa wa mafuta ya petroli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia inahama kutoka kwenye mafuta kwenda kwenye vyombo vinavyotumia umeme. Sisi tunapoendelea ku-*delay*, tutakuja kuachwa kwa sababu dunia sasa mataifa yanayoendelea yanatengeneza vyombo vya umeme ikiwemo magari, lakini na vyombo mbalimbali vya matumizi ya nyumbani na matumizi ya miundombinu vinatumia umeme. Kwa hiyo, basi tutoke hapo tulipo tuweze kusogea haraka ili tukimbizane na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo *Nickel,* watu wa Wizara ya Madini wakimbie na hili. *Nickel* ndiyo inayotengeneza betri hizi ambazo zinatumika kwenye magari ya kisasa na kichanganyio kingine ni *cobalt*. Inawezekana hatuna *cobalt* ya kutosha kwa

hapa Tanzania, lakini nchi jirani zinazotuzunguka *cobalt* iko nyingi sana na uhitaji wa *cobalt* ni kiasi kidogo sana na *cobalt* kwenye matumizi haya hata gharama zake siyo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapo-*delay* kuingia katika *LNG,* tunapo-*delay* kuingia kwenye matumizi ya kutengeneza betri za umeme, tutajikuta tunaendelea kuwa wategemezi wa mafuta wakati ambapo dunia inakimbia na inatoka huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninataka kuishauri Serikali yangu. Kule vijijini kwetu kunapokuwa na miradi hii ambayo inafanyika na miradi ya Serikali ukiwemo ujenzi mbalimbali wa Barabara, lakini na miradi ambayo inatekelezwa na Serikali. Basi vijana wetu walioko kule vijijini waweze kuhusika kwenye kazi zile za nguvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na changamoto sana za ajira za nguvu kwa sababu watu wetu wamekuwa wanadhani labda nazo zinahitaji mchakato mkubwa. Tumeona kwenye bomba la mafuta, ajira hizi zimehusishwa kwenye vijiji. Ninaomba mfano huu uende katika maeneo mengine ili wananchi wetu waweze kupata hizi ajira za nguvu katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nilikuwa na machache sana ya kuchangia katika eneo hili, lakini pia kuna jambo ambalo ardhi zilizotwaliwa kwa ajili ya kupisha ujenzi wa miundombinu ya reli ya kisasa *(SGR)*. Wananchi wale katika eneo langu la Itigi hawajalipwa baadhi yao. Ninaomba basi mchakato huu nao uende haraka ili wananchi waliopisha ujenzi wa miundombinu hii waweze kulipwa ili wajue Serikali yao sasa nao inawajali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Yahaya Omary Massare. Nilimtaja Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji. Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo na Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, wajiandae.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa na hali ya uzima na afya. Niwashukuru na wenzangu humu wote tuliomo katika Bunge hili Tukufu, wamekaa na kutulia ili kusikiliza mpango unaoendelea sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwamba bajeti hii ni bajeti yetu ya mwisho kwa kipindi hiki. Tukimaliza kufunga kwa sasa hivi kutakuwa hakuna bajeti tena. Kwa hiyo, kwanza nachukua fursa hii ya kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wangu wote waliomo humu ndani. Ninawashukuru sana kwa kukaa pamoja, kwa kutulia na kuweza kufanya kazi kwa pamoja. Ninashukuru sana na tuendelee kukaa nao pamoja ili tuweze kujenga mustakabali wetu wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Waziri wangu wa Fedha pamoja na Naibu wake kwa kazi kubwa wanazozifanya katika Serikali yetu hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wanafanya kazi kubwa na leo hii wapo mezani ili kupitisha Bajeti yao ya Mpango katika Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru pia Mheshimiwa Rais wangu Samia Suluhu Hassan kwa jitihada zake anazozifanya, anafanya kazi kubwa ambazo kazi hizo zinaonekana Tanzania nzima pamoja na Serikali zake nyingine. Kwa hiyo, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuendelea sasa ili na mimi sasa hivi niweze kuishauri Serikali yangu. Nimeliona jambo kubwa katika Jiji hili la Dodoma: Jiji la Dodoma hivi sasa limekuwa linakua kwa kila hatua, kwa kila wakati, kwa kila saa. Kwa kipindi cha mwaka 1990 na 2014 sivyo ilivyo sasa hivi Dodoma. Sasa hivi imekua sana. Kwa hiyo, katika kutazama kwangu, ushauri wangu nimesema niulete katika mpango ili iangalie nayo Serikali yangu. Je, hili nitakalolisema wataweza kulifanya kwa sababu Serikali yetu ina miradi mikubwa mingi sana. Miradi hiyo inaendelea kufanya kazi lakini na sasa hivi ninataka nilitie mkazo hili ili liweze

kufanyika katika Jiji letu hili la Dodoma na hii pia ni mradi huu mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jiji la Dodoma hivi sasa limekuwa kubwa na kuna msongamano wa barabara na magari. Yaani sisi tukitoka hapa sasa hivi Bungeni, kama watatoka Waheshimiwa Mawaziri wao mwanzo, basi uhakikishe nyumbani unaweza ukafika saa mbili, tatu kutokana na msongamano ulioko huko nje barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ushauri wangu ninamwomba Mheshimiwa Waziri wangu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu pamoja na Naibu wake walichukue hili suala, tuweze kujengewa barabara ya juu ile *flyover* kama inawezekana iwe kama Dar es Salaam kwa sababu hili jiji kubwa na kila siku linakua. Je, tukijengewa hii barabara huku *(flyover)* tukapita kule juu na wengine wakapita chini, basi ule msongamano unakuwa mdogo. Hauwi mkubwa kama ulivyo hivi sasa. Kwa hiyo, ninaishauri Serikali yangu hili suala na Serikali yangu sikivu kama inawezekana nalo pia lifanyiwe kazi katika Jiji la Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, ninachangia kuhusu Mkoa wangu wa Kusini Unguja. Mkoa wa Kusini Unguja ni mkoa wenye wilaya mbili. Mkoa ule umejaa utalii baina ya Kati na Kusini lakini mie nitazungumzia kuhusu suala la askari walioko kule Kusini Unguja hasa hususan kuhusu zile nyumba. Nyumba za Polisi zimeanza kujengwa hiki kipindi cha mwaka wa pili bado hazijamalizika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipiga kelele kuhusu vituo lakini vituo tayari vimemalizika na hivi sasa vinafanya kazi vizuri lakini nyumba zao askari Kusini Unguja zinajengwa kwa kusuasua na hatujui lini nyumba zile zitaweza kumalizika. Ninaishauri Serikali, zile nyumba zimalizwe haraka ili wale askari wetu waweze kupata sehemu sahihi ya kuweza kukaa ili wafanye kazi vizuri na ukizingatia Mkoa wa Kusini ni mkoa wa watalii, lakini ikiwa wanakaa kule bado wakati wa utalii unapopamba moto, wako kule basi watazidi kujenga usalama katika kile kijiji chetu cha kule Kusini Unguja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na hayo mawili. Sina mambo makubwa sana isipokuwa hayo. Ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nawapongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Naibu ingawa wanazungumza huko, lakini ninajua wamesikia. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji. Nilimtaja Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo. Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga na Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, wajiandae.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu katika hii Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Mipango. Nichukue nafasi hii kwanza kuendelea kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa namna alivyoweza kutujaalia na sasa tunaenda kufika mwisho wa awamu yetu katika hiki kipindi cha miaka yetu mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi ninawashukuru sana Wananchi wa Jimbo langu la Musoma Mjini kwa ushirikiano mkubwa walionipatia. La pili, ninaendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri na kazi kubwa aliyofanya katika hii awamu yake hasa katika Huduma za Jamii kwa namna alivyoweza kuleta maendeleo makubwa katika Nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tu nimetoka Musoma, nilienda tu kufanya kazi moja ya kuwashukuru wananchi kwa ushirikiano wao, lakini jambo moja kubwa ambalo wananchi wameridhika nalo ni kwa namna walivyoweza kupata huduma za kijamii kwa kiasi kikubwa sana. Kwa maana kwamba, fedha nyingi mama yetu amepeleka kwenye upande wa elimu, ameweza kupeleka fedha nyingi shule zimejengwa na vijana wetu wameendelea kupata elimu pasipokuwa na malipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika huduma ya afya kazi kubwa sana imefanyika, vituo vingi vya afya vimejengwa, hospitali zimejengwa na huduma za afya zimeendelea kuboreshwa. Pia hata ungegusa katika sekta ya maji, kama kwangu pale Musoma

Mjini habari ya maji tulishasahau kama tuna tatizo la maji tena. Hata ungegusa upande wa umeme na leo ukiangalia tuna umeme ambao wa ziada sasa na tunazalisha megawati zaidi ya 4,000 lakini matumizi yetu tunatumia tuseme kama 50%. Kwa hiyo, hapo pote panaonekana kwamba ni kwa kiasi gani Serikali yetu ya Awamu ya Sita imepeleka fedha nyingi kabisa hasa katika huduma za jamii na watu wetu wameendelea kufaidi matunda ya nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo mafanikio makubwa zipo changamoto ambazo bado zinatusumbua kama nchi na bado zinawasumbua watu wetu. Kusema ukweli katika hili sasa ni ushauri wangu kwamba hebu tuangalie namna kujikita katika kutatua hizi changamoto. Changamoto kubwa tuliyonayo inayowasumbua watu wetu ni changamoto ya ajira, pamoja na mafanikio yote haya tuliyoyapata, lakini ajira bado ni changamoto kubwa sana. Ukienda kule mijini, ukienda vijijini vijana wengi hawana ajira, kwa hiyo wapo tu mtaani wanaendelea kurandaranda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninajaribu kuangalia hapa katika hotuba ya Waziri wa Fedha ameonesha kwamba ni kweli Serikali imefikia lengo lake, kiasi cha ajira kimefikia lengo na kuvuka kidogo, lakini tunasema bado watu wanaoingia kwenye soko la ajira kila mwaka ni wengi zaidi kuliko ajira yenyewe inayopatikana. Ndiyo maana pamoja na furaha ambazo watu wanazo katika huduma za jamii zilizoboreshwa, lakini suala la ajira sasa ninashauri kabisa kwamba hebu tuone namna gani sasa tutaelekeza huko nguvu zetu kubwa. Hata katika hii bajeti sijaona mikakati mahsusi ambayo itaendelea kupunguza tatizo la ajira kwa watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia viwanda vingi vimekufa, hivi viwanda vilikufa hasa pale Serikali ilipojitoa kwenye biashara ikaachia sekta binafsi, kama pale kwangu Musoma sasa sina kiwanda hata kimoja. Mheshimiwa Waziri wa Fedha ninakuomba na hili nimekuwa nikikuambia kila mara kwamba wale wananchi wangu wa Musoma hata kile kiwanda kilipobinafsishwa kulikuwa na mafao ya wale watumishi waliokuwa wa Kiwanda cha *MUTEX*, sasa hili nimekuwa kila leo nikilisema na kama Serikali mmekuwa

mkiahidi kwamba baada ya muda wale watu watapata haki zao, sasa wale watu wanaendelea kutaabika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba wale watu walitoka katika mikoa mbalimbali, sasa wengine hata wameshindwa kurudi makwao, sasa wanazeekea hapo, wanafia hapo lakini kila siku, leo wanaenda ofisini kwa Mkuu wa Mkoa, kesho wanakuja kwa Mbunge, keshokutwa wanaenda kwa Mkuu wa Wilaya kwa ajili ya kuomba basi waweze kupata haki zao ili waweze kuendelea na maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba tu Mheshimiwa Waziri atakaposimama ni vizuri sasa unipe kauli ya mwisho hivi ninavyoenda Jimboni, basi nijue kwamba ninakwenda kuwaambia nini, kwa sababu miaka mitano yote nimekuwa nikiomba haya mafao yao, lakini mpaka leo sijafanikiwa chochote. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ninaomba katika hilo aweze kulipa kipaumbele kutuambia kama watapata chochote na kama hawapati, basi ni vizuri tukawaambia na wakaweza kuelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, sasa kwa sababu hivi viwanda ambavyo vingi karibu vyote vimekufa bahati nzuri ile miundombinu kwa maana ya yale ma-*godown* yaliyokuwa ya vile viwanda bado yapo, sasa tunadhani tukiendelea tu kusema tusubirie mwekezaji aje, tumkabidhi vile viwanda, kwanza teknolojia imeshabadilika, leo viwanda ambavyo vinafanya kazi kulingana na teknolojia iliyokuja ni vile viwanda tu vidogovidogo. Kwa hiyo, ni vizuri tungeyabaini hizi *godown* zilizopo kwa maana sasa hivi tuseme ni *godown* na *scrap* yaliyoko mule kwa maana vile tena vimeshapitwa na wakati kulingana na teknolojia siyo viwanda tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sasa hivi tuhesabu tu kwamba tuna *godown* na yale *godown* sasa tuone namna ambavyo tunaweza kuwashawishi na kuwaleta wawekezaji wapya wanaoweza kuja na teknolojia za kisasa ili hizo *godown* ziweze kutumika katika viwanda vidogovidogo ambavyo vinaweza vikawapatia vijana wetu ajira. Tukiendelea tu kung'ang'ania tu tunasema kwamba anayekuja tunampa

kiwanda na zile *machine* zilizomo ninadhani haiwezi kusaidia sana kwa sababu zile *machine* zote zimeweza kupitwa na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo kwa sababu sisi kazi yetu ni ushauri na kwangu nilichotaka kukishauri au nilichoona nishauri kwenye upande huo ili tuweze kupunguza tatizo la ajira. Kwanza tunakubaliana kwamba, kwenye upande wa kilimo walau tija imeongezeka na kwa sababu tija imeongezeka basi walau kilimo kimeendelea kuchukua baadhi ya vijana wetu, lakini bado kulingana na vijana walivyo wengi hao walichukuliwa kwenye upande wa kilimo na katika baadhi ya maeneo mengine kama mifugo na uvuvi ni kwamba ile *gap* bado ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu sasa ninadhani ile *BBT* ambayo ilikuwa inalenga tu kwenye kilimo hebu tuone namna ya kuipanua. Nami kama ni ushauri wangu sasa ningeweza kushauri kwamba, badala ya *BBT* ikae huku Wizarani halafu ikae kwa mfano kwenye Wizara ya Kilimo ni kwa nini tusiishushe sasa *BBT*, kwanza iwe katika kila mkoa, ikishakuwa katika kila mkoa kule tuwape wale Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya tuwaongezee kazi nyingine kwa maana kazi yao kubwa waliyonayo pamoja na shughuli nyingine, lakini wana jukumu la kufanya kazi ya ulinzi na usalama. Sasa ninadhani kuna haja ya kuwaongezea hilo jukumu la kuona namna wanavyoweza kuongeza ajira kupitia hii *BBT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachoweza kukifanya ni vizuri basi kila Mkoa wakakaa, wakabuni kwamba ni namna gani wanaweza kutumia fursa zilizopo katika namna ya kuongeza ajira. Kwanza ungeniuliza leo ningesema JKT iwe katika kila mkoa, ikishakuwa kila mkoa hawa Wakuu wa Mikoa hawa kwa sababu ni Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama tuone namna tunavyoweza kuunganisha. Kwa sababu kati ya shida moja ambayo mara nyingi tunaiona, yaani unakuta kwa kawaida mtu, mfano, njaa ikiingia tunasema Serikali ni lazima ihusike, lakini unapokuta sasa watu wanazurura, wanazembea kufanya kazi, Serikali haijihusishi katika kuwabana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake ndiyo kama hayo kwamba, hata zile ajira zinazoweza kupatikana kama hatuna namna ya kuwabana yaani tutafute hizo ajira, tuzi-*plan* katika mikoa, lakini tuone namna ya kuzisimamia. Tunadhani kwamba kwa kufanya hivyo itaendelea kupunguza hii *gap* iliyopo ya vijana wengi ambao wanakaa mtaani, wanarandaranda, lakini vilevile ni kwa sababu hiyo ya kukosa ajira. Kwa hiyo, niendelee tu kushauri kwamba, hii *BBT* tukiisogeza kule mkoani inaweza ikafanya vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nililishauri sambamba na hilo katika kuongeza ajira, kuna maeneo ambayo kulikuwa na fursa, lakini kama Serikali kusema ukweli wamezembea na baada ya kuwa wamezembea sasa ile athari inarudi kwa wananchi. Mfano, kwetu ambao tupo kandokando ya Ziwa, kuna hili suala la uvuvi haramu. Suala la uvuvi haramu kusema ukweli ndiyo limetupatia umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukulie mfano Kanda ya Ziwa; pale Musoma kwenyewe tulikuwa na viwanda visivyopungua vitano vya samaki, vile vyote vilikuwa vinatoa ajira kubwa kwa sababu wale wavuvi waliokuwa wanaenda kuvua walikuwa wanapata ajira, wale wachuuzi waliokuwa wananunua walikuwa wanapata ajira, wale waliokuwa wanafanya kwenye viwanda vile vya kuchakata samaki walikuwa wanapata ajira, kwa hiyo ulikuwa unakuta mzunguko wa fedha ulikuwa mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali ikafika mahali kusema ukweli ni lazima tukubali ikazembea zembea hivi, vile viwanda vyote vimekufa. Leo ukienda Musoma viwanda vyote havifanyi kazi, ukienda Mwanza kuna kiwanda kimoja tu ndiyo kinafanya kazi, ukienda Bukoba hakuna kiwanda kinafanya kazi. Kwa hiyo hawa wote waliokuwa wanapata riziki hiyo sasa hivi wako tu mtaani wanarandaranda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninachotaka kukishauri sasa na hiki nilishashauri mara nyingi nikasema, hebu tufike mahali tuunde mamlaka inayoweza kuangalia Maziwa pamoja na Bahari. Tukishaunda zile mamlaka zitatusaidia kulinda, kwa

sababu haya tumeyaona, leo unapozungumza kwa mfano Mamlaka ya Ngorongoro unaona kabisa kwamba, yaani hao ndiyo wanasababisha mpaka ile Ngorongoro inaendelea kuwepo. Kwa hiyo ziko mamlaka kama hizi zote leo ukitaja yoyote ilimradi ni mamlaka ni kwamba kazi ya kwanza inajitahidi ku-*protect* kile ilichonacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo unapokuja kwenye habari ya Ziwa ambapo ndiyo kuna uchumi mkubwa wale samaki hawana mwangalizi, kwa hiyo watu wanavua tu hovyo hovyo. Ziwa kwa sababu limeunga katika nchi, kwa mfano lile Ziwa Victoria ziko nchi zisizopungua tatu tuna-*share* pale. Kwa sababu hakuna mamlaka hata namna ya kudhibiti kwamba hili ni la upande huu, hili ni la upande huu na yenyewe haipo, kwa hiyo, suala la uvuvi haramu linaendelea kutupatia taabu kubwa na kwa kufanya hivyo ndiyo maana watu wetu wanaendelea kuwa maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa na hili suala la mamlaka ninakumbuka hata Waziri aliyekuwepo alikubali kwamba yuko tayari sasa kwa ajili ya kuileta hiyo sheria ili tuweze kuipitisha, lakini mpaka leo wala hakuna anayeizungumzia. Kwa hiyo maana yake ni kwamba, Serikali ni kama inakwepa jukumu lake badala isimamie ule uvuvi haramu uishe sasa imeendelea kuwa na hali hiyo kwa hiyo matokeo yake shida zimeendelea kutuandama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni suala la Balozi zetu. Tunatambua kwamba, mojawapo ya zile Balozi zetu wanaangalia Diplomasia ya mahusiano, vilevile kazi kubwa nyingine wanayopaswa kuangalia ni namna ambavyo watu wetu wanaweza wakapata fursa zinazopatikana katika nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuamini wako Watanzania wengi wanazo fedha, wangependa kuona fursa zinazopatikana ili waweze kufaidika nazo, lakini kwa bahati mbaya sana ni kwamba, kwa sababu unakuta Watanzania wengi ambao wana fedha angependa kwenda kwenye nchi zingine kwa mfano kama India, kama China, lakini anashindwa aanzie wapi. Kwa hiyo, kwa sababu anashindwa aanzie wapi unakuta tu akienda

anaenda kufanya biashara ya *trading* ile ya kwenda, ataenda pale Guangzhou atanunua mali, atakuja hapa anauza biashara imefanyaje, imeisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mabalozi wetu, ofisi zetu za Ubalozi zingekuwa *active* wakawa, kwa mfano wale watu wa *Business* kile Kitengo cha *Business Attache* kikafanya kazi vizuri, maana yake ni kwamba kama Balozi wetu wa India angeweza kuwa anatueleza fursa zinazopatikana India na akaangalia ili watu wetu kila anapokuja huku anasema na anaweza kupata nafasi ya kukaa nao, lakini hata watu wetu wakienda kule waweze kupokelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalisema hivyo kwa sababu gani, kwa nafasi yangu kama mjasiliamali nimezunguka nchi nyingi na kila ninapoenda nimekuwa ninaenda hata katika Balozi, yaani ukifika pale unamwambia Balozi unakuja, ukifika pale anachoweza kufanya ni kukukaribisha, atakusikiliza halafu, yaani atakupa msaada mdogo sana. Kwa hiyo, ninadhani hilo nalo ni changamoto kubwa tuliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi juzi hapa mimi nilienda hapa jirani tu hapa Comoro, nilipoenda pale Comoro kwa bahati nzuri kwa sababu kwa bahati mbaya ile nchi hawajui Kiingereza na hawajui Kiswahili, wanajua Kifaransa na hiyo lugha yao ya Kikomoro. Kwa hiyo, nililazimika kabla ya kwenda nimtafute Balozi, baada ya kuwa nimempata Balozi ninashukuru sana kwanza kwa mapokezi aliyonipatia, siyo hilo tu, nilipofika kule alinipa usaidizi wote na baada ya kunipatia ule usaidizi, umenifanya nikaangalia fursa zilizopo kule na sasa nikaona kumbe kama Mabalozi wote wangekuwa wanafanya hivyo, maana yake ni kwamba katika kukuza uchumi wa nchi yetu, Watanzania wangeweza kufaidika kupitia hizo Balozi zetu zilizoko katika nchi mbalimbali. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE (MHE. COSATO D. CHUMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Muda wake ulikuwa umeisha alikuwa anamalizia. Mheshimiwa malizia *point* ya mwisho.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nichukue nafasi hii kusema kwamba, tunadhani kuna haja ya Balozi zetu nazo zikiwa *active* zitasaidia sana katika kupunguza hili tatizo la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Vedastus Manyinyi. Kabla sijamtaja mchangiaji niliyekuwa nimemtaja mwanzo, nina matangazo ya wageni ambao wapo muda huu.

Kuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao ni wageni 12 wa Mheshimiwa Felista Deogratius Njau ambao ni wanawake wafanyabiashara *Team No Excuse* kutoka Jijini Dar es Salaam na Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 106 wa Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge, ambao ni wanafunzi 90 na walimu 16 wa Shule ya *Moshi Academy* na *Guardian Angels Academy*. Karibuni sana wanafunzi wetu kutoka huko Moshi. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Ni wageni Saba kutoka Wilaya ya Kigamboni Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana wageni wetu kutoka huko Wilaya ya Kigamboni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa na Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mheshimiwa Robert Chacha Maboto na Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, wajiandae.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niungane na wenzangu kuweza kuunga mkono bajeti hii nzuri. Kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea bajeti nzuri ya trilioni 56.4 ukilinganisha na bajeti ya 2024/2025 ya trilioni 50. Maana yake nini? Ametupatia bajeti nzuri ambayo sasa tunayo imani inakwenda kufanya kazi nzuri katika kuwaletea maendeleo Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ninampongeza Waziri Mwigulu na Waziri mwenzake Profesa, pamoja na Naibu Mawaziri kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa kweli tumeona mabadiliko ni makubwa sana. Mawaziri na Naibu Mawaziri wenu tunawapongeza sana. Vilevile sekta mbalimbali ambazo wanaziongoza ikiwemo *TRA* na nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tuwapongeze Mawaziri hawa kwa sababu kodi wanayokusanya *TRA*, mfumo ambao upo sasa, huko nyuma mfumo wa kukusanya kodi kwa wafanyabiashara ulikuwa ni wa nginjenginje, mshikemshike, kodi ilikuwa ni kama za kunyang'anya wafanyabiashara, lakini leo kodi inayokusanywa ni kodi iliyotulia, wanafanya mazungumzo na wafanyabiashara. Tunampongeza sana Waziri wa sekta na Kamishna Mkuu anayesimamia suala hili la kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya ya Wafanyabiashara walikaa, wakaleta changamoto nyingi walizoeleza zinazoleta vikwazo katika biashara zao, tunampongeza Rais alimtuma Waziri Mkuu Mheshimiwa Majaliwa Majaliwa pamoja na Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango wakakae na hawa watu, tunawapongeza baadhi ya hoja wamezishughulikia, tunawapongeza sana. Ombi letu ni kwamba, hoja zilizobaki sasa na zenyewe ziweze kushughulikiwa ili shughuli za biashara ziweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano nitamke moja ambayo ni hii kwamba wageni walikuwa wanafanya biashara ambazo wazawa tunaweza kufanya. Jambo hili lilikuwa siyo sawa na sasa wameliondoa; kwa hiyo, tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie sasa kwenye hela hizi ambazo bajeti hii ipo mbele yetu. Ombi langu kwa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na mwenzake; kwenye maeneo yetu tuna maboma mengi sana ambayo kila halmashauri walisema yaletwe. Tunaomba fedha hizi sasa tutakapokuwa tumepitisha tarehe 24 ya kupiga kura (kura tutapiga ndiyo hakuna lingine) ili ziende sasa zikafanye kazi ya kutatua changamoto ya maboma haya ambayo yamejengwa yakiwemo ya Jimbo la Makambako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Makambako lina maboma ya zahanati, maboma ya majengo ya shule na mengineyo. Sasa ombi ambalo ninakuomba kuna kituo cha afya ambacho nilisema siku ile hapa kwenye swali ambacho kimejengwa kule Kitandililo, kimejengwa kule Mahongole pale kwenye Kijiji cha Mahongole kwamba haya yalishajengwa, walishatupa fedha na zilizobaki ni kumalizia. Waliagiza Mkurugenzi alete makisio na yameshaletwa Hazina; tunaomba fedha hizi ziende kwa wakati ili zikamalizie majengo haya ambayo tayari yameshaanza kutumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna hela ambazo walishatupa, shilingi milioni 583 fedha za kujenga shule ya ufundi na fedha zilizobaki bado hawajatupatia. Siku ile kwenye swali hapa Mheshimiwa Waziri alisema sasa wanajiandaa kupeleka fedha hizi za shule za ufundi ambazo zimepelekwa ninadhani kila baadhi ya halmashauri. Tunaomba sasa ziende ili zikakamilishe shule hizi za ufundi ziweze kufanya kazi ile iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipo Kituo kingine cha Afya pale Usetule. Ninaomba na chenyewe hiki fedha ziende ili zikaweze kutatua. Kipo kingine tena kituo cha afya kipo pale Kata ya Kivavi na eneo linalojengwa linaitwa Kivavi. Kwa kweli niombe sana fedha hizi ziweze kwenda zikafanye kazi hiyo ya kutatua changamoto za wananchi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile zipo fidia kwenye Jimbo la Makambako kuhusu suala la umeme wa upepo. Wawekezaji wa suala la umeme wa upepo kama imeshindikana basi Serikali itoe kauli ili maeneo haya yarudishwe kwa wananchi kwa sababu limechukua sasa ni miaka 18, (miaka 18 wananchi hawajalipwa fidia). Sasa kama mwekezaji wa suala la umeme wa upepo limeshindikana, basi tutamke kwamba imeshindikana tuwarudishie wananchi ili itakapofika muda Serikali inahitaji, watafanya mazungumzo upya kuliko hivyo sasa imekaa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupongeze hili suala la bodaboda na bajaji. Katika Mji wa Makambako tuna bodaboda nyingi, tuna bajaji nyingi zinasaidia sana wananchi. Suala hili ambalo limepitishwa hapa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu tunapongeza sana

kwa kweli kwa dhati kabisa na wananchi jambo hili wamelifurahia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo lingine hapa ninaomba niliseme. Nchi hii ni yetu sote. Tunapoona tunapokwenda wapo watu sasa wameanza kuleta viashiria ambavyo vinaweza kuvunja amani katika nchi hii. Mheshimiwa Rais amesimamia jambo hili vizuri sana. Hivyo tuombe taasisi inayohusika na baadhi ya watu kupitia mitandao mbalimbali wameanza kuchora picha mbaya kwa Mheshimiwa Rais (wanamchora kama vikatuni) nilisema siku ile hapa nilipochangia kipindi kilichopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inayohusika ishughulikie jambo hili. Mheshimiwa Rais wetu anaheshimika sana ndani ya nchi na nje ya nchi kwa mambo makubwa anayoyafanya ya kusimamia kuhakikisha nchi hii inakuwa ya amani. Kwa hiyo, niombe sana jambo hili Wizara inayohusika iweze kusimamia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo hapa vilevile ambalo biashara mbalimbali ambazo zinafanywa na wageni ambao nimesema hapa sisi wenyewe tunaweza kuzifanya. Jambo hili Watanzania walio wengi wana uwezo mkubwa wa kufanya. Kikubwa ni ninyi kutuwezesha kupitia benki za kukopa kwa riba nafuu ili tuweze kufanya kazi ambazo wanaweza wakafanya wageni. Sisi wenyewe tuna uwezo; wataalam tutaajiri na wapo wasomi wengi tutaajiri. Kwa hiyo jambo hili lisimamiwe kwa uzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho; ukanda wetu wa Kusini pale Makambako tumejengewa Kiwanda cha *IDOFFI*. Kuna mashine au mitambo ambayo ilishaletwa pale kwa ajili ya kutengeneza vidonge na *syrup*. Mashine hizi ni hela za Serikali za mabilioni zipo pale, majengo yapo haijafunguliwa. Alipokuja Mheshimiwa Makamu wa Rais kuangalia kile kiwanda na kuzindua tulimwonesha na aliagiza. Mpaka leo, nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwigulu wakae na Mheshimiwa Waziri wa Afya, tatizo ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda hiki hakifunguliwi, majengo yapo, mitambo ipo na fedha; wamekwama nini? Kamati ya Bunge ilipokuja iliona suala hili na waliagiza pia mwaka jana, mwaka juzi mpaka leo ipo. Kwa hiyo nimwombe sana watu wa ukanda huo tunategemea sana kiwanda hiki kifunguliwe ili wapate ajira vijana ambao watakuwa si wataalam wanaotokana na eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho wenzangu wamesema hapa. Unajua mtu akifanya vizuri ni lazima umpongeze. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na Mheshimiwa Profesa tangu wameingia kila mmoja kwenye Wizara yake tumeona mabadiliko. Tunawaombea waendelee, Wizarani mambo yanakwenda vizuri na shughuli zinakwenda vizuri; tunawapongeza sana, sana, sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawaombea kwenye majimbo yao, wananchi wa majimbo yao; Waheshimiwa Naibu Mawaziri na Waheshimiwa Mawaziri, watu wakawachague wawarudishe tena. Wamewatumikia Watanzania vizuri wakiwepo na Watanzania wa Jimbo la Makambako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pia...

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wake umeisha huyu, anamalizia tu. Malizia Mheshimiwa.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Makambako kwa kuniamini na kuendelea kuniamini. Pia, jana na juzi nimepita kwao kwenda kuwaambia mambo yaliyotekelezwa kwa bajeti hii ambayo inaishia mwezi huu Juni. Sasa ninawaomba waendelee kuniamini, nipo vizuri. Nitahakikisha ninakwenda kuwatumikia kwa bajeti hii ambayo tunakwenda. Ninawashukuruni na Mungu awabariki sana wananchi wangu ninawapenda sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, ahsante sana.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane na Mheshimiwa Janejelly James Ntate wajiandae.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi, lakini pia ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa fursa hii ya jioni hii ya leo ya kuweza kupata nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya katika Taifa letu. Tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu amjalie afya njema ili inapofika Oktoba 25, wananchi waweze kumwamini tena kwa kipindi kingine cha miaka mitano kwa kazi kubwa ambazo ameendelea kuzifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watu wa Halmashauri ya Mji wa Bunda, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya jambo kubwa la kihistoria ambalo limekaa pale Bunda kwa muda mrefu ambapo aliidhinisha zaidi ya shilingi bilioni 50 kuwalipa wananchi wetu wa Kata ya Nyatwali ambao baadhi yao wameshaondoka na baadhi yao bado hawajaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hilo pia, bado kuna changamoto ndogondogo ambazo bado wananchi wetu wanazidai kwenye Serikali. Niwaombe watu wa Serikali kabla ya kumaliza bajeti hii waweze kuwalipa wale wananchi wetu waondoke katika eneo lile ili waweze kwenda kuanza maisha yao sehemu nyingine. Kwa hiyo tunawashukuru na watu wa Wizara ya Fedha kwa kufanya jambo hili ili wananchi wetu hawa waweze kupata maisha yao katika eneo lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ninapenda niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Bunda Mjini kwa namna ambavyo waliniamini miaka mitano na ninaamini kupitia Serikali ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan tumefanya kazi kubwa na kuubadilisha mji wetu wa Halmashauri ya Mji wa Bunda kwani si kama tulivyoingia, lakini leo mji ule umebadilika na unaonekana ni mji wa kisasa. Pia, shughuli za maendeleo zinakwenda kwa *speed. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe tu wananchi wetu wa Jimbo la Bunda Mjini itakapofika 25 ya mwezi wa 10 waweze kuendelea kuiamini Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Chama chetu Cha Mapinduzi. Mimi pia mwenyewe bado nitakuwa tayari kama Mungu akinijalia uzima kuendelea kuwahudumia wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunajadili Bajeti ya Wizara ya Fedha. Hivyo, tunajadili Bajeti ya Wizara ya Fedha kwa muunganiko wa Wizara zote ambazo tumeshazijadili (Wizara ya Fedha na Wizara zingine zote ambazo zimepita) ili haya yote ambayo tumeyazungumza hapa zaidi ya miezi mitatu tuyamalizie hapa kwenye Wizara ya Fedha. Pia, Wizara ya Fedha ili iyafanye haya mambo yote yaweze kufanyika vizuri, lazima kupatikane pesa na hizo pesa mahali pa kupatikana lazima zitoke kwa wananchi wetu wale wanaofanya shughuli mbalimbali wakiwemo wafanyabiashara na watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ombi langu kwa wananchi wenzangu, Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Watanzania wote kila mmoja kwa nafasi yake; kwa sababu bajeti yetu inategemea makusanyo yetu tujitoe wale wanaofanya biashara kila mmoja kwenye nafasi yake ili aweze kulipa mapato kwenye Serikali. Hii ni kwa sababu bila kufanya hivyo wananchi hawawezi kudai barabara wala maji, vituo vya afya, shule za misingi na sekondari na mambo mengine kama watakuwa hawawezi kulipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima watu walipe kodi. Bahati nzuri tunaendelea kuishukuru Serikali kwa sababu imeendelea kutengeneza mazingira mazuri ya ulipaji kodi kama hivyo

ambavyo inaendelea kupunguza kero mbalimbali za wafanyabiashara ili wafanyabiashara waweze kulipa kodi kwa hiari zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na vizuizi vyote ambavyo vinaondolewa kwa ajili ya kuleta kero kwa wafanyabiashara, lazima sisi kama wafanyabiashara tujue kwamba kulipa kodi ni suala la lazima. Tunalipa kodi ili kuiletea nchi yetu maendeleo. Nje na kodi, haya yote ambayo tunazungumza hapa hakuna kinachoweza kufanyika na hatuwezi kupata maendeleo kwenye nchi yetu yasiyotokana na sisi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata zikiwa ni fedha za misaada tunazipata, hizo baadaye zinalipwa na zinalipwa kutokana na kazi zetu ambazo sisi wenyewe wananchi wa Tanzania tunazifanya. Kwa hiyo, niiombe Wizara ya Fedha iendelee kuboresha miundombinu ya utozaji kodi kwa wananchi na wafanyabiashara mbalimbali ili kwamba wananchi waweze kulipa kodi zao vizuri kwa ajili ya manufaa ya nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi kero mbalimbali ambazo zilikuwa zinawapata wafanyabiashara za kufungiwa biashara zao ni kweli kwamba Mheshimiwa Waziri wa Fedha jambo hili limekuwa likifanyika. Mamlaka ndogo za halmashauri au za kata, jambo dogo tu kwa mfanyabiashara wanaweza kwenda wakafunga biashara na unaona kama ni jambo ambalo wangeweza kuzungumza wakaelewana na maisha yakaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu pia wanapofunga biashara ya mtu wanamfanya pia asipate nguvu ya kulipa hicho ambacho wao walienda kukidai. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, kwa jambo hili ambalo amelisisitiza hapa kwenye hotuba yako tunaiomba sana Serikali ilisimamie vizuri. Ninaamini Watanzania leo wameelimika kwa kiasi kikubwa na wana uelewa mzuri sana kwa ajili ya kulipa kodi kwa ajili ya maendeleo ya Taifa lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninataka kuzungumza jambo la hizi *control number* ambazo tunatumiwa kwenye mifumo ya Serikali na sisi tunazitumia kwa ajili ya kufanya

malipo kwenye Serikali. Kuna mahali ambapo panaonyesha bado *control number* hizi inawezekana zikatolewa ukafanya malipo lakini malipo yale yasifike mahali husika. Sasa kwa jambo hili likionekana ni kweli na likaendelea kuwepo linaweza kuja kuleta madeni makubwa sana kwa wafanyabiashara wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana watalaam wetu wa Serikali ambao wao ndiyo wanasimamia mifumo hii waisimamie vizuri. Tulipe malipo ya Serikali kupitia hizo *control number* za Serikali, lakini na malipo hayo yenyewe yafike Serikalini pia ili kwa baadaye lisije likageuka kuwa tatizo kwa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni jambo la vyuo hivi vya ufundi na shule za amali ambazo Serikali imetoa fedha na zimejengwa karibu katika kila halmashauri. Jambo hili Serikali ikilisimamia vizuri vijana wetu wengi wakapata uwezo wa kufanya kazi na wakawa wamefundishwa; kwa sababu zile shule kwa mfano shule ya amali ambayo imejengwa pale Bunda Mjini, hata kama wale wanafunzi watafundishwa kwenye maeneo yale watafundishwa vitu ambavyo pia vinaendana na jiografia ya maisha yao na pale wanapoishi na vitu ambavyo wanaweza wakavitumia wao wenyewe. Kwa hiyo niiombe sana Serikali iendelee kuboresha shule hizi na vyuo vyetu vya ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu likipata watu wenye uwezo wa kufanya kazi kwa kiasi kikubwa ndiyo njia pekee ambayo tunaweza tukaisaidia nchi yetu kwa kufanya walipakodi waongezeke zaidi kuliko wale walipakodi wachache waliopo ambao wanapewa mzigo mkubwa wa kulipa kodi. Kwa hiyo kupitia shule hizi na vyuo vyetu vya ufundi kama Serikali itasimama vizuri na jambo hili, ikawajengea vijana wetu uwezo wa kufanya kazi vizuri kama vile ambavyo tuliona jambo hili la pikipiki lilipojitokeza pamoja na kwamba unaona vijana wetu wanavyochangamka nalo ni jambo ambalo linawasaidia kwa sababu pia limepunguza sehemu kubwa ya tatizo la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wote wale ambao wanaendesha pikipiki leo au bajaji na vitu vingine wasingekuwa na kazi hiyo wakategemea kwenda kuomba kazi Serikalini, Serikali

isingekuwa na uwezo wa kuwaajiri watu wote hao; isingewezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuiombe sana Serikali iendelee kuboresha vyuo hivi vya ufundi na shule hizi za amali ili ziweze kuwafundisha vijana wetu kujitegemea na kuwajengea uwezo wa kuweza kufanya kazi zao za mikono ambazo zinaweza zikawafanya pia na wao wawe sehemu ya kuchangia pato kwenye nchi yao na Serikali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili likisimamiwa vizuri kwa sababu, leo ukija kuangalia kwa mfano, bajeti yetu ya trilioni 56 fedha ambazo zinakusanywa katika nchi yetu ni takribani trilioni 30, trilioni 26 ni ambazo tunategemea kupata kutoka maeneo mbalimbali. Kwa hiyo tukiwaongezea watu uwezo wa kufanya kazi, wakajiajiri wao wenyewe, wakafanya kazi zao wenyewe, watakuwa ni sehemu ya kupunguza tatizo la nchi yetu kutegemea misaada kutoka nje. Jambo hili ni muhimu na ni ambalo Serikali inapaswa kulisimamia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti,  jambo la mwisho ni kuiomba Serikali. Kuna miradi mbalimbali ambayo imeanzishwa katika Halmashauri ya Mji wa Bunda; tuna vituo vya afya Kata ya Waliku, tuna kituo cha afya tumepata katika Kata ile ya Guta, tuna Hospitali yetu ya Halmashauri ya Mji wa Bunda, vyote hivi bado havijakamilika vizuri, bado tunaomba fedha kutoka Serikalini, ili Hospitali hii ya Halmashauri ya Mji wa Bunda iweze kukamilika vizuri, iweze kutoa huduma kuwasaidia wananchi wetu na vituo vyetu vile vya afya ambapo kimoja kipo Kata ya Waliku na chenyewe kimepata majengo, lakini bado hakijakamilika. Tunaiomba Serikali ifanye kila linalowezekana itoe fedha, ili vituo hivi vya afya viweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na barabara za mitaa ambazo kwa kiasi kikubwa leo zinapitika, vilevile changamoto bado zipo. Tunaiomba Serikali pia, iweze kutoa fedha, ili kuhakikisha kwamba, barabara hizi zinaweza kupitika kwa wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo nilikuwa na hayo. Ninakushukuru kwa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Robert Chacha Maboto. Nilimtaja Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mheshimiwa Janejelly James Ntate, ajiandae.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia Bajeti yetu ya Serikali. Awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuweza kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu kuchangia. Pia, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia amani, utulivu, umoja na upendo katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefanya udadisi katika Wimbo wetu wa Taifa nikagundua kwamba, tumemwomba Mwenyezi Mungu mara kumi alete baraka katika Taifa hili. Kwa hiyo, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupokea maombi yetu na kuliwezesha Taifa letu liendelee kuwa na baraka na maendeleo. Pia, ninasema tu kwa wale wachache wenye nia mbaya ya kutaka kuvuruga umoja, amani na utulivu kwa uweza wa Mwenyezi Mungu wetu na manabii wake waliompendeza tangu kale, washindwe na walegee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru na kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa, ambayo ameifanya kwenye jimbo imeonekana hata na nchi nzima. Kwa ujumla tumeshuhudia miradi mingi ya kimkakati; miradi ya maendeleo katika sekta zote imefanyika na kuwezesha kutimiza dhamira aliyokuwanayo, ambayo aliitoa kwenye hotuba yake ya tarehe 19 Machi, 2021 wakati alipoapishwa kushika hatamu ya uongozi wa nchi yetu, lakini pia, alirudia maneno yaleyale wakati alipofika hapa Bungeni kwa mara ya kwanza kulihutubia Bunge, Siku ya tarehe 22 Aprili, 2021. Kwa hiyo, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kusimamia vizuri kutoa fedha nyingi na kuzielekeza katika miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza na kuwashukuru rafiki zangu, *schoolmates* wangu, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Uwekezaji, Manaibu wao

pamoja na watumishi waliopo katika Wizara hizo kwa kutuletea bajeti nzuri, ambayo ina *reflect* maono ya Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Pia, nitakuwa mchache wa fadhila nisipompongeza *RC* wangu, dada yangu, Mheshimiwa Zainab Telack.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, amefanya kazi kubwa sana katika Mkoa wa Lindi kusimamia miradi mbalimbali inayoelekezwa huko, sanasana kwenye eneo la kukomesha migogoro ya wakulima na wafugaji, lakini pia, kupandisha kiwango cha elimu. Kwa kweli, tumefanya vizuri sana katika miaka hii ya karibuni na sasa tunashuhudia matunda ambayo yamewekezwa na Mheshimiwa Rais wetu katika maeneo mbalimbali, ikiwemo hiyo sekta ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchache wa fadhila pia nisipowapongeza na kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Kilwa Kaskazini katika kata zote 13 kwa kuniunga mkono katika mambo mbalimbali ambayo yaliainishwa katika utekelezaji wa ilani ya uchaguzi, lakini pia, yaliyokuwa yanatatiza katika jimbo letu. Ninawashukuru sana wananchi wa Kata ya Kipatimu, Chumo, Kibata, Kandawale, Namayuni, Mingumbi, Tingi, Somanga, Kinjumbi, Miteja, Mitole, Njinjo na Miguruwe. Ninamwomba Mwenyezi Mungu anijalie afya njema ili niendelee kuwatumikia katika kipindi kijacho cha miaka mitano wananchi wa Jimbo langu la Kilwa Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata mambo mengi sana kupitia bajeti ambazo zimewekezwa, ambazo zina *reflect* dhamira njema, ambayo anayo Rais wetu katika Jimbo la Kilwa Kaskazini. Tumepata zahanati zaidi ya nane, vituo vya afya zaidi ya vitatu na kingine kimeletewa fedha juzi katika Kata ya Kandawale, shilingi milioni 250. Tumepata shule za sekondari tatu, za msingi sita na pia, miradi ya maji zaidi ya vijiji 14 imetekelezwa. Tumepata madarasa ya kutosha, matundu ya vyoo ya kutosha, vifaa vya kufundishia na kujifunzia pamoja na vifaa tiba vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, minara ya simu zaidi ya 16 imewekwa katika Jimbo la Kilwa Kaskazini, maboti ya uvuvi, mpango wa matumizi bora ya ardhi umefanyika katika zaidi ya

vijiji 44 na unaendelea. Pia awamu ya mwisho ambayo imetolewa Mwezi Januari tumepata mikopo zaidi ya shilingi bilioni 1.3, kwa ajili ya wanawake vijana na kundi la wahitaji maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa kuliko yote ni tulipopatwa na janga la mafuriko Serikali imeleta zaidi ya shilingi bilioni 119 na 47%, sawa na shilingi bilioni 56, imekwenda katika Jimbo letu la Kilwa Kaskazini kujenga miundombinu mipya wezeshi katika maeneo hayo ya barabara. Kwa hiyo, namshukuru tena Mheshimiwa Rais na ninamuombea kwa Mwenyezi Mungu amjalie afya njema, ili tuweze kumpa tena kipindi cha miaka mitano. Tumejiandaa Wanakilwa Kaskazini na Wanakilwa kwa ujumla kuweza kumpa ushindi wa kishindo. Mwenyezi Mungu amjalie sana mama huyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo machache ya kushauri. Jambo la kwanza, ninaomba miradi ya maji iendelezwe, hasa katika vyanzo vikubwa vya mito. Sisi bahati nzuri Mikoa ya Kusini hatuna ziwa, ukiondoa kule Ruvuma, lakini tuna mito mingi inayotiririsha maji mengi yanayokwenda baharini; Mto Ruvuma, Mto Lukuledi, Mto Ruhuhu, Mto Rufiji na ipo mito ya msimu zaidi ya mitatu, Mto Mbwemkuru, Mto Matandu na Mto Hanga, ninafikiri Serikali sasa ijikite katika kuona namna ambavyo itaboresha miundombinu hiyo ya maji katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatarajia Serikali iweke mabwawa katika mito hii, ambayo ni *seasonal,* kwa sababu itasaidia kwanza itapunguza mafuriko ambayo tumeyaona mara kwa mara, lakini pili, kupata malisho ya mifugo. Pia, itasaidia kupata maji, kwa ajili ya mifugo pamoja na kupata maji safia na salama, kwa ajili ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninaomba miradi yetu ya *BBT* Serikali iiangalie katika maeneo ambayo mazao yake hayavunwi kwa wingi, yale ya kimkakati ambayo yatakwenda kutatua matatizo ya msingi tuliyonayo. Tumeona miradi mingi imeelekezwa kulima pilipili hoho, kabichi, vitunguu; mimi ninafikiri kwa sababu, hizi bidhaa zinapatikana kwa wingi na nyingine nyingi tunauza nje ya nchi tuwekeze, labda kwa mfano kwenye zao la kimkakati ambalo tutapata uzalishaji wa mafuta kwa

sababu, mpaka leo tunatumia fedha nyingi za kigeni kwenda kununua mafuta kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna changamoto, kwa mfano ya wakulima na wafugaji katika Mikoa ya Kusini, hasa Mkoa wa Lindi na wilaya zake. Ninafikiri katika eneo hilo Miradi ya *BBT* ilenge katika kutatua changamoto za msingi, kama hii ya migogoro ya wakulima na wafugaji. Kwa hiyo, ninafikiri tukienda hivyo basi maisha ya wananchi wetu yatakuwa mazuri, lakini pia, uchumi utaimarika na mambo mengine yatakwenda sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali iongeze nguvu katika barabara za vijijini. Barabara nyingi za vijijini, hasa katika Wilaya ya Kilwa, Wilaya ya Rufiji na majimbo yote mawili ya Kilwa Kusini na Kaskazini, Liwale, Nachingwea na kwingineko zilikumbwa na tufani ya Mvua za *El-Nino* na Kimbunga Hidaya. Tunaishukuru Serikali, kama nilivyosema mwanzo, Mkoa mzima wa Lindi umeleta shilingi bilioni 119, miradi inaendelea na jana nilikuwa jimboni, baadhi ya makalavati yameanza kukamilika kwa hiyo, ni hivi karibuni tutapata tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kule kwenye barabara za vijijini, ambako huko ndiko mazao ya korosho, ufuta na mengine yanatoka yapate kusafirishwa kirahisi kufika kwa walaji, kwenye masoko, ninafikiri bado kunahitajika fedha nyingi ziongezwe. Hii ni, ili kuhakikisha uchumi wa wananchi wetu unaendelea kuimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, Serikali imekuwa ikitumia nguvu kubwa sana inayotokana na mapato yake ya ndani kuendesha miradi ya kimkakati na yenye vigezo vya kibiashara. Katika eneo hili tunayo taasisi yetu iliyoundwa, ambayo inahusika na miradi ya ubia au *PPPC (Public Private Partnership Centre);* ninafikiri kitengo au taasisi hii iwezeshwe vya kutosha, ili itoe msaada mkubwa kwa mtaji wa kuendesha hii miradi. Matokeo yake ni Serikali itapunguziwa mzigo wa kibajeti katika kuhudumia hii miradi, lakini pia, tutapata teknolojia kutoka kwa hawa wawekezaji kwenye hiyo miradi ya ubia, tutapa ufanisi mkubwa na pia, ubunifu wa kutosha wa kuendeleza hiyo miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba, miradi ikishirikisha watu binafsi maana yake ni tutatanua wigo wa watu binafsi kuweza kushiriki katika shughuli za maendeleo na hivyo, wananchi kukua kiuchumi, kama mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Kwa hiyo, ninaomba Serikali iangalie hata ile *SGR,* aliyozungumza rafiki yangu hapa Mheshimiwa Mpakate, inaweza ikaingia katika utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ifanye bidii ipate wawekezaji wabia tuweze kujenga kwa haraka hata ile ambayo bado haijaingizwa kwenye mpango, ya kutoka Dar es Salaam kupitia Lindi mpaka Mtwara nayo iweze kujengwa bila shida. Kuna Nchi kama Korea, Malaysia zimepiga hatua kubwa sana kwa kutumia hii miradi ya *PPP* kwa hiyo, naiomba sana Serikali yangu Tukufu isimamie jambo hili, ili kuhakikisha kwamba, utekelezaji wa miradi siyo tu unatekelezwa kwa mtaji wa Serikali, bali pia, unashirikisha watu binafsi chini ya utaratibu wa *PPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninakushukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane. Mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku ya leo ni Mheshimiwa Janejelly James Ntate.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninaungana na wenzangu kumshukuru Mungu kwanza, aliyetupa uweza, ametupa nguvu na mkono wake ulituatamia, leo tunasoma bajeti ya mwisho ya Bunge la Kumi na Mbili. Sifa na utukufu turudishe kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mambo aliyofanya kwa watumishi wa Serikali. Unajua mimi nikiamka ni watumishi, lakini kabla sijaenda huko ninakumbusha kidogo, nilikuwa mtumishi wa Wizara ya Fedha, wakati Tume ya Mipango inavunjwa watumishi wote tulichanganyikiwa. Kwa sababu, nilikuwa kiongozi wa wafanyakazi, nilitumwa nipeleke hoja kwenye Baraza la Wafanyakazi, wakati huo sijajua kama nitakuwa Mbunge, tuongelee kurudishwa kwa Tume ya Mipango, hatukufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuja Bungeni nimeshirikiana na wenzangu kupaza sauti kuomba Tume ya Mipango. Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, hii ni bajeti ya mara ya pili tukiwa na Tume ya Mipango. Ukilinganisha bajeti za nyuma na bajeti hizi mbili ni mbingu na ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuja mpango wa maendeleo na bajeti vinaendana na hiyo ndio maana ya kuwa na Tume ya Mipango, lakini wakamkabidhi Waziri ambaye anajua kuchambua mambo. Mimi huwa namwambia Profesa Kitila yaani akishaanza mosi, ujue kinachofuata ni kitu cha mikakati. Kumekuwa na ushirikiano mzuri sana kati za Wizara ya Fedha na Tume ya Mipango, wanashirikiana kwa karibu sana. Ukiangalia mpango wa maendeleo, ukaangalia na bajeti, unaona hawa wataalam walikaa pamoja chini ya Mawaziri wanaonena jambo moja na wakatuletea bajeti ambayo ime-*cover* nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivi kwa sababu, nikianza na watumishi, kwa mara ya kwanza kwa miaka minne wakati naingia kuwa Mbunge wao humu watumishi walikuwa na miaka sita hawajapandishwa mshahara, lakini kwa miaka minne wamepandisha mshahara mara mbili. Mwaka wa Fedha 2022/2023 kima cha chini walikitoa kwenye shilingi 300,000 mpaka shilingi 370,000 sawa na 23.3%, lakini leo Mwaka wa Fedha 2025/2026 wamepandisha kutoka shilingi 370,000 mpaka shilini 500,000 sawa na 35.1%, sio jambo dogo na sio la kubeza. Niwaambie, watumishi wote wanasema Oktoba wao wana-*tick,* iwe mvua, iwe jua, kura zao ni kwa Mheshimiwa Rais kwa sababu, anawadai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baraka walizofanya Mungu atawalipa. Kitabu Kitakatifu cha Biblia kinataja mistari ya kuwaenzi wazee na kuwatumia mara 100, tuwatumie wazee, tuwapende wazee, tuwasaidie wazee, tuwalee wazee. Leo wale wazee wastaafu wanaolipwa na Hazina, Naibu Waziri nimekusumbua sana, nilikuwa nakuja na wale wazee, lakini kila wakati alikuwa anawapa imani kwamba, Serikali itafanya na leo wamefanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupandisha kutoka shilingi 100,000 mpaka shilingi 250,000, sawa na 149.8%, sio jambo la kawaida. Bahati mbaya wakati Mheshimiwa Waziri anasoma bajeti aliruka kipengele chao, jirani yangu ni shahidi, simu zilikuwa zinaita hapa mpaka ninawawekea jamani niko Bungeni; "mbona Waziri katusahau na ulisema atatukumbuka?"

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipotoka nje nimewapigia nikawaambia, kiwango chenu kimepanda mpaka shilingi 250,000. Wale wazee wanasema wameamini hakika, kumbe mama kuwa kiongozi ni mlezi na anayejali. Ilikuwa ni miaka mingi sana hawajawahi kufanyiwa jambo la aina hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumamosi tulikuwa na Mkutano Dar es Salaam na Vijana wa Temeke wanawaambia wana shaka na kura za Mama Samia kwa sababu, mikopo ya halmashauri ndiyo wanayotumia kununua bajaji, maguta na pikipiki. Leo wameenda wamewapunguzia ushuru, wamewagusa vijana wa Kitanzania, akinamama wa Kitanzania wamewagusa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameenda kwenye Mifuko ya Jamii, Mwaka 1999 ndiyo tulibadilisha Sheria ya Kikokotoo. Kwa hiyo, wale waliokuwa wameanza toka miaka ya nyuma mpaka 1999 walikuwa hawachangii kikokotoo, lakini Serikali ikabeba, itawalipia na hili deni lilienda likataka kuangusha mifuko yetu, lakini leo ninaona wametoa hapo zaidi ya shilingi trilioni mbili kwenda kulipa deni hilo, si suala dogo, wameweza kuienzi, lakini hata waliokuwa na vyeti *fake* waliwalipa. Tunaishukuru sana Serikali hela waliyowapa si kidogo, imewasaidia kwenye maisha yao. Tuseme nini zaidi ya kurudisha ahsante kwa Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi uliopita nilikuwa naagana na Watumishi wa Serikali kwamba, sitaendelea kuwa Mbunge wa Wafanyakazi, walinipa tuzo, lakini niwaambie tuzo hii iende kwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, iende kwa Baraza la Mawaziri. Mawaziri niliwasumbua sana na mambo ya watumishi, lakini hawakuniacha walikuwa na mimi kwa masuala ya watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaongea kwa uchungu sana, watumishi wa Tanzania walikuwa wanaumia sana, walikuwa wananyanyasika sana, lakini leo wamelipa madeni yao yote; wamelipa mishahara, wamewapandisha vyeo, Mungu awabariki sana Baraza la Mawaziri. Ninawaombea sana walio kwenye majimbo na Viti Maalum Mungu akawaguse wanaoenda kupiga kura wawarudishe, lakini mwenzangu wa Dar es Salaam, Mheshimiwa Kitila, namwahidi iwe mvua iwe jua nitaweka kambi Ubungo, ili arudi na jicho la Mheshimiwa Rais limwone, ampe hii Tume na Wizara ya Mipango aendelee kufanya mambo yatakayosaidia nchi hii. Ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwaambia tuzo hii iwe ya Mheshimiwa Spika na wasaidizi wake kwenye Kiti pale; nilikuwa nikianza kuchangia mambo ya wafanyakazi, ukimwangalia Spika kama umechangia kitu cha maana huwa anacheka, ukiona ameshika kichwa kainama acha, hapo umeshapoteana. Kwa hiyo, nilikuwa nikianza kuchangia namwangalia, nikiona ametabasamu ninaendelea kukomelea mambo ya watumishi, lakini saa nyingine ananisaidia. Hata yeye alisaidia sana kwenye kuwaomba *document* watumishi wanapoenda kustaafu na leo wamejirekebisha. Sasa hivi wanaichukua kwa mfumo na mtumishi anapata pensheni yake muda mfupi baada ya kustaafu. Ninawashukuru na Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru wanawake wa Mkoa wa Dar es Salaam, mimi ni nani Janejelly, mtoto wa mnyonge, mkulima, ambaye nilikuwa sina jina, wanawake wa Dar es Salaam wakanipa jina. Ndiyo maana ninawaahidi na kuwaambia ninarudi, wasinichoke, wanitume sasa nikawafanyie wao kazi. Kwa watumishi nimefanya, sasa ninarudi kwao nikawafanyie kazi, niwalipe walichoniazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza Watumishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania maana inawezekana nisipate nafasi nyingine ya kuwapongeza. Watumishi wa Bunge Mungu awabariki sana, nimefanya kazi sehemu nyingi, nimefanya kazi Nishati, nimefanya kazi Wizara ya Fedha, kule kuna sifa ya kazi sana, lakini Bunge nimekuta sifa ya kazi na nidhamu iliyotukuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijawahi kuona mtumishi wa Bunge amekasirika na tunawakera saa zingine, lakini atakwambia Mheshimiwa samahani, unahitaji nini? Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtaona hata waliomo humu ndani Bungeni unaweza ukamwita, saa zingine huna sababu ya msingi, lakini unamnyooshea kikaratasi, anakuja na atacheka, ataondoka. Endeleeni hivyo hivyo na niwaambie, mtumishi wa Bunge akihama hapa akaenda Wizara nyingine kila mwaka atakuwa mfanyakazi bora. Wana nidhamu iliyotukuka, wana uvumilivu ambao umepitiliza, Mungu awabariki sana, lakini watuweke kwenye maombi yao, ili basi nasi turudi tuungane nanyi kwa sababu, tutawa-*miss* sana tusiporudi. Wanajua nilikuwa Kamishna wao, ninawapenda sana marafiki zangu sana, waniombee sana, ili nirudi tena tuendeleze gurudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niseme tu ninaaga, lakini ninawaombea ninajua wote tutarudi. Mungu hajaacha kumwacha mja wake, wote tutarudi mahali humu. Mungu humpa ampendaye na humnyima ampendaye, usipopata usiumie, Mungu bado anakupenda na ukipata ufurahi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia muda huu kwa Mzee wangu Mkuchika, ametangaza hatarudi. Huyu ndiyo nilianzanaye kazi na siku ya kwanza niliyosema mshahara, aliniita akaniambia wewe bwana wewe mbona unakuja na *speed* kali sana bwana? Hayo si uje uniambie kule Wizarani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikamwambia hapana! Humu ndiyo nalindwa na ninachoomba ni mshahara wa watumishi, lakini aliniambia tutafanya. Bahati mbaya akaumwa, alivyorudi nikaendelea na Mheshimiwa Jenista, lakini kila Waziri niliyefanya naye kazi utumishi, leo hii ninapoaga hapa niko na Mheshimiwa Simbachawene, ninadhani ofisini kwake nilikuwa na kiti, pole sana kwa usumbufu. Ninamshukuru sana yote ilikuwa ni kuwatumikia Watumishi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Janejelly James Ntate kwa kukamilisha mchango wako kwa namna hiyo. Ninatumia fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza wote ambao wametoa michango yao kwenye hii bajeti kuu. Ninawapongeza pia, Mawaziri wote na timu zao, wamekaa toka asubuhi wanasikiliza kwa umakini kabisa. Basi niwatakie kila la kheri na jioni njema.

Baada ya kusema hayo, ninaahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.04 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 17 Juni, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*